

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Arobaini na Tano – Tarehe 13 Juni, 2019

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mkutano wa Kumi na Tano Kikao cha leo ni Kikao cha Arobaini na Tano. Katibu

NDG. STEPHEN KAGAIGAI –KATIBU WA BUNGE:

HATI ZA KWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Tamko la Sera za Fedha kwa kipindi cha mwaka 2018/2019 na Mwelekeo wa Sera za Fedha kwa mwaka 2019/2020 (*The Monetary Policy Statement for the Year 2019/2020*).

Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 – 2018/2019.

SPIKA: Ahsante sana kwa mawasilisho hayoMheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Katibu

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Tunaanza na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa swali litaulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Mtwara Mjini Mheshimiwa Maftaha Nachuma uliza swali lako tafadhali

Na. 375

Kuwalipa Mishahara Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa

MHE. MAFTAH A. NACHUMA aliuliza:-

Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji na Vitongoji wanafanya kazi kubwa na ngumu sana hasa Mtwara Mjini na maeneo mengine ya nchi yetu.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwalipa mishahara kama ilivyo kwa Watendaji wa Vijiji na Mitaa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kazi kubwa na nzuri inayofanywa na Wenyeviti wa Vijiji, Mitaa na Vitongoji katika shughuli za maendeleo. Hata hivyo, kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Wenyeviti wa Serikali za Vijiji, Mitaa,

Vitongoji na Wajumbe wa Serikali za Vijiji pamoja na Wajumbe wa Mitaa za mwaka 2014 zilizotolewa kuitia Tangazo la Serikali Na. 322 na Na. 323, sifa zinazomwezesha mkazi wa Mitaa, Kijiji na Kitongoji kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti au Mjumbe wa Serikali za Mitaa ni pamoja na kuwa na shughuli halali inayomwingizia kipato.

Mheshimiwa Spika, Wenyeviti wa Vijiji, Mitaa na Vitongoji siyo watumishi wa umma na hivyo hawaajiriwi na kulipwa mishahara kama ilivyo kwa Watendaji Vijiji na Mitaa. Hata hivyo, kwa kuzingatia kazi kubwa inayotekelvezwa na viongozi hawa katika kusimamia shughuli za maendeleo katika maeneo yao, Serikali inawalipa posho kutokana na asilimia 20 ya mapato ya ndani ya Halmashari kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290. Ulipaji wa posho ya viongozi hao unategemea hali ya makusanyo ya kila Halmashauri. Serikali inatoa wito kwa Halmashauri zote ikiwemo Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani kuthamini mchango mkubwa wa viognozi hao na kuwalipa posho kutokana na mapato ya ndani. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Mtwara Mjini uliza swali lako

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza kwa kuwa hawa Wenyeviti wa Serikali za Vijiji na Mitaa wanafanya kazi inayofanana kabisa na hawa Watendaji wa Vijiji na Mitaa, lakini Serikali inawalipa Watendaji tu. Je, Serikali haioni kwamba inawabagua Wenyeviti hawa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwa kuwa Halmashauri nyingi hivi sasa mapato yake yamechukuliwa na Serikali ikiwemo kodi ya majengo pale Mtwara Mjini na nchi nzima kiujumla ambayo ilikuwa inasaidia sana kupata makusanya ili kuweza kuwalipa posho kwa mujibu wa sheria hawa Wenyeviti wa Vijiji Serikali ama Vijiji vingi ama Halmashauri

nyingi zinashindwa kutoa hata posho ya shilingi 20,000 kwasababu haina vyanzo vy a mapato ikiwemo kodi ya majengo.

Je, Serikali ni lini itarudisha kodi hii ili halmashauri nyingi ziweze kukusanya na kuwapa posho Wenye viti wa Mitaa?

SPIKA: Ahsante sana, majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge swalii lake la kwanza anasema Serikali inawabagua Wenye viti kwa sababu Watendaji wanalipwa. Suala hili siyo kweli kwa sababu wanapokuwa wanaomba hizi kazi utaratibu unatofautiana, Wenye viti wa Mitaa wanachaguliwa na wananchi wao na wale Watendaji wanaomba kazi na wanaajiriwa na Serikali na nimeeleza kwenye jibu la msingi ni kwamba malipo ya Wenye viti wa Mitaa na Wenye viti wa Vijiji na Wajumbe wao inategemea makusanyo ya mapato ya ndani na tumeshapitisha bajeti, hatujazuia Halmashauri kuwa na uwezo wa kuwalipa Wenye viti tukazuia, ndiyo maana tukasema tunatambua kazi nzuri inayofanya kwa sasa utaratibu uliopo Halmashauri yenye uwezo italicipa posho kulingana na uwezo ule na Wenye viti wa Mitaa waendelee kutuvumilia uwezo ukiruhusu hatujakataa kuwalipa ila uwezo ukiruhusu watalipwa.

Kwa hiyo, Halmashauri zetu kama watabuni vyanzo vingine vy a mapato wakipata uwezo wa kuwalipa watalipa Serikali hajizua kabisa. Lakini hakuna ubaguzi na Wenye viti wanajua kwamba hawa ni waajiriwa, wanaombwa na vyeti, wana-*qualify* na hawa ni watumishi wa wananchi ambao wamechaguliwa na wananchi wale na wanafanyakazi nzuri sana kama tulivyosema.

Mheshimiwa Spika, swalii lake la pili anazungumza kurudisha kodi ya majengo, kwa hiyo, kuwezesha Serikali zetu kwenye Halmashauri kuwalipa Wenye viti wa Mitaa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kodi hii kuchukuliwa kodi ya majengo pamoja na mabango pamoja na kodi zingine hii fedha inachukuliwa yote kwa ujumla wake nchi nzima inapelekwa kwenye kapu kuu la Serikali, kwa hiyo, hata miradi ya kimkakati barabara zinazojengwa, miradi ya maji, mishahara ya watumishi hii ni fedha ambayo inatumika kule, kwa hiyo siyo kwamba haina kazi. Lakini tumeelekeza Halmashauri na tumewaambia wabuni miradi mbalimbali ya kimkakati na Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Fedha tunawezesha kuanzisha miradi mikubwa mikubwa na Mtwara nimekuja pale kuna miradi mikubwa inaanizishwa.

Kwa hiyo ukipata uwezo kama huu ukapata fedha katika eneo lile na vyanzo vingine ukibuni bila kunyanyasa wananchi wataongezewa posho zao. Kwa sasa Halmashauri itaendelea kulipa kwa kadri itakavyoweza na pamoja kazi nzuri inayofanyika hatujazuia Halmashauri kulipa kulingana na uwezo wake.

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana. Nani hapa amehusika na mambo ya Halmashauri, Halmashauri Mheshimiwa Mbunge wa Moshi Mjini nimekuona uliza swali lako.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuwa Halmashauri nyingi nchini zinalipa hiyo posho ya Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji kati ya shilingi 5,000 mpaka shilingi 10,000. Je, Serikali haioni sasa kwamba imefika wakati ambapo wanapaswa kutoa maelekezo viwango vya posho hizo kupanda na vikawa vinafanana kwa Halmashauri zote nchini?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, nyongeza ya posho.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Moshi Mjini ambaye pia alikuwa Mwenyekiti wa Halmashauri Mstaafu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hoja ya nyongeza ya posho ya Wenyeviti wa Mitaa inategemea na uwezo wa Halmashauri, mimi nafahamu natoka katika Halmashauri ya Ilala. Ilala wanalipa posho kwa mwezi shilingi 100,000 Wenyeviti wa Mitaa na wanalipa kila baada ya miezi mitatu, mitatu, lakini hiyo inategemea na mapato makubwa ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, Kinondoni na Temeke.

Kwa hiyo, kama Moshi na maeneo mengine yana uwezo kama nilivyosema hatujazuia kabisa, fedha inayokusanya kwenye Halmashauri kuna maelekezo yametoka, kwa mfano asilimia 10 itaenda kwenye vijana, akinamama na watu wenyе ulemavu. Fedha zingine kuna maelekezo mengine yametoka, lakini inayobaki fedha ya maendeleo itatengwa, lakini inapohusika na uendeshaji kama ni Halmashauri ngazi ya Kata, Vijiji na Vitongoji inahusika. Kwa hiyo Halmashauri yenye uwezo itaendelea kulipa posho kubwa kulingana na uwezo wake. Hilo linaruhusiwa hatujazuia. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Lubeleje, Senator.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri mimi nimekuwa niliwahi kuwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya wakati ule Halmashauri zote vyanzo vyote vilikuwa pale, lakini kwa kuwa Serikali imechukua vyanzo vyote na tulikubaliana mpeleke ruzuku ya kutosha kwenye Halmashauri ili viongozi hawa Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji na Madiwani walipwe. Kwa nini hamuongezi ruzuku kwenye Halmashauri za Wilaya?

SPIKA: Majibu ya swali hilo la Senator Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, Mwenyekiti wa Halmashauri wa enzi hizo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa

Spika, ahsante kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Senator Mzee Lubeleje kama ifuatavyo:-

Ni kweli ni Mwenyekiti wa Halmashauri Mstaafu na alivyozungumza ni kweli wakati huo, lakini sasa hivi ni kweli kwamba baadhi ya vyanzo vimechukuliwa ili viweze kuratibu kwa sababu kuna Halmashauri ambazo zilikuwa na majengo mengi na mabango mengi na walikuwa wanaweza kupata fedha nydingi kwa wakati mmoja tofauti na maeneo mengine, Serikali imetumia busara kwamba fedha hizi zikusanywe *centrally*, lakini zipelekwe kwenye miradi ya wananchi ambayo ni nchi nzima hata Halmashauri ambayo ilikuwa na mapato machache ya mabango au na majengo inapata miradi mikubwa ya kimkakati ili maendeleo yaende katika msambao unaofanana katika nchi yetu.

Lakini hoja yake ya kuongeza posho na kupeleke ruzuku, miradi mingi ya ruzuku ilikuwa inategemea pia na wafadhili kutoka nje, sasa hivi ndiyo tukasema fedha zipo za kuanzisha miradi ya kimkakati na maelekezo yameenda kwenye Mikoa yote na Halmashauri zote. Ni wataalamu wa Halmashauri yako Mheshimiwa Lubeleje wanakaa, wanaandaa andiko, wanakaa na watu wa Wizara za Fedha na TAMISEMI, miradi inapelekwa ndiyo maana nikasema ukipata miradi ya kimkakati, masoko, *stand* kubwa kubwa zile mapato yataongezeka na kwa hiyo Halmashauri itaweza kulipa posho za Wenyeviti wa Mitaa.

Mheshimiwa Spika, niseme maneno ya nyongeza wenyeviti wa mitaa tunatambua kazi kubwa sana ambayo wanafanya na ndiyo maana miradi yote mikubwa ya kimkakati ipo kule wanaisimamia kwa kushirikiana na viongozi wa Kata na Madiwani na wengine, uwezo wetu wa Serikali ukiwa mkubwa tungeweza kulipa mishahara na posho kubwa kubwa, kwa sasa hatujafikia huko.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wenyeviti wa Mitaa waendelee kufanya kazi kwa sababu wameaminwa na watu wao, uwezo wa Serikali ..., lakini Halmashauri zetu wajipange

kila kinachopatikana wasiwashau Wenye viti wa Mitaa, wawawezeshe ili waweze kufanya kazi zao vizuri. Ahsante.

SPIKA: Ahsante, majibu hayo yanatosha kwa swali hilo. Sasa Mheshimiwa Mary Deo Muro bado anafuatilia *FDC Kibaha*. Mheshimiwa Mary.

Na. 376

Kuboresha Chuo cha FDC

MHE. MARY D. MURO aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha Chuo cha *FDC* kilichoko Shirika la Elimu Kibaha ambacho hakina vifaa vya kujifunzia, karakana zimechoka pamoja na miundombinu milbovu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mary Deo Muro, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi (*Kibaha Folk Development College -KFDC*) kilianzishwa mwaka 1964 kikijulikana kama *Farmers Training Centre* kwa ufadhilli wa Serikali ya Norway chini ya Mradi wa *Tanganyika Nordic Project*. Baada ya mradi huu kukabidhiwa kwa Serikali ya Tanzania mwaka 1970, jina la mradi lilibadilika na kuitwa Shirika la Elimu Kibaha na hivyo chuo kikawa chini ya Shirika hili. Mwaka 1975 wakati huo Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vilipoanzishwa nchi nzima, chuo hiki kilianza kuitwa *Kibaha FDC* chini ya Wizara ya Elimu kikiwa miongoni mwa vyuo 55 nchini. Kwa kipindi kirefu chuo hiki hakijafanyiwa ukarabati mkubwa, hata hivyo, kupitia mapato yake ya ndani chuo kimekuwa kikifanya ukarabati mdogo mdogo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kupitia Chuo Kikuu cha Ufundi cha Dar es Salaam

(DIT) imekifanya chuo tathmini na kuandaa mpango mkubwa wa ukarabati. Vilevile chuo kiliandaan andiko la mradi na kuomba fedha kutoka Serikali ya Uhlanzi ili kuboresha chuo ambapo vifaa vyenye thamani ya shilingi milioni 70 vilipatikana na kusaidia kupunguza tatizo la ukosefu wa vifaa chuoni.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kukarabati chuo hicho utakaoteklezwa kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mary swali la nyongeza tafadhalii.

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Spika, ahsante nafikiri hata wewe umeshangaa ukiwa kwenye kiti hicho hicho mwaka jana nilisimama mbele yako nikiuliza kwa nini chuo hiki hakifanyiwi ukarabati na ilijibowi na Wizara ya Elimu mpaka mwaka jana ilikuwa hajulikani kama chuo hiki kiko chini ya Wizara ya Elimu au TAMISEMI, walipeleka Wizara ya Elimu pesa ya chakula wakaenda kuwanyang'anya wakasema kwamba chuo hiki hakiko chini ya Wizara ya Elimu na mpaka tunavyoongea saa hizi watoto wa shule pale hawana chakula sasa hivi tunajibowi na TAMISEMI ina maana mpaka sasa hivi ndiyo imejulikana kwamba chuo hiki kiko chini ya TAMISEMI.

Sasa swali je, ni lini chuo hiki kitapata ruzuku ya chakula kwa sababu makusanyo yao ni madogo sana?

La pili, ni lini majengo na miundombinu ya chuo hicho yatafanyiwa uboreshaji?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo ya chuo hiki muhimu kiko pale pemberi ya Kibaha Sekondari.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifuatilia suala hili na fedha zilipelekwa pale, hiki chuo kiko chini ya TAMISEMI, kwa hiyo ilipogundulika kwamba fedha

zimepelekwa pale na Wizara ya Elimu, ikabidi zirudishwe zipelekwe kwa malengo yaliyokuwa yamekusudiwa. Lakini nimesema kwamba chuo hiki kimeshafanyiwa tathmini, tumepeleka fedha pale milioni 70 kwa mapato ya ndani kwa maana ya kupunguza shida iliyopo, lakini tunaendelea kutafuta fedha zikipatikana wakati wowote hata leo kitaanza kufanyiwa ukarabati huo mkubwa wala hamna shida.

Mheshimiwa Spika, lakini swalilake la pili anauliza habari ya chakula, hili naomba nilipokee tulifanyie kazi kwa sababu utaratibu ni kwamba wanafunzi wote ambao wapo maeneo yote nchi nzima wanaosoma lazima wapewe chakula na tunapeleka fedha ya chakula kulingana na idadi ya wanafunzi katika eneo hili na hawezikukaa shulenii bila kuwa na chakula.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niahidi kwamba hili tutalifanyia kazi mapema iwezekanavyo liweze kufanyiwa kazi kama kweli ni tatizo katika eneo hilo.

SPIKA: Ahsante nilikuona Mheshimiwa Waziri wa Elimu Kivuli.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, wote tunatambua lengo kubwa la vyuo hivi ni pamoja na kuondoa ujinga lakini vilevile kufanya watu waweze kujajiri wenyewe na lengo kubwa nilikuwa na mimi nashangaa ni kwa sababu gani *what is the uniqueness* ya hiki chuo mpaka hiki kiwe chini ya Wizara ya TAMISEMI wakati tunajua vyuo vyote vya maendeleo vilikuwa chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na vyote vikapelekwa Wizara ya Elimu.

Sasa nataka kujua *what is uniqueness* yaani nini upekee wa chuo hiki kuwa chini ya TAMISEMI wakati tunajua Wizara ya Elimu ndiyo ingeweza zaidi kuhakikisha kwamba vinajengewa labda hata hizi changamoto zisingekuwepo? Nilitaka kujua hilo.

SPIKA: Mheshimiwa Profesa Ndalichako, Waziri wa Elimu majibu ya swali hilo.

WAZIRI WA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI kwa majibu yake mazuri kuhusiana na swali hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Lyimo kama ifuatavyo; ni kweli kwamba vyuo vyote vya maendeleo ya wananchi viko chini ya Wizara yangu na Wizara imekuwa ikivifanyia ukarabati vyote 54 ambavyo viko chini ya Wizara na hapa katika majibu ya msingi Mheshimiwa Naibu Waziri ameелеza historia ya hicho chuo. Lakini historia inaweza ikabadilika, naomba kama Serikali tulipokee hilo wazo tuangalie ni namna gani hiki chuo kinaweza tukakifanyia utaratibu ili kiweze kupata huduma vizuri zaidi kama ambavyo vyuo vingine 54 vinapata huduma. (*Makof*)

SPIKA: Nashukuru sana Mheshimiwa Profesa, *actually* Shirika la Elimu Kibaha lote kama *unit* lina hizo *entities* zake ndani yake, sasa kukichomoa chuo peke yake kikaenda Wizara hii halafu Shirika lenyewe likawa Wizara nyingine itakuwa ni kitu kidogo hakijakaa sawasawa. Litakakoenda Shirika na chuo kinaenda huko huko itakuwa ni vizuri zaidi kiutawala. (*Makof*)

Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano swali la Mheshimiwa Agness Marwa. Mheshimiwa Agness tafadhali. Mheshimiwa Chatanda tafadhali.

Na. 377

Ujenzi wa Barabara ya Makutano – Sanzate hadi Natta

MHE. MARY P. CHATANDA (K.n.y. MHE. AGNESS M. MARWA) aliuliza:-

Tangu ujenzi wa barabara ya Makutano, Sanzate hadi Natta uanze umepita muda mrefu bila mkandarasi huyo kukamiisha kazl.

Je, ni lini ujenzi huu wa barabara utakamilika ili kuwaondolea adha wananchi wanaotumia barabara hiyo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiw Elias Kwandikwa tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa Agness Mathew Marwa, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Makutano Juu – Sanzate – Natta ni sehemu ya barabara ya Makutano Juu – Natta – Mugumu – Loliondo – Mto wa Mbu – Makuyuni yenye urefu wa kilometra 437.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya barabara hii kuanza Makutano Juu-Sanzate kilometra 50 inaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami na ubia wa Wakandarasi wazawa waitwao *M/s Mbutu Bridge JV* kwa gharama shilingi bilioni 50.4 na kusimamiwa na Kampuni ya Mshauri Elekezi *M/s UWP Consulting (T) Ltd.* ya Tanzania kwa kushirikiana na Kampuni ya Mshauri Elekezi *M/s Consulting Ltd.* kutoka Afrika Kusini.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara hii ulianza tarehe 5 Aprili, 2013 na ilipaswa kukamilika tarehe 16 Mei, 2015 na aliongezewa muda hadi tarehe 28 Februari, 2019.

Hata hivyo kutokana na changamoto mbalimbali zikiwemo mabadiliko ya usanifu wa tabaka la msingi wa barabara kutoka usanifu wa awali wa G45 kwenda usanifu tabaka la saruji (CM) kucheleweshwa kwa malipo ya fidia

pamoja na mvua nyingi zilizonyesha wakati wa ujenzi huo zilisababisha maradi huu kusimama kwa muda mrefu. Kutokana na changamoto zilizijitokezo wakati wa ujenzi wa barabara hiyo, mkandarasi ameomba muda wa nyongeza utakomwezesha kumaliza ujenzi wa barabara hii mwezi Januari, 2020 ambapo maombi hayo yanafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa ujenzi wa barabara hii unaendelea vizuri ambapo maendeleo ya kazi kwa ujumla yamefikia asilimia 70.8. Aidha, ujenzi wa daraja kubwa la Kyaramo na madaraja madogo saba katika mradi kusika yamekamilika kwa asilimia 100, hivyo endapo Serikali itaridhia maombi ya mkandarasi kuongezwa muda, inatarajiwa kwamba ujenzi wa barabara hii utakamilika mwezi Januari, 2020.

SPIKA: Muuliza swali ameshakuja, Mheshimiwa Agness uliza swali lako sasa la nyongeza.

MHE. AGNESS M. MARWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa majibu mazuri ijapokuwa naonewa kila siku maswali sipewi.

MBUNGE FULANI: Hee! Yeye mwenyewe amechelewa.

MHE. AGNESS M. MARWA: Mheshimiwa Spika, swali langu la nyongeza, Mheshimiwa Naibu Waziri huyu mkandarasi kama ameomba muda wa nyongeza na atapewa na Serikali, je, ikifikia muda huo ikiwa barabara hiyo hajjamalizika nini kitafanyika? Je, atapewa muda tena aendelee au atapewa muda mkandarasi mwingine ili aimalizie hii barabara?

SPIKA: Ahsante sana, majibu kuhusiana na swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano; Natta - Mgumu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, kwanza

uniruhusu nimpongeze sana Mheshimiwa Agness amekuwa akifuatilia sana juu ya maendeleo ya Mkoa wa Mara juu ya barabara nyingi ambazo kimsingi Serikali imepeleka miradi mingi sana katika Mkoa huu na hivi karibuni Mheshimiwa Marwa unakumbuka Mheshimiwa Rais ameongeza miradi kadhaa ya ujenzi wa barabara ya lami katika Mkoa wa Mara, kwa hiyo nakupongeza sana.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu swali lake anasema kwamba endapo tutamuongezea mkandarasi huyu kwamba muda na asipokamilisha itakuwaje; kimsingi niseme kwamba zoezi la kumuongezea muda linazingatiwa kitaalam ili kuona nini kazi iliyo mbele ya safari ili kukamilisha mradi huu. Kwa hiyo, ninaamini muda ambao utaongezwa utakuwa ni muda ambao utawezesha kutekeleza mradi huu kwa wakati kulingana na utaalam kulingana na taratibu. Kwa vile suala hili ni la kimkataba nikuhakikishie Mheshimiwa Marwa kwamba sisi tunatasimamia vizuri mkataba huu ili kazi ikamilike na zipo hatua za kuchukua kulingana na utaratibu wa kimkataba kama wakandarasi hawa watakiuka mkataba basi sheria itachukua nafasi yake.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme kwamba mradi huu unajengwa kwa kutumia *joint venture* na nia ya Serikali kuwasadia wakandarasi wazawa ili waweze kujenga uwezo, ili waweze kujenga mitaji, lakini ili waweze kusababisha ajira nyingi kwa vijana wetu lakini hili pia ile faida inayopatikana iweze kubaki hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni nia ya Serikali kuwawezesha hapa, sasa watumie fursa hiyo ambayo Serikali niwaombe sana wakandarasi hawa wakiingia kwenye *joint venture* watumiea fursa hii nzuri ili kuhakikisha kwamba tunawasidia kama Serikali na kama watashindwa basi Serikali itaendelea na taratibu ambazo zipo. Kwa maana hiyo kwamba kulikuwa kuna changamoto za kiuendeshaji na za kiutawala katika JV hizi ambapo tumeelekeza wenzetu au pande wa CRB na wenzetu wa ERB kwamba ndio walezi wa hizi taasisi wawasimamie vizuri na wahakikishe ubora,

wahakikishe nidhamu ili tuwajenge vizuri waweze kusaidia nchi yetu, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana eeeh Mheshimiwa Naibu Waziri umeona maswali ya barabara yalivyo mengi namna hii, maana yake sijui hata nani sasa! Ngoja tulibakize huko huko Mara, Mheshimiwa Mbunge wa Bunda Mjini.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nakushuru sana kwa kunipa nafasi tatizo la kusuasua kwa miradi ya barabara Mkoa wa Mara halijaanza kwenye Bunge hili tu, tangu Bunge liilopita na Wabunge wa Mkoa wa Mara kujali itikadi zetu katika vikao vyetu tumekuwa tukionesha uhitaji wa miradi hii kukamilika mapema. *Issue* ya mradi wa Natta - Mgumu - Serengeti ni wa muda mrefu na unafanana kabisa na mradi wa ujenzi wa barabara kutoka Kisolya - Bunda - Nyamuswa na wenyewe umekuwa ukisusua mbali na tatizo la wakandarasi, lakini tatizo kubwa ni Serikali kutopeleka pesa ili miradi hii ikamilike haraka.

Sasa ni lini Serikali itapeleka pesa za kutosha barabara hizi za muda mrefu takribani miaka 10 ziweze kukamilika?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano lini mtapeleka rasilimali barabara hizi zikamilike?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, kwanza nimuombe Mheshimiwa dada yangu Ester Bulaya kwamba hata hiki kinachofanyika na kwa sasa na kwa kasi hii angalau aone shukrani, aweze kushukuru kwa sababu niseme kazi kubwa inafanyika barabara hii ya Bulamba - Kisolya ni muda mrefu imekuwepo na kumekuwa na changamoto nyingi. Zipo changamoto ambazo zimekuwa kwa upande wa mkandarasi na zipo changamoto ambazo zimekuwepo kwa upande wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali sasa ipo kazini, Serikali sasa inafanya kazi nzuri na wiki iliyopita mkandarasi huyu kwa miradi

ambayo anaendelea amelipwa zaidi ya bilioni tano. Nitumie nafasi hii niishukuru sana Wizara ya Fedha. Sasa kazi yetu kubwa ni kusimamia yale ambao yaikuwa saa nyingine tunaona kwamba tumekuwa na madeni mengi, lakini wakandarasi wote nchini wamelipwa sasa tupo *current* tunaenda vizuri.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Ester nenda Bunda uone kazi inavyoendelea na tumepokea wiki mbili tu zilizopoita zaidi ya shilingi bilioni 184 kwa ajili ya kulipa wakandarasi nchi nzima. Kwa hiyo kwa upande wa Serikali tupo vizuri, Wizara ya Fedha inafanya vizuri na sisi kwenye usimamizi tuko vizuri.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kweli kwa sababu unaona tunaanza mradi wa kutoka Bulamba kuja Bunda kwenda Nyamuswa kilometra 56 na Bunge lako limetenga fedha kuhakikisha kwamba mradi huu nao unaenda.

Mheshimiwa Spika, niseme kama nilivyosema mwanzoni kwamba ipo mradi mingi, ipo mradi mzuri iko hatua katika Mkoa wa Mara, miradi mingi inaendelea kutekelezwa, ahsante.

SPIKA: Ahsante, Kamishna Mary Chatanda.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza niwapongeze wenzetu wa *TARURA* kwa kazi nzuri wanazofanya pale Korogwe ajili ya ujenzi wa zile barabara kwa kiwango cha lami na kiwango cha changarawe. Nina swali la nyongeza.

Kwa kuwa mnawapa fedha kwa ajili ya ujenzi wa zile barabara za changarawe na Mji wa Korogwe umekaa bondeni, mvua zikinyesha kama hivi sasa barabara zile zote zinasombwa na maji.

Je, Serikali itakuwa tayari sasa mnapotupa fedha hizo kutuwekea na fedha za kujenga mifereji ili kusudi ziweze kuhimili hizo barabara kwa muda mrefu?

SPIKA: Majibu ya barabara za Korogwe Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias Kwandikwa tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, ni kweli tumekuwa na chombo hiki cha *TARURA* ambacho wenzetu upande wa *TAMISEMI* wanakismamia, hata jana nilizungumza hapa kwamba *TARURA* wameanza vizuri kwa sababu kazi iliyokuwa inafanyika ilikuwa ni kuzitambua barabara zetu, kuzichambua barabara zetu na hivi ninavyozungumza lipi zoezi linaloendelea kule Morogoro kwa ajili ya kuzipanga barabara zetu pamoja na kuainisha changamoto ambazo zimejitokea katika maeneo yetu. Kwa hiyo Mheshimiwa Chatanda uvute subra najua tumezungumza sana mara nydingi, sasa uchambuzi unaendelea.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu kwamba pamoja na hayo zoezi hili la kuangalia juu ya mifereji sio kwa Korogwe peke yake lakini nchi zima tunaingalia, kwa sababu barabara zetu zikijengwa kwa namna yoyote ile kama hatutazingatia kuweka vizuri mifereji hii, maji ya mvua ni chanzo cha uharibifu wa barabara zetu. Kwa hiyo, hii tunalizingatia na nilipokee tu pia kama ushauri na tulingalia kwa macho mawili ili kuhakikisha kwamba wakati tunaboresha barabara zetu vizuri lakini suala la *ku-control* maji hasa maji ya mvua tunalifanya ili barabara zetu ziweze kudumu, ili pia katika makazi ya watu wananchi wetu waweze kuwa salama.

SPIKA: Wa mwisho kwenye eneo hili Mheshimiwa Jerome Bwanausi tafadhalii uliza swali lako.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali.

Kwa kuwa barabara ya kutoka Mwitika kwenda Maparawe na kutoka Chiungutwa - Mipande hadi Mtengula haipitiki kutokana na madaraja hayo kung'olewa na mafuriko miaka mitano iliyopita na Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba madaraja hayo yatajengwa.

Je, ni lini ahadi ya Mheshimiwa Rais itatekelezwa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, ni kweli zipo ahadi za Mheshimiwa Rais zipo ahadi nyingi na niseme tu kwamba ni ukweli baadhi ya ahadi zimetekeliza 100%. Zipo baadhi ya maeneo ambazo tumetekeliza kwa kiasi fulani na tunaendelea kutekeleza na niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge ahadi zote za Mheshimwa Rais na viongozi wakuu tunaendelea kuzitekeleza.

Mheshimiwa Spika, Iakini Mheshimiwa Bwanausi umezungumza juu ya haya madaraja na utakuwa shaidi kati haya madaraja ambao yalikuwa ni sehemu ya ahadi madaraja manne kama zikosei matatu tayari yamekwisha tekelezwa, tumbakiza lile daraja moja naomba uvute subira kwa sababu tunawenda hatua kwa hatua kwa dhamira ile ile kuhakikisha kwamba tunafanya maboresho makubwa katika kutekeleza ahadi ya kiongozi wetu mkuu Mheshimiwa Rais wetu, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana wakati tunahama Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye *design* ya ile barabara kwenye swali la msingi illikuwa ni Natta – Mugumu kuititia Nsanzate moja kwa moja, sijui kwa nini wali-*design* hivyo mwanzoni, Iakini ingekuwa Natta ikapita Fort Ikoma kwenda Mugumu ingesaidia sana kwenye utalii kwa *Western Gate* ya Serengeti, sijui kwa nini walifanya mkato lakini ingezunguka hivi ingekuwa na *impact* kubwa zaidi kitaifa kifedha na kiatalii.

Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi kwa niaba yake.

Na. 378

Ajali Zinazosababishwa na Waendesha Bodaboda

MHE. BONIPHACE M. GETERE (K.n.y. MHE. VEDASTUS M. MANYINYI) aliuliza:-

Licha ya kazi nzuri ya waendesha bodaboda ya kurahisisha usafiri na kupunguza tatizo ya ajira bado ziko changamoto mbalimbali wanazosababisha kama ajali za mara kwa mara pamoja na wizi.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza tatizo hilo?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kutofautisha adhabu ya waendesha bodaboda na ile ya magari makubwa kulingana na vipato vyao?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, *Engeneer Masauni*.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vipo vyanzo vikuu vitatu vinavyosababisha ajali za barabarani hapa nchini. Vyanzo hivyo ni makosa ya kibinadamu ambayo kuchangia kwa asilimia 76, ubovu wa magari asilimia 16 na mazingira ya barabara huchangia kwa asilimia nane. Makosa ya kibinadamu ni pamoja na uendeshaji wa kizembe/hatari, mwendo kasi, ulevi, uzembe wa wapanda pikipiki, uzembe wa wapanda balskeli, uzembe wa watembea kwa miguu na sababu nyinginezo kama hizo.

Mheshimiwa Spika, aidha Serikali kupitia Jeshi la Polisi iimekuwa ikitoa elimu kwa waendesha bodaboda namna

nzuri ya utumiaji wa pikipiki ikiwa ni pamoja na kuvala kofia ngumu, kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa leseni za waendesha bodaboda ili kupunguza wale waendeshaji wasio na leseni ambao wanawenza kusababisha ajali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekwishaliona hilo na kwamba kuna hatua mbalimbali zinaendelea kufanyika ili hatimaye adhabu zitofautiane kati ya waendesha bodaboda na wale wa magari makubwa.

SPIKA: Mheshimiwa Getere uliza swali la nyongeza.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza naipongeza Serikali kwa majibu mazuri waliyoyatoa, lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa utafiti na maeneo mengi yanaonyesha kwamba bodaboda wengu katika nchi na hasa kwa Mkoa wa Mara wanafanya kazi ile bila kupata mafunzo rasmi ya kazi yao. Sasa ni lini Serikali itatoa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa vijana wote wanaoendesha bodabora katika Mkoa wa Mara?

Swali la pili, kwa jimbo langu la Bunda na hasa Wilaya ya Bunda kumekuwepo na usumbufu mkubwa wa bodaboda wakati wa siku za minada, hasa Mnada wa Mgeta, Bitalaguru na mnada wa Bulamba. Sasa je, Waziri uko tayari kuja Bunda na hasa Jimbo la Bunda kukutana na viongozi wa bodaboda na watalaaam wako wa *traffic* katika jimbo la Bunda ilikuona namna gani ya kutatua kero hiyo hasa siku za mnada inakuwa kama inafanya *operation*?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi tafadhili.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YANDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeza sana Mheshimiwa Mwita Getere, nakumbuka niliwhi kufanya ziara katika jimbo

lake tulishirikiana kwa karibu sana kuhakikisha kwamba changamoto ambazo zinawakabili wananchi wake zinazohusu vyombo vyetu vinavyohusu Mambo ya Ndani ya Nchi tunavikabili.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie kwamba hata katika hili suala ambalo amelizungumza la usumbufu wa wananchi wake kwenye minada na amenitaka niende basi namhakikishia kwamba nitafanya hivyo kama ambavyo nilifanya wakati ule.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusiana na mafunzo kwa Mkoa wa Mara tumekuwa na utaratibu mzuri kupitia Jeshi la Usalama barabarani kwa kutoa mafunzo watumiaji wa vyombo vyta usafiri barabarani. Hata hivyo nichukue nafasi hii kumhakikishi kwamba kwa kuwa nitakwenda katika jimbo lake basi tunaweza kushauriana kuwa mpango mahususi wa jimbo lake kuhusiana na utararibu wa kutoa elimu ili kuepusha usumbufu kwa wananchi wake au hususani vijana wanaendesha bodaboda waweze kutii sheria na kuepusha usumbufu na hatimaye kupunguza ajali zinaendelea kupoteza maisha ya wananchi.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Mbunge wa Mbozi uliza swali la nyongeza.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, katika Wilaya ya Mbozi kumekuwa na usumbufu mkubwa sana kwa vijana wa bodaboda ambao wameamua kujiajiri ili kuweza kujikimu katika maisha na wamekuwa wakinyanganywa pikipiki hasa katika Mji Mdogo wa Mlowo pamoja na Mji wa Vwawa na maeneo mengine wamekuwa wakisumbuliwa sana na pikipiki zao zimekuwa zikichukuliwa kupelekwa Vituo vyta Polisi.

Je, Serikali haioni kwamba huko ni kuwanyanya vijana ambao wameamua kujiajiri kupitia kazi hii ya bodaboda inayo wapatia kipato wao na wengine wameamua kuachana na maisha yao ya awali ambao hayakuwa mazuri wameamua kujiajiri. Sasa ni lini Serikali

itakataza askari wasiwanyanyase vijana hao ambao wanafanya kazi hii ya bodaboda katika Wilaya Mbozi?

SPIKA: Ahsante sana majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa *Engineer Masauni tafadhali.*

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YANDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, hatukubali kuona wala haturuhusu kuona askari wakinyanyasa wananchi. Si jukumu la askari kunyanyasa wananchi, lakini kuhusiana na suala ambalo amelizungumza kuhusiana na jimbo la Mbozi kuhusu vijana hawa ambao anadai kwamba wananyanyaswa na waendesha bodaboda nisema yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza hili tulishalitolea maelekezo hapa Bungeni kwamba kuna aina ya makosa ambayo pikipiki zikikamatwa zinakuwa katika Vituo vya Polisi kuanzia sasa na tumeshatoa waraka huo katika Makao Makuu ya Jeshi la Polisi ili wautekeleze. Sasa sina hakika kama hawa anaowazungumzia Mheshimiwa Haonga wapo katika yale makosa ambayo tumeyaruhusu waweze kukamatwa ama katika makosa ambayo tulishakata yasikamatwe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninachoweza kumhakikisha ni kwamba tutafuutilia kujua kama yatakuwa makosa ambayo tulishaelekeza yasikamatwe vijana hao basi tutachukua hatua kwa kushindwa kutekeleza maelekezo ya Wizara. Lakini kama itakuwa ni makosa ambayo yanaruhusika na tumeruhusu waweze kukamatwa basi tutamuelimisha Mheshimiwa Haonga ili aweze kuelimisha wananchi wake wafahamu na waepuke kufanya makosa kama hayo.

SPIKA: Mheshimiwa Bhagwanji halafu Mheshimiwa Selasini.

MHE. BHAGWANJI MAGANLAL MEISURIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nataka nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri, hao watu wa bodaboda wana tabia moja mbaya sana, na mimi wameshafanyiwa wageni wangu, wanapora

simu, halafu wanakimbia na hapa juzi katika eneo la *Area D* ninapokaa mimi, mama mmoja alikuwa na simu wamekuja watu wa bodaboda wamepora, sasa hatua gani Mheshimiwa Rais anawapenda wanyonge watu wa bodaboda lakini tabia hii ni mbaya sana kwa kupora.

Mheshimiwa Spika, kesho watakuwa na bastora watakwenda majumbani au madukani, kwa hiyo, mimi naomba Mheshimiwa Naibu Waziri atuambie ni sheria gani hawa watu wa bodaboda wanafanya tabia hiyo mbaya kwa kupora simu pamoja na begi? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo muhimu kutoka kwa baniani pekee Mheshimiwa Bhagwanji. (*Kicheko/Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:
Mheshimiwa Spika, si sahihi nadhani kuwajumuisha waendesha bodaboda na matukio ya wizi, waendesha bodaboda ni raia ambaao wanafanya kazi zao, wanapaswa kufanya kazi zao kwa mujibu wa sheria ya kujipatia riziki ambazo zimeruhusiwa kisheria ni shughuli za kihalali.

Mheshimiwa Spika, sasa kama kuna watu ambaao wanatumia pikipiki ama hiyo pikipiki ya kawaida ama iwe bodaboda kwa ajili ya uporaji hao ni wahalifu kama wahalifu wengine na kwa hiyo basi kama ambavyo ilivyo kawaida na desturi ya Jeshi letu la Polisi kuweza kukabiliana na wahalifu imekuwa ikifanya hivyo kushughulika na watu ambaao wakitumia pikipiki ama bodaboda kwa ajili ya kupora wananchi na tutaendelea kufanya hivyo kuwashughulikia bila huruma wale wote ambaao wanatumia pikipiki ama bodaboda kwa ajili ya kufanya uporaji.

SPIKA: Nilishakutaja Mheshimiwa Selasini tafadhali.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kutokana na uhaba wa ajira na ukosefu wa mitaji, vijana wengi wanaomaliza shule sasa hivi wameiona kazi ya bodaboda kama ni kazi ambayo inawaingizia kipato. Jimboni kwangu ukienda Mamsera pale, Mengwe, Mkuu, Useri na

Tarakea vijana waliomaliza chuo kikuu na *form six* wamejiingiza katika biashara hii na inawaletea kipato kizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sambasamba na hilo, kuna vijana wengine ambao tabia zao siyo njema sana, nao wamejiingiza kufanya sasa vijana wote wa bodaboda waonekane kwamba ni vijana ambao hawafai na baadhi ya polisi wanalamikiwa kufanya hii kazi ya bodaboda ionekane ngumu zaidi kwa kuchukua rushwa na kuwabambikia makosa.

Je, Jeshi la Polisi au Wizara hamuoni sasa kutokana na ukubwa wa kazi hii ya bodaboda kuweka polisi maalum, trafiki maalum kabisa katika kila Kituo ambaye kazi yake itakuwa ni ku-deal tu na bodaboda ili kuweza kupunguza haya matatizo yao?

SPIKA: Kuweka trafiki maalum Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, Nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Selasini kwamba biashara ya bodaboda ni biashara ambayo ni kama biashara nyingine na ndiyo maana mara nyingi sana tumekuwa tukiwaelimisha watumiaji hasa viongozi wa vijiwe hivi vya bodaboda kwamba watusaidie kuwaelimisha wenzao ambao wanafanya kazi hii kwa pamoja ama ambao wanawaongoza ili biashara ya bodaboda isivunjiwe heshima ikaonekana kwamba ni kazi ya kihuni.

Mheshimiwa Spika, na kwa kufanya hivyo nadhani itasaidia sana kuondoa taswira mbaya iliyopo kwa baadhi ya wananchi mbele ya waendesha bodaboda ama biashara za bodaboda. Sasa kuhusiana na hoja yake kwamba tuweke askari maalum, sisi tuna Kitengo cha Usalama Barabarani ambacho kinashughulika na masuala yote yanayohusu usalama barabarani yakiwemo ya waendesha bodaboda na kazi hiyo imekuwa ikifanyika kwa ufanisi mkubwa. Kwa hiyo sioni kama kuna haja ya kusema tubague labda

bodaboda iwe mbali, magari ya daladala yawe mbali, mabasi yawe mbali, nahisi kwamba utaratibu uliopo unakidhi mahitaji na tutaendelea kuboresha pale ambapo tutaona kuna mapungufu katika kusimamia Sheria za Usalama Barabarani kwa bodaboda na vyombo vingine.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Salma Kikwete na Mheshimiwa Kemilembe Lwota.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii.

Mheshimiwa Spika, bodaboda ni kitu chema na bodaboda imerahisisha usafiri, bodaboda imesaidia sana kuleta ajira kwa vijana wa Taifa letu la Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, lakini kuna changamoto zinazoweza kujitokeza pale inapotokea bodaboda imesababisha ajali barabarani, baadhi yao kwa muda mfupi wanajaa eneo la tukio na hatimaye kuweza kuchukua hatua za papo kwa papo na matokeo yake wanaweza kusababisha vifo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inachukua hatua gani juu ya kutoa elimu kwa waendesha bodaboda kwamba wasichukue hatua za mkononi? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo muhimu Mheshimiwa Naibu Waziri ni kweli ikitokea tu tatizo wanajaa pale inakuwa shida.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salma Kikwete, swali zuri na muhimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli matukio kama haya yamekuwa yakinoteka, na ni matukio ambayo yanositishaa sana na hayakubaliki katika jamii iliyoitaarabika kama jamii ya Watanzania na kwa hiyo, naendelea kutoa wito hapa, kwanza nichukue fursa hii nikitumia jukwaa hili la Bunge kama

ni moja katika njia ya elimu kwa waendesha bodaboda wote nchini kuepuka kuchukua sheria mkononi na wale wote ambao wamekuwa wakifanya hivyo hatma yao hajawa njema. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sidhani kama kuna mwendesha bodaboda ambaye anataka hatma ya maisha yake iishie gerezani au iishie kwa kuhukumiwa hukumu ya kunyongwa kwa kusababisha mauaji yasiyokuwa na lazima. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niendee kusisitiza kwamba utaratibu wetu wa utoaji wa elimu kwa bodaboda utiliwe maanani na mkazo zaidi katika eneo la kuhakikisha kwamba waendesha bodaboda hawatumlii, hawachukui sheria mkononi inapotokea matatizo ya usalama barabarani na kuacha vyombo na sheria za nchi zifuate mkondo wake. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Kemilembe swali la mwisho.

MHE. KEMILEMBE J. LWOTA: Mheshimiwa Spika, ahsante nakushukuru kwa kuweza kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, suala la ajali za bodaboda siyo kwa Mkoa wa Mara tu, ni Tanzania nzima kwa ujumla wake. Bodaboda hawa wengi wao wanakata *third part insurance* ambayo kimsingi inatakiwa iwasaidie pale wanapopata matatizo lakini kiuhalisia *insurance* hii haiwasaidii chochote bodaboda hawa wanapopata matatizo.

Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kukaa na hawa watu wa *insurance* ili baadhi ya fedha inayotozwa/ wanayolipa hawa watu wa bodaboda iweze kwenda kwenye Halmashauri zetu ili waweze kupata msaada kwenye hospitali ambapo hospitali hizi ndiyo zinawapokea na kuwatibu watu hawa? Nashukuru. (*Makof*)

SPIKA: Matibabu ya bodaboda na *insurance* kwa ujumla, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:
Mheshimiwa Spika, wazo lake linafikirika na kwa hiyo basi tunalichukua, tulitafakari.

SPIKA: Ahsante sana nakushukuru sana. Sasa tunaenda swali la mwisho la siku ya leo la Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mbunge wa Mtera.

Na. 379

Hitaji la Kituo Kikubwa cha Polisi – Mtera

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kituo kikubwa cha polisi katika Jimbo la Mtera hususani katika Kijiji cha Mvumi Misheni ili kukabiliana na wimbi kubwa la uhalifu katika Jimbo la Mtera?

SPIKA: Majibu ya swali hilo bado tuko Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Naibu Waziri *Engineer Masauni tafadhali.*

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mbunge wa Mtera kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi ya vijijini nchini yameongezeka idadi ya watu, shughuli zao za kiuchumi na mambo mengine ambayo yanahitaji huduma ya ulinzi na usalama toka Jeshi la Polisi ikiwa ni pamoja na Kijiji cha Mvumi Misheni.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi inao mpango wa kuboresha na kujenga Vituo vya Polisi katika ngazi ya Tarafa na Kata nchi nzima ambavyo vitasaidia

kusogeza huduma kwa wananchi hadi waliopo katika maeneo ya vijiji ikiwemo Kijiji cha Mvumi Misheni katika Jimbo la Mtera.

SPIKA: Mheshimiwa Livingstone Lusinde.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, nikushukuru tena kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mtera lina kata 22, na lina vijiji zaidi ya 60 na kitu, Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye jibu lake la msingi anasema wana mpango wa kujenga vituo kila kata, haelezi mpango huo unaanza lini? Lakini Jimbo la Mtera lina Tarafa tatu.

Swali langu la kwanza dogo la nyongeza linasema, kama kwenye Tarafa tu hawajajenga Kituo hata kimoja, je hiyo kwenye kata itawezekana? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, barabara kubwa ya Iringa - Dodoma inayopita kwenye Jimbo la Mtera, Kibakwe, Isimani Waheshimiwa Wabunge wengi na Mawaziri wanapita njia ile lakini haina Kituo cha Polisi hata kimoja chenye gari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, matokeo yake ajali zote kubwa zinazotokea njia ile, polisi inawachukua muda mrefu sana kufika, kwa mfano wiki mbili zilizopita iliokea ajali mbaya sana mama mmoja mzazi alipoteza maisha, nesi alipoteza maisha, pamoja na wasindikizaji, polisi walikuwa wanakuja wengine na lori, fuso iliwachukua muda sana kwenda kumaliza tatizo pale.

Je, Serikali ni basi itakipatia Kituo cha Mvumi Misheni gari, walau liweze kusaidia kufanya mzunguko katika barabara hiyo kubwa? Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo ya Mbunge wa Mtera, Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza linahusu ujenzi wa Kituo cha Polisi kutokana na majibu yangu ya msingi kwamba nilimwambia tuna mpango wa kujenga vituo vya polisi nchi nzima katika kila kata.

Mheshimiwa Spika, nataka nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba ujenzi huu au mpango huu wa ujenzi wa vituo ni mchakato ambao mchakato unahuishisha pia upatikanaji wa rasilimali fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo dhamira tunayo, sababu tunayo na uwezo pia tunao, lakini uwezo huo utaenda sambasamba na kadri ambavyo hali ya kibajeti itaruhusu kwa awamu, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ujenzi wa Kituo cha Polisi katika Kata ya Mvumi Misheni utapewa kipaumbele pale ambapo bajeti itakaa vizuri na mpango wetu utaanza utekelezaji wake mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Lusinde kwa sababu inaonekana ni Mbunge ambaye hapendi kujipa ujiko mwenyewe, lakini Kiukweli hili jambo tulilizungumza mimi na yeYe pamoja na Mheshimiwa Chumi ambao Majimbo yao yanapakana katika eneo hilo na wenyewe wao walikuja na wazo zuri sana la upatikanaji wa magari mawili katika eneo hilo na mchakato huo umeshaanza, naamini kabisa mimi nikishirikiana na wao tutafanikisha kupata hayo magari mawili kwa utaratibu ambao tumezungumza mimi, yeYe pamoja na Mheshimiwa Chumi na wananchi wasikie waone jitihada za Mheshimiwa Lusinde katika hili na manufaa yake watayaona muda siyo mrefu kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kwa sababu leo tuna mambo mengi sana, naomba tuishie hapo hatukuweza kuwa na maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu leo kwa sababu ya ratiba ya mambo ilivyo, tuna ratiba ambayo imejaa sana, lakini atajiunga na sisi baadae kidogo kwa sasa ana kazi maalum.

Naomba niwatangaze wageni tulionao leo tukianza na wageni 81 wa Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango Waziri wa Fedha na Mipango kutoka Wizara ya Fedha na Mipango; kwanza ni Katibu Mkuu - Ndugu Doto James, ahsante sana karibu, Naibu Katibu Mkuu - Dkt. Khatib Kazungu, karibu sana, Naibu Katibu Mkuu - Ndugu Adolf Ndunguru, karibu sana, Gavana wa Benki wa Kuu ya Tanzania (*BOT*) - Profesa Florence Luoga, karibu Gavana, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) - Dkt. Edwin Mhede karibu hongera na pole. (*Makofi*)

Pia yupo Kamishna wa Bajeti - Ndugu Mary Maganga, karibu pale ulipo, Kamishna wa Sera - Ndugu Benedicto Mgonya karibu pale utakapokuwa, Kamishna wa Fedha za Nje - Ndugu John Rubuga pia karibu, Kaimu Mhasibu Mkuu wa Serikali - Ndugu Vitus Tesha, karibu, Msajili wa Hazina - Ndugu Athuman Mbuttuka, karibu, Mtendaji Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu Dkt. Albina Chuwa, karibu sana Dkt. Albina. (*Makofi*)

Lakini pia tunaye Kamishna wa Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu - Ndugu Onesmo Makombe, karibu, Katibu wa Tume ya Pamoja ya Fedha - Ndugu Ernest Mchanga, karibu, Kamishna wa Idara ya Usimamizi wa Sera ya Ubia ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi - Dkt. John Mboya, karibu sana. (*Makofi*)

Pia viongozi hawa wameambatana na Wakurugenzi na Wakuu wa Idara na Taasisi zilizopo chini ya Wizara hiyo ya Fedha na Mipango, pia wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango ambao ni pamoja na Mkwe wa Mheshimiwa Waziri Ndugu Emmanuel Kuwese, karibu, yuko wapi, karibu sana kama upo. (*Makofi*)

Yupo pia mjukuu wa Mheshimiwa Waziri, Philip Emmanuel Kuwese karibu sana, karibu Philip amechukua jina la babu, lakini yuko mjukuu mwingine Anna Emmanuel Kuwese karibuni sana kama hamjafika nafikiri watafika baadae kidogo. (*Makofi*)

Yuko mke wa Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Ndugu Gerwalda Luoga karibu sana Mama Luoga na mtoto wa Gavana wa Benki Kuu Ndugu Karen Luoga, karibu Karen na mtoto mwingine wa Gavana wa Benki Kuu Ndugu Urso Luoga, karibu sana Urso, yuko na mtoto wa Gavana pia Osric Luoga, karibu sana Osric. (*Makofi*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni wageni 94 wa Mheshimiwa Innocent Lughashungwa ambaao ni walimu wanane na wanafunzi 84 kutoka Shule ya Sekondari ya Nyakahanga iliyoko Karagwe, Mkoa wa Kagera ambaao ni Kablu ya Wapinga rushwa, wakiongozwa na Afisa TAKUKURU Ndugu Rashida Mfaume, wageni kutoka Kagera kule Karagwe, simameni karibuni sana, sana, oohhh, mmesafiri kutoka mbali kweli watoto wetu karibuni sana hapa Bungeni ehehe, karibuni sana, ahsante sana Mheshimiwa Waziri kuwaleta vijana. (*Makofi*)

Wageni 54 wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro - Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambaao ni walimu na wanafunzi kutoka shule ya msingi ya St. Joseph ya Jijini Dar es Salaam na wanafunzi wa Chuo cha Diplomasia waliopo Wizarani kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo wakiongozwa na Mwalimu Headad Gichuhi, simameni pale mlipo, ahsante sana wale pale, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro nafikiri wapo katika *group lile lile* la Chuo cha Diplomasia.

Mgeni wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula ambaye ni mdogo wake kutoka Jijini Mwanza, Ndugu Steven Kabelinde, ahsante sana Kabelinde. (*Makofi*)

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Japhet Hasunga kutoka Vwawa Ndugu George Kibona, karibu sana George popote pale ulipo.

Wageni saba wa Mheshimiwa Zainab Bakar ambaao ni familia yake kutoka Kusini Pemba wakiongozwa na mtoto

wake Ndugu Leila Mussa wale kule karibuni sana kutoka Pemba. (*Makofi*)

Wageni 24 wa Mheshimiwa Fatma Toufiq ambaao ni wake wa Wachungaji wa Anglikana na wake wa Maaskofu wa Anglikana, Viongozi wa UWT Kata ya Msalato kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Mwenyekiti wa UWT wa Kata ya Msalato Ndugu Jemina Nchimbi, karibuni sana, karibuni sana UWT Msalato, pamoja na Mama Maaskofu karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wa wanne wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambaao ni Timu ya Taifa ya Watu Wenye Ulemavu ya wanyanya vitu vizito kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu John Jamal, karibuni sana sana sana. (*Makofi*)

Hebu simameni tena, mko wangapi? Okay, mbona siaona misuli ya kunyanya vitu vizito, jamani mnawaona! Eeeh! Wanaweza, kabisa kabisa. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Victor Mwambaliaswa ambaao ni marafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Evans Mlelwa, Emma Oriyo na Stanley Derick, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ambaao ni walimu ambaao shule zao zimefanya vizuri kutoka Liwale Mkoa wa Lindi, Mwalimu Noeli Nkoma, Joseph Sika na Mwalimu Diskoson Shinunje. Karibuni sana walimu kutoka Liwale, karibuni sana sana, hongereni kwa watoto wenu kufanya vizuri kwenye mitihani. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Mendrad Kigola kutoka Mufindi Mkoa wa Iringa, Ndugu Abeid Mhongole na Ndugu Josephati Mkini. Karibuni sana kutoka Mufindi. (*Makofi*)

Wageni 44 wa Mheshimiwa Desderius Mipata kutoka Shirikisho la Walimu Mkoa wa Rukwa, ooh! karibuni sana sana

kutoka Rukwa kule Shirikisho la Walimu, karibuni sana sana sana. Karibuni sana, tunafarijika kuwapokeeni. (*Makofi*)

Tunaendelea na matangazo machache yaliyobakia, wakati wa kuingia humu asubuhi kwenye mashine zetu kule za ukaguzi kuna Wabunge wawili wamebadilishana mikanda hapa. Kila mmoja amevaa mkanda usiokuwa wa kwake, sasa naomba uangalie mkanda wako kama siyo wenyewe basi niandikie hapa nikwambie umrudishie nani. Haraka haraka ile unajua tena! (*Makofi/Kicheko*)

Naomba niwatangazieni tangazo linalotoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, Mheshimiwa Ngeleja anasema siku ya Jumapili kutakuwa na bonanza kati ya *Bunge Sports Club* na *CRDB Bank* ambayo itafanyika uwanja wa Jamhuri.

Kwanza kutakuwa na *jogging* kuanzia saa 12 asubuhi, hizi ni za mwendo wa pole zinaanzia kwenye lango kuu la Bunge kuelekea *Morogoro road*. Ni *jogging* wala haitakuwa ndefu sana, kwa hiyo, tunaombwa tufike kwenye *joggings* saa 12 asubuhi siku ya Jumapili, baadae jioni kwenye michezo uwanja wa Jamhuri kutakuwa na *basketball*/wanaume peke yake; kutakuwa na kuvuta kamba wanaume na wanawake, kutakuwa na mpira wa pete (*netball* na mpira wa miguu (*football*)). (*Makofi*)

Bonanza hili litakuwa ni burudani kubwa na katika bonanza lile kule Jamhuri ambapo tunaomba Waheshimiwa Wabunge kama mtakuwepo Dodoma siku hiyo mfike, kutakuwa na muziki mkubwa pale utakaoongozwa na mwanamuziki anaitwa akina Harmonize lakini pia Profesa Jay ataweka mambo yake pale. Mazungumzo yanaendelea kama Mheshimiwa Mbilinyi pia anaweza akatumbuiza siku hiyo ya Jumapili. (*Makofi*)

Wageni rasmi katika bonanza hilo siku hiyo atakuwepo Mheshimiwa Waziri Mkuu na mimi nitakuwepo pia. Naomba sote siku ya Jumapili tufike tuburudike pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Haonga pia ana mgeni wake anaitwa Philipo Haonga, ahsante sana. Karibu sana, karibu sana, karibu. (*Makof*)

Mwisho siyo kwa umuhimu Waheshimiwa Wabunge, kuhusiana na ule mpango wetu wa safari ya kwenda Misri kwenye *AFCON*. Wabunge wamejiandikisha kwa kweli.

Kabla ya hapo kuna skauti 34 kutoka Dar es Salaam, wageni wa Mheshimiwa Mtuli. Skauti kutoka Dar es Salaam, karibuni sana, karibuni sana sana sana. Karibuni sana skauti, mnapendeza kweli kweli karibuni sana. (*Makofi*)

Kwa hiyo, *AFCON* leo ndiyo itakuwa mwisho wa uandikishaji wa Wabunge ambao mtapenda kwenda kule Misri kama tulivyokwisha kuhamasisha tangu mwazo, siyo vizuri timu yetu ya Taifa wakabaki peke yao kule, ni vizuri kabisa tukashiriki. Nilikuwa naongea na Spika wa Burundi jana na Spika wa Kenya, Wabunge wenzetu wanajiandaa kwa nguvu kubwa na Spika wa Uganda pia watakuwa kule Misri kushangilia timu zao. Nadhani kwenye ratiba kuna mahali tunakutana na Kenya sasa siyo vizuri sisi tukawa hatupo hatupo hivi, lazima wenyewe tuwepowepo hivi kwa namna moja au nyingine. Hii itaongeza hamasa kubwa zaidi kwa watanzania wote kuweza kuona namna gani wale ambao watamudu kuweza kwenda *AFCON*.

Kwa hiyo nitaomba tutakapo ahirisha shughuli hizi asubuhi baada ya Waziri wa Fedha na Mipango kusoma hotuba yake, tukishaahirisha wale ambao wanania ya kwenda kule Misri wabakie hapa kwenye ukumbi ili wapate maelezo sasa yale *technical* ya mambo yote. Wale ambao wameamua kabisa kwenda basi itatakiwa pasi ya kusafiria tuiwasilishe kwa waandaji *Bunge Sports Club* akina Mheshimiwa Ngeleja na wenzake, lakini pia na *passport size* mbili ili maandalizi yaweze kuanza haraka haraka kwa ajili ya safari hiyo ya kwenda Misri. (*Makofi*)

Kama nilivyowaambieni na mimi mwenyewe nitakuwepo huko, tutakuwa pamoja na wale ambao

tutakwenda *batch* ya pamoja kutakuwa na ziara ya kutembelea Bunge la Misri pia pale wakati wa mchana kabla ya mechi za jioni. Tutaandaa na utalii kidogo kule tufike kwenye *pyramids* na mambo mengine mazuri kwa kweli ni *outing* nzuri kwa Waheshimiwa Wabunge, ni fursa ya kipekee kabisa lakini leo ndiyo mwisho.

Kwa hiyo, kuanzia kesho tena usijitokeze kusema na mimi nina nia maana yake nafasi zitakuwa zimejaa, lazima tuanze *booking* za kila kitu, *booking* za ndege, *booking* za hoteli, kila jambo likae sawasawa mapema.

Sasa kwa sababu ya muda na mambo jinsi yalivyo leo, naomba kwa kweli tuendelee sasa. Katibu, tuendelee.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

SPIKA: Ahsante sana, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango ili sasa aweze kutuelezea kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa lakini pia atupitishe kwenye Mpango wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango karibu sana kwa hotuba yako, karibu Dkt. Mpango. (*Makof!*)

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2019/2020. Pamoja na hotuba hii nawasilisha vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2019/2020 ambapo taarifa hizi ndio msingi wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka ujao wa fedha 2019/2020 itakayowasilishwa Bungeni leo jioni. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutujalia uzima na afya njema. Kipekee nimshukuru sana kwa jinsi anavyoendelea kulijalia Taifa letu amani na utulivu na kutuwezesha kukutana katika Mkutano huu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kujadili namna ya kuharakisha maendeleo ya Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Taifa letu limebarikiwa kuwa na kiongozi shupavu, mchapakazi, mwenye maono na uthubutu wa kimaendeleo. Naomba uniruhusu nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyoendelea kuliongoza vema Taifa letu. Kwa kipindi hiki cha miaka mitatu na nusu ya utawala wake tumeshuhudia kuimarika kwa uchumi ambapo ukuaji umefikia asilimia 7.0. Mfumuko wa bei umedhibitiwa kuwa katika tarakimu moja, miradi milkubwa ya maendeleo inatekelezwa, uwajibikaji katika utumishi wa umma unaimarika na kero za wanyonge zinatatuliwa. Mimi na wenzangu Serikalini tunaahidi kuendelea kumpatia Mheshimiwa Rais ushirikiano wa hali ya juu. Aidha, ninamshukuru kwa kuendelea kuniamini kuongoza Wizara ya Fedha na Mipango. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba niwapongeze Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan - Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia ni Kiongozi wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni kwa uongozi wao mahiri katika kumsaidia Mheshimiwa Rais. Aidha, naomba kumpongeza Mheshimiwa Innocent Luga Bashungwa - Mbunge kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hoja ninayoiwasilisha hapa imetayarishwa kwa kuzingatia dhana ya ushirikishwaji mpana wa jamii ambapo tumepata maoni na ushauri kutoka katika makundi mbalimbali ya jamii na Taasisi za Serikali. Siwezi kuwataja mmoja mmoja wale wote waliota maoni na

ushauri hadi kufikia hapa, lakini ni vema nitambue mchango mkubwa wa Bunge hili kuititia kwako Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile nichukue fursa hii adhimu kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti - Mheshimiwa George Boniface Simbachawene (Mbunge) na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki (Mbunge) pamoja na Wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti kwa ushauri makini waliotupatia wakati wa uandaaji wa kitabu cha Hali ya Uchumi kwa mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2019/2020. Ushauri wao umetumika kikamilifu katika uandaaji wa hotuba na vitabu ninavyowasilisha mbele ya Bunge lako tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2019/2020 vimeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 ili kuleta mchango wa haraka katika maendeleo ya uchumi wa Taifa, umuhimu wa kumalizia miradi inayoendelea ili kupata matokeo tarajiwa, kuweka msukumo mkubwa katika kuboresha mazingira ya kufanya biashara na kuwekeza hapa nchini ili kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika kukuza uchumi na kujenga uchumi wa viwanda na maendeleo ya watu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa hali ya uchumi 2018 na naomba nianze na uchumi wa dunia; mwaka 2018 uchumi wa dunia ulikuwa kwa asilimia 3.6 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.8 mwaka 2017. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi kulitokana na kushuka kwa ukuaji wa uchumi kwa nchi zilizoendelea na zinazoendelea kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kupungua kwa mahitaji ya bidhaa na huduma kutoka nje, hali ya wasiwasi kuhusu madhara ya Uingereza kujitoa Jumuiya ya Ulaya (*Brexit*), kushuka kwa kasi ya uwekezaji, mvutano wa kibashara baina ya China na Marekani, kudorora kwa soko la fedha katika nchi za Argentina na Uturuki na mvutano wa kisiasa Mashariki

ya Kati. Aidha, mfumuko wa bei wa dunia uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 3.8 kutoka wastani wa asilimia 3.1 mwaka 2017.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa Afrika na Kikanda; kwa upande wa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara wastani wa kasi ya ukuaji wa uchumi iliongezeka hadi asilimia 3.0 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 2.9 mwaka 2017. Ukuaji huu ultokana na ongezeko la mahitaji ya bidhaa pamoja na marekebisho ya sera za kiuchumi. Mwenendo wa uchumi wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki unaonesha kuwa uchumi wa Rwanda ulikua kwa asilimia 8.6 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 6.1 mwaka 2017; uchumi wa Uganda ulikua kwa asilimia 6.1 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 5.9 mwaka 2017 na uchumi wa Kenya ulikua kwa asilimia 6.3 ikilinganishwa na asilimia 4.9 mwaka 2017.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa Taifa; Pato la Taifa, mwaka 2018 Serikali kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilifanya maboresho ya takwimu za Pato la Taifa kwa kutumia mwaka 2015 kama mwaka wa kizio kutoka mwaka wa kizio wa 2007. Kufuatia marekebisho hayo, mabadiliko kadhaa yalijitoneza ikiwa ni pamoja na mfumo na ukubwa wa Pato la Taifa, viwango vya ukuajiwa Pato la Taifa kisekta, mchango wa sekta mbalimbali katika Pato la Taifa na uwiano wa viashiria mbalimbali kwa Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu mpya za mwaka wa kizio wa 2015, pato halisi la Taifa liliukua kwa kiwango cha asilimia 7.0 mwaka 2018 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.8 mwaka 2017. Ukuaji huu ulichochewa zaidi na kuongezeka kwa uwekezaji hususan katika miundombinu kama vile ujenzi wa barabara, reli na viwanja vya ndege; kutengemaa kwa upatikanaji wa nishati ya umeme; kuimarika kwa huduma za usafirishaji na hali nzuri ya hewa iliyopelekea uzalishaji mzuri wa chakula na mazao mengine ya kilimo. Shughuli za kiuchumi zilizokua kwa kasi kubwa ni pamoja na sanaa na burudani ambayo ilikuwa kwa asilimia 13.7; ujenzi asilimia 12.9; uchukuzi na uhifadhi mizigo asilimia 11.8; shughuli za kitaaluma, sayansi na ufundi asilimia 9.9; habari na

mawasiliano asilimia 9.1. Sekta ya kilimo ilikua kwa asilimia 5.3; sekta zilizotoa mchango mkubwa katika pato la Taifa ni kilimo ambayo ilichangia asilimia 28.2, ujenzi asilimia 13.0 na biashara na matengenezo asilimia 9.1.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2018 pato la wastani la kila mtu lilifiki shilingi 2,458,496 kutoka shilingi 2,327,395 mwaka 2017 sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 5.6. Kiasi hicho cha pato la wastani kwa kila mtu kwa mwaka 2018 ni sawa na dola za Marekani 1,090 ikilinganishwa na dola za Marekani 1,044 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 4.4.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa bei; mwaka 2018 mfumuko wa bei uliendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja na kufikia kiwango cha chini kabisa kuwahi kutokea katika kipindi cha miaka 40 iliyopita. Mfumuko wa bei ulipungua kutoka wastani wa asilimia 5.3 mwaka 2017 hadi wastani wa asilimia 3.5 mwaka 2018. Hadi mwezi Aprili, 2019 mfumuko wa bei ulifikia asilimia 3.2 ikilinganishwa na asilimia 3.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Kiwango hicho cha chini cha mfumuko wa bei kilitokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kwanza, kuimarika kwa hali ya upatikanaji wa chakula katika masoko ya ndani na nchi jirani. Uzalishaji wa chakula nchini ulifikia tani milioni 15.9 ikilinganishwa na mahitaji ya tani milioni 13.3 kwa kipindi hicho, hivyo kuwa na utoshelevu wa chakula kwa asilimia 124 na sababu ya pili ni utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa sera za fedha 2018/2019; Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania iliendelea kutekeleza sera ya fedha kwa lengo la kuhakikisha kuna utoshelevu wa ukwasi kwenye uchumi kuendana na malengo mapana ya uchumi ya kuwa na utulivu kiuchumi na ukuaji endelevu jumuishi. Katika kipindi kinachoishia Aprili, 2019 Serikali ilichukua hatua mbalimbali za kuongeza ukwasi kwenye uchumi ili kuziwezesha benki na taasisi za fedha kuongeza utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi kwa ajili ya kuendeleza shughuli mbalimbali za kiuchumi. Hatua hizo ni pamoja na kutoa mikopo ya muda mfupi kwa benki, kununua

fedha za kigeni kutoka katika benki za biashara na taasisi za Serikali, kushusha kiwango cha riba ya mikopo kwa benki mwezi Agosti, 2018 kutoka asilimia 9.0 hadi asilimia 7.0 na kulipa malimbikizo ya madai mbalimbali ya wakandarasi, watoahuduma na watumishi ambapo takribani shilingi bilioni 598.4 za madai yaliyohakikiwa zililipwa katи ya Julai, 2018 na Mei, 2019.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi zilisaidia kuongeza....

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge ningewaombeni sana, hebu tumsikilize Mheshimiwa Waziri wa Fedha hii ndiyo Hali ya Uchumi wa Taifa, baada ya hapo tunatakiwa tuchangie. Sasa kama hatusikilizi, Mheshimiwa Waziri endelea.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, hatua hizi zilisaidia kuongeza ukwasi kwenye benki na taasisi za fedha pamoja na kushusha riba katika masoko ya fedha ambapo katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Aprili, 2019 riba ya siku moja katika soko la fedha baina ya benki za biashara (*overnight interbank cash market rate*) imeendelea kuwa tulivu katika wastani wa asilimia 3.18 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.67 katika kipindi kama hicho mwaka 2017/2018. Riba za dhamana za Serikali zilifikia wastani wa asilimia 8.07 katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Aprili, 2019 ikilinganishwa na asilimia 7.75 katika kipindi kama hicho mwaka 2017/2018.

Vilevile riba za mikopo inayotolewa na benki za biashara zilishuka kidogo na kufikia wastani wa asilimia 17.15 katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Aprili, 2019 kutoka wastani wa asilimia 17.93 katika kipindi kama hicho mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, ujazi wa fedha na karadha; hadi Aprili, 2019 ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) uliongezeka kwa wastani wa asilimia 4.9 na kufikia shilingi triliuni 25.62 kutoka shilingi triliuni 24.43 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Ukuaji huu ulikuwa sawia na mahitaji ya uchumi kutohana na kuongezeka kwa kasi ya mzunguko wa fedha kufuatia ongezeko la matumizi ya mifumo ya

kielektroniki ya malipo ambayo imechochea kupungua hitaji la kubeba sarafu.

Mheshimiwa Spika, amana katika benki za biashara; hadi Aprili, 2019 amana katika benki za biashara ziliongezeka na kufikia shilingi trilioni 21.32 kutoka shilingi trilioni 20.29 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Hii ilitokana na jitihada za benki za biashara kuhamasisha wananchi kuweka fedha benki kwa kutumia vivutio mbalimbali vyatyaakaunti, kuongeza matawi ya benki pamoja na matumizi ya wakala wa benki.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa mikopo kwa sekta binafsi; hadi Aprili, 2019 mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka kwa wastani wa asilimia 10.6 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 0.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Kuongezeza kwa kasi ya ukua ji wa mikopo kwa sekta binafsi kulichangiwa na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali za kuboresha mazingira ya biashara; usimamizi thabiti wa sera ya fedha; pamoja na kupungua kwa mikopo chechefu kwenye benki za biashara kulikotokana na matumizi ya kanzidata ya taarifa za wakopaji katika kuidhinisha mikopo. Mikopo hii imesaidia kuanzisha na kuimarisha shughuli mbalimbali za kiuchumi zikiwemo biashara, ujenzi na kilimo.

Mheshimiwa Spika, sekta ya nje; katika kipindi cha mwaka ulioishia Aprili, 2019 urari wa jumla wa malipo ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani bilioni 1.08 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 299.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Hali hii ilisababishwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeza kwa nakisi kwenye akaunti ya bidhaa, huduma, kipato cha msingi na cha pili (*primary and secondary income account*) ambapo nakisi iliongezeka kwa dola za Marekani milioni 423.1 na kufikia dola za Marekani milioni 1,132.6 mwezi Aprili, 2019.

Mheshimiwa Spika, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Aprili, 2019 ilifikia dola za Marekani bilioni 7.2 ikilinganishwa na dola

za Kimarekani bilioni 7.29 katika kipindi kama hicho mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Aprili, 2019 thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje ya nchi zilifikia dola za Marekani bilioni 9.024 ikilinganishwa na dola za Marekani bilioni 8.464 katika kipindi kama hicho mwaka 2017/2018 sawa na ongezeko la asilimia 6.6. Ongezeko hili, kwa kiasi kikubwa lilitokana na uagizwaji mkubwa wa vifaa vya ujenzi wa miundombinu ya reli, viwanja vya ndege, bandari na barabara.

Mheshimiwa Spika, akiba ya fedha za kigeni; akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kuridhisha na kuendelea kukidhi mahitaji ya kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi, na pia kuongeza imani kwa wawekezaji katika uchumi. Akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani bilioni 4.39 Aprili, 2019 kiasi ambacho kinatosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha takriban miezi 4.3. Kiwango hiki ni zaidi ya lengo la nchi la kuwa na akiba ya kutosha kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi kwa muda wa miezi 4.0.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa thamani ya shilingi; thamani ya shilingi imeendelea kuwa imara ambapo katika kipindi kinachoishia Aprili, 2019 dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shillingi 2,300.9 ikilinganishwa na shilingi 2,270.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Utulivu katika mwenendo wa thamani ya shilingi umetokana na utekelezaji wa sera ya fedha, usimamizi madhubuti wa mapato na matumizi ya Serikali, matumizi ya gesi asilia badala ya mafuta katika kuzalisha umeme na baadhi ya viwanda kuzalisha bidhaa ambazo awali zilikuwa zikiagizwa kwa wingi kutoka nje ikiwemo vigae na marumaru.

Mheshimiwa Spika, deni la Serikali; hadi Aprili, 2019 deni la Serikali lilifikia shilingi trilioni 51.036 ikilinganishwa na shilingi bilioni 49.866 Aprili 2018 sawa na ongezeko la asilimia 2.4. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani lilifikia shilingi trilioni 13,251.66 na deni la nje lilifikia shilingi trilioni 37.784. Ongezeko

la deni lilitokana na kupokelewa kwa mikopo mipyga kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa reli ya *standard gauge*, madaraja ya juu na miradi ya barabara. Aidha, kwa mujibu wa tathmini ya uhimilivu wa deni ambayo ilifanyika Desemba, 2018 nchi ina uwezo wa kukopa ndani nan je na kulipa mikopo hiyo bila kuwa na athari hasi kwenye ukuaji wa uchumi na maendeleo ya sekta ya fedha.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika kuhakikisha kuwa deni linaendelea kuwa himilivu, Serikali itaendelea kukopa kutoka kwenye vyanzo nafuu na kuhakikisha mikopo inaelezwa kwenye miradi ambayo itachochea kasi ya ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu hali ya uchumi yanapatikana ukurasa wa nne hadi wa 27 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya utekelezaji wa mpango kwa kipindi cha mwaka 2016/17 mpaka mwaka 2018/2019; katika kipindi cha miaka mitatu na nusu ya utawala wa Serikali ya Awamu ya Tano yamepatikana mafanikio mbalimbali katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo yakiwemo kwanza ukuaji wa uchumi. Kuendelea kuimarika kwa uchumi wa Taifa ambapo kwa kipindi hicho ya miaka mitatu na nusu uchumi ulikuwa kwa wastani wa asilimia 6.9 na mfumuko wa bei kuendelea kupungua na kuwa katika wastani wa kiwango cha tarakimu moja chini ya asilimia 5.0.

Pili, upande wa reli, ujenzi wa reli ya katika kwa kiwango cha *standard gauge* unaendelea ambapo kwa awamu ya kwanza ya Dar es Salaam – Morogoro (kilometra 300) utekelezaji umefikia asilimia 48.9 na Morogoro - Makutupora (kilometra 422) utekelezaji umefikia asilimia 7.12. Mafanikio mengine ni kuendelea na uboreshaji na ufufuaji wa reli ambapo ufufuaji wa njia ya reli ya Tanga – Arusha (kilometra 439) umefikia asilimia 80. Vichwa 11 vya treni kwa ajili ya njia kuu vimenunuliwa na mabehewa 15 yamekarabatiwa na

ufungaji wa vipuri kwenye mitambo ya mgodi wa kokoto wa Tura umekamilika.

Kwa upande wa ukarabati wa reli na uimarishaji wa TAZARA, ununuzi wa vipuri vya injini vinavyoju likana kwa jina la *traction motor* na mitambo (*Excavator, Dumper Track na Drill Rig*) ya kusaidia uzalishaji wa kokoto na mataruma ya zege katika mgodi wa Kongolo unaendelea ambapo *Drill Rig* iliwasili mwezi Aprili, 2019.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuboresha Shirika la Ndege Tanzania; katika mafanikio zimenunuliwa ndege sita ambazo zimekwishawasili nchini ambapo moja ni aina ya *Boeing 787 - 8 Dreamliner*, na tatu ni *Bombardier Dash 8 - Q400* na mbili ni *Airbus A220-300*. Pia tumelipa sehemu ya gharama za ununuzi wa ndege moja aina ya *Boeing 787-8 Dreamlinerna* ndege nyingine moja *Bombardier Dash 8 - Q400* zinazotarajiwa kuwasili mwishoni mwa mwaka huu 2019. (Makof)

Kutokana na kuboreshwa kwa ATCL, idadi ya abiria imeongezeka kutoka 49,854 mwaka 2015/2016 hadi 242,668 mwaka huu 2018/2019; kuongezeka kwa idadi ya miruko (*flights*) kutoka 672 hadi 3,808 mwaka 2018/2019; kuongezeka kwa idadi ya vituo vya nje kutoka kimoja ambacho kilikuwa ni Hahaya kule Comoro hadi vituo vitano ambavyo ni Hahaya, Bujumbura, Entebbe, Harare na Lusaka na kuongezeka kwa mapato ya shirika kutoka shilingi bilioni 11.756 hadi shilingi bilioni 45.632. Hivi karibuni ATCL inatarajia kuanza safari za moja kwa moja kwenda Mumbai (India), Guangzhou (China) na Johannesburg (Afrika Kusini). (Makof)

Mheshimiwa Spika, nne ni mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji Mto Rufiji (*Rufiji Hydro Power Project*) ambao ukikamilika utazalisha MW 2,115. Mkandarasi wa mradi wa kufua umeme unaotokana na nguvu ya maji katika Mto Rufiji ambaye ni kampuni ya ubia kati ya *Arab Contractors* na *Elsewedy Electric S.A.E* kutoka Misri amepatikana ambapo mkataba wa ujenzi umesainiwa na mkandarasi alikabidhiwa eneo la mradi mwezi Februari, 2019 na kwa sasa anaendelea

na utekelezaji wa kazi za awali. Kazi zilizokamilika ni pamoja na ujenzi wa miundombinu wezeshi ikijumuisha njia ya kusafirisha umeme wa MW 8 yenye msongo wa KV33 kutoka Msamvu, Morogoro hadi eneo la mradi yenye urefu wa kilometra 170, barabara za kiwango cha changarawe za Ubena – Zomozi na Kibiti – Mloka hadi eneo la mradi, mifumo ya maji, mawasiliano ya simu; na nyumba za kuishi Mkandarasi. Aidha, ujenzi wa mradi huu utakapokamilika kutaifanya nchi yetu ya Tanzania kuwa na umeme wa uhakika na gharama nafuu na hivyo kuchochaea shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, eneo la tano ni Mradi wa Bomba la kusafirisha mafuta ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima (Uganda) hadi Bandari ya Tanga. Kazi zilizofanyika ni kukamilika kwa tathmini ya fidia kwa maeneo ya kipaumbele (*camps and coating yard*) na eneo lote la mkuza. Kazi zinazoendelea ni pamoja na majadiliano ya mkataba kati ya kampuni ya mradi na nchi hodhi.

Mheshimiwa Spika, sita niviwanja vya ndege; kazi zilizokamilika ni pamoja na ujenzi wa jengo jipya la abiria (*Terminal III*) na miundombinu yake yenye uwezo wa kuhudumia abiria milioni sita kwa mwaka katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere; ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Kilimanjaro, Kiwanja cha Dodoma, Kiwanja cha Ndege cha Tabora (awamu ya I na ya II) na Kiwanja cha ndege cha Bukoba. Maboresho na ukarabati huu wa viwanja vya ndege unatarajiwaa kuchochaea ukuaji wa miji na shughuli za kiuchumi kwenye maeneo husika, kuchagiza maendeleo na ukuaji wa sekta ndogo ya usafiri wa anga (*aviation industry*), kusaidia katika juhudzi za kulifufua Shirika la Ndege (ATCL) kwa kufanya ndege za shirika ziweze kufika maeneo mengi (hivyo kuongeza njaza shirika) na kuchochaea ukuaji wa Sekta ya Utalii nchini.

Mheshimiwa Spika, eneo la saba ni bandari; naomba nianze na Bandari ya Dar es Salaam, ujenzi wa Gati Na.1 umekamilika na kuanza kutumika; ujenzi wa Gati la Ro-Ro (gati la magari) upo katika hatua ya ujenzi wa sakafu ngumu

ya gati na ujenzi wa Gati Na. 2 sambamba na kuongeza kina chake umeanza. Vilevile upanuzi wa Bandari za Tanga na Mtwara umefikia asilimia 86 na 50 kwa mtiririko huo. Aidha, kwa upande wa Bandari za Maziwa Makuu, Ziwa Victoria ujenzi wa Gati za Nyamirembe, Chato na Magarine unaendelea ambapo utekelezaji umefikia asilimia 30 na 54 kwa mtiririko huo. Upande wa Ziwa Tanganyika ujenzi wa Gati la Kalya/Sibwesa unaendelea ambapo utekelezaji umefikia asilimia 93. Upande wa Ziwa Nyasa ujenzi wa gati la Ndumbi unaendelea ambapo utekelezaji umefikia asilimia 37.

Mheshimiwa Spika, nane ni upande wa barabara na madaraja; Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanya uwekezaji mkubwa katika kujenga na kukarabati barabara nchini ili kuhakikisha maeneo yote yanaflikika kwa uhakika mwaka mzima. Juhudi hizi zitasaidia sana kuchochea kilimo na shughuli nyingine za uzalishaji mali kwa kurahisisha usafirishaji wa pembejeo na malighafi kwenda maeneo ya uzalishaji pamoja na usafirishaji wa mazao na bidhaa zingine katika maeneo mbalimbali ya masoko nchini. Barabara zilizokamilika ni pamoja na Daraja la *Mfugale Flyover – TAZARA* ambalo lina mita za urefu 1,998; lakini pia Same – Mkumbara (kilometra 96); Tunduru - Nakapanya - Mangaka - Mtambaswala (kilometra 202.5); Namtumbo - Kilimasera - Matemanga – Tunduru (kilometra 193) na Sumbawanga - Kanazi - Kizi – Kibaoni (kilometra 151.6). Vilevile madaraja yaliyokamilika ni pamoja na Daraja la Magufuli katika Mto Kilombero na barabara unganishi, Daraja la Kavuu – Katavi, daraja la waenda kwa miguu la Furahisha – Mwanza. Aidha, ujenzi wa barabara na madaraja unaendelea katika maeneo mbalimbali ikijumuisha *Ubungo Interchange*; barabara ya Kimara – Kibaha (kilometra 19) ambayo itakuwa na njia nane na daraja jipya la Selander ikijumuisha barabara unganishi zitakazokuwa na urefu wa kilometra 5.2.

Mheshimiwa Spika, tisa ni ununuzi na ukarabati wa meli katika maziwa makuu; nikianza na Ziwa Victoria, tunaendelea na ujenzi wa meli mpya yenye uwezo wa

kubeba abiria 1,200 na kubeba tani 400 za mizigo, ujenzi wa chelezo na ukarabati wa meli ya MV Victoria na MV Butiama. Kwa upande wa Ziwa Tanganyika mikataba ya ujenzi wa meli mpya moja yenye uwezo wa kubeba abiria 600 na kubeba tani 400 na ukarabati wa meli ya MV Liemba imekamilika. Kwa upande wa Ziwa Nyasa ujenzi wa meli moja mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na mizigo tani 200 katika Ziwa Nyasa unaendelea ambapo utekelezaji umefikia asilimia 86. Aidha, ujenzi wa matishari mawili katika Ziwa Nyasa nao umekamilika.

Mheshimiwa Spika, kumi upande wa nishati; uzalishaji wa umeme umeongezeka kutoka *GWh* 7092.13 mwaka 2015/2016 hadi *GWh* 7374 mwaka 2018/2019 ambao umewezesha kuongezeka kwa upatikanaji wa umeme wa uhakika, kuongezeka kwa kasi ya kusambaza umeme vijiji ambapo hadi kufikia Mei, 2019 jumla ya vijiji 7,127 vimeunganishiwa umeme ambapo jumla ya taasisi za elimu 3,165 maeneo ya biashara 3,451 *pump* za maji 210 Taasisi za Afya 1,211 na nyumba za ibada 984 zimeunganishiwa umeme. Kufikisha umeme katika vijiji vya wilaya na hal mashauri 15, ujenzi wa njia za kusambaza umeme za Msongo wa *KV*33 zenyne urefu wa kilometra 18,227; ujenzi wa vituo vidogo vya kupoza na kusambaza umeme 4,100 na ujenzi wa njia ndogo ya usambazaji umeme zenyne urefu wa kilometra 30,797.

Mheshimiwa Spika, kumi na moja upande wa Kilimo: Upatikanaji wa mbegu bora uliongezeka na kufikia tani 49,040.66 mwaka 2018/2019 kutoka tani 36,482 mwaka 2015/2016, na tani 492,394 za mbolea zilinunuliwa na kusambazwa katika mwaka 2018/2019 ikillinganishwa na tani 302,450 zilizonunuliwa katika mwaka 2015/2016. Aidha, katika kuimarisha Ushirika na Masoko ya Mazao, Vyama vya Ushirika viliongezeka kutoka 7,888 mwaka 2015 hadi 11,331 mwaka 2018. Vilevile Serikali imeendelea na ujenzi wa vihenge na maghala vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 250,000 na maghala yenye uwezo wa kuhifadhi tani 60,000 unaendelea katika mikoa ya Ruvuma kule Songea, Njombe pale Makambako, Songwe pale Mbozi, Sumbawanga (Rukwa), Mpanda (Katavi), Shinyanga, Manyara na Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kumi na mbili upande wa huduma za afya; kununuliwa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kuititia Bohari ya Dawa na kusambazwa katika vituo vya umma vya kutolea huduma nchini ambapo upatikanaji wa dawa muhimu (*tracer medicine*) katika vituo vya kutolea huduma za afya umefikia asilimia 94.4 na kusambazwa lita 239,020 za viuadudu vya kuangamiza viluwiluvi vya mbu katika maeneo ya mazalia ulifanyika katika Halmashauri zote nchini; (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuongeza utoaji wa chanjo kufikia asilimia 98; kununuliwa mashine za *x-ray* 36, ambapo 28 za kidijitali na 8 za huduma ya kinywa; kuendelea na ujenzi wa hospitali za wilaya 67, Vituo vya kutolea huduma za afya 352 na nyumba za watumishi wa afya 318. Bajeti ya ununuzi wa dawa, chanjo, vifaa, vifaatiba na vitendanishi illongezeka kutoka Shilingi bilioni 31 mwaka 2015/2016 hadi Shilingi bilioni 260 mwaka 2018/2019; na kuanza kutoa huduma ya kupandikiza figo kwa wagonjwa 45. Wagonjwa 38 katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na wagonjwa saba katika Hospitali ya Benjamini Mkapa hapa Dodoma na hivyo kupunguza gharama kwa wastani kutoka shilingi milioni 100 hadi shilingi milioni 20 kwa mgonjwa mmoja endapo angepelekwa nje ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kumi na tatu ni huduma za maji; kukamilika kwa miradi 1,659 ya maji na hivyo kuongeza vituo vya kuchotea maji kufikia 131,370 vyenye uwezo wa kuhudumia wananchi 25,359,290; upatikanaji wa huduma za maji Jijini Dar es Salaam umefikia asilimia 85, katika mikoa mingine asilimia 80, miji midogo asilimia 64 na vijijini asilimia 64.8; mradi wa huduma za maji katika miji mikuu ya mikoa mipyaa unaendelea kutekelezwa ambapo katika Mkao wa Geita umekamilika, Njombe umefikia asilimia 95 na Songwe asilimia 90; kuendelea na ulazaji wa bomba la kusambaza maji kwenye mradi wa maji wa Ziwa Victoria kutoka Kahama Shinyanga katika Miji ya Kagongwa na Isaka ambapo utekelezaji umefikia asilimia 87 na ujenzi wa miundombinu ya maji katika miji ya Tabora, Igunga, Uyui na Nzega pamoja na vijiji 89 vilivyo pembezoni mwa bomba kuu umefikia asilimia 68.5. Kukamilika kwa miradi hii ya maji kutawanufaisha

wananchi katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu ikiwa ni pamoja na kuimarisha shughuli za uzalishaji mali na kuwakinga na maradhi hususan katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, eneo la kumi na nne ni viwanda; Serikali iliendelea kusimamia utekelezaji wa azma yake ya ujenzi wa uchumi wa viwanda ambapo viwanda vipyta zaidi ya 3,530 vilijengwa katika mikoa mbalimbali ikijumuisha viwanda vya kuzalisha bidhaa za ujenzi (saruji, marumaru, nondo) na kilimo, hususan, kusindika matunda, mafuta na ngozi. Ujenzi wa viwanda vipyta umechangia kupatikana kwa ajira mpya takribani 482,601 nchi nzima. Vilevile Serikali imeendelea kuunganisha matrekta katika Kiwanda cha Kuunganisha Matrekta – *TAMCO*, Kibaha ambapo Jumla ya matrekta 822 aina ya *URSUS* yameingizwa nchini kutoka Poland yakiwa katika vipande (*semi knocked down*) ambapo matrekta 571 yameunganishwa na matrekta 399 yameuzwa.

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya yamewezesha jumla ya ekari 85,464 kulimwa kwa kutumia matrekta hayo hadi Aprili, 2019. Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundii Vijijini – *CAMARTEC*; kutengeneza zana zikijumuisha mashine 64 za kupandia mbegu za pamba, kusaga karanga, kukausha mboga mboga na kukata majani pamoja na ujenzi wa mitambo 55 ya *biogas*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *SIDO*; kuendelea na ujenzi wa majengo ya viwanda 11 katika Mikoa ya Dodoma, Geita, Kagera, Katavi, Manyara, Mtwara na Simiyu na ujenzi wa ofisi za *SIDO* katika mikoa mipyta ya Geita na Katavi. Aidha, Serikali inaendelea na uendelezaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi katika maeneo mbalimbali nchini ambapo Kanda Maalum za Kiuchumi za Kigoma na Mtwara uwekezaji umeanza.

Mheshimiwa Spika, kumi na tano ni kuhamishia Makao Makuu ya Serikali hapa katika Jiji la Dodoma; Serikali ya Awamu ya Tano imefanikiwa kuhamisha Makao Makuu ya Serikali kutoka katika Jiji la Dar es Salaam kuja katika Jiji la Dodoma ambapo Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na

watumishi wa umma 8,883 kutoka Wizara na Taasisi wamehamia Dodoma. Aidha, ujenzi wa Ofisi za Serikali katika Mji wa Serikali pale Mtumba umekamilika na kuzinduliwa rasmi ambapo Wizara zote zimehamia na kuanza kutoa huduma katika eneo la Mji wa Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kumi na sita ni upande wa madini; kazi zilizokamilika ni pamoja na ujenzi wa jengo la wafanyakishara wa madini (*brokers house*) na kuendelea na ujenzi wa kituo cha pamoja (*one stop centre*) eneo la Mirerani; uanzishwaji wa masoko ya madini mikoani katika kuhakikisha kuwa wachimbaji wa madini wanapata masoko rasmi na Serikali kupata mapato stahiki; ufungwaji wa mitambo ya uchenjuaji wa madini ya dhahabu kwenye vituo vya mfano vya Lwamgasha na Katente kule Geita na Itumbi-Mbeya kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo kuhusu uchimbaji, uchenjuaji, biashara ya madini, afya, usalama migodini na utunzaji wa mazingira.

Aidha, Serikali ilikamilisha ujenzi wa ukuta wenye mzingo wa kilometra 24.5 kuzunguka Migodi ya *Tanzanite*, Mirerani na uwekaji wa mfumo wa ulinzi wa kidijitali ambao umewezesha kupunguza utoroshwaji wa madini. Juhudi hizi na nyinginezo ziliwezesha kuongezeka kwa makusanyo ya maduhuli yanayotokana na madini kutoka shilingi bilioni 194.4 mwaka 2016/2017 hadi shilingi bilioni 244.3 katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu; Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ambaye pia ni Mwenyekiti wa CCM, ilianzisha na imeendelea kutekeleza utaratibu wa kutoa elimu msingi bila ada kwa kutoa shilingi bilioni 24.4 kila mwezi. Juhudi hizi zimechangia ongezeko la wanafunzi walioandikishwa darasa la kwanza kutoka 1,568,378 mwaka 2015 hadi wanafunzi 1,670,919 mwaka huu 2019 na kidato cha kwanza kutoka wanafunzi 448,826 mwaka 2015 hadi wanafunzi 710,436 mwaka 2019. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na ukarabati na ujenzi wa miundombinu kwa shule za msingi 219 na shule za sekondari 285 katika mikoa yote;

ukarabati wa shule kongwe 17; kukamilisha maboma ya madarasa, mabweni na nyumba za walimu 39; kukamilika na kuzinduliwa kwa maktaba ya kimataifa yenyewe uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,100 kwa wakati mmoja katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kutolewa kwa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu 122,734. Mafanikio haya yamechangia kupunguza gharama za elimu msingi nchini na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa watoto wetu pamoja kuchocheara mwamko wa elimu kwa wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa Mpango yanapatikana katika ukurasa wa 17 mpaka ukurasa wa 37 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka ujao wa fedha 2019/2020; shabaha na malengo ya uchumi jumla kwa mwaka 2019/2020; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka ujao umezingatia shabaha kuu za uchumi jumla kama ifuatavyo:-

(a) Kukua kwa pato halisi la Taifa kufikia asilimia 7.1 mwaka 2019 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.0 mwaka 2018;

(b) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja kati ya asilimia 3.0 hadi asilimia 4.5;

(c) Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.1 ya Pato la Taifa mwaka ujao wa fedha kutoka matarajio ya asilimia 12.1 mwaka huu 2018/2019;

(d) Matumizi ya Serikali yanatarajiwa kuwa asilimia 22.7 ya Pato la Taifa mwaka 2019/2020; na

(e) Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) inatarajiwa kuwa asilimia 2.3 mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, miradi ya kipaumbele kwa mwaka ujao wa fedha 2019/2020, miradi na shughuli za kipaumbele kwa mwaka 2019/2020 ni mwendelezo wa kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 mpaka mwaka 2020/2021. Miradi itakayotekeliza itaelekezwa katika maeneo ya kipaumbele ni kama ifuatavyo:-

(a) Viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda; eneo hili litatilia mkazo ujenzi wa viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana kwa wingi nchini na miradi mahsus katika eneo hili itajumuisha ifuatayo:-

Kwanza ni uendelezaji wa viwanda na hususan kuendeleza kongane za viwanda – *TAMCO* (Kibaha); kongane ya viwanda vya ngozi (Dodoma); maeneo maalum ya uwekezaji ya Bunda, Dodoma na Benjamin William Mkapa na kuendeleza vituo vya utafiti wa teknolojia na bidhaa za viwandani vya *CAMARTEC, TIRDO, TEMDO* na *SIDO*;

Pili, kwa upande wa kilimo ni kuongeza tija katika uzalishaji kwa kuwezesha upatikanaji wa mbegu na pembejeo, huduma za ugani, maghala na masoko kwa mazao ya kimkakati ya kahawa, pamba, chai, mpunga, tumbaku na miwa; Serikali itaendeleza juhudhi katika ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya skimu za umwagiliaji; na kuimarisha utafiti wa mbegu bora na magonjwa ya mazao;

Eneo la tatu ni mifugo na itakuwa ni kuimarisha mashamba ya kuzalisha mitamba na vituo vya uhamilishaji mifugo na kuhamasisha matumizi ya teknolojia sahihi ili kuongeza kasi ya uzalishaji wa mitamba na madume kwa ajili ya maziwa na nyama, kudhibiti na kukabiliana na magonjwa mlipuko kwa mifugo ili kuongeza uzalishaji na kukidhi ubora wa malighafi zitokanazo na mifugo kwa viwanda vinavyoendelea kujengwa nchini, kupima na kutenga maeneo ya malisho kwa ajili ya mifugo ili kupunguza migogoro ya ardhi kati ya wakulima, wafugaji...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa mara nyingine tena naombeni tena usikivu wenu, tafadhalini, hotuba hii inasikilizwa na Taifa zima. Mheshimiwa Waziri endelea.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uvuvi; katika mwaka ujao tutajielekeza kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa bandari ya uvuvi na ununuzi wa meli kubwa za uvuvi; kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania - *TAFICO* ili kuimarisha uwekezaji katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari na Bahari Kuu; kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika Ukanda wa Ziwa Victoria, Tanganyika na Ukanda wa Pwani ili kuongeza udhibiti na kukomesha biashara haramu ya mazao ya uvuvi;

Mheshimiwa Spika, na tano ni upande wa madini; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; uendelezaji wa masoko ya madini; kukamilisha ujenzi wa mtambo wa kuyeyusha madini (*smelter*) na vituo vya umahiri; kuwezesha shughuli za utafiti wa madini ili kuongeza taarifa za kijiolojia na kuvutia uwekezaji; kuelimisha umma kuhusu matumizi ya takwimu za rasilimali za madini, mafuta na gesi na; usimamizi wa masuala ya mazingira, afya na usalama migodini.

(b) Kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu; miradi ya kipaumbele itakayotekelozwa katika mwaka 2019/2020 itajielekeza katika eneo hili mwaka ujao wa fedha ni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni upande wa elimu; kuendelea kusomesha kwa wingi wataalam kwenye ujuzi na fani adimu kama vile udaktari, mafuta na gesi; kuendelea kugharamia utoaji wa elimu msingi bila ada; ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kujifunzia na kufundishia katika shule na vyuo vya ualimu; kuimarisha vyuo vya ufundi stadi kwa kukarabati, kujenga na kuweka vifaa vya kufundishia na kujifunzia; kuboresha na kununua vifaa vya kujifunzia na kufundishia katika shule 500 za sekondari ili kuziwezesha kuwa vituo vya mafunzo kazini kwa walimu wa masomo ya sayansi, hisabati na lugha; kujenga ofisi 55 za wathibiti ubora wa shule;

kuongeza utoaji wa mikopo ya elimu ya juu na kusimamia marejesho yake na kuendeleza shughuli za utafiti kwa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa shughuli hizi utaboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia na hivyo kuongeza ufaulu wa watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili katika kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu ni afya, na hapa tutajielekeza kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za tiba katika Hospitali za Rufaa za mikoa, kanda na Taifa; kuimarisha usambazaji wa dawa, chanjo, vifaa, vifaatiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya; kuimarisha hali ya lishe na usafi wa mazingira; kuimarisha huduma katika taasisi ya Saratani *Ocean Road*, Taasisi ya Tiba ya Moyo ya Jakaya Kikwete na Taasisi ya Mifupa Muhimbili (*MOI*); kuendeleza ujenzi wa Hospitali za Wilaya na vituo vya afya; ujenzi na ukarabati wa vyuo vya Maendeleo ya Jamii; kuimarisha huduma za ustawi wa jamii kwa wazee na watoto walio katika mazingira hatarishi na kukuza usawa wa jinsia na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa shughuli hizi utaboresha upatikanaji wa huduma za afya katika ngazi mbalimbali nchini na hivyo kuimarisha afya za wananchi.

Mheshimiwa Spika, eneo la nne ni maji, na hapa tutajielekeza kuimarisha upatikanaji wa maji mijini na vijiji; kuendelea na ujenzi wa miradi ya maji ikiwemo Makonde kule Mtwara, Wanging'ombe (Njombe), Chalinze (Pwani), Mugango/Kiabakari kule Butiama (Mara); maji kutoka Ziwa Victoria hadi miji ya Tabora, Nzega, Igunga, Sikonge na vijiji 89 vilivyo pembezoni mwa bomba kuu na kuanza ujenzi kupeleka maji katika miji ya Busega, Bariadi, Lagangabilili na Mwanhuzi na kuendeleza rasilimali za maji nchini na maabara za maji. (*Makof*)

(c) Uboreshaji wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji:

Mheshimiwa Spika, miradi itakayotekelawa katika eneo hili ni ile yenye lengo la kuendeleza ujenzi na ukarabati wa miundombinu kwa ajili ya kurahisisha ufanyaji biashara na kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi. Miradi katika eneo hili itajumuisha kuendelea na ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha *Standard Gauge*; mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji wa Mto Rufiji – MW 2,115; na Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ni pamoja na kuboresha miundombinu ya reli za *TAZARA*, Tanga – Arusha, usafiri wa reli Dar es Salaam pamoja na kuboresha *engine* na mabehewa ya treni; kuendelea na ujenzi wa barabara zikijumuisha barabara za Mtwara – Masasi – Songea – Mbamba Bay (kilometra 1,470.9); barabara ya Kidahwe - Kasulu – Kibondo - Nyakanazi (kilometra 413), Usagara - Geita - Buzirayombo – Kyamyorwa (kilometra 230); madaraja ya Sibiti (Singida), *New Wami* (Pwani); Daraja la Kigongo/Busisi kule Mwanza, Simiyu (Mwanza), Selander (Dar es Salaam); ujenzi na ukarabati wa vivuko; usambazaji wa umeme vijijini kupitia mradi wa *REA*; miradi mikubwa ya njia za kusambaza umeme wa msongo mkubwa ikijumuisha njia ya umeme wa msongo wa KV 400 ya Rufiji – Chalinze – Dodoma kilometra 512, uboreshaji wa Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara na miundombinu ya viwanja vya Ndege na kuendelea na utekelezaji wa Mpango wakuboresha mfumo wa udhibiti wa biashara na uwekezaji ikijumuisha kuhuisha mfumo, viwango na idadi ya kodi, ushuru na tozo na mifumo ya Kitaasisi, Kisera na Kisheria ili kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, na eneo la nne nikumarisha usimamizi wa utekelezaji wa mpango; katika eneo hili miradi itakayotekelawa inalenga kuimarisha mifumo na taasisi za utekelezaji wa mpango, kuweka mfumo utakaowezesha upatikanaji wa uhakika wa rasilimali fedha na kuweka vigezo vya upimaji wa mafanikio ya utekelezaji. Miradi hii itajumisha ile ya utawala bora hususani utoaji wa haki...

SPIKA: Mbunge wa Moshi Mjini umesimama kwa muda wa saa nzima sasa rudi kwenye kiti chako, rudi kwenye kiti

chako tafadhali. Mpisheni aende akakae. Tuwe na utulivu jamani saa nzima mtu umesimama *what is it?* Endelea Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: ...kuimarisha Mifuko ya Mahakama na Bunge, kuimarisha vyombo nya ulinzi na usalama kwa kuvipatia vitendea kazi na mafunzo pamoja na kuimarisha usajili wa vizazi na vifo.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu miradi ya kipaumbele yapo katika Sura ya Nne ya Kitabu cha Mpango.

Mheshimiwa Spika, ugharamiaji wa mpango wa mwaka 2019/2020; Serikali imetenga shilingi trilioni 12.248 kwa ajili ya kugharamaia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka kesho 2019/2020 ambapo shilingi trilioni 9.737 ni fedha za ndani na shilingi trillioni 2.510 ni fedha za nje. Fedha hii ya maendeleo ni sawa na asilimia 37 ya bajeti yote ya mwaka 2019/2020 kiwango kinachoshabihiana na lengo la Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano la kutenga kati ya asilimia 30 na 40 ya bajeti yote kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Serikali inatarajia kugharamia mpango kutokana na vyanzo mbalimbali vikijumuisha mapato ya kodi, mikopo na misaada ya washirika wa maendeleo, ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje na mifuko ya kimataifa ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu ugharamiaji na vihatarishi nya utekelezaji wa mpango yanapatikana katika ukurasa wa 45 hadi 47 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji; katika kuhakikisha kuwa ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa mpango wa mwaka ujao unazingatia Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano Serikali ya Awamu ya Tano imejipanga kuzingatia viashiria nya utekelezaji vilivyobainishwa katika maeneo ya kipaumbele ya mpango.

Aidha, ufuatiliaji na tathmini utazingatia taarifa ya tathmini ya muda wa kati wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano hususani hatua halisi ya utekelezaji, changamoto na mapendekezo ya hatua za kukabiliana na changamoto zilizojitokeza.

Mheshimiwa Spika, katika kila robo ya mwaka 2019/2020 Wizara ya Fedha na Mipango itafuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi ya kielelezo, kimkakati na inayotekelawa na sekta binafsi ili kujuu mafanikio na upungufu utakaojitokeza wa utekelezaji wa miradi katika maeneo ya kipaumbele ya mpango. Ofisi ya Rais, TAMISEMI itaratibu ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo inayotekelawa katika ngazi za Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti, Sura ya 439. Taarifa za utekelezaji zitasaidia Serikali katika kufanya maamuzi na kuhamasisha jamii kujituma zaidi katika kufikia malengo ya mpango.

Mheshimiwa Spika, majumuisho; azma ya Serikali ni kujenga uchumi wa kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Pamoja na jitihada nyingine katika kufanikisha lengo hili Serikali itaendelea kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu wezeshi ya undelezaji wa viwanda na kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vitakavyotumia malighafi zinazopatikana nchini hususani mazao ya kilimo, madini na gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika kufanikisha ujenzi wa uchumi wa kipato cha kati, Serikali itaendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato na kukusanya mapato kutoka vyanzo bunifu vilivyoainishwa katika Mkakati wa Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, kuhakikisha mipango na bajeti inawekewa viashiria, vigezo na shabaha bayana ambavyo usimamizi wa utekelezaji utazingatia, kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi hususan katika sekta ya viwanda na kutekeleza maoni na ushauri unaotolewa na Bunge juu ya utekelezaji wa mipango na bajeti.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; tunapokaribia kuhitimisha kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano wenyewe dhima ya kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya uchumi na maendeleo ya watu, niwaombe viongozi wa Serikali, Waheshimiwa Wabunge na wananchi tushirikianewote kwa pamoja katika kuleta ufanisi wa utekelezaji wa Mpango.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali ninaomba niwashukuru wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi wakiwemo washirika wa maendeleo, sekta binafsi na wananchi kwa ujumla kwa michango yao katika kuleta mafanikio katika ukuaji wa uchumi na utekelezaji wa mpango. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba nitoe shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijiji (Mbunge) - Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Wizara zote, Wakuu walidara zinazojitegemea na taasisi kwa ushirikiano wao katika kutayarisha Taarifa ya Hali ya Uchumi ya mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2019/2020. Aidha, ninawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu Bwana Doto Mgosha James kwa kusimamia vizuri kazi za kila siku za Wizara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kipekee niwashukuru Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa kunisikiliza. Aidha, hotuba hii na vitabu vya taarifa za uchumi vya mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2019/2020 vinapatikana katika tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango www.mof.go.tz.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa Waheshimiwa Wabunge wapokee, wajadili na kupitisha Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2019/2020. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO, MHESHIMIWA
DKT. PHILIP I. MPANGO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI
TAARIFA YA HALI YA UCHUMI WA TAIFA KWA MWAKA 2018
NA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA
2019/20 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2019/20. Pamoja na hotuba hii nawasilisha vitabu vyta ya Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2019/20, ambapo taarifa hizi ndio msingi wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2019/20 itakayowasilishwa Bungeni leo jioni.
2. **Mheshimiwa Spika**, kwanza nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutujalia uzima na afya. Kipekee nimshukuru sana kwa jinsi anavyoendelea kulijalia Taifa letu amani na utulivu na kutuwezesha kukutana katika m Kutano huu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kujadili namna ya kuharakisha maendeleo ya Taifa letu.
3. **Mheshimiwa Spika**, Taifa letu limebarikiwa kuwa na kiongozi shupavu, mchapakazi, mwenye maono, na uthubutu wa kimaendeleo. Naomba uniruhusu nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyoendelea kuliongoza vema Taifa letu. Kwa kipindi hiki cha Miaka mitatu na nusu ya utawala wake tumeshuhudia kuimariika kwa uchumi ambapo ukua jifunzo asilimia 7.0, mfumuko wa bei umedhibitiwa na kuwa katika tarakimu moja, miradi mikubwa ya maendeleo inatekelezwa, uwajibikaji katika utumishi wa umma unaimariika na kero za wanyonge zinatatuliwa. Mimi na wenzangu Serikalini tunaahidi kuendelea kumpatia Mheshimiwa Rais ushirikiano wa hali ya juu. Aidha, ninamshukuru kwa kuendelea kuniamini kuongoza Wizara ya Fedha na Mipango.

4. **Mheshimiwa Spika**, kipekee naomba niwapongeze Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia ni Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, kwa uongozi wao mahiri katika kumsaidia Mheshimiwa Rais. Aidha, naomba kumpongeza Mhe. Innocent Lugha Bashungwa (Mb), kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara.

5. **Mheshimiwa Spika**, hoja ninayoiwasilisha hapa imetayarishwa kwa kuzingatia dhana ya ushirikishwaji mpana wa jamii ambapo tumepata maoni na ushauri kutoka katika makundi mbalimbali ya jamii na Taasisi za Serikali. Siwezi kuwataja mmoja mmoja wale wote waliota maoni na ushauri hadi kufikia hapa, lakini ni vema nitambue mchango mkubwa wa Bunge hilli kupitia kwako Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile, nichukue fursa hii adhimu kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti Mheshimiwa George Boniface Simbachawene (Mb) na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki (Mb) pamoja na wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti kwa ushauri makini waliotupatia wakati wa uandaaji wa kitabu cha Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2019/20. Ushauri wao umetumika kikamilifu katika uandaaji wa hotuba na vitabu ninavyowasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu.

6. **Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2019/20 vimeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 ili kuleta mchango wa haraka katika maendeleo ya uchumi wa Taifa; umuhimu wa kumalizia miradi inayoendelea ili kupata matokeo tarajiwa; kuweka msukumo mkubwa katika kuboresha mazingira ya kufanya biashara na kuwekeza hapa nchini ili kuongeza ushiriki wa Sekta Binafsi katika kukuza uchumi na kujenga uchumi wa viwanda na maendeleo ya watu.

MWENENDO WA HALI YA UCHUMI 2018

Uchumi wa Dunia

7. **Mheshimiwa Spika**, mwaka 2018, uchumi wa dunia ulikua kwa asilimia 3.6 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.8 mwaka 2017. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi kulitokana na kushuka kwa ukuaji wa uchumi kwa nchi zilizoendelea na zinazoendelea kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo: kupungua kwa mahitaji ya bidhaa na huduma kutoka nje; hali ya wasiwasi kuhusu madhara ya Uingereza kujitoa Jumuiya ya Ulaya (Brexit); kushuka kwa kasi ya uwekezaji; mvutano wa kibashara baina ya China na Marekani; kudorora kwa soko la fedha katika nchi za Argentina na Uturuki, na mvutano wa kisiasa Mashariki ya Kati.

8. **Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2018, mfumuko wa bei wa dunia uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 3.8 kutoka wastani wa asilimia 3.1 mwaka 2017. Ongezeko hilo lilitokana na kupungua kwa uzalishaji viwandani hususan, katika nchi zinazoendelea, majanga ya asili, na kulegezwa kwa sera za bajeti na fedha kwa baadhi ya nchi. Mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea uliongezeka na kuwa asilimia 2.0 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 1.7 mwaka 2017. Katika kipindi hicho, mfumuko wa bei kwa nchi zinazoendelea za Asia uliongezeka hadi asilimia 2.6 ikilinganishwa na asilimia 2.4 mwaka 2017.

Uchumi wa Afrika na Kikanda

9. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, wastani wa kasi ya ukuaji wa uchumi iliongezeka hadi asilimia 3.0 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 2.9 mwaka 2017. Ukuaji huu ultokana na ongezeko la mahitaji ya bidhaa pamoja na marekebisho ya sera za kiuchumi. Mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 8.5 kutoka wastani wa asilimia 11.0 mwaka 2017. Mwenendo huo wa mfumuko wa bei ultokana na kuimarika kwa sera za fedha ikiwemo viwango imara vya kubadilisha fedha na kuimarika kwa sera za matumizi.

10. **Mheshimiwa Spika**, mwenendo wa uchumi wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki unaonesha kuwa uchumi wa Rwanda ulikua kwa asilimia 8.6 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 6.1 mwaka 2017. Uchumi wa Uganda ulikua kwa asilimia 6.1 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 5.9 mwaka 2017. Uchumi wa Kenya ulikua kwa asilimia 6.3 ikilinganishwa na asilimia 4.9 mwaka 2017.

11. **Mheshimiwa Spika**, hadi Desemba 2018, mwenendo wa mfumuko wa bei katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki uliendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja ambapo ulipungua hadi wastani wa asilimia 2.9 kutoka wastani wa asilimia 7.9 mwaka 2017. Katika kipindi hicho, wastani wa mfumuko wa bei kwa Tanzania ulikuwa asilimia 3.5, Kenya asilimia 4.6, Rwanda asilimia 1.4, Uganda asilimia 2.6, na Burundi asilimia 2.3. Mwenendo huu ultokana na kuimarika kwa upatikanaji wa chakula ndani ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Uchumi wa Taifa

Pato la Taifa

12. **Mheshimiwa Spika**, mwaka 2018, Serikali kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilifanya maboresho ya takwimu za Pato la Taifa kwa kutumia mwaka 2015 kama mwaka wa kizio kutoka mwaka wa kizio wa 2007. Kufuatia maboresho hayo, mabadiliko kadhaa yalijitokeza ikiwa ni pamoja na mfumo na ukubwa wa Pato la Taifa; viwango vya ukuaji wa Pato la Taifa kisekta; mchango wa sekta mbalimbali katika Pato la Taifa; na uwiano wa viashiria mbalimbali kwa Pato la Taifa.

13. **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa takwimu mpya za mwaka wa kizio wa 2015, Pato halisi la Taifa lilikua kwa kiwango cha asilimia 7.0 mwaka 2018 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.8 mwaka 2017. Ukuaji huu ulichochewa zaidi na kuongezeka kwa uwekezaji hususan katika miundombini kama vile ujenzi wa barabara, reli, na viwanja vya ndege; kutengemaa kwa upatikanaji wa nishati ya umeme; kuimarika kwa huduma za usafirishaji; na hali nzuri ya hewa iliyopelekea

uzalishaji mzuri wa chakula na mazao mengine ya kilimo. Shughuli za kiuchumi zilizokua kwa kasi kubwa ni pamoja na: sanaa na burudani (asilimia 13.7); ujenzi (asilimia 12.9); uchukuzi na uhifadhi mizigo (asilimia 11.8); Shughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundı (asilimia 9.9); na habari na mawasiliano (asilimia 9.1). Sekta ya kilimo ilikua kwa asilimia 5.3. Sekta zilizotoa mchango mkubwa katika Pato la Taifa ni kilimo (asilimia 28.2), ujenzi (asilimia 13.0) na biashara na matengenezo (asilimia 9.1).

14. Mheshimiwa Spika, Pato la Taifa kwa bei za mwaka husika lilikuwa Shilingi trillioni 129.4 mwaka 2018 ikilinganishwa na Shilingi trillioni 118.7 mwaka 2017. Aidha, mwaka 2018, Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa na watu 52,619,314 ambapo Pato la wastani la kila mtu lilitifika shilingi 2,458,496 kutoka shilingi 2,327,395 mwaka 2017 sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 5.6. Kiasi hicho cha Pato la wastani kwa kila mtu kwa mwaka 2018 ni sawa na dola za Marekani 1,090 ikilinganishwa na dola za Marekani 1,044 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 4.4.

Mwenendo wa Bei

15. Mheshimiwa Spika, mwaka 2018, mfumuko wa bei uliendelea kubakia katika wigo wa tarakimu moja na kufikia kiwango cha chini kabisa kuwahi kutokea katika kipindi cha miaka 40 iliyopita. Mfumuko wa bei ulipungua kutoka wastani wa asilimia 5.3 mwaka 2017 hadi wastani wa asilimia 3.5 mwaka 2018. Hadi mwezi Aprili 2019, mfumuko wa bei ulifikia asilimia 3.2 ikilinganishwa na asilimia 3.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Kiwango hicho cha chini cha mfumuko wa bei kilitokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

(i) Kuimarika kwa hali ya upatikanaji wa chakula katika masoko ya ndani na nchi jirani. Uzalishaji wa chakula nchini uliofikia tani milioni 15.9 ikilinganishwa na mahitaji ya tani milioni 13.3 kwa kipindi hicho, hivyo kuwa na utoshelevu wa chakula kwa asilimia 124; na

(ii) Utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti.

Utekelezaji wa Sera za Fedha 2018/19

16. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupyitia Benki Kuu ya Tanzania iliendelea kutekeleza sera ya fedha kwa lengo la kuhakikisha kuna utoshelevu wa ukwasi kwenye uchumi kuendana na malengo mapana ya uchumi ya kuwa na utulivu kiuchumi na ukuaji endelevu na jumuishi.

17. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19 malengo ya sera ya fedha yalikuwa ni:

- (i) Ukuaji wa wastani wa fedha taslim usiozidi asilimia 11.5;
- (ii) Ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) usiozidi asilimia 12.2;
- (iii) Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi usiozidi asilimia 10.2; na
- (iv) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

18. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi kinachoishia Aprili 2019, Serikali ilichukua hatua mbalimbali za kuongeza ukwasi kwenye uchumi ili kuziwezesha benki na taasisi za fedha kuongeza utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi kwa ajili ya kuendeleza shughuli mbalimbali za kiuchumi. Hatua hizo ni pamoja na: kutoa mikopo ya muda mfupi kwa benki; kununua fedha za kigeni kutoka katika benki za biashara na taasisi za Serikali; kushusha kiwango cha riba ya mikopo kwa benki kulikofanyika mwezi Agosti 2018 kutoka asilimia 9.0 hadi asilimia 7.0; na kulipa malimbikizo ya madai mbalimbali ya wakandarasi, watoa huduma na watumishi ambapo takribani Shilingi bilioni 598.4 za madai yaliyohakikiwa zililipwa kati ya Julai 2018 na Mei 2019.

19. **Mheshimiwa Spika**, hatua hizi zilisaidia kuongeza ukwasi kwenye benki na taasisi za fedha pamoja na kushusha riba katika masoko ya fedha ambapo katika kipindi cha Julai

2018 hadi Aprili 2019, riba ya siku moja katika soko la fedha baina ya benki za biashara (*overnight interbank cash market rate*) imeendelea kuwa tulivu katika wastani wa asilimia 3.18 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.67 katika kipindi kama hicho mwaka 2017/18. Riba za dhamana za Serikali zilifikia wastani wa asilimia 8.07 katika kipindi cha Julai 2018 hadi Aprili 2019 ikilinganishwa asilimia 7.75 katika kipindi kama hicho mwaka 2017/18. Vile vile, riba za mikopo inayotolewa na benki za biashara zilishuka kidogo na kufikia wastani wa asilimia 17.15 katika kipindi cha Julai 2018 hadi Aprili 2019 kutoka wastani wa asilimia 17.93 katika kipindi kama hicho mwaka 2017/18.

20. Mheshimiwa Spika, wastani wa riba za mikopo umeendelea kupungua kwa kasi ndogo kutokana na benki za biashara kuendelea kuweka tahadhari kubwa kwa wateja wanaoshindwa kurejesha mikopo kwa wakati. Aidha, Benki Kuu ya Tanzania inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kuwa riba za mikopo zinakuwa nafuu ili kuendana na hali halisi ya uchumi. Hatua hizo ni pamoja na kuhakikisha kuwa sekta ya benki na taasisi za fedha zinapata taarifa sahihi za wakopaji kwa kutumia kanzidata ili kupunguza athari za mikopo chechefu pamoja na kuendelea na marekebisho ya sheria katika usimamizi wa sekta ya fedha nchini.

Ujazi wa Fedha na Karadha

21. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2019 ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) uliongezeka kwa wastani wa asilimia 4.9 na kufikia shilingi bilioni 25,629.1 kutoka shilingi bilioni 24,433.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Ukuaji huu ulikuwa sawia na mahitaji ya uchumi kutokana na kuongezeka kwa kasi ya mzunguko wa fedha kufuatia ongezeko la matumizi ya mifumo ya kielektroniki ya malipo ambayo imechochea kupungua hitaji la kubeba sarafu.

Amana katika Benki za Biashara

22. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2019, amana katika benki za biashara ziliongezeka na kufikia shilingi bilioni 21,322.7

kutoka shilingi bilioni 20,298.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Hii ilitokana na jitihada za benki za biashara kuhamasisha wananchi kuweka fedha benki kwa kutumia vivutio mbalimbali vya akaunti, kuongeza matawi ya benki pamoja na matumizi ya wakala wa benki.

Mwenendo wa Mikopo kwa Sekta Binafsi

23. **Mheshimiwa Spika**, hadi Aprili 2019 mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka kwa wastani wa asilimia 10.6 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 0.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kulichangiwa na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali za kuboresha mazingira ya biashara; usimamizi thabiti wa sera ya fedha; pamoja na kupungua kwa mikopo chechelu kwenye benki za biashara kulikotokana na matumizi ya kanzidata ya taarifa za wakopaji katika kuidhinisha mikopo. Mikopo hii imesaidia kuanzisha na kuimarisha shughuli mbalimbali za kiuchumi zikiwemo biashara, ujenzi na kilimo.

24. **Mheshimiwa Spika**, sehemu kubwa ya mikopo kwa sekta binafsi imeendelea kuelekezwa katika shughuli binafsi/ kaya ambazo zilipata wastani wa asilimia 28.8 ya mikopo yote ikifuaatiwa na shughuli za biashara zilizokuwa na wastani wa asilimia 18.5 na shughuli za uzalishaji viwandani asilimia 11.3. Aidha, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha benki za biashara zina ukwasi wa kutosha na kuongeza kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Hatua hizo ni pamoja na kuboresha masoko ya fedha na utendaji wa benki, kuboresha mazingira ya kufanya biashara na upatikanaji wa taarifa za wakopaji ili kuongeza uwazi na ufanisi katika utoaji wa mikopo.

Ukuzaji Rasilimali

25. **Mhemishiwa Spika**, ukuzaji rasilimali kwa bei za miaka husika ulifikia shilingi bilioni 50,383.14 mwaka 2018 ikiwa ni ongezeko la asilimia 24.6 ikilinganishwa na shilingi bilioni 40,427.43 mwaka 2017. Uwiano wa ukuzaji rasilimali kwa Pato

la Taifa kwa bei za miaka husika uliongezeka kufikia asilimia 39.0 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 34.0 mwaka 2017. Ukuzaji rasilimali za kudumu kwa bei za miaka husika uliongezeka kwa asilimia 19.4 kutoka Shilingi bilioni 42,141.92 mwaka 2017 hadi shilingi bilioni 50,316.24 mwaka 2018. Aidha, thamani ya limbikizo la rasilimali kwa bei za miaka husika iliongezeka kwa Shilingi bilioni 66.9 mwaka 2018 ikilinganishwa na punguzo la Shilingi bilioni 1,714.49 mwaka 2017. Ukuzaji rasilimali katika sekta ya umma ulifikia Shilingi bilioni 15,265.61 mwaka 2018 kwa bei za miaka husika, sawa na ongezeko la asilimia 17.2 wakati ukuzaji rasilimali katika sekta binafsi uliongezeka kwa asilimia 20.4 kufikia Shilingi bilioni 35,050.63.

Sekta ya Nje

26. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka ulioishia Aprili 2019, urari wa jumla wa malipo ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,089.2 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 299.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Hali hii ilisababishwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeka kwa nakisi kwenye akaunti ya bidhaa, huduma, kipato cha msingi na cha pili (*primary and secondary income account*) ambapo nakisi iliongezeka kwa dola za Marekani milioni 423.1 na kufikia dola za Marekani milioni 2,132.6 mwezi Aprili 2019.

27. Mheshimiwa Spika, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi katika kipindi cha Julai 2018 hadi Aprili 2019 ilifikia dola za Marekani milioni 7,210.6 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 7,291.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2017/18.

28. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2018 hadi Aprili 2019, thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje ya nchi zilifika dola za Marekani milioni 9,024.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 8,464.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2017/18, sawa na ongezeko la asilimia 6.6. Ongezeko hili, kwa kiasi kubwa, lilitokana na uagizwaji mkubwa wa vifaa vya ujenzi wa miundombinu ya reli, viwanja vya ndege, bandari na barabara. Thamani ya mafuta yaliyoagizwa kutoka nje nayo iliongezeka hususan kutokana

na kupanda kwa bei katika soko la dunia kutoka wastani wa dola za Marekani 52.81 kwa pipa mwaka 2017 hadi wastani wa dola za Marekani 68.33 kwa pipa mwaka 2018. Aidha, uagizaji wa bidhaa za chakula ulipungua kwa kiasi kikubwa kutokana na kuongezeka kwa mavuno kipindi cha msimu wa mwaka 2018/19. Kwa upande wa huduma, thamani ya malipo kwenda nje ya nchi ilipungua na kufikia dola za Marekani milioni 1,709.3 mwezi Aprili 2019 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,848.5 Aprili 2018.

Akiba ya Fedha za Kigeni

29. **Mheshimiwa Spika**, akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kuridhisha na kuendelea kukidhi mahitaji ya kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi, na pia kuongeza imani kwa wawekezaji katika uchumi. Akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 4,395.2 Aprili 2019, kiasi ambacho kinatosha uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha takriban miezi 4.3. Kiwango hiki ni zaidi ya lengo la nchi la kuwa na akiba ya kutosha kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi kwa muda wa miezi 4.0.

Mwenendo wa Thamani ya Shilingi

30. **Mheshimiwa Spika**, thamani ya Shilingi imeendelea kuwa imara ambapo katika kipindi kinachoishia Aprili 2019, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa Shilingi 2,300.9 ikilinganishwa na shilingi 2,270.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Utulivu katika mwenendo wa thamani ya Shilingi umetokana na utekelezaji wa sera ya fedha, usimamizi madhubuti wa mapato na matumizi ya Serikali, matumizi ya gesi asilia badala ya mafuta katika kuzalisha umeme, na baadhi ya viwanda kuzalisha bidhaa ambazo awali zilikuwa zikiagizwa kwa wingi kutoka nje ikiwemo vigae na marumaru.

31. **Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa sheria ya usimamizi wa Fedha za Kigeni, mwezi Novemba 2018 Benki Kuu ya Tanzania ilifanya ukaguzi wa ghafla katika maduka ya kubadilisha fedha jijini Arusha na kuyafunga maduka

yasiyozingatia taratibu na sheria za biashara hiyo. Vile vile, mwezi Februari 2019 Benki Kuu ilifanya ukaguzi wa kawaida wa maduka ya kubadilisha fedha za kigeni jijini Dar es Salaam na kubaini kwamba maduka mengi yanaendesha biashara hiyo pasipo kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za utoaji wa huduma ya kubadilisha fedha za kigeni. Kufuatia ukaguzi huo, Benki Kuu ilianza utaratibu wa kufuta leseni za maduka yote yaliyokutwa yanaendesha biashara hiyo bila kuzingatia masharti ya leseni ambapo zoezi hili linaendelea. Hata hivyo, huduma ya ubadilishaji wa fedha za kigeni imeendelea kupatikana kwa ufanisi na baadhi ya benki za biashara zimeingia katika biashara hii na zinatoa huduma vizuri.

Deni la Serikali

32. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2019, deni la Serikali lilifika Shillingi billioni 51,036.42 ikillinganishwa na Shillingi billioni 49,866.17 Aprili 2018, sawa na ongezeko la asilimia 2.4. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani lilifika shilingi billioni 13,251.66 na deni la nje Shilingi billioni 37,784.76. Ongezeko la deni lilitokana na kupokelewa kwa mikopo mipyta kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa reli ya *standard gauge*, madaraja ya juu na miradi ya barabara. Aidha, kwa mujibu wa tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanywa Desemba 2018, nchi ina uwezo wa kukopa ndani na nje, na kulipa mikopo hiyo bila kuwa na athari hasi kwenye ukuaji wa uchumi na maendeleo ya sekta ya fedha. Aidha, katika kuhakikisha kuwa deni linaendelea kuwa himilivu, Serikali itaendelea kukopa kutoka kwenye vyanzo nafuu na kuhakikisha mikopo inaelekezwa kwenye miradi ambayo itachochea kasi ya ukuaji wa uchumi.

MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO KWA KIPINDI CHA 2016/17 – 2018/19

33. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitatu na nusu ya utawala wa Serikali ya Awamu ya Tano (2016/17 – 2018/19), yamepatikana mafanikio mbalimbali katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo yakiwemo:

(i) **Ukuaji wa Uchumi:** kuendelea kuimarika kwa uchumi wa Taifa, ambapo kwa kipindi hicho cha miaka mitatu na nusu uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 6.9 na mfumuko wa bei kuendelea kupungua na kuwa katika wastani wa kiwango cha tarakimu moja, chini ya asilimia 5.0.

(ii) **Reli:** ujenzi wa reli ya katika kiwango cha *standard gauge* unaendelea, ambapo kwa awamu ya kwanza ya Dar es Salaam – Morogoro (km 300) utekelezaji umefikia asilimia 48.9 na Morogoro - Makutupora (km 422) asilimia 7.12. Vile vile, taratibu za ujenzi kwa sehemu za Makutupora - Tabora (km 294), Tabora - Isaka (km 133), Isaka - Mwanza (km 249), Isaka – Rusumo (km 371), Tabora - Kigoma (km 411), Keza - Ruvubu (km 36) na Kaliua – Mpanda - Karema (km 321) unaendelea. Mafanikio mengine ni kuendelea na ukarabati wa reli iliyopo katika sehemu ya Dar es Salaam hadi Isaka ambapo shughuli zillizofanyika ni pamoja na kuboresha eneo la kupakia/kupakua mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam na kukarabati vituo vya kuhudumia mizigo vya llala na Isaka, utekelezaji umefikia asilimia 13 na unatarajiwa kukamilika Juni 2020. Aidha, Serikali inaendelea na uboreshaji na ufufuaji wa reli ambapo Ufufuaji wa Njia ya Reli ya Tanga – Arusha (km 439) umefikia asilimia 80; vichwa 11 vya treni kwa ajili ya njia kuu vimenunuliwa na mabehewa 15 yamekarabatiwa; na ufungaji wa vipuri kwenye mitambo ya mgodi wa kokoto wa Tura umekamilika. Kwa upande wa Ukarabati wa Reli na Uimarishaji wa TAZARA, ununuzi wa vipuri vya injini vinavyojulikana kwa jina la Traction Motor, na mitambo (*Excavator, Dumper Track na Drill Rig*) ya kusaidia uzalishaji wa kokoto na mataruma ya zege katika mgodi wa Kongolo unaendelea ambapo *Drill Rig* iliwasili mwezi Aprili 2019.

(iii) **Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania:** Kununuliwa kwa ndege sita ambazo zimeshawasili nchini ambapo moja (1) ni aina ya Boeing 787 – 8 Dreamliner, tatu (3) ni Bombardier Dash 8 – Q400 na mbili (2) ni Airbus A220-300; kulipa sehemu ya gharama za ununuzi wa ndege moja (1) aina ya Boeing 787-8 Dreamliner na moja (1) Bombardier Dash 8 – Q400 zinazotarajiwa kuwasili mwishoni mwa mwaka 2019; kugharamia Mafunzo ya marubani (51), wahandisi (14) na

wahudumu (66); na kuanza kwa ukarabati wa Karakana ya Matengenezo ya Ndege katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA). Kutokana na kuboreshwa kwa ATCL: idadi ya abiria imeongezeka kutoka 49,854 mwaka 2015/16 hadi 242,668 mwaka 2018/19; kuongezeka kwa idadi ya miruko (*flights*) kutoka 672 hadi 3,808 mwaka 2018/19; kuongezeka kwa idadi ya mikoa iliyofikiwa kwa huduma kutoka mikoa 3 hadi mikoa 11; kuongezeka kwa idadi ya vituo vya nje kutoka kimoja (Hahaya - Comoro) hadi vituo 5 (Hahaya, Bujumbura, Entebbe, Harare, na Lusaka); kuongezeka kwa idadi ya ajira kutoka 134 hadi 448; na kuongezeka kwa mapato ya Shirika kutoka Shilingi 11,756,709,000 hadi Shilingi 45,632,442,000. Vile vile, kuimariika kwa Shirika la Ndege Tanzania kumechangia kuongezeka kwa idadi ya watalii kutoka 1,137,182 mwaka 2016 hadi watalii 1,505,702 mwaka 2018 ambao wameliingizia Taifa mapato ya dola za Marekani billioni 2.4. Hivi karibuni ATCL inatarajia kuanza safari za moja kwa moja kwenda Mumbai (India), Guangzhou (China) na Johannesburg (Afrika Kusini).

(iv) **Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Mto Rufiji (Rufiji Hydro Power Project) – MW 2,115:** Mkandarasi wa mradi wa kufua umeme utokanao na nguvu ya maji katika Mto Rufiji ambaye ni Kampuni ya Ubia kati ya *Arab Contractors* na *Elsewedy Electric S.A.E* kutoka Misri amepatikana ambapo mkataba wa ujenzi umesainiwa na mkandarasi alikabidhiwa eneo la mradi mwezi Februari 2019 na kwa sasa anaendelea na utekelezaji wa kazi za awali. Kazi zilizokamilika ni pamoja na ujenzi wa miundombinu wezeshi ikijumuisha: njia ya kusafirisha umeme wa MW 8 yenye msongo wa KV 33 kutoka Msamu, Morogoro hadi eneo la mradi yenye urefu wa kilomita 170; barabara za kiwango cha changarawe za Ubena – Zomozi na Kibiti – Mloka hadi eneo la mradi; mifumo ya maji; mawasiliano ya simu; na nyumba za kuishi Mkandarasi. Kazi zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa njia ya pili ya umeme msongo wa KV 33 kutoka kituo cha kupoza umeme cha Gongo la Mboto kuitia Kisarawe hadi eneo la mradi urefu wa kilomita 245 itakayosafirisha umeme wa MW 22. Aidha, ujenzi wa mradi huu utakapokamilika

kutaifanya Tanzania kuwa na umeme wa uhakika na gharama nafuu na hivyo kuchochea shughuli za kiuchumi;

(v) **Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kutoka Hoima (Uganda) hadi Bandari ya Tanga (Tanzania):** kukamilika kwa tathmini ya fidia kwa maeneo ya kipaumbele (camps and coating yard) na eneo lote la mkuza. Kazi zinazoendelea ni pamoja na majadiliano ya mkataba kati ya kampuni ya mradi na Nchi Hodhi.

(vi) **Viwanja vya Ndege:** kazi zilizokamilika ni pamoja na ujenzi wa jengo jipya la abiria (Terminal III) na miundombinu yake yenye uwezo wa kuhudumia abiria milioni sita (6) kwa mwaka katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere; ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Kilimanjaro, Kiwanja cha Ndege cha Dodoma, Kiwanja cha Ndege cha Tabora (Awamu ya I na ya II) na Kiwanja cha Ndege cha Bukoba. Kazi zinazoendelea ni: ufungaji wa rada nne za kuongozea ndege za kiraia JNIA, KIA Mwanza na Songwe ambapo JNIA umefikia asilimia 95, KIA asilimia 90 na Mwanza asilimia 50; ukarabati wa Kiwanja cha Mwanza ambapo utelezaji umefikia asilimia 75, Kiwanja cha Ndege cha Songwe asilimia 70 na Kiwanja cha Ndege cha Geita umefikia asilimia 72. Maboresho na ukarabati huu wa viwanja vya ndege unatarajiwa kuchochea ukuaji wa mijini na shughuli za kiuchumi kwenye maeneo husika, kuchagiza maendeleo na ukuaji wa sekta ndogo ya usafiri wa anga (aviation industry), kusaidia katika juhudini za kulifufua Shirika la Ndege (ATCL) kwa kufanya ndege za shirika ziweze kufika maeneo mengi (hivyo kuongeza route za shirika) na kuchochea ukuaji wa sekta ya utalii nchini.

(vii) **Bandari: Bandari ya Dar es Salaam:** ujenzi wa gati Na.1 umekamilika na kuanza kutumika; ujenzi wa gati la Ro-Ro (gati la Magari) upo katika hatua ya ujenzi wa sakafu ngumu ya gati na ujenzi wa gati Na. 2 sambamba na kuongeza kina chake umeanza. Vile vile, upanuzi wa bandari za Tanga na Mtwara umefikia asilimia 86 na 50 kwa mtiririko huo. Kukamilika kwa upanuzi wa gati katika bandari ya Dar es Salaam kutaongeza uwezo wa bandari hiyo kuhudumia magari kati

ya 300,000 hadi 500,000 kwa mwaka; muda wa kupakua magari utapungua na hivyo kuongeza ufanisi wa bandari. Hatua hiyo itaongeza mapato ya Serikali na kuiwezesha bandari yetu kuhimili ushindani kutoka bandari za nchi jirani. Aidha, kwa upande wa **Bandari za Maziwa Makuu: Ziwa Victoria**: ujenzi wa gati za Nyamirembe Chato na Magarine unaendelea ambapo utekelezaji umefikia asilimia 30 na 54 kwa mtiririko huo. **Ziwa Tanganyika**: ujenzi wa gati la Kalya/ Sibwesa unaendelea ambapo utekelezaji umefikia asilimia 93. Vile vile, Serikali inakamilisha majadiliano na JICA kwa ajili ya kugharamia upanuzi wa bandari ya Kigoma. Aidha, upembuzi yakinifu wa ujenzi wa gati la Karema, umekamilika. **Ziwa Nyasa**: ujenzi wa gati la Ndumbi unaendelea ambapo utekelezaji umefikia asilimia 37.

(viii) **Barabara na Madaraja:** Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanya uwekezaji mkubwa katika kujenga na kukarabati barabara nchini ili kuhakikisha maeneo yote yanafikika kwa uhakika mwaka mzima. Juhudi hizi zitasaidia sana kuchochea kilimo na shughuli nyingine za uzalishaji mali kwa kurahisisha usambazaji wa pembejeo na malighafi kwenda maeneo ya uzalishaji pamoja na usafirishaji wa mazao na bidhaa zingine katika maeneo mbalimbali ya masoko nchini. Barabara zilizokamilika ni pamoja na: Mfugale Flyover – TAZARA (mita 1,998); Same – Mkumbara (km 96); Barabara ya Nzega - Tabora sehemu ya Nzega – Puge (km 58.8); Tunduru - Nakapanya - Mangaka - Mtambaswala (km 202.5); Namtumbo - Kilimasera - Matemanga – Tunduru (km 193); Bariadi-Lamadi (km 71.8); Sumbawanga - Kanazi - Kizi – Kibaoni (km 151.6); Kyaka - Bugene (km 59.1); Usagara - Kisesa Bypass (km 17); Magole - Turiani (km 48.6); Dodoma - Mayamaya - Mela - Bonga (km 231.85); KIA - Mererani (km 26); Mwigumbi - Maswa (km 50.3); Uyovu - Bwanga (km 45); Kaliua - Kazilambwa (km 58.9); Tabora - Nyahua - Chaya sehemu ya Tabora – Nyahua (km 85); Sitalike – Mpanda (km 36.90); Ndono - Urambo (km 52); na Tabora - Usesula (km 30). Vile vile, madaraja yaliyokamilika ni pamoja na Daraja la Magufuli katika Mto Kilombero na barabara unganishi (m 9,523); Daraja la Kavuu – Katavi (mita 85.3); Daraja la waenda

kwa miguu la Furahisha – Mwanza (mita 45). Aidha, ujenzi wa barabara na madaraja unaendelea katika maeneo mbalimbali ikujumuisha: Ubungo *interchange*; barabara ya Kimara – Kibaha (km 19) kuwa njia nane; daraja jipya la Selander ikijumuisha barabara unganishi zenyе urefu wa km 5.2; Makutano - Natta - Mugumu/Liliondo - Mto wa Mbu sehemu ya Makutano – Sanzate (km 50); Kidatu – Ifakara – Lupilo - Mahenge /Malinyi - Londo - Lumecha/Songea, km 499; Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua - Tabora (km 389.7); Sumbawanga - Matai – Kasanga Port (km 112); na Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (Nyakanazi – Kakonko (Kabingo) km 413.

(ix) **Ununuzi na Ukarabati wa Meli katika Maziwa Makuu: Ziwa Victoria:** Kuendelea na Ujenzi wa meli mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo, ujenzi wa chelezo na ukarabati wa meli ya MV Victoria na MV Butiama. Aidha, makandarasi kwa ajili ya ukarabati wa meli za MV Umoja na MV Serengeti zilizopo katika ziwa Victoria wamepatikana na uandaaji wa mikataba kwa ajili ya ukarabati wa meli tajwa umekamilika. **Ziwa Tanganyika:** mikataba ya ujenzi wa Meli Mpya moja yenye uwezo wa kubeba abiria 600 na tani 400 na ukarabati wa meli ya MV Liemba imekamilika. **Ziwa Nyasa:** ujenzi wa meli moja mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na mizigo tani 200 katika Ziwa Nyasa unaendelea ambapo utekelezaji umefikia asilimia 86. Aidha, ujenzi wa matishari mawili katika Ziwa Nyasa umekamilika.

(x) **Nishati:** uzalishaji wa umeme umeongezeka kutoka GWh 7,092.13 mwaka 2015/16 hadi GWh 7,374 mwaka 2018/19 ambao umewezesha kuongezeka kwa upatikanaji wa umeme wa uhakika; kuongezeka kwa kasi ya kusambaza umeme vijiji ambapo hadi kufikia Mei, 2019 jumla ya vijiji 7,127 vimeunganishiwa umeme ambapo jumla ya taasisi za elimu 3,165, maeneo ya biashara 3,451, pampu za maji 210, taasisi za afya 1,211 na nyumba za ibada 984 zimeunganishiwa umeme; kufikishwa umeme katika vijiji vya Wilaya na Halmashauri 15 ambazo ni Mafia, Iringa Vijiji (Isimani), Pangani, Rufiji, Bahi, Siha, Moshi, Hai, Mwanga,

Rombo, Madaba, Buhigwe, Makambako, Korogwe Mjini na Mafinga; ujenzi wa njia za kusambaza umeme za Msongo wa KV 33 zenyne urefu wa kilomita 18,227; ujenzi wa Vituo Vidogo vya kupoza na kusambaza umeme 4,100; na ujenzi wa njia ndogo ya usambazaji umeme zenyne urefu wa kilomita 30,797.

(xi) **Kilimo:** kiwango cha ukuaji wa sekta ya kilimo kilongezeka kufikia asilimia 5.3 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 4.8 mwaka 2016. Ukuaji huu umewezesha kuongezeka kwa usalama wa chakula, kupungua kwa mfumuko wa bei ya chakula kufikia asilimia 2.7 Aprili 2019 ikilinganishwa na asilimia 7.3 Aprili 2016 na kuongezeka kwa mapato ya mauzo ya bidhaa asilia nje ya nchi kutoka dola za Marekani milioni 793.4 mwaka 2015 hadi kufikia dola za Marekani milioni 1,020.7 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 28.6. Vile vile, upatikanaji wa mbegu bora uliongezeka na kufikia tani 49,040.66 mwaka 2018/19 kutoka tani 36,482 mwaka 2015/16, na tani 492,394 za mbolea zilinunuliwa na kusambazwa katika mwaka 2018/19 ikilinganishwa na tani 302,450 zilizonunuliwa katika mwaka 2015/16. Aidha, katika kuimarisha Ushirika na Masoko ya Mazao, Vyama vya Ushirika viliongezeka kutoka 7,888 mwaka 2015 hadi 11,331 mwaka 2018. Vile vile, Serikali imeendelea na ujenzi wa vihenge na maghala vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 250,000 na maghala yenye uwezo wa kuhifadhi tani 60,000 unaendelea katika mikoa ya Ruvuma (Songea), Njombe (Makambako), Songwe (Mbozi), Rukwa (Sumbawanga), Katavi (Mpanda), Shinyanga, Manyara (Babati) na Dodoma. Utoshelevu wa Chakula kwa mwaka 2018/19 umefikia asilimia 124. Aidha, Serikali imeanza utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo awamu ya pili (ASDP II) na mkazo umewekwa katika kuendeleza mazao ya kimkakati yakiwemo Kahawa, Pamba, Chai, Korosho, Tumbaku, Alizeti, Michikichi, Mpunga na Mahindi.

Vile vile, Serikali kuititia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) imeendelea kutoa mikopo ya pembejeo na zana za kilimo. Tangu kuanzhishwa kwa Mfuko huu mwaka 1994, jumla ya mikopo yenye thamani ya Shilingi 82,103,746,770

imetolewa na katika kipindi cha Julai 2018 hadi Machi 2019, mikopo 33 yenye thamani ya Shilingi 1,495,362,060 ikiwemo 22 ya mitambo ya mashambani, sita (6) ya pembejeo za kilimo na mitano (5) ya umwagiliaji imetolewa. Aidha, utoaji wa mikopo hii unaenda sanjari na ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo ya nyuma ambapo katika mwaka 2018/19, shilingi 1,842,698,117.73 zimerejeshwa. Juhudi hizi zinalenga kuwawezesha wakulima kuongeza matumizi ya zana bora na za kisasa katika kilimo ili zisaidie kuongeza tija katika uzalishaji hasa ikizingatiwa kilimo chetu bado kinakabiliwa na changamoto ya uzalishaji mdogo kutokana na matumizi ya zana duni.

(xii) **Huduma za Afya:** Kununuliwa kwa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kupitia Bohari ya Dawa na kusambazwa katika vituo vya umma vya kutolea huduma nchini ambapo upatikanaji wa dawa muhimu (Tracer Medicine) katika vituo vya kutolea huduma za afya umefikia asilimia 94.4 na kusambazwa lita 239,020 za viuadudu (biolarvicides) vya kuangamiza viluwiluvi vya mbu katika maeneo ya mazalia ulifanyika katika Halmashauri zote nchini; kuongeza utoaji wa chanjo kufikia asilimia 98; kununuliwa mashine za X-ray 36 (28 za kidigitali na 8 za huduma ya kinywa); kuendelea na ujenzi wa hospitali za wilaya (67) Vituo vya kutolea huduma za Afya (352) na nyumba za watumishi wa afya 318; kuajiriwa kwa watumishi wa sekta ya afya 7,680; bajeti ya ununuzi wa dawa, chanjo, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi illongezeka kutoka Shilingi bilioni 31 mwaka 2015/16 hadi Shilingi bilioni 260 mwaka 2018/19; kuanza kutoa huduma ya kupandikiza figo kwa wagonjwa 45 (wagonjwa 38 katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na wagonjwa 7 katika Hospitali ya Benjamini Mkapa – Dodoma) na hivyo kupunguza gharama kwa wastani kutoka shilingi milioni 100 hadi shilingi milioni 20 kwa mgonjwa mmoja endapo angepelekwa nje ya nchi; Vile vile, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za matibabu ya kibingwa kwa kuboresha miundombinu ya kutolea huduma, ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa na hivyo kupunguza rufaa za wagonjwa nje ya nchi kufuatia kuimarika kwa huduma katika hospitali za Muhimbili, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI), Taasisi ya

Mifupa (MOI), Benjamin Mkapa na Hospitali ya Taaluma na Tiba ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi – Mloganzila. Kuimarika kwa huduma za kibingwa nchini kumepunguza kwa kiasi kikubwa gharama za matibabu kwa wananchi ambao awali walikuwa wakipewa rufaa kwenda kutibiwa nje ya nchi.

(xiii) **Huduma za Maji:** kukamilika kwa miradi 1,659 ya maji hivyo kuongeza vituo vya kuchotea maji kufikia 131,370 vyenye uwezo wa kuhudumia wananchi 25,359,290; upatikanaji wa huduma za maji jijini Dar es Salaam umefikia asilimia 85, katika mikoa mingine asilimia 80, miji midogo asilimia 64 na vijijini asilimia 64.8; kuendelea kujenga na kukarabati ofisi za maji za mabonde na maabara za maji katika mabonde mbalimbali ambapo hatua zilizofikiwa ni: Ruvuma na Pwani ya Kusini (asilimia 90), Ziwa Nyasa (asilimia 50), Rufiji (asilimia 65 Mkoji na Kimani), Ziwa Rukwa (asilimia 65) na Bonde la Kanda ya Kati (asilimia 95); kuendelea na ujenzi, ukarabati, na upanuzi wa miradi ya maji katika miji mikuu ya wilaya, miji midogo na miradi ya Kitaifa; mradi wa huduma za maji katika miji mikuu ya mikoa mipyä unaendelea kutekelezwa ambapo kwa mkoa wa Geita umekamilika, Njombe umefikia asilimia 95 na Songwe asilimia 90; kuendelea na ulazaji wa bomba la kusambazia maji kwenye mradi wa maji wa Ziwa Victoria - Kahama Shinyanga katika miji ya Kagongwa na Isaka ambapo utekelezaji umefikia asilimia 87 na ujenzi wa miundombinu ya maji katika miji ya Tabora, Igunga, Uyui na Nzega pamoja na vijiji 89 vilivyo pembezoni mwa bomba kuu umefikia asilimia 68.5.

Vile vile, mradi wa maji Same – Mwanga – Korogwe umeendelea kutekelezwa ambapo miundombinu ya msingi ikiwemo bomba kuu la kusafirisha maji, kitekeo cha maji, mtambo wa kusafisha maji na matanki ya kuhifadhi maji, maabara na eneo la kuhifadhia dawa za kutibu maji vimekamilika. Kukamilika kwa miradi hii ya maji kutawanufaisha wananchi katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu ikiwa ni pamoja na kuimarisha shughuli za uzalishaji mali na kuwakinga na maradhi hususan katika maeneo ya vijijini.

(xiv) **Viwanda:** Serikali iliendelea kusimamia utekelezaji wa azma yake ya ujenzi wa uchumi wa viwanda ambapo viwanda vipyta zaidi ya 3,530 vilijengwa katika mikoa mbalimbali ikijumuisha viwanda vya kuzalisha bidhaa za ujenzi (saruji, marumaru, nondo) na kilimo, hususan, kusindika matunda, mafuta na ngozi. Ujenzi wa viwanda vipyta umechangia kupatikana kwa ajira mpya takribani 482,601 nchi zima. Aidha, ili kutatua changamoto ya upatikanaji wa mikopo kwa wafanyabiashara wadogo, Serikali kuititia Mfuko wa Maendeleo ya Wajasiriamali (NEDF) imetoea mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 7.264 na kuzalisha ajira mpya takriban 186,138 kutokana na mikopo 91,584. Serikali imeendelea kuunganisha matrekta katika Kiwanda cha Kuunganisha Matrekta – TAMCO, Kibaha ambapo Jumla ya matrekta 822 aina ya URsus yameingizwa nchini kutoka Poland yakiwa katika vipande (semi knocked down) ambapo matrekta 571 yameunganishwa na matrekta 399 yameuzwa. Mafanikio haya yamewezesha jumla ya ekari 85,464 kulimwa kwa kutumia matrekta hayo hadi Aprili 2019. **Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundu Vijiji – CAMARTEC:** kutengeneza zana zikijumuisha mashine 64 za kupandia mbegu za pamba, kusaga karanga, kukausha mbogamboga na kukata majani pamoja na ujenzi wa mitambo 55 ya *biogas*; **SIDO:** kuendelea na ujenzi wa majengo ya viwanda 11 katika Mikoa ya Dodoma, Geita, Kagera, Katavi, Manyara, Mtwara na Simiyu na ujenzi wa ofisi za SIDO katika mikoa mipyta ya Geita na Katavi. Aidha, Serikali inaendelea na uendelezaji wa kanda Maalum za Kiuchumi katika maeneo mbalimbali nchini ambapo Kanda Maalum za Kiuchumi za Kigoma na Mtwara uwekezaji umeanza.

(xv) **Kuhamishia Makao Makuu ya Serikali Dodoma:** Serikali ya awamu ya tano imefanikiwa kuhamisha Makao Makuu ya Serikali kutoka katika jiji la Dar es Salaam kuja katika jiji la Dodoma ambapo Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Watumishi wa Umma 8,883 kutoka Wizara na Taasisi wamehamia Dodoma. Aidha, Ujenzi wa Ofisi za Serikali katika Mji wa Serikali Mtumba umekamilika na kuzinduliwa rasmi ambapo Wizara zote zimehamia na kuanza kutoa huduma katika eneo la mji wa Serikali.

(xvi) **Madini:** kazi zilizokamilika ni pamoja na ujenzi wa jengo la wafanyabiashara wa madini (Brokers house) na kuendelea na ujenzi wa kituo cha pamoja (one stop centre) eneo la Mirerani ambapo uwekezaji huo utaimarisha upatikanaji wa takwimu na kudhibiti utoroshaji wa madini ya tanzanite; ujenzi wa jengo la taaluma la Chuo cha Madini (MRI) Dodoma; uanzishwaji wa masoko ya madini mikoani katika kuhakikisha kuwa wachimbaji wa madini wanapata masoko rasmi na Serikali kupata mapato stahiki; ufungwaji wa mitambo ya uchenjuaji wa madini ya dhababu kwenye vituo vya mfano vya Lwamgasha na Katente (Geita) na Itumbi (Mbeya) kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo kuhusu uchimbaji, uchenjuaji, biashara ya madini, afya, usalama migodini na utunzaji wa mazingira. Vituo hivi vitawezesha wachimbaji wadogo kujifunza kwa vitendo ili waweze kuwekeza na kufunga mitambo ambayo haitumii kemikali za zebaki (mercury); ujenzi na ukarabati wa ofisi za madini Moshi na Nachingwea; ujenzi wa vituo Saba (7) vya umahiri katika maeneo ya Bariadi, Bukoba, Musoma, Handeni, Mpanda, Chunya na Songea vitakavyotumika kutoa mafunzo na maarifa kuhusu ujasiriamali, utafutaji na uchimbaji wa madini kwa wachimbaji wadogo ambapo kati ya hivyo, vituo vya Bariadi, Musoma, Bukoba na Handeni vimekamilika; na mapitio ya Sheria za Madini ili kuiwezesha Serikali kunufaika zaidi na rasilimali za madini. Aidha, Serikali ilikamilisha ujenzi wa ukuta wenye mzingo wa km 24.5 kuzunguka migodi ya Tanzanite Mirerani na uwekaji wa mfumo wa ulinzi wa kidigitali ambaeo umeweza kupunguza utoroshwaji wa madini. Juhudi hizi na nyinginezo ziliwezesha kuongezeka kwa makusanyo ya maduhuli yanayotokana na madini kutoka Shilingi bilioni 194.4 mwaka 2016/17 hadi Shilingi bilioni 244.3 kwa kipindi cha Julai 2018 hadi Machi 2019.

(xvii) **Elimu:** Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Mwenyekiti wa CCM, ilianzisha na imeendelea kutekeleza utaratibu wa kutoa elimumsingi bila ada kwa kutoa Shilingi bilioni 24.4 kila mwezi. Juhudi hizi zimechangia ongezeko la wanafunzi walioandikishwa darasa la kwanza kutoka 1,568,378 mwaka 2015 hadi wanafunzi 1,670,919 mwaka 2019,

na kidato cha kwanza kutoka wanafunzi 448,826 mwaka 2015 hadi wanafunzi 710,436 mwaka 2019. Mafanikio mengine yallyopatikana ni pamoja na: ukarabati na ujenzi wa miundombinu kwa shule za msingi 219 na sekondari 285 katika mikoa yote; ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya vyuo 7 vya ualimu; ununuzi wa kemikali na vifaa vya maabara kwa shule za sekondari 1,696; kuimarisha ubora wa elimu ya msingi na sekondari kwa kuboresha na kuchapa vitabu vya shule ya msingi na sekondari; kuimarisha ufundishaji kwa vitendo kwa kununua vifaa vya maabara kwa ajili ya Chuo Kikuu cha Dodoma; ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia ikijumuisha madarasa 938, matundu ya vyuo 2,141, mabweni 210, mabwalo 76; ukarabati wa shule kongwe 17; kukamilisha maboma ya madarasa, mabweni na nyumba za walimu 39; ukarabati wa vyuo 20 kati ya vyuo 54 vya Maendeleo ya Wananchi (*FDCs*), kukamilika na kuzinduliwa kwa Maktaba ya Kimataifa yenye uwezo wa kuhudumila wanafunzi 2,100 kwa wakati mmoja katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; kukamilika kwa ukarabati wa mabweni sita (6) katika Chuo Kikuu cha Mzumbe; ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika vyuo vikuu vya Sokoine na Dar es Salaam; na mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu 122,734; uimarishaji wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vya ufundi stadi na kukuza ujuzi kwa vijana; na kukamilika kwa ujenzi wa shule ya sekondari maalum ya Patandi kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 640. Mafanikio haya yamechangia kupunguza gharama za elimu msingi nchini na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa watoto wetu pamoja kuchochea mwamko wa elimu kwa wananchi.

MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2019/20

Shabaha na Malengo ya Uchumi Jumla kwa Mwaka 2019/20

34. Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20 umezingatia shabaha kuu za uchumi jumla zifuatazo:

- (a) Kukua kwa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 7.1 mwaka 2019 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.0 mwaka 2018;
- (b) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja kati ya asilimia 3.0 hadi asilimia 4.5;
- (c) Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.1 ya Pato la Taifa mwaka 2019/20 kutoka matarajio ya asilimia 12.1 mwaka 2018/19;
- (d) Matumizi ya Serikali yanatarajiwa kuwa asilimia 22.7 ya Pato la Taifa mwaka 2019/20; na
- (e) Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa asilimia 2.3 mwaka 2019/20.

Miradi ya Kipaumbele 2019/20

35. Mheshimiwa Spika, miradi na shughuli za kipaumbele kwa mwaka 2019/20 ni mwendelezo wa kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21. Miradi itaelekezwa katika maeneo ya kipaumbele ni kama ifuatavyo:

(a) Viwanda vya Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda: Eneo hili litatilia mkazo ujenzi wa viwanda vinavyotumia maliqhafi zinazopatikana kwa wingi nchini. Miradi mahsusni katika eneo hili itajumuisha:

(i) Uendelezaji wa Viwanda: kuendeleza kongane za viwanda – TAMCO (Kibaha); Kongane ya viwanda vya ngozi (Dodoma); maeneo maalumu ya uwekezaji ya Bunda, Dodoma na Benjamin William Mkapa; na kuendeleza vituo vya utafiti wa teknolojia na bidhaa za viwandani vya CAMARTEC, TIRDO, TEMDO na SIDO;

(ii) Kilimo: kuongeza tija katika uzalishaji kwa kuwezesha upatikanaji wa mbegu na pembejeo, huduma za ugani, maghala na masoko kwa mazao ya kimkakati ya kahawa, pamba, chai, mpunga, tumbaku na miwa; Serikali

itaendeleza juhudi katika ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya skimu za umwagiliaji; na kuimarisha utafiti wa mbegu bora na magonjwa ya mazao;

(iii) **Mifugo:** kuimarisha mashamba ya kuzalisha mitamba na vituo vya uhamilishaji mifugo na kuhamasisha matumizi ya teknolojia sahihi ili kuongeza kasi ya uzalishaji wa mitamba na madume kwa ajili ya maziwa na nyama, kudhibiti na kukabiliana na magonjwa mlipuko kwa mifugo ili kuongeza uzalishaji na kukidhi ubora wa malighafi zitokanazo na mifugo kwa viwanda vinavyoendelea kujengwa nchini, kupima na kutenga maeneo ya malisho kwa ajili ya mifugo ili kupunguza migogoro ya ardhi katи ya wakulima, wafugaji na watumiaji wengine.

(iv) **Uvuvi:** kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa bandari ya uvuvi na ununuzi wa meli kubwa za uvuvi; kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania - TAFICO ili kuimarisha uwekezaji katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari na Bahari Kuu; kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika Ukanda wa Ziwa Victoria, Tanganyika na Ukanda wa Pwani ili kuongeza udhibiti na kukomesha biashara haramu ya mazao ya uvuvi; na

(v) **Madini:** kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; uendelezaji wa masoko ya madini; kukamilisha ujenzi wa mtambo wa kuyeyusha madini (smelter) na vituo vya umahiri; kuwezesha shughuli za utafiti wa madini ili kuongeza taarifa za kijiolojia na kuvutia uwekezaji; kuelimisha umma kuhusu matumizi ya takwimu za rasilimali za madini, mafuta na gesi asilia na; usimamizi wa masuala ya mazingira, afya na usalama migodini.

(b) **Kufungamanisha Ukuaji wa Uchumi na Maendeleo ya Watu:** Miradi ya kipaumbele itakayoteklezwa katika mwaka 2019/20 itajielekeza katika maeneo yafuatayo:

(i) **Elimu:** kuendelea kusomesha kwa wingi wataalam kwenye ujuzi na fani adimu kama vile udaktari, mafuta na gesi; kuendelea kugharamia utoaji wa elimu msingi bila ada;

ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kujifunzia na kufundishia katika shule na vyuo vya ualimu; kuimarisha vyuo vya ufundi stadi kwa kukarabati, kujenga na kuweka vifaa vya kufundishia na kujifunzia; kuboresha na kununua vifaa vya kujifunzia na kufundishia katika shule 500 za sekondari ili kuziwezesha kuwa vituo vya mafunzo kazini kwa walimu wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Lugh; kujenga ofisi 55 za wathibiti ubora wa shule; kuongeza utoaji wa mikopo ya elimu ya juu na kusimamia marejesho yake; na kuendeleza shughuli za utafiti kwa maendeleo. Utekelezaji wa shughuli hizi utaboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia na hivyo kuongeza ufaulu wa watoto wetu.

(ii) Afya: kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za tiba katika Hospitali za Rufaa za mikoa, kanda na Taifa; kuimarisha usambazaji wa dawa, chanjo, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya; kuimarisha hali ya lishe na usafi wa mazingira; kuimarisha huduma katika taasisi ya Saratani Ocean Road, Taasisi ya Tiba ya Moyo ya Jakaya Kikwete na Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOL); kuendeleza ujenzi wa Hospitali za Wilaya na vituo vya afya; ujenzi na ukarabati wa vyuo vya Maendeleo ya Jamii; kuimarisha huduma za ustawi wa jamii kwa wazee na watoto walio katika mazingira hatarishi; na kukuza usawa wa jinsia na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi. Utekelezaji wa shughuli hizi utaboresha upatikanaji wa huduma za afya katika ngazi mbalimbali nchini na hivyo kuimarisha afya za wananchi.

(iii) Maji: kuimarisha upatikanaji wa maji mijini na vijiji; kuendelea na ujenzi wa miradi ya maji ikiwemo Makonde (Mtwara), Wanging'ombe (Njombe), Chalinze (Pwani), Mugango/Kiabakari – Butiama (Mara); maji kutoka Ziwa Victoria hadi miji ya Tabora, Nzega, Igunga, Sikunge na vijiji 89 vilivyo pembezoni mwa bomba kuu na kuanza ujenzi kupeleka maji katika miji ya Busega, Bariadi, Lagangabilili na Mwanhuzi; na kuendeleza rasilimali za maji nchini na maabara za maji.

(c) Uboreshaji wa Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji

Biashara na Uwekezaji: Miradi itakayotekelawa katika eneo hili ni ile yenye lengo la kuendeleza ujenzi na ukarabati wa miundombinu kwa ajili ya kurahisisha ufanyaji biashara na kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi. Miradi katika eneo hili itajumuisha: kuendelea na Ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha Standard Gauge; Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Mto Rufiji – MW 2,115; na Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania. Miradi mingine ni pamoja na: Kuboresha miundombinu ya reli za TAZARA, Tanga – Arusha, usafiri wa reli Dar es Salaam pamoja na kuboresha injini na mabehewa ya treni; kuendelea na ujenzi wa barabara zikijumuisha barabara za Kigoma - Kidahwe - Uvinza - Kaliua - Tabora (km 389.7), Mtwara – Mingoyo – Masasi – Songea – Mbamba Bay (km 1,470.9), Barabara ya Kidahwe - Kasulu – Kibondo - Nyakanazi (km 413), Usagara - Geita - Buzirayombo - Kyamyorwa (km 230); madaraja ya Sibiti (Singida), New Wami (Pwani); Daraja la Kigongo/Busisi (Mwanza), Daraja la Mtera (Dodoma), Simiyu (Mwanza), Selander (Dar es Salaam); ujenzi na ukarabati wa vivuko; usambazaji wa umeme vijijini kupitia mradi wa REA; miradi mikubwa ya njia za kusambaza umeme wa msongo mkubwa ikijumuisha njia ya umeme wa msongo wa KV 400 ya Rufiji – Chalinze – Dodoma (km 512); uboreshaji wa bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara; na miundombinu ya viwanja vya Ndege; kuimarisha upatikanaji wa ardhi na huduma za fedha kwa ajili ya mitaji ya uwekezaji; na kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara na Uwekezaji ikijumuisha kuhuisha mfumo, viwango na idadi ya kodi, ushuru na tozo; na mifumo ya kitaasisi, kisera na kisheria ili kuvutia uwekezaji; na

(d) Kuimarisha Usimamizi wa Utekelezaji wa Mpango:

Miradi inayotekelawa katika eneo hili inalenga kuimarisha mifumo na taasisi za utekelezaji wa Mpango, kuweka mfumo utakaowezesha upatikanaji wa uhakika wa rasilimali fedha na kuweka vigezo vya upimaji wa mafanikio ya utekelezaji. Miradi hii itajumuisha ile ya Utawala Bora hususan utoaji Haki na Huduma za Kisheria, Kuimarisha Mifuko ya Mahakama na Bunge, kuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama kwa

kuvipatia vitendea kazi na mafunzo pamoja na kuimarisha Usajili wa Vizazi na Vifo.

36. Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu Miradi ya Kipaumbele yapo katika Sura ya Nne ya Kitabu cha Mpango.

Vihatarishi Vya Utekelezaji wa Mpango 2019/20

37. Mheshimiwa Spika, Vipo vihatarishi mbalimbali ambavyo endapo vitajitokeza vitaathiri utekelezaji wa Mpango. Vihatarishi hivyo vinajumuisha vihatarishi vya ndani na nje. Vihatarishi vya ndani ni pamoja na upungufu wa rasilimali fedha, ushiriki mdogo wa sekta binafsi, umiliki wa ardhi na utatuzi wa migogoro, uharibifu wa mazingira na usalama mtandaoni. Vihatarishi vya nje ni pamoja na mtikisiko wa kiuchumi kikanda na kimataifa, matukio asilia, migogoro ya ndani na ya kimataifa na mabadiliko ya tabia nchi.

38. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na vihatarishi vya utekelezaji wa Mpango, Serikali ya awamu ya tano itachukua hatua mbalimbali ikijumuisha: kuharakisha urasimishaji wa sekta isiyo rasmi ili iweze kuingizwa kwenye wigo wa kodi; kuimarisha nidhamu katika usimamizi wa matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo; kuendelea kuboresha mazingira wezeshi ya biashara ili kupunguza gharama za uwekezaji; kusimamia matumizi bora ya ardhi kwa kuandaa na kuimarisha Mpango Miji ili kurahisisha utoaji wa huduma mbalimbali za kijamii; na kuendelea kuimarisha mifumo ya kutabiri majanga na kuchukua tahadhari pamoja na kutekeleza miradi ya kuhimili athari za matukio asilia.

Ugharamiaji wa Mpango 2019/20

39. Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga Shilingi bilioni 12,248.6, kwa ajili ya kugharamaia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20, ambapo shilingi bilioni 9,737.7 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 2,510.9 ni fedha za nje. Fedha hii ya maendeleo ni sawa na asilimia 37 ya bajeti yote ya mwaka 2019/20, kiwango kinachoshabihiana na lengo la Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano la

kutenga kati ya asilimia 30 na 40 ya bajeti yote kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Serikali inatarajia kugharamia Mpango kutokana na vyanzo mbalimbali vilijumuisha mapato ya kodii, mikopo na misaada ya Washirika wa Maendeleo, Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje na Mifuko ya Kimataifa ya Mabadiliko ya Tabianchi.

Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje

40. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini ili kuvutia uwekezaji wa kimataifa hususan uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (FDIs) katika maeneo ya kipaumbele ya Mpango ikijumuisha viwanda, kilimo, maliasili, gesi, mafuta, madini, mawasiliano, ujenzi na utalii. Maboresho hayo yatajumuisha ujenzi wa miundombinu ya msingi, utengaji wa maeneo maalum ya uwekezaji na kuweka miundombinu wezeshi, kuhuisha sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia uwekezaji pamoja na kuhamasisha sekta binafsi ya ndani ya nchi kuwekeza kwa ubia na sekta binafsi ya nje.

Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

41. Mheshimiwa Spika, Serikali itatoa elimu kuhusu uwekezaji wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ikijumuisha hatua za uibuaji, maandalizi na utekelezaji wa miradi ya ubia. Vile vile, Serikali itaendelea kutafuta wabia wa kimkakati katika miradi ya kipaumbele kwa utaratibu wa PPP.

Mifuko ya Kimataifa ya Mabadiliko ya Tabianchi

42. Mheshimiwa Spika, Vile vile, Serikali itaendelea kutumia mifuko mbalimbali ya kimataifa ya mabadiliko ya tabianchi katika ufadhili wa miradi ya maendeleo hususan ile ya mazingira. Hatua mbalimbali zitakazochukuliwa zitahusisha majadiliano na Washirika wa Maendeleo na wadau mbalimbali ili kuwezesha upatikanaji wa fedha kutoka mifuko hiyo kama vile *Least Developed Countries Fund (LDCF)*;

Global Environmental Facility (GEF): Adaptation Fund (AF); United National Environmental Programme (UNEP) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

Ufutiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji

43. Mheshimiwa Spika, Katika kuhakikisha kuwa ufutiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango 2019/20 unazingatia Mkakati wa Ufutiliaji na Tathmini wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali ya awamu ya tano imejipanga kuzingatia viashiria vya utekelezaji vilivyoainishwa katika maeneo ya kipaumbele ya Mpango. Aidha, ufutiliaji na tathmini utazingatia taarifa ya tathmini ya muda wa kati wa utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano hususan hatua halisi ya utekelezaji, changamoto na mapendekezo ya hatua za kukabiliana na changamoto zillizojitekeza.

44. Mheshimiwa Spika, katika kila robo ya mwaka 2019/20 Wizara ya Fedha na Mipango itafutilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi ya kielelezo, kimkakati na inayotekelawa na sekta binafsi ili kujua mafanikio na upungufu utakaojitekeza wa utekelezaji wa miradi katika maeneo ya kipaumbele ya Mpango. Ofisi ya Rais – TAMISEMI itaratibu ufutiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo inayotekelawa katika ngazi za Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti, SURA 439. Taarifa za utekelezaji zitasaidia Serikali katika kufanya maamuzi na kuhamasisha jamii kujituma zaidi katika kufikia malengo ya Mpango.

MAJUMUISHO NA HITIMISHO

MAJUMUISHO

45. Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali ni kujenga uchumi wa kipato cha kati ifikapo mwaka 2025 kama ilivyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025. Pamoja na jitihada nyingine katika kufanikisha lengo hili, Serikali

itaendelea kuwekeza katika ujenzi wa miundombini wezeshi ya undelezaji wa viwanda na kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vitakavyotumia malighafi zinazopatikana nchini hususan mazao ya kilimo, madini na gesi asilia.

46. Mheshimiwa Spika, vile vile katika kufanikisha ujenzi wa uchumi wa kipato cha kati Serikali itaendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato na kukusanya mapato kutoka vyanzo bunifu vilivyoainishwa katika Mkakati wa Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, kuhakikisha mipango na bajeti inawekewa viashiria, vigezo na shabaha bayana ambavyo usimamizi wa utekelezaji utazingatia, kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi hususan katika sekta ya viwanda na kutekeleza maoni na ushauri unaotolewa na Bunge juu ya utekelezaji wa mipango na bajeti.

HITIMISHO

47. Mheshimiwa Spika, tunapokaribia kuhitimisha kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano wenyе dhima ya "Kujenga Uchumi wa Viwanda ili kuchochea Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo ya Watu", niwaombe Viongozi wa Serikali, Waheshimiwa Wabunge na wananchi kushirikiana wote kwa pamoja katika kuleta ufanisi wa utekelezaji wa Mpango.

48. Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali ninaomba niwashukuru wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi wakiwemo Washirika wa Maendeleo, Sekta Binafsi na wananchi kwa ujumla kwa michango yao katika kuleta mafanikio katika ukuaji wa uchumi na utekelezaji wa Mpango.

49. Mheshimiwa Spika, vile vile naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Dkt. Ashatu K. Kijaji (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Wizara zote, Wakuu wa Idara zinazojitegemea na Taasisi kwa ushirikiano wao katika kutayarisha taarifa ya Hali ya Uchumi ya mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa

wa Mwaka 2019/20. Aidha, ninawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu Bw. Doto M. James kwa kusimamia vizuri kazi za kila siku za Wizara.

50. Mheshimiwa Spika, kipekee niwashukuru Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wote kwa kunisikiliza. Aidha, hotuba hii na vitabu vyta Taarifa ya Uchumi ya mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2019/20 vinapatikana katika tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango www.mof.go.tz.

51. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa Waheshimiwa Wabunge wapokee, wajadili na kupitisha Taarifa ya Hali ya Uchumi Mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20.

52. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, alichokifanya Mheshimiwa Waziri ni kutusomea hali ya uchumi wa Taifa kwa mwaka 2018 lakini pia ametupitisha kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa fedha 2019/2020. Amefanya hivi kwa maandalizi sasa ya jioni ya leo kuanzia saa 10:00 jioni ambapo sasa atatusomea Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2019/2020. Tafsiri yake ni kwamba sasa ndiyo tutapata maelezo kwa undani ya mapato yote ya Serikali na matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, vitabu vyote natumaini mmevipata, wameleta vitabu vingi; viro vitabu vyta Benki Kuu (*Monetary Policy Statement/Muhtasari*

wa Tamko la Sera ya Fedha), tuna Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2018 ni vizuri kuititia na kuona nini kinaendelea, lakini pia kuna kitabu kinachohusu Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kuanzia 2016/2017 mpaka 2018/2019; lakini pia tuna Mpango wa Maendeleo ya Taifa 2019/2020. Zote mtazipata na baadhi ya vitabu hivi kwenye *pigeon hole* zenu wale ambao mnapitia kule ni vizuri mkapitia mkachukua siyo rahisi kugawa kila kimoja lakini vinapatikana vyote. Nawashukuru sana kwa usikivu wenu, nisisitize kuhusu usikivu leo jioni.

Waheshimiwa Wabunge, wengi huwa mnaandika, mnalalamika kwamba kwa nini *Bunge live* hakuna, moja ya sababu ni hii hali, ndiyo ukweli wenyewe. Unapoonesha *live* hii hali ambayo Spika kila wakati lazima awaambie Wabunge msikilizane yaani ninyi wenyewe hamuwezi kusikiliza na kuona tu kila mmojawapo akaona jinsi ya...ni aibu kubwa sana. (*Makofii*)

Kwa mfano, hotuba ya leo itasomwa Afrika Mashariki nzima. Burundi watakuwa wanasona Hotuba ya Bajeti saa 10:00 ya Kati, Rwanda watakuwa wanasona, Uganda, Kenya na sisi na uhakika kama ukiweza kuangalia Mabunge yote utaona utulivu ni tofauti kabisa. Kwa wenzetu wanasikiliza sisi watu hawana habari. Sijui kwa sababu takwimu zinasomwa hapa!! Unajua siyo watu wote wanavumilia kusikiliza hesabu!! Kwa hiyo tuwe na utulivu. Kila *gallery* zetu zitakuwa zimejaa wageni watu maalum wengi sana. Wanapokuja wanaona hiki kinachoendelea humu ndani wanashangaa hili Bunge la aina gani. Watu wanapiga michapo, wengine wamegeuka nyuma, yaani mwengine anakaa saa nzima anaongea na mwenzake hata huyo unayeongea naye unambughudhi anashindwa tu kukwambia bwana hebu ondoka na kadhalika.

Kwa hiyo vitu vingine tunahitaji kuwa ni Wabunge, Serikali inaleta taarifa mbele yetu taarifa *serious*, tunaonekana tunasikiliza taarifa hiyo mpaka mwisho wake, mbona siyo ya muda mrefu kitabu hiki cha hotuba hiki hakikumchukua Waziri muda mrefu hata kidogo.

Kwa hiyo nawaombeni sana tujenga utamaduni huo wa kusikiliza vitu ili hata wakati wa kuchangia unachangia kutokana na taarifa hizi tulizonazo kuliko sasa unakuja kivyako kwa sababu hukusikiliza na Mbunge unapozungumza unasikilizwa na nchi kwa hiyo matokeo yake unaiyumbisha nchi kumbe ukweli uko tofauti.

Kwa hiyo, nawaombeni sana hili la usikivu tuwe pamoja katika hili tusiwe tunakumbushana kumbushana mara kwa mara kuhusu hili jambo. Kutembea tembea yaani haipendezi kwa kweli, nawaombeni sana. Jioni nitakachofanya mimi nitakuwa nataja majina tu kwa sababu nina uhakika nchi nzima itakuwa inaangalia kwenye Majimbo yenu fulani hatulii, fulani na mnajua ni keshokutwa watakuwa wanakumbuka. Ninyi mnafikiri ni jambo la kawaida, hizi *camera* hizi tuzipenda lakini zina...na zinatembea humu. Wale mnaopiga michapo wanangalia yaani huyu ndiyo tumemtuma akasikilize ndiyo hivi! Msifikiri kwamba ni...,*camera* ni nzuri lakini ina mambo yake, ina *discipline* yake kwahiylo nawaombeni jioni tuwe pamoja.

Spika wa Rwanda aliondoka jana, anawashukuru sana, anawashukuruni sana sana na wao kama nilivyosema leo watakuwa wanasoma bajeti yao, wao wana Mabunge mawili, kwa hiyo siku ya bajeti kama leo Mabunge yote mawili yanakutana kwa pamoja, *Senate* na lile *Chamber of Deputies* ambapo sasa Spika wa lile *Chamber of Deputies* yule aliyejuka ndiyo anakuwa Spika wa kikao kile cha Mabunge ya pamoja yanaposomewa hotuba hizo na ni vivyo hivyo kwa Burundi na ni vivyo hivyo kwa Kenya kwa sababu wao wana Mabunge mawili mawili ila sisi na Uganda tuna Bunge moja kwa utaratibu huu ambaao tunao lakini bajeti zitasomwa katika utaratibu huo.

Kwa hiyo, tumejifunza mengi kutoka kwake, yule Mama alipata nafasi ya kuzungumza Wabunge akinamama tunawashukuru sana wale ambaao walipata nafasi ya kwenda, lakini wengi hawakwenda ndiyo yale yale anakuja mgeni watu hawaendi. Tuwe tunakwendajamani tutajifunza vitu vingi wanapokuja wageni. Wabunge Wanawake kidogo

mlituangusha kwenye hilo, mahudhurio hayakuwa kama tulivyokuwa tumetarajia, lakini lilienda vizuri. (*Makofi/Kicheko*)

Wao Bunge lao kwa sababu hawana hii *official opposition*, Wabunge wote wanakaa kwa *alphabet*, kwa hiyo haijalishi umetoka chama cha upinzani, umetoka chama gani, ni *alphabet*, kwa hiyo kuna hiyo *small difference* na siyo kwamba hawana upinzani kiasi hicho, hapana, wana upinzani kiasi fulani kama nilivyoeleza ambapo Spika anatoka *opposition*, lakini *opposition* yao wao ni ile ya ushindani kwa maana kwamba kama nchi wanakuwa wamekubaliana kwenye haya malengo aliyokuwa anasoma Waziri. Wakishakubaliana kwenye malengo, wanachokubaliana hapa katikati ni namna gani bora ya kufikia yale malengo kwahiylo kwasabbau wanajadiliana, wanabishana hapa katikati kwenye namna bora zaidi ya kufikia yale malengo ndiyo manaa ni ushindani tu, lakini siyo hilyo. Lakini hiyo ni *system* yao kwa historia yao na mazingira yao.

Basi kwa hatua hii kwa sababu leo tuna kazi maalum kuanzia saa 10:00 jioni ya kusikiliza bajeti ya nchi tunahitaji muda wa kujianaa. Naomba itakapofika 10:00 juu ya alama kila mmoja wetu awe amekaa kwenye kiti kwa sababu hotuba itaanza kusomwa *immediately* na kama nilivyo sema itakuwa *live*, haipendezi wapiga kura wako wanaona saa 10:15 wewe ndiyo unaingia humu ndani, ndiyo *camera* inakuonyesha unaingia na kadhalika haipendezi. Saa 10:00 juu ya alama wote tuwe tumekaa na kama nilivyo sema tutakuwa na wageni wengi sana tutawa-*introduce* baadae ili *immediate* tukiingia tumkaribishe Mheshimiwa Waziri aweze kutoa hotuba hii muhimu ambayo inasubiriwa na Taifa zima.

Mwisho niwakumbushe wale ambao mmejiandikisha au mnajjandikisha kuelekea Misri mbaki baada ya kuahirisha shughuli za Bunge hapa mbaki humu humu ndani ili Mheshimiwa Ngeleja na wenzake wawape kidogo picha ya baadhi ya mambo na nitamuomba Mheshimiwa Waziri Mwakyembe pia naye abaki ili kusaidia kupeana picha ya nini kinatakiwa kifanyike ili kufanikisha safari hiyo.

Basi kwa hatua hiyo Waheshimiwa Wabunge naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 10:00 jioni ya leo.

(Saa 5:16 Asubuhi Bunge lilitishwa hadi Saa 10:00 Jioni)

(Saa 10:00 Jioni Bunge Lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge naomba tukae. Waheshimiwa Wabunge mkiona Spika ametokea huko mjue mambo mazito, niwashukuruni sana. (*Makofi/Kicheko*)

Katibu!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

SPIKA: Ahsante sana Katibu. Sasa naomba nimkaribishe Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Mheshimiwa Waziri wa Fedha sasa unaweza kuingia. (*Makofi/Vigegele*)

(Hapa Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt. Philip I. Mpango Alilingia Ukumbini)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, CCM oyeee...

SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge sasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango yupo mbele yetu tayari kutuletea Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Bajeti ya Serikali ya Awamu ya Tano, bajeti ya nne. Mheshimiwa Waziri wa Fedha Dkt. Philip Mpango, karibu sana kutupitisha kwenye bajeti yako. (*Makofi*)

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu lipokee, lijadili na kukubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2019/2020. Hii ni bajeti ya nne ya Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bajeti hii inawasilishwa kwa kuzingatia matakwa ya Ibara ya 137 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ikisomwa pamoja na kifungu cha 26 cha Sheria ya Bajeti namba 11 ya mwaka 2015. (*Makofii/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, hotuba hii inaambatana na vitabu vinne vya bajeti; kitabu cha kwanza ni Makadirio ya Mapato, kitabu cha pili ni Makadirio ya Matumizi ya kawaida kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala wa Serikali, kitabu cha tatu ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kitabu cha nne ni Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, upo Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2019 pamoja na Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Serikali wa mwaka 2019 ambavyo ni sehemu ni bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumuinulia Mungu moyo wangu wote kwa shukurani kwa kuwa amenijalia mema mengi katika maisha yangu na katika utumishi wangu kwa Taifa. Ninamshukuru kwa kuendelea kuijalia nchi yetu amani na umaja na kutupatia safu ya juu ya viongozi wa Taifa hili unaomtanguliza Mungu katika kuwatumikia Watanzania wote na kujielekeza kutatua kero za wanyonge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya shukurani hizo kwa Mwenyezi Mungu naomba nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia ni Amiri Jeshi Mkuu na Mwenyekiti wa CCM Taifa kwa uongozi wake shupavu na wa mfano katika Bara la Afrika hususani katika kufanya maamuzi magumu yenye maslahi mapana kwa

Taifa. Katika kipindi cha uongozi wake amesimamia kwa ujasiri uvunaji adili wa rasilimali za Taifa, ameongoza mapambano dhidi ya rushwa na ujisadi bila kigugumizi, amedhibiti biashara haramu ya madawa ya kulevyo, ameimarisha nidhamu na uwajibikaji katika utumishi wa umma na ameendelea kusikiliza na kushughulikia malalamiko na kero za makundi mbalimbali katika jamii wakiwemo wajasiriamali wadogo, wamachinga na mama na baba lishe, wafayabiashara wadogo wa madini, wakulima na wafugaji na wafanyabiashara wa kati na wakubwa kutoka katika Wilaya zote nchini. Vilevile ameendelea kudumisha amani na usalama katika nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha, amethubutu kutekeleza miradi mikubwa ya kielelezo ili kujenga Tanzania mpya. Nitaeleza hapo baadae mafanikio makubwa ya Serikali ya awamu ya tano katika kuleta mabadillo chanya ya kiuchumi na kijamii nchini. Kwa sasa itoshe tu niseme kuwa yalihitajika maamuzi magumu kutoka kwa Kiongozi jasiri kuelekeza utekelezaji wa mageuzi makubwa na miradi ya kielelezo ambayo yameleta maendeleo makubwa na kuvuita katika miaka hii mitatu na nusu tu. Watanzania tunayo kila sababu ya kumpata Kiongozi shupavu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli mwenye uthubutu na uzalendo wa hali ya juu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo ninapenda kumshukuru kipekee Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini katika dhamana hii kubwa ya Waziri wa Fedha na Mipango na hivyo kuniwezesha kuandaa na kusoma hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali hivi sasa kwa mara ya nne mfululizo. Kwa unyenyekevu ninasema ahsante sana Mheshimiwa Rais kwa heshima hii kubwa uliyonipatia mimi na wananchi wenzangu wa Wilaya ya Buhigwe na Mkoa wa Kigoma kwa ujumla. Ninayasema haya nikitambua kwamba wapo Watanzania wengi wenye sifa ya kuwa Waziri wa Fedha na Mipango, mimi ni nani basi hata nikateuliwa na kukabidhiwa majukumu haya makubwa. Kama alivyonijibu ye ye mwenyewe siku aliponiteua kazi hii nimepewa kwa neema tu kutoka kwa Mungu, hivyo napenda niwaahidi tena

Watanzania kuwa nitaendelea kuifanya kazi hii ya Mungu kwa uadilifu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naamini Watanzania watakulaliana na mimi kuwa nguzo ya uongozi thabiti ni wasaidizi imara na wanaojituma, hivyo kwa namna ya pekee napenda nimpongeze Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa busara na bidii katika kazi zake za kumsaidia Rais kuliongoza Taifa letu. Nimpongeze pia Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuiongoza Zanzibar kwa hekima, hali ambayo imewaletea wananchi wa Zanzibar maendeleo yanayoonekana katika kipindi cha uongozi wake.

Kadhalika napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Rwangwa kwa uongozi hodari ndani ya Serikali na hapa Bungeni pamoja na kumsaidia Mheshimiwa Rais kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa ahadi zilizomo katika llani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Vilevile kwa namna ya pekee sana nimpongeze Dkt. Bashiru Ally Kakurwa, Katibu Mkuu wa CCM kwa utendaji wake uliotukuka na kusimamia misingi ya Chama cha Mapinduzi ya kupigania usawa wa binadamu na haki za wanyonge. (*Makofii/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, niwapongeze pia Wakuu wa mihimili mingine ya dola kwa usimamizi na uongozi shupavu hususani wewe Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Kongwa kwa kuongoza vyema muhimili wa Bunge. Hakuna shaka hata kidogo na kila mtu sasa anajua kwamba Bunge hili ni chombo chenye nguvu sana chini ya Mheshimiwa Spika Job Yustino Ndugai na Naibu Spika Mheshimiwa Dk. Tulia Ackson (Mbunge). Aidha, ninapongeza sana Mheshimiwa Profesa Ibrahim Hamisi Juma Jaji Mkuu wa Tanzania kwa uongozi makini wa muhimili wa Mahakama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Balozi John Kijazi, Katibu Mkuu Kiongozi ambaye pia ni Katibu wa Baraza la Mawaziri na Mkuu wa Utumishi wa Umma kwa kutekeleza kazi zake kwa weledi mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda niwapongeze na kuwashukuru kwa dhati Wakuu wote wa vyombo vyatatu na usalama, makamanda na askari wanaovaa na wasiovaas sare za majeshi kwa utumishi wao kwa umakini na uzalendo wa hali ya juu. Kipekee naomba niwatambue Mkuu wa Majeshi - Jenerali Venance Salvatory Mabeo; Inspeka Jenerali wa Polisi - Simon Nyakoro Sirro; Kamishina Jenerali wa Magereza - Dkt. Faustine Martin Kasike, Kamishina Jenerali wa Uhamiaji - Dkt. Anna Peter Makakara, Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa - Dkt. Modestus Francis Kipilimba; Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa - Kamishina wa Polisi Diwani Athumanu Msuya; Kamishina Jenerali wa Mamlaka ya Kuzuia na Kupamba na Madawa ya Kulevyaa - Rogers William Siang'a na Kamishina Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji - Thobias Andengenye. Hakika Watanzania tunatembea kifua mbele na kutekeleza shughuli mbalimbali ya kijamii na kiuchumi bila wasiwasi kwa sababu vyombo vyetu ya ulinzi na usalama viko macho na imara kuliko chuma. Tunawaombe muendelee kutimiza wajibu wenu wa kulinda mipaka na amani ya nchi yetu kwa vivu na moyo wa kizalendo na hivyo kuzidi kuimarisha mazingira ya kuwasha moto wa maendeleo na ustawi wa Taifa letu na wananchi wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee ninamshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa - Profesa Adelardus Lubango Kilangi kwa kutayarisha kwa wakati Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2019 na Muswada wa Sheria ya Matumizi wa mwaka 2019. Napenda pia nitumie fursa hii kumpongeza kwa dhati Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Jimbo la Kibakwe na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Jimbo la Maswa Magharibi kwa umakini wao

katika kuongoza shughuli za Kamati hii muhimu sana. Chini ya uongozi wao wa Kamati ya Bajeti imetupatia maoni mengi na ushauri wa kujenga ambao umeisadia sana Serikali katika kuboresha mapendekezo ya Bajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi chote ambacho nimekuwa kwenye nafasi hii napenda nishuhudie kwa Bunge hili na Taifa kwa ujumla kwamba Kamati hii ya Bajeti imetoe mchango mkubwa sana katika kuboresha sera za uchumi na bajeti kuliko Watanzania wengi wanavyofahamu. Kusema kweli wanastahili kutambulika kipekee, kama kuna nishani au tuzo ya Spika kwa Kamati ya Bunge inayojitanabaisha kwa utumishi uliotukuka basi kama itakupendeza napendekeza iwe Kamati ya kwanza kutunukiwa heshima hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha, ninawapongeza Wenyevitii, Makamu Wenyevitii na Wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Bunge kwa michango yao waliyoitoa kupita vikao vya Kamati za Kisekta katika kuboresha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara mbalimbali na Serikali kwa ujumla kwa mwaka 2019/2020. Maboresho hayo yalilenga kuwapatia Watanzania maendeleo hususani uboreshaji wa huduma za kijamii na miundombinu.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka 2019/2020 imeandaliiwa kwa kuzingatia dhamira ya Serikali ya Awamu ya tano ya kuwainua wananchi wanyonge kiuchumi na kuboresha mazingira ya kufanya biashara na kuwekeza hapa nchini. Dhima Kuu kama ilivyokubaliwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki bado itaendelea kuwa ni kujenga uchumi wa viwanda utakaochochchea ajira na ustawi endelevu wa jamii. Bajeti hii inaendelea kufungamanisha juhudii za kuimarisha sekta ya viwanda na uendelezaji wa sekta ya kilimo inayoajiri wananchi wengi na hasa waishio vijiji huku msisitizo ukiwa katika kuhamasisha tija na uzalishaji, kujenga miundombinu ya kiuchumi, kutafuta masoko, kupunguza kero kwa wakulima, wafugaji, wavuvi, wafanyabiashara na wawekezaji na kuimarisha huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, leo asubuhi niliwasilisha hotuba ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2019/2020 ambapo nilieleza kwa kina mwenendo wa viashiria mbalimbali nya uchumi katika mwaka 2018. Aidha, katika hotuba hiyo nilifanua juu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2018/2019 na kuainisha maeneo ya vipaumbele kwa mwaka 2019/2020. Hivyo katika hotuba hii nitajielekeza kutoa tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2018/2019 na ahadi zilizomo katika llani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. (*Makofi*)

Pia nitawasilisha maboresho ya mfumo wa viwango nya kodi na tozo mbalimbali pamoja na mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2019/2020, ambayo yanatoa picha ya namna gani Serikali inakusudia kuendelea kukuza uchumi, kuboresha kilimo, milundombinu, huduma na kujenga uchumi wa viwanda ili kuongeza ajira na kuboresha ustawi wa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tathimini ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2018/2019 nikianza na mwenendo wa mapato; katika bajeti ya 2018/2019 Serikali ilitarajia kupata jumla ya shilingi triliuni 32.48 kutoka katika vyano vyote nya ndani na nje. Mchanganuo wa mapato yaliyopatikana hadi Aprili 2019 ikilinganishwa na lengo la kipindi hicho ni kama ifuatavyo:-

- i. Mapato ya kodi yalifikia shilingi triliuni 12.9 sawa na asilimia 87.4 ya lengo.
- ii. Mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi triliuni 2.04 sawa na asilimia 122 ya lengo na mapato yasiyo ya kodi yalivuka lengo kutokana na kuimarika kwa matumizi ya teknolojia katika ukusanyaji wa maduhuli kwenye Taasisi za Serikali kuititia Mfumo wa Kielektroniki wa Serikali wa Ukusanyaji wa Mapato yaani *Government Electronic Payment Get way*;
- iii. Mapato ya halmashauri yalifikia shilingi bilioni 529.25 sawa na asilimia 72 ya lengo;

iv. Misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ilifikia shilingi trilioni 1.70 sawa na asilimia 86 ya lengo;

v. Mikopo ya ndani ikijumuisha mikopo ya kulipia dhamana za Serikali zilizoiva ilifikia shilingi trilioni 3.3 sawa na asilimia 57.4 ya lengo; na

vi. Mikopo ya Masharti ya kibashara ya nje ilifikia shilingi billioni 692.3.

Mheshimiwa Spika, kutofikiwa kwa malengo ya mapato ya kodi kulitokana na sababu mbalimbali zikiwemo ugumu wa kutoza kodi sekta isiyo rasmi, kuendelea kuwepo kwa upotevu wa mapato kunakosababishwa na tatizo la magendo hususani kupitia bandari bubu kwenye mwambao mrefu wa bahari ya Hindi na mwamko mdogo wa wananchi kudai risiti za kielektroniki wanapofanya manunuzi au baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu kutotoa risiti wanapofanya mauzo.

Mheshimiwa Spika, kutopatikana kwa mikopo ya ndani kama ilivyotarajwa kumetokana na kupungua kwa washiriki katika soko la fedha la ndani hususani Mifuko ya Jifadhi ya Jamii iliyouwa kwenye zoezi la kuunganishwa. Kwa upande wa mikopo ya nje ya kibashara upungufu uliojitokeza ultokana na hali ya masoko ya fedha kimataifa kubana zaidi yaani kwa kiingereza *Taiter Global Financial Conditions* hususani kuimarika kwa dola ya Marekani na liba kubwa za mikopo. Hali pia ilipelekea majadiliano na taasisi za fedha za kimataifa kuchukua muda mrefu ili kuhakikisha kuwa Serikali inapata mikopo hiyo kwa gharama zinazoimilika.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa upokeaji wa misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo ulikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo baadhi ya washirika wa maendeleo kutotimiza ahadi zao kama walivyoahidi kwenye bajeti kinyume na misingi ya makubaliano kama ilivyoahidi kwenye mwongozo wa

ushirikiano wa maendeleo Tanzania yaani *Development Cooperation Frame Work*.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa matumizi; bajeti ya mwaka 2018/2019 iliyoidhinishwa na Bunge ilikuwa shilingi triliioni 32.48 ambapo shilingi triliioni 20.47 ni matumizi ya kawaida na shilingi triliioni 12.01 ni matumizi ya maendeleo. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Aprili, 2019 Serikali imetoa jumla ya shilingi triliioni 22.19 zikijumuisha shilingi bilioni 529.25 kutoka kwenye makusanyo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kati ya kiasi hicho, shilingi triliioni 16.75 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambazo zinajumuisha shilingi triliioni 6.28 kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa umma, shilingi triliioni 2.49 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi triliioni 7.98 kwa ajili ya kugharamia deni la Serikali na mahitaji mengine ya Mfuko Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kufikia mwezi Aprili, 2019 Serikali imetoa jumla ya shilingi triliioni 5.44 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo shilingi triliioni 4.89 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 547.38 ni fedha za nje. Hata hivyo, kiasi hiki hakijumuishi baadhi ya fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo zilizopelekwa moja kwa moja kwenye utekelezaji wa miradi yaani *D-Funds*, ambazo hazikupita kwenye mfumo wa malipo wa Serikali. Fedha hizi zitajumuishwa pindi taratibu za kiuhasibu zitakapokamilika mwishoni mwa mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa hadi Aprili, 2019 jumla ya shilingi bilioni 529.25 ambazo zinatokana na makusanyo yao ya ndani zimetumika. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 211.7 zimetumika kugharamia miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 317.55 zimetumika kugharamia matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa maeneo ya kimkakati ambayo yamepatiwa fedha katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Aprili, 2019 ni pamoja na yafuatayo:-

1. Kulipa mishahara ya watumishi kila mwezi kwa wakati ambapo hadi Aprili, 2019 jumla ya shilingi triliuni 6.3 zimelipwa. (*Makofii*)
2. Kuendelea kulipa madeni ya Serikali kwa mujibu wa mikataba ambapo jumla ya shilingi triliuni 5.7 zilitumika, ikijumuisha shilingi triliuni 2.8 kwa ajili ya kulipa mtaji wa deni la ndani kwa utaratibu wa *rollover*.
3. Kugharamia uendeshaji wa ofisi ambapo jumla ya shilingi triliuni 2.2 zimelipwa.
4. Mradi wa kufua umeme utokanao na nguvu za maji katika Mto Rufiji ambapo kiasi cha shilingi bilioni 723.6 kimetolewa. (*Makofii*)
5. Kugharamila elimu msingi bila ada na mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ambapo zimetolewa shilingi bilioni 616.9.
6. Awamu ya Tatu ya Mradi wa Kupeleka Umeme Vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) jumla ya shilingi bilioni 269.3 zimetolewa.
7. Ununuzi na uendeshaji wa ndege mpya ambapo zimetolewa shilingi bilioni 238.8.
8. Kuendeleza ujenzi wa meli mpya katika maziwa makuu, zimetolewa shilingi bilioni 27.6. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ulipaji wa malimbikizo ya madai; Serikali imeendelea kuhakiki na kulipa madeni ya wazabuni, makandarasi na watumishi ambapo hadi Mei, 2019 kiasi cha shilingi bilioni 598.4 kimelipwa kati ya bajeti iliyotengwa ya shilingi bilioni 600.0 kwa mwaka 2018/2019. Kati ya kiasi kilicholipwa shilingi bilioni 300.5 ni kwa ajili ya wakandarasi, shilingi bilioni 232.9 ni kwa ajili ya watoa huduma, shilingi bilioni 65.0 ni kwa ajili ya watumishi. Aidha, Serikali imelipa malimbikizo ya kimshahara ya watumishi 790 waliostaafu

kabla hawajalipwa, ambapo hadi Aprili, 2019 jumla ya shilingi bilioni 3.10 zililipwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kulipa madai yaliyohakikiwa na kuchukua hatua mbalimbali kwa lengo la kupunguza ulimbikizaji wa madai ikiwa ni pamoja na kuhimiza uzingatiaji wa Sheria ya Bajeti namba 11 ya mwaka 2015, Sheria ya Ununzi wa Umma - Sura 410, Sheria ya Fedha za Umma- Sura 348 na Miongozo na Maelekezo mbalimbali yanayotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda nisitisize kuwa japokuwa rasilimali fedha zinazopatikana hazitoshii kugharamia mahitaji yote ya kawaida na miradi ya maendeleo, hakuna shaka kwamba kuititia jitihada tunazofanya hivi sasa, tunapanda mbeguleo ambazo zimeanza na zitaendelea kuzaa matokeo mazuri ya Tanzania ya uchumi wa kati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano katika Kutekeleza Ilani ya CCM 2015; Serikali ya Awamu ya Tano inatekeleza kwa dhati ahadi zake kama zilivyobainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 mpaka mwaka 2020/2021 na vipaumbele vilivyobainishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa ufunguzi rasmi wa Bunge la Kumi na Moja mnamo tarehe 20 Novemba, 2015. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bajeti hii ni ya nne, niruhusu tujikumbushe kwa uchache maeneo ambayo Mheshimiwa Rais aliyawekea mkazo mkubwa mwanzoni mwa utawala wake. Maeneo hayo ni pamoja na; kuendeleza ukuaji wa uchumi na kujenga uchumi wa kipato cha kati, kuongeza mapato na kuimarisha usimamizi wa matumizi ya Serikali, kuendeleza na kuimarisha ujenzi wa miundombinu ya barabara na madaraja, viwanja vya ndege, reli mpya, bandari na umeme, ujenzi wa viwanda, kuongeza kasi ya kuzalisha ajira na kupunguza umaskini, kuhakikisha kwamba madini na maliasili zetu zinatumika kwa manufaa ya Taifa letu, kuboresha sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi, kuongeza

ubora na upatikanaji wa huduma za maji, afya na elimu ikiwa ni pamoa na kuwekea mkazo katika viwango vya ubora wa elimu na stadi za kazi, lakini pia mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi, kuboresha mazingira ya uwekezaji, kuendeleza utalii, kushughulikia migogoro ya ardhi, kurejesha nidhamu katika utumishi wa umma na kuhakikisha kila mmoja wetu anafanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitatu na nusu ya uongozi wa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, mafanikio mengi yamepatikana katika maeneo niliyoyataja hapo juu ikiashiria kwamba llani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 inatekelezwa ipasavyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mionganoni mwa mafanikio ya utekelezaji wa llani ya Uchaguzi ya CCM katika kipindi cha miaka mitatu na nusu ya Serikali ya Awamu ya Tano ni pamoa na yafuatayo:-

Kwanza, ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha standard gauge, ambapo hadi Aprili 2019 ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro, kilometra 300, umefikia asilimia 48.9 na kipande cha Morogoro – Makutupora, kilometra 422, ujenzi umefikia asilimia 7.12. Mradi huu utakapokamilika utaboresha usafiri nchini na kuwezesha usafirishaji wa mizigo, yaani mazao, mifugo, madini na mazao ya misitu, lakini pia abiria kwenda na kutoka nchi jirani zisizo na bahari yaani Uganda, Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na kuiwezesha Tanzania kuwa kitovu cha biashara na huduma yaani *trade and logistics hub* katika nchi za maziwa makuu. Aidha, mradi huu utapunguza uharibifu wa barabara unaotokana na usafirishaji wa mizigo mizito kwa malori, utapunguza msongamano wa shehena ya mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam na kutoa fursa za ajira.

Pili, ufulufuaji wa Shirika la Ndege la Tanzania (*ATCL*) ambapo hadi Aprili, 2019 jumla ya ndege sita mpya zimenunuliwa na kuanza kutoa huduma za usafiri wa anga nchini na zinakwenda Dar es Salaam, Mwanza, Bukoba, Kigoma, Tabora, Dodoma, Iringa, Mbeya, Songea, Mtwara,

Arusha na Mpanda, lakini pia kimataifa Hahaya kule Comoro, Lusaka, Harare, Entebbe na Bujumbura. Aidha, ndege nyingine mpya aina ya *Boeing 787-8 Dreamliner* na *Bombadier Q400* zinatarajiwa kuwasili nchini mwishoni mwa mwaka huu wa 2019. Hivi karibuni, ATCL inatarajiwa kuanza safari kwenda Mumbai, India, Johannesburg, Afrika ya Kusini na Guangzhou, China. Kuimashwa kwa usafiri wa anga kutasaidia sana kukuza biashara na sekta ya utalii nchini. (*Makofii*)

Tatu ni ujenzi wa Jengo la Tatu la abiria (*Terminal III*) na miundombinu yake katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere lenye uwezo wa kuhudumia abiria milioni sita kwa mwaka umekamilika.

Nne ni ujenzi wa barabara kuu na za mikoa kwa kiwango cha lami ikiwemo Daraja la Juu la Mfugale katika makutano ya *TAZARA*, ujenzi wa barabara ya juu yenye ngazi tatu (*Ubungo Interchange*) katika Makutano ya Ubungo, barabara ya njia nane kutoka Kimara Dar es Salaam hadi Kibaha kilometra 19, Daraja la Magufuli katika Mto Kilombero na kuanza ujenzi wa Daraja jipya la Selander Jijini Dar es Salaam ikijumuisha barabara unganishi zenye urefu wa kilometra 5.2.

Tano, ujenzi wa meli mpya za kubeba mizigo na abiria kwenye Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa.

Sita, kukamilika kwa upanuzi wa Gati Namba Moja, kuanza ujenzi wa Gati Namba Mbili na kuendelea na ujenzi wa sakafu ngumu katika gati la kupakua na kupakia magari katika Bandari ya Dar es Salaam. Upanuzi huu utawezesha meli kubwa kuingia na kutoka bandarini kwa ajili ya kushusha na kupakia mizigo.

Saba, ujenzi wa mradi wa kihistoria wa kufua umeme utokanao na nguvu ya maji katika Mto Rufiji wenye uwezo wa kuzalisha megawati 2115 ambapo ujenzi wa miundombinu wezeshi umekamilika na mkandarasi wa kutekeleza ujenzi huo ameshapatikana. Mradi huu

utaiwezesha nchi yetu kuwa na umeme wa uhakika na wa gharama nafuu ambaao ni wa lazima katika jitihada na dhamira yetu kama Taifa ya kujenga uchumi wa viwanda. Mradi huu pia utafungua fursa za utalii, uvuvi na kilimo cha umwagililaji.

Nane, kuendelea na utekelezaji wa mradi kabambe wa kupeleka umeme vijiji (REA) ambapo mpaka Mei, 2019 jumla ya vijiji 7,127 vimeunganishiwa umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, yapo pia mafaniko makubwa yaliyopatikana katika kuongeza ubora na upatikanaji wa huduma za jamii kwa kipindi cha Awamu ya Tano ambayo ni pamoja na yafuatayo:-

Moja, kuendelea na utekelezaji wa ahadi ya kugharamia elimu msingi yaani kuanzia shule za msingi hadi kidato cha nne bila ada na kuongezeka kwa utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. (*Makofii*)

Pili, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya vyuo vikuu ikiwemo kukamilika na kuzinduliwa kwa maktaba ya kimataifa yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,100 kwa wakati mmoja katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (*Makofii*)

Tatu, kuboreshwa kwa huduma za afya katika hospitali za rufaa, mikoa, wilaya, vituo vya afya na zahanati nchini. Aidha, upatikanaji wa dawa, vifaa tiba, vitendanishi na huduma za kibingwa umeimarika, lakini vile vile, idadi ya wagonjwa waliokuwa wanapelekwa kutibiwa nje imepungua na hivyo kuokoa fedha ambazo zingetumika kwa ajili ya matibabu nje ya nchi na nne, kuimarika kwa upatikanaji wa huduma za maji safi mijini na vijiji ambapo katika Jiji la Dar es Salaam umefikia asilimia 85, katika mikoa mingine asilimia 80, miji midogo asilimia 64 na vijiji asilimia 64.8.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine yaliyopatikana katika utawala wa Serikali ya Awamu ya Tano ni yafuatayo:-

Moja, kutengamaa kwa viashiria vya uchumi jumla ikiwemo ukuaaji wa Pato la Taifa kwa wastani wa asilimia 6.9 katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita yaani 2016 mpaka 2018. Kukua kwa sekta ya kilimo kwa wastani wa asilimia 5.3; mfumuko wa bei wa tarakimu moja ya kiwango cha wastani wa asilimia 4.7 katika kipindi hicho; utulivu wa thamani ya shilingi na kupungua kwa kiwango cha umaskini kutoka asilimia 28.2 hadi asilimia 26.4.

Pili, Serikali kuhamia makao makuu ya nchi Dodoma na kuendeleza eneo la Mji wa Serikali kwa kujenga majengo 23 ya Ofisi za Wizara zote na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na miundombinu yake, yaani umeme, maji na barabara.

Mheshimiwa Spika, tatu, kudhibiti utoroshaji na uuzaaji wa madini nje ili kuwezesha Taifa kunufalka na rasillimali zake ikiwa ni pamoja na kufanya marekebisho ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010, kutunga Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusiana na Umiliki wa Maliasili ya mwaka 2017, ujenzi wa uzio kuzunguka eneo la Migodi ya Tanzanite Mirerani na kuanzisha masoko ya madini.

Mheshimiwa Spika, nne, kuanza utekelezaji wa mkakati wa kuharakisha maendeleo ya viwanda nchini, yaani *fast tracking industrialization strategy*. Aidha, sekta binafsi pamoja na mifuko ya hifadhi ya jamii imewekeza kwenye miradi ya viwanda ambapo mifuko hiyo inaendeleza miradi saba kati ya miradi 25.

Tano, mifumo ya kielektroniki ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato kuimarishwa.

Sita, usimamizi wa fedha za Serikali umeimarishwa, ikiwa ni pamoja na kuanzisha kwa Akaunti Jumuifu ya Hazina.

Saba, kuimarishwa kwa taasisi za umma na zile ambazo Serikali ina hisa. Serikali imeendelea kufuatilia na kusimamia kwa karibu zaidi utendaji katika mashirika ya umma ili kuhakikisha kuwa michango na gawio stahiki

inatolewa kwa Serikali. Katika kuimarisha mashirika ya umma na taasisi ambazo Serikali ina hisa, Serikali imepata mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na mashirika mengi ambayo yalikuwa hayatoi gawio na michango stahiki kwa Serikali kuanza kufanya hivyo. Mwaka 2015/2016 kulikuwa na mashirika 13 tu yaliyotoa gawio kwa Serikali kiasi cha shilingi bilioni 119.2 na sasa yameongezeka kufikia mashirika 28 ambayo hadi Mei, 2019 yametoa gawio la jumla ya shilingi bilioni 497.5.

Nane, Serikali imefanya majadiliano yenyе maslahi kwa Taifa na baadhi ya makampuni ikiwemo Kampuni ya *Airtel Tanzania* ambayo yameleta mafanikio yafuatayo:-

- (i) Umiliki wa hisa za Serikali umeongezeka kutoka asilimia 40 hadi asilimia 49 bila kuzilipia;
- (ii) Mwenyekiti wa Bodi na Afisa Mkuu wa Ufundı, yaani *Chief Technical Officer*, wameteuliwa na Serikali;
- (iii) Kampuni imekubali kulipa Serikali shilingi bilioni moja kila mwezi kwa kipindi cha miaka mitano ambapo kiasi cha shilingi bilioni tatu kimeshalipwa kwa kipindi cha mwezi Aprili, Mei na Juni 2019;
- (iv) Lakini pia kupatikana kwa kiasi cha dola za Marekani milioni moja kutoka kwa Mwenyekiti wa *Bharti Airtel* kama sehemu ya uwajibikaji kwa umma yaani *corporate social responsibility* ambazo zimeelekezwa kujenga hospitali mpya ya kisasa Jijini Dodoma;
- (v) Lakini pia kufutwa kwa madeni na madai ya *Bharti Airtel* kwa *Airtel Tanzania* kiasi cha shilingi bilioni 937 yaani sawa na dola milioni 407.38, na Serikali kupata gawio maalum kutoka mapato ghafi ya *Airtel Tanzania* kwa mwaka 2019.

Mheshimiwa Spika, tisa, tumeputa mafanikio katika mapambano dhidi ya rushwa na ujisadi ambapo Ripoti ya Uwazi ya Kimataifa (*Transparency International*) ya mwaka 2018 imeonesha Tanzania imeshika nafasi ya 16 kwa nchi za

Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara ikilinganishwa na nafasi ya 27 mwaka 2015. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa matokeo haya niliyoyaeleza, ni wazi kabisa kuwa Taifa letu linakwenda mbele chini ya Serikali hii ya tano ya CCM na liko katika mwelekeo sahihi (*moving forward in the right direction*). Serikali ya CCM chini ya Jemadari Dkt. John Pombe Joseph Magufuli inawashukuru sana wananchi wote wa Tanzania waliotimiza wajibu wao wa msingi wa kulipa kodi ipasavyo na hivyo kuwezesha Taifa kupata mafanikio hayo makubwa sana katika kipindi kifupi. Wananchi wamejitoa na kuonesha uzalendo wa hali ya juu kwa kushiriki kwenye ujenzi wa Tanzania mpya. Mafanikio haya pia ni matunda mazuri ya kutunza nidhamu katika usimamizi wa uchumi, udhibiti wa mianya ya upotevu wa mapato na matumizi yasiyo na tija ya fedha za umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ninayoiwasilisha mbele ya Bunge lakot itaendelea kutekeleza malengo ya Serikali kama yalivyoanishwa katika llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/2017 mpaka 2020/2021. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sera za bajeti kwa mwaka ujao wa fedha 2019/2020, nikianza na shabaha za uchumi jumla; shabaha za uchumi jumla katika kipindi cha mwaka 2019/2020:-

Mheshimiwa Spika, moja pato la Taifa kukua kwa asilimia 7.1 mwaka 2019 kutoka ukuaji halisi wa asilimia 7.0 mwaka 2018; pili, mfumuko wa bei kuendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja kati ya asilimia 3 hadi 4.5 katika kipindi cha muda wa kati; tatu; mapato ya ndani kufikia asilimia 15.8 ya Pato la Taifa mwaka 2019/2020 kutoka matarajio ya asilimia 14.3 mwaka 2018/2019; nne, mapato ya kodi kufikia asilimia 13.1 ya Pato la Taifa mwaka 2019/2020 kutoka matarajio ya asilimia 12.1 mwaka 2018/2019; tano; matumizi ya Serikali kufikia asilimia 22.7 ya Pato la Taifa mwaka ujao wa fedha kutoka matarajio ya asilimia 21.6 mwaka 2018/2019 na sita,

nakisi ya bajeti inakadiriwa kufikia asilimia 2.3 ya Pato la Taifa mwaka 2019/2020 kutoka matarajio ya asilimia 2.0 mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, Sera na Mikakati ya Kuongeza Mapato. Katika mwaka 2019/2020 Serikali imekusudia kuongeza na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa lengo la kuiwezesha kugharamia shughuli za Serikali ikiwemo miradi mikubwa ya miundombinu na huduma za jamii. Katika kufanikisha azma hii, Serikali itatekeleza sera zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, moja, kuboresha mazingira ya kufanya biashara ili kuvutia uwekezaji, ukuaji wa biashara ndogo na za kati ili kupanua wigo wa kodi na mapato mengine ya Serikali; pili, kurekebisha viwango vya kodi kwa lengo la kuhamasisha uzalishaji na kulinda viwanda vya ndani dhidi ya ushindani kutoka nje na tatu, kuboresha mazingira ya ulipaji kodi kwa hiyari, upanuzi wa wigo wa kodi na matumizi ya TEHAMA katika usimamizi wa kodi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nne, kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi ili kutatua changamoto za ukwepajji kodi na kupunguza upotevu wa mapato pamoja na kuweka mkazo zaidi katika kutoa elimu kwa mlipa kodi; tano, kuimarisha makusanyo yasiyo ya kodi kwa kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA; sita, kuendelea kuianisha na kupunguza tozo na ada mbalimbali zinazotozwa na wakala, taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa na saba, ni kuongezea Mamlaka ya Mapato Tanzania uwezo hususan watumishi, vitendea kazi bora na mafunzo ili kutambua na kudhibiti mbinu za ukwepajji kodi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo ya makadirio ya mapato ya ndani, Serikali imeandaa mikakati mahsus ya kiutawala itakayoteklezwa katika kipindi cha muda wa kati. Mikakati hiyo inajumuisha kuongeza ufanisi katika usimamizi na ukusanyaji wa kodi za ndani kwa kutekeleza mfumo jumuishi wa usimamizi wa mapato ya ndani (*integrated domestic revenue administrative system*) na mbili, ni kupanua wigo wa kodi kuititia utambuzi wa usajili wa walipa kodi

wapya pamoja na kuendelea na zoezi la urasimishaji wa sekta isiyo rasmi.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuwekeza kwenye maeneo ambayo Serikali inaweza kupata mapato zaidi hususan katika uvuvi wa bahari kuu kwa kujenga bandari ya uvuvi na ununuzi wa meli za uvuvi; nne, kuimarisha uwezo wa ufuatiliaji na udhibiti wa uhamishaji wa faida unaofanywa na kampuni za kimataifa na tano, kuimarisha usimamizi wa misamaha ya kodi kwa kuhakikisha inaelekezwa kwenye miradi inayokusudiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sita, kuhakikisha kuwa maduhuli yote yanapitia katika Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (*GePG*) ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato na saba, kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji katika taasisi za Serikali ili kuhakikisha kuwa michango stahiki ya taasisi za umma kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali inawasilishwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa misaada na mikopo nafuu kutoka nje, Serikali itaendelea kuimarisha uhusiano na ushirikiano na washirika wa maendeleo. Aidha, Serikali itaendeleza mazungumzo na washirika wa maendeleo ili kila upande uzingatie misingi na kanuni za ushirikiano wa maendeleo pamoja na kuendeleza majadiliano ya kimkakati (*strategic dialogue*) na kumaliza tofauti za kisera au kimatizamo pindi inapojitekeza, pasipo kuathiri utoaji wa fedha za utekelezaji wa bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo ya kibiashara ya ndani na nje Serikali itaimarisha uhamasishaji wa wadau katika soko la ndani kwa lengo la kuimarisha ushiriki wao katika minada ya dhamana za Serikali. Aidha jitihada zinafanyika ili kuvutia wawekezaji mbalimbali kutoka nje ya nchi wenye nia ya kuikopesha Tanzania ili kuiwezesha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo yenye tija kwa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, sera za matumizi; katika mwaka 2019/2020 Serikali itaendelea kusimamia nidhamu katika matumizi ya fedha za umma na kufanya ufuatililaji na tathmini ya matumizi hususan katika miradi ya maendeleo, lengo kuu ni kuwa na matumizi bora ya fedha katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuhakikisha upatikanaji wa thamani ya fedha. Aidha, Serikali itaendelea kuhakiki, kulipa na kuzuia kuongezeka kwa malimbikizo ya madai kwa Serikali, lakini pia Serikali itaendelea kuelekeza fedha kwenye maeneo ya kipaumbele yenye kuchochcea ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya vipaumbele kwa mwaka 2019/2020; katika hotuba niliyoiwasilisha asubuhi kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2019/2020, niliajishaa vipaumbele kwa mwaka 2019/2020 ambavyo vitatekelezwa kwa kutuzingatia umuhimu wa kipekee wa kulinda mazingira nchini (*environmental sustainability*). Bajeti hii inalenga kutekeleza vipaumbele hivyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni viwanda na kilimo; katika kuendeleza azma ya kujenga uchumi wa viwanda, katika mwaka 2019/2020 Serikali itajikita kuvutia uwekezaji zaidi kwenye viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana nchini kama vile mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, misitu na madini; kuzalisha bidhaa kwa ajili ya soko la ndani na ziada kwa ajili ya kuuza nje pamoja na kuongeza fursa za ajira. Vilevile kama wote tunavyofahamu, sekta ya kilimo yaani mazao, uvuvi, mifugo na misitu ni muhimu sana kwa uendelezaji wa viwanda Tanzania kwa kuwa sehemu kubwa ya malighafi za viwanda zinatokana na kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha sekta hii, Serikali itaendelea kutekeleza programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (*ASDP II*) hususan kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora, pembejeo, huduma za ugani, masoko, miundombinu wezeshi na tafiti ikiwa ni pamoja na kupeleka fedha zaidi kwenye maeneo wezeshi kwa kilimo na kutoa nafuu za kikodi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaendelea kuimarisha bodi za mazao, kuboresha na kuhamasisha uanzishwaji wa vyama vya ushirika vya mazao ili kuvizezesha kupata mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha kwa ajili ya kuwekeza kwenye shughuli mbalimbali za kilimo na uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo vya kuongeza thamani ya mazao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu. Licha ya kutilia mkazo kuongeza ukuaji wa sekta kuu za uchumi zinazotegemewa na kuajiri Watanzania wengi, bajeti ya mwaka 2019/2020 itaelekezwa kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya, elimu na ujuzi, chakula na lishe bora na huduma za majisafi na salama. Aidha, kupitia bajeti hii msukumo utawekwa katika kuongeza ubora wa nguvu kazi ili iendane na mahitaji ya soko la ajira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ni uboreshaji wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji; bajeti hii imeweka msisitizo mkubwa katika kuendeleza ujenzi na ukarabati wa miundombinu hususan reli, bandari, nishati, barabara, madaraja na viwanja vya ndege. Aidha, Serikali itaendelea kupitia na kuimarisha mifumo ya kisera, kisheria na kitaasisi sambamba na kuimarisha ulinzi na usalama ili kushawishi na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje. (*Makofii*)

Napenda niwahakikishie wafanyabiashara, wawekezaji na wananchi kwa ujumla kuwa kuanzia mwaka ujao wa fedha Serikali itaanza kutekeleza kwa nguvu zaidi mpango kazi wa kuboresha mazingira ya biashara (*Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment*) ili mazingira ya biashara nchini kwetu yawe rafiki zaidi na yenye gharama nafuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, eneo la nne la kipaumbele ni ufuatiliaji na tathmini. Bajeti hii pia inakusudia kuimarisha zaidi ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika ngazi zote. Aidha, Serikali itaimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ili kuongeza

ufanisi katika utekelezaji wa bajeti lakini wakati huo huo kuhakikisha kuwa ukusanyaji wa kodi unafanyika bila kuathiri biashara.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwasisitiza tena watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) kwamba hairuhusiwi kufunga biashara ili kushinikiza mfanyakabiashara alipe kodi au malimbikizo ya kodi isipokuwa kwa kibali cha Kamishna Mkuu wa *TRA*. (*Makof*)

Narudia tena, watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) kwamba hairuhusiwi kufunga biashara ili kushinikiza mfanyakabiashara alipe kodi au malimbikizo ya kodi isipokuwa kwa kibali cha Kamishna Mkuu wa *TRA*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, maboresho ya mfumo wa kodi, ada na tozo mbalimbali; napendekeza kufanya marekebisho ya mfumo wa kodi ikiwemo baadhi ya viwango vya kodi na usimamizi wa mapato ya Serikali. Marekebisho haya yamezingatia dhamira ya Serikali ya kuendelea kuwa na mfumo wa kodi ambao ni tulivu na wa kutabirika (*stable and predictable*). Vilevile pamoja na mambo mengine yanalenga kuchochaea kasi ya ukuaji wa uchumi hususan katika Sekta ya Kilimo, viwanda, kukuza ajira na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeanza kutekeleza mpango wa kuboresha mfumo wa udhibiti na biashara (*blueprint*) ulioidhinishwa mwaka 2017/2018 kwa kuanza kuititia mfumo wa tozo na ada mbalimbali zinazotozwa na mamlaka za udhibiti kwa lengo la kupunguza au kuzifuta baadhi ya tozo na ada, kupunguza na kuondoa muingiliano katika kutoza tozo hizo. Marekebisho yanayopendekezwa yanahu sheria zifuatazo:-

- (a) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura 148;
- (b) Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332;
- (c) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura 147;
- (d) Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura 438;
- (e) Sheria ya Usalama Barabarani Sura 168;

- (f) Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004;
- (g) Sheria ya Bajeti Sura 439;
- (h) Marekebisho madogomadogo katika baadhi ya Sheria za Kodi na sheria nyingine mbalimbali;
- (i) Kuanza utekelezaji wa mpango wa kuboresha mfumo wa udhibiti wa biashara kwa kurekebisha ada na tozo mbalimbali;
- (j) Hatua za kisera na kiutawala katika kuboresha ukusanyaji wa mapato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura ya 148; napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura ya 148 kama ifuatavyo:-

Moja, kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye makasha yenye majokofu yanayotumika katika kilimo cha kisasa cha mboga mboga (*horticulture*)kwa wakulima watakaoingiza makasha hayo kutoka nje ya nchi kwa matumizi ya kilimo. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama na kutoa unafuu katika uzalishaji na uhamasishaji wa kilimo cha kisasa cha mboga mboga nchini. (*Makofii*)

Pili, ni kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 68(3)(d) ili kisihushe uuzaaji wa mazao ghafi ya kilimo nje ya nchi. Lengo la hatua hii ni kuwawezesha wauzaji wa mazao ghafi ya kilimonje ya nchi kuendelea kufanya biashara hiyo kwa kadri ya kibali kitakavyotolewa na Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tatu, kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye vifaa vya kukaushia nafaka (*grain drying equipment*). Msamaha huu unatarajiwa kutoa unafuu kwenye gharama za kukausha nafaka kwa ajili ya kuzihifadhi. Aidha, hatua hii itachochea ukuaji wa kilimo chamazao ya nafaka.

Mheshimiwa Spika, nne, kupunguza kiwango cha Kodi ya Ongezeko la Thamani kutoka asilimia18 hadi asilimia sifuri kwenye huduma ya umeme unaouzwa kutoka Tanzania Bara

kwenda Tanzania Zanzibar ili kuwapunguzia gharama za maisha wananchi wa Tanzania Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali iliridhia na kuelekeza kuwa umeme unaouzwa kutoka Tanzania Bara kwenda Tanzania Visiwani utozwe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia sifuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tano, kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwa vilainishi vyta ndege vinavyoagizwa nchini na waendeshaji wa ndani, Shirika la Ndege la Taifa au mashirika ya ndege yanayotambulika katika Mikataba ya Kimataifa ya Huduma za Anga (*Bilateral Air Services Agreements*) kwa kufanya marekebisho ya sehemu ya pili ya jedwali la misamaha ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani katika kipengele cha 11. Hatua hii itawezesha nchi yetu kusaini mikataba ya kimataifa ya huduma za anga ambayo ilishhindikana kusainiwa hapo awali kutokana na kutokuwepo kwa msamaha huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sita, kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye tiketi za ndege, vipeperushi, kalenda, shajara, karatasi zenyet nembo na sare za wafanyakazi zilizowekwa nembo ya shirika husika la ndege kwa kufanya marekebisho ya Sehemu ya Pili ya Jedwali la Misamaha la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kuongeza kipengele kipyaa kinachotoa msamaha pale vinapoingizwa nchini na mashirika ya ndege yanayotambulika katika Mikataba ya Kimataifa ya Huduma za Anga. Hatua hii itawezesha nchi yetu kusaini Mikataba ya Kimataifa ya Huduma za Anga ambayo ilishhindikana kusainiwa hapo awali kutokana na kutokuwepo kwa msamaha huo.

Mheshimiwa Spika, saba, ni kufuta msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani uliokuwa unatolewa kwenye taulo za kike kwa kuwa haujawezesha kupatikana kwa bidhaa hiyo muhimu kwa bei nafuu kwa walengwa na badala yake unawanufaisha wafanyabiashara. Aidha, wakati Serikali ilipoweka msamaha huu ilitarajia kwamba wazalishaji wa

taulo za kike wataziuza kwa bei nafuu baada ya kusamehewa kodi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hatua zote za Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa ujumla wake zinatarajija kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 1,646.7.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tusikilizane, Mheshimiwa Waziri endelea.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 kama ifuatavyo:-

Moja, kupunguza kiwango cha Kodi ya Mapato ya Makampuni (*Corporate Income Tax*) kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato kutoka asilimia 30 hadi asilimia 25 kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia mwaka 2019/2020 hadi mwaka 2020/21 kwa wawekezaji wapya wa viwanda vya kuzalisha taulo za kike. (*Makofii*)

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaingia...

SPIKA: Ndio maana mnapaswa kuwa mnasikiliza Waheshimiwa na mnakuwa watulivu. Eeh hii ni hesabu ya kujumlisha na kutoa. Tumpe nafasi Mheshimiwa Waziri tafadhali, Mheshimiwa Waziri wa Fedha endelea na hotuba hii nzuri.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaingia mkataba wa makubaliano (*Performance Agreement*) na kila mwekezaji ambao utaainisha wajibu wa kila upande. Lengo la hatua hii ni

kuvutia uwekezaji katika uzalishaji wa bidhaa hiyo muhimu, kuongeza ajira na mapato ya Serikali. Vilevile hatua hii itapunguza matumizi ya fedha za kigeni zinazotumika kuagiza bidhaa hiyo kutoka nje na kuhamasisha uzalishaji wake ndani ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, kusamehe kodi ya zuio inayotozwa kwenye gharama zinazoambatana na mikopo kwa mfano ada za bima, gharama ya usimamizi, na uandaaji wa mkopo, na ada nyingine zinazoendana na gharama za mkopo kwa mikopo inayotolewa na benki, taasisi za fedha za nje na wahisani mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Serikali. Lengo la hatua hii ni kuiwezesha Serikali kupata mikopo kwa gharama nafuu na kwa muda mfupi. Aidha, msamaha huu utaiwezesha Serikali kutekeleza miradi yake kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatu, ni kutoa msamaha wa kutengeneza hesabu ambazo zinatakiwa kuwasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa ajili ya ukokotoaji wa kodi ya mapato kutoka kiwango cha sasa cha shilingi milioni 20 hadi shilingi milioni 100. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama kwa mlipa kodi ya kutafuta mtaalam (*Certified Public Accountant*) kwa ajili ya kutengeneza hesabu. Aidha, hatua hii inalenga pia kuchochea ulipaji kodi wa hiari na kuongeza mapato ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nne, kusamehe kodi kwenye mauzo ghafi yasiyozidi shilingi milioni nne kwa wenye vitambulisho vya wajasiriamali na kupunguza kiwango cha chini cha kodi kutoka shilingi 150,000 kwa mwaka hadi shilingi 100,000 kwa mwaka kama ilivyofafanuliwa kwenye Jedwali Na. 1 na Na. 2 kwenye kitabu changu cha hotuba. Lengo la hatua hii ni kupunguza mzigo wa kodi kwa walipakodi wadogo pamoja na kuoanisha viwango vya kodi na kiwango cha chini kinachotakiwa kwa mfanyabiashara kutumia mashine ya kodi ya kielektroniki (*EFD*) ambacho kwa sasa ni shilingi milioni 14. Aidha, hatua hii inalenga pia katika kusisitiza matumizi ya mashine za kielektroniki ili kuwezesha ukokotoaji wa kodi ulio sahihi na kuongeza ulipaji kodi wa hiari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatua hizi za kodi ya mapato kwa ujumla wake zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa shilingi milioni 35,192.5.

Hatua

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147; kwa mujibu wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa kifungu cha 124(2) marekebisho ya viwango maalum vya ushuru wa bidhaa (*specific duty rates*) kwa bidhaa zote zisizo za petroli yanaweza kufanyika kila mwaka ili kuvivianisha na mfumuko wa bei na viashiria vingine vya uchumi jumla. Kwa msingi huo wa sheria, napendekeza kutokufanya mabadiliko ya viwango maalum vya ushuru wa bidhaa kwa bidhaa zote zisizo za petroli. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, narudia, napendekeza kutokufanya mabadiliko ya viwango maalum vya ushuru wa bidhaa kwa bidhaa zote zisizo za petroli. Aidha, hatua hii inazingatia kiwango kidogo cha mfumuko wa bei nchini na azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda, na hivyo kuhamasisha uwekezaji kwenye sekta ya viwanda, kuvilinda na hatimaye kukuza ajira na mchango wa sekta hiyo kwenye pato la Taifa. Hata hivyo, napendekeza kurekebisha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa kwa bidhaa chache tu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kupunguza ushuru wa bidhaa kwenye mvinyo unaotengenezwa kutokana na usindikaji wa matunda kama ndizi, mabibo, rozela/choya, nyanya na kadhalika yanayozalishwa hapa nchini tofauti na zabibu kwa kiwango cha asilimia 75 kutoka shilingi 200 kwa lita hadi shilingi 61 kwa lita ikiwa ni punguzo la shilingi 139 kwa lita.

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kuhamasisha ulipaji wa kodi wa hiari na pia kuvutia uwekezaji kwenye viwanda vidogo vidogo vya aina hii. Aidha, bei ya mvinyo huu kwa lita inafanana na bei ya vinywaji baridi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mbili, kutoza ushuru wa bidhaa wa asilimia 10 kwenye nywele za bandia zinazotengenezwa... (*Makof*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hapo inabidi iongezeke hiyo kodi eeh? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri unaungwa mkono, hebu rudia tena hapo. (*Kicheko*)

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, napendekeza kutoza ushuru wa bidhaa wa asilimia 10 kwenye nywele za bandia zinazotengenezwa ndani ya nchi na asilimia 25 kwenye nywele bandia zinazoagizwa kutoka nje ya nchi. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tatu, ni kusamehe ushuru wa bidhaa...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, tatu...

SPIKA: Waheshimiwa tusikilizane. (*Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Na kucha!

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Wabunge wanasema bado kucha bandia. (*Kicheko*)

Tumpe nafasi Mheshimiwa Waziri asome bajeti, Mheshimiwa endelea.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, tatu ni kusamehe ushuru wa bidhaa kwenye vilainishi vya ndege (*lubricants*) vinavyoingizwa nchini na Shirika la Ndege la Taifa au mashirika ya ndege yanayotambulika katika mikataba ya kimataifa ya huduma za anga na lengo la hatua

hii ni kuiwezesha nchi yetu kusaini mikataba ya kimataifa ya huduma za anga ambayo ilishindikana kusainiwa hapo awali kutokana na kutokuwepo kwa msamaha huo.

Mheshimiwa Spika, nne ni kutoza ushuru wa bidhaa wa asilimia 10 kwenye bidhaa za mabomba na vifaa vya plastiki vinavyotumika kwenye ujenzi wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya maji kwa kuwa hivi sasa kuna viwanda vingi vyenye uwezo wa kuzalisha bidhaa hizo na kutosheleza mahitaji hapa nchini. Hatua hii inahusisha bidhaa za mabomba na plastiki ambazo zinatambuliwa katika *HS Code* 39.17. Lengo la kuanzisha ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa hizo ni kulinda viwanda na kuongeza fursa za ajira na mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, hatua za ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa zisizo za petroli kwa ujumla wake zinatarajiwा kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 2,955.50.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438; napendekeza kuongeza muda wa ziada wa miezi sita hadi Desemba, 2019 kwa walipa kodi waliokubaliwa kulipa kodi wanazodaiwa kwa utaratibu maalum wa kusamehe malimbikizo ya nyuma ya riba na adhabu (*Tax Amnesty on Interest and Penalties*) kwa asilimia 100 kwa kufanya marekebisho ya kifungu cha 70(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015. Hatua hii inapendekezwa kutokana na muitikio mzuri wa walipakodi wakati msamaha huo ulipotolewa mwezi Julai, 2018 ambapo dhamira ya Serikali ilikuwa ni kutoa ahueni kwa walipakodi waliokuwa na malimbikizo makubwa yanayoathiri biashara zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hatua hiyo ya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi inatarajiwা kuongeza mapato ya Serikali kwa shilingi milioni 367,000.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usalama Barabarani, Sura 168; napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168 kama ifuatavyo:-

(i) Kuongeza muda wa Leseni za udereva kutoka miaka mitatu ya sasa hadi miaka mitano; (*Makofii*);

(ii) Kuongeza tozo ya leseni ya udereva kutoka shilingi 40,000 kwenda shilingi 70,000; na (*Makofii*)

(iii) Kuongeza ada ya kadi ya usajili wa magari kutoka shilingi 10,000 hadi shilingi 50,000; pikipiki za matairi matatu kutoka shilingi 10,000 hadi shilingi 30,000 na pikipiki kutoka shilingi 10,000 hadi shilingi 20,000.

Mheshimiwa Spika, lengo la mapendekezo haya ni kupunguza gharama za kuchapisha leseni kwa kipindi cha miaka mitatu kwa kuwa leseni hizo zinaweza kudumu zaidi ya miaka mitano. Hatua hizi kwa pamoja zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 18,147.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004; kikao cha Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki cha Maandalizi ya Bajeti (*Pre-Budget Consultations of Ministers of Finance*) kilichofanyika tarehe 3 Mei, 2019 Mjini Arusha, kilipendekeza kufanya marekebisho ya Viwango vya Ushuru wa Pamoja wa Forodha (*EAC – Common External Tariff – CET*) na Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The EAC Customs Management Act, 2004*) kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Mapendekezo haya yanalenga katika kuendeleza viwanda, kukuza ajira na kuboresha maisha ya wananchi katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Mawaziri wa Fedha ya kufanya marekebisho kwenye Viwango vya Pamoja vya Ushuru wa Forodha yanahusisha hatua mpya na zinazoendelea ambazo zimekuwa zikitekelezwa katika mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya hatua mpya za viwango vya Ushuru wa Forodha ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, (a) kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia sifuri kwenye malighafi ya kutengeneza taulo za watoto (*baby diapers*) zinazotengenezwa hapa nchini kwa mwaka mmoja. Aidha, watakaonufaika na punguzo hili ni viwanda vinavyozalisha bidhaa hizo hapa Tanzania na utaratibu utakaotumika katika kuagiza malighafi hizo ni ule wa kuwapa unafuu wa ushuru wa forodha (*duty remission*). Aidha, Serikali itaendelea kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 kwa taulo za watoto za kutoka nje ya nchi. Hatua hii inatarajiwa kutoa unafuu wa gharama za uzalishaji, ajira na mapato ya Serikali. Aidha, ni matarajio ya Serikali kuwa viwanda vinavyonufaika na msamaha huu wa ushuru wa forodha vitazalisha bidhaa hizi muhimu kwa afya ya watoto na kuziua kwa bei nafuu ili Watanzania wengi waweze kuzinunua.

(b) Kupunguza ushuru wa forodha kutoka kiwango cha asilimia 25 hadi asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwenye vifaa vinavyotumika katika kukata, kung'arisha na kuongeza thamani ya madini ya vito. Hatua hii itawanufaisha wanaofanya shughuli hizo na utaratibu wa *duty remission* ndiyo utatumika katika kuagiza vifaa hivyo. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu wa gharama na kuhamasisha ukataji na usafishaji wa madini hayo hapa nchini na hivyo kuongeza thamani yake kabla ya kuuzwa. Aidha, hatua hii itaongeza mapato ya Serikali na ajira.

(c) Kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwenye makaratasi yanayotumika kama malighafi ya kutengeneza vifungashio vya mboga mboga kwa ajili ya kuuza nje ya nchi. Na utaratibu wa *duty remission* utatumika ambapo viwanda vinavyotengeneza vifungashio hivyo tu ndivyo vitakavyonufaika. Lengo la kuondoa ushuru wa forodha kwenye malighafi hizo ni kupunguza gharama ya utengenezaji wa vifungashio ili kulinda viwanda vya ndani dhidi ya ushindani wa nje, kuvutia uwekezaji katika uzalishaji wa vifungashio vya aina hii na hatimaye kuhamasisha uuza jje wa mboga mboga kwa ajili ya kupata fedha za kigeni.

(d) Kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya mbegu vinavyotumiwa na wazalishaji wa mbegu hapa nchini. Lengo la hatua hii ni kuongeza ubora wa mbegu na pia kuzipa unafuu wa gharama taasisi zinazozalisha mbegu hapa nchini. Aidha, utaratibu wa *duty remission* utatumika katika kuagiza vifungashio hivyo. (*Makof*)

(e) Kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwa utaratibu wa *duty remission* kwenye malighafi (*aluminium alloys*) zinazotumika katika kutengeneza sufuria. Hatua hii inalenga katika kupunguza gharama za uzalishaji, kuhamasisha uzalishaji wa bidhaa hiyo muhimu hapa nchini, kulinda viwanda vya ndani ili viweze kuongeza uzalishaji wa kutosheleza mahitaji na kuongeza ajira.

(f) Kulinda na kuhamasisha uzalishaji wa kahawa hapa nchini pamoja na kuongeza mapato ya Serikali, napendekeza kuongeza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye kahawa inayoagizwa nje ya nchi. (*Makof*)

(g) Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 10 au dola za Kimarekani 125 kwa kila tani moja ya ujazo (*metric ton*) kwenye bidhaa za chuma kwa mwaka mmoja kutegemea na kiwango kipi ni kikubwa badala ya asilimia 10 pekee. Lengo la kuweka viwango hivyo vya ushuru wa forodha ni kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo na kulinda viwanda vya hapa nchini na ajira. (*Makof*)

(h) Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 au dola za Kimarekani 200 kwa kila tani moja ya ujazo kwenye bidhaa za mabati kwa mwaka mmoja kutegemea na kiwango kipi ni kikubwa badala ya asilimia 25 pekee. Hatua hii ina lengo la kulinda viwanda vya ndani kutokana na udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo zinapoingizwa kutoka nje (*under-invoicing and under valuation*) na kulinda ajira na mapato ya Serikali.

(i) Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 10 au dola za Kimarekani 250 kwa kila tani moja ya ujazo kwa mwaka mmoja kutegemea na kiwango kipi ni kikubwa kwenye bidhaa za mabati badala ya kutoza ushuru wa asilimia 10 pekee. Na lengo la hatua hii ni kulinda viwanda nya ndani kutokana na udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo zinapoingizwa kutoka nje na kulinda ajira na mapato ya Serikali.

(j) Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 au dola za Kimarekani 250 kwa kila tani moja ya ujazo kwenye bidhaa za mabati kwa muda wa mwaka mmoja kutegemea na kiwango kipi ni kikubwa badala ya ushuru wa asilimia 25 pekee na bidhaa zinazohusika tumezieleza kwenye kipengele hicho kwa utambuzi wake wa *HS Codes*. Lengo la hatua hiyo ni kuwalinda wazalishaji wa bidhaa hizo hapa nchini kutokana na ushindani wa nje.

(k) Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 au dola za Kimarekani 250 badala ya kiwango cha asilimia 25 au dola za Kimarekani 200 kwa kila tani moja ya ujazo kwenye bidhaa za chuma kwa mwaka mmoja kutegemea na kiwango kipi ni kikubwa kwenye nondo kwa mwaka mmoja na hizi zinahusu *reinforcement bars and hollow profile* na zitahusu bidhaa ambazo zinatambulika katika *HS Codes* ambazo zinasomeka kwenye kitabu cha hotuba na lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha nondo hapa nchini na kuongeza ajira. (*Makofii*)

(l) Kwa kuwa mbogamboga zinalimwa kwa wingi hapa nchini, napendekeza kuongeza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa za mbogamboga (*horticultural products*) zinazoagizwa kutoka nje. Hatua hii itaongeza mapato ya Serikali.

(m) Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa za fito za plastiki zижиликаназо kama *PVC Profiles HS Code 3916.10.00; 3916.20.00 na 3916.90.00* ambazo hutumika

kwa ajili ya kutengenezea fremu za milango, madirisha na kadhalika na lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya kuendelea na utekelezaji wa viwango vya ushuru wa forodha vya mwaka 2018/2019 ni kama ifuatavyo:-

(a) Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 badala ya asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwenye karatasi ambazo zinazalishwa na Kiwanda chetu kule Mufindi.

(b) Kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 35 hadi asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye ngano inayotambulika kwa *HS Code 1001.99.00* na *HS Code 1001.99.90*. Hatua hii imezingatia kwamba uzalishaji wa ngano katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki hautoshelezi mahitaji, na bidhaa hii ni muhimu katika kutengeneza vyakula mbalimbali. Lengo la Serikali ni kuwezesha viwanda na walaji wa vyakula viliviotengenezwa kwa ngano waweze kupata vyakula husika kwa bei nafuu na tulivu. Aidha, utaratibu wa *duty remission* utaendelea kutumika katika kuagiza ngano hiyo ambapo viwanda vinavyotumia ngano ya aina hii katika uzalishaji ndivyo vitahusika katika kutumia kiwango hicho nafuu cha ushuru wa forodha. Kutokana na mahitaji makubwa ya ngano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na SADC, wakati umefika sasa kwa wananchi kuchangamkia fursa ya kulima ngano katika maeneo mbalimbali nchini yanayofaa kwa kilimo cha ngano ikiwemo eneo la shamba la Basuto.

(c) Kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwenye mashine za kielektroniki zinazotumika kukusanya mapato ya Serikali. (*Makofifi*)

(d) Kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa zinazojulikana kama *Printed Aluminium Barrier Laminates*

ambayo hutumika kama malighafi ya kutengeneza dawa ya meno kwenye viwanda vya ndani. (*Makofi*)

(e) Kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwa utaratibu wa *duty remission* kwenye bidhaa ya kutengeneza sabuni ijulikanayo kama *RBD Palm Stearin* (*HS Code 1511.90.40*).

(f) Kutoza kwa mwaka mmoja ushuru wa forodha wa asilimia 25 au dola za Kimarekani 1.35 kwa kilo moja ya viberiti (*safety matches*) vinavyotambuliwa kwenye *HS code 3605.00.00* kutegemea kiwango kipi ni kikubwa.

(g) Kutoza kwa mwaka mmoja ushuru wa forodha wa asilimia 25 au dola za Kimarekani 350 kwa kila tani moja ya ujazo kutegemea kiwango kipi ni kikubwa kwenye bidhaa za chuma za misumari (*nails, tacks, drawing pins, corrugated nails, staples other than those of heading 83.05*).

(h) Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye soseji (*sausages*) na bidhaa za aina hiyo.

(i) Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye chingamu (*chewing gum*) zinazotambuliwa kwa *HS Code 1704.10.00*.

(j) Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 35 badala ya 25 kwa mwaka mmoja kwenye peremende.

(k) Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 35 badala ya 25 kwenye *chocolate* kwa mwaka mmoja.

(l) Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwenye biskuti kwa mwaka mmoja.

(m) Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 35 badala ya 25 kwa mwaka mmoja kwenye nyanya zilizosindikwa (*tomato sauces*) zinazotambuliwa kwenye *HS Code 2103.20.00*.

(n) Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 60 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye maji (*mineral water*).

(o) Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwenye nyama (*meat and edible meat offal*) kwa mwaka mmoja.

(p) Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 25 kwenye mafuta ghafi ya kula mfano alizeti, mawese, soya, mizeituni, nazi, karanga, mahindi na kadhalika kwa mwaka mmoja. Hatua hii inalenga katika kulinda na kuhamasisha uzalishaji wa mbegu za mafuta na mafuta ya kula hapa nchini. Nchi yetu ina fursa kubwa ya kukuza uzalishaji wa bidhaa hiyo. Hivyo, kuna umuhimu wa kuchochaea na kuhamashisha uzalishaji wa mbegu za mafuta na uchakataji wa mafuta ghafi kwa kutumia mbegu zinazosalishwa hapa nchini na lengo la hatua hii ni kuongeza ajira mashambani, viwandani na pia kulinda fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mafuta hayo nje ya nchi.

(q) Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye mafuta ya kula yaliyochakatwa kwa kiwango cha mwisho (*semi-refined, refined/double refined oil*) mfano alizeti, mawese, soya, mizeituni, karanga, nazi, mahindi na kadhalika. Ongezeko la ushuru wa forodha linatarajiwaa kuhamasisha uchakataji wa mbegu za mafuta hapa nchini na kuongeza ajira viwandani na mashambani.

(r) Kutoza ushuru wa forodha wa asilimia 10 badala ya asilimia 0 kwenye *gypsum powder* kwa mwaka mmoja.

(s) Kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 100 hadi asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye sukari ya matumizi ya kawaida (*consumption sugar*) inayoagizwa kutoka nje ya nchi kwa vibali maalum kwa lengo la kuziba pengo (*gap sugar*) la uzalishaji hapa nchini. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani vinavyozalisha sukari, ajira na mapato ya Serikali.

(t) Kutoza kwa mwaka mmoja ushuru wa forodha wa asilimia 35 kwenye mitumba inayoingia kutoka nje (badala ya asilimia 35au dola za Marekani 0.40 kwa kilo moja kutegemea kiwango kipi ni kikubwa);

(u) Kusamehe ushuru wa forodha kwenye malighafi, vipuri na mashine vinavyotumika katika kutengeneza nguo na viatu vya ngozi. Aidha, Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wameridhia orodha iliyooanishwa (*harmonized list*) ya malighafi na vipuri ili kutoa msamaha wa ushuru wa forodha na kuwezesha nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ziweze kufanya biashara kwa bidhaa za nguo na viatu vya ngozi vitakavyozalishwa ndani ya Jumuiya.

(v) Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kutoza ushuru wa mauzo nje (*export levy*) wa asilimia 10 kwenye ngozi iliyosindikwa kwa kiwango cha katii (*wet blue*). Lengo la hatua hii ni kuhamasisha usindikaji wa ngozi, kuongeza thamani, na kuongeza ajira katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri wa Fedha wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walifanya pia marekebisho kwenye Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC Customs Management Act, 2004*) kama ifuatavyo:-

(i) Kufanya marekebisho katika kipengele cha 1(a) Sehemu B ya Jedwali la Tano la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuingiza vilainishi kwa ajili matengenezo ya ndege (*Lubricants for Aircraft*), sare, kalenda, shajara na peni kwenye orodha inayopata msamaha wa ushuru wa forodha kwenye huduma za ndege. Lengo la msamaha huo ni kuiwezesha nchi yetu kusaini mikataba ya Kimataifa ya Huduma za Anga ambayo haikuweza kusainiwa hapo awali kutokana na kutokuwepo kwa msamaha huo.

Hatua hizi za ushuru wa forodha kwa pamoja zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 31,074.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Bajeti, Sura 339; ili kuwezesha utekelezaji wa miradi mikubwa yenyе manufaa kwa Taifa kama vile ujenzi wa miundombinu, ununuzi wa ndege, mabehewa au vichwa vya treni, miradi ya umeme na kadhalika, Serikali inapendekeza kurekebisha Kanuni ya 23 ya Kanuni za Sheria ya Bajeti za mwaka 2015 ili kumpa mamlaka Mlipaji Mkuu wa Serikali kuongeza muda wa matumizi ya fedha za mwaka wa fedha uliomalizika hususan zinazohusu miradi ya maendeleo. Hivi sasa kanuni hii imeweeka ukomo wa miezi mitatu kwa kutumia fedha za mwaka wa fedha uliomalizika ambapo baada ya muda huu wa miezi mitatu kuisha, fedha hizo hupaswa kurejeshwa Mfuko Mkuu wa Serikali. Utaratibu huu kwa sasa wa kurejesha fedha za miradi Mfuko Mkuu wa Serikali baada ya kumalizika kwa muda wa miezi mitatu unaathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutokana na kutokuwepo kwa fedha za kulipia hati za madai hadi hapo mgao mpya wa fedha utakapotolewa kwenye bajeti ya mwaka mpya wa fedha. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, marekebisho madogo madogo katika baadhi ya Sheria za Kodi na Sheria nyingine mbalimbali; napendekeza kufanya marekebisho mengine madogo madogo yasiyo ya kisera katika sheria mbalimbali za kodi pamoja na sheria nyingine ili ziwe sanjari na azma ya kurahisisha utekelezaji wake. Marekebisho hayo yataainishwa katika Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2019 na Matangazo ya Serikali (*Government Notices*).

Mheshimiwa Spika, kuanza utekelezaji wa mpango wa kuboresha mfumo wa udhibiti wa biashara (*blueprint*) kwa kurekebisha ada na tozo mbalimbali. Kufuatia matokeo ya mukutano wa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na wafanyabiashara kutoka Wilaya zote nchini uliofanyika Ikulu, Dar es Salaam tarehe 7 Juni, 2019 Serikali inapendekeza kufuta au kupunguza ada na tozo jumla yake 54 zinazotozwa na Wizara, Idara na taasisi zinazojitegemea ili kuondoa kero na urasimu kwa wafanyabiashara na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi ni sehemu ya kwanza ya utekelezaji wa mpango wa kuboresha mfumo wa udhibiti wa biashara (*Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment*). Aidha, hatua hii imelenga kuondoa muingiliano wa majukumu ya kiutendaji baina ya Wizara, Taasisi na Mamlaka za Udhibiti. Marekebisho hayo yataainishwa katika Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2019 na Matangazo ya Serikali (*Government Notices*). Marekebisho hayo yatajumuisha yafuatayo:-

I. Upande wa Mamlaka ya Dawa (*TFDA*)

(a) Kufuta tozo za Kushikilia usajili wa dawa za chanjo (*Vaccines and Biologicals*) inayotozwa kwa kiasi cha dola za Kimarekani 150; dawa za miti shamba (*Herbal medicines*) inayotozwa kwa kiasi cha dola za Kimarekani 150; vifaa tiba (*medical devices*) inayotozwa kwa kiasi cha dola za Kimarekani 100; vitendanishi (*diagnostics*) zinazotozwa kwa kiasi cha dola za Kimarekani 250; chakula kinachotozwa kwa kiasi cha dola za Kimarekani 100; vipukusi (*antiseptics and diagnostics*) vinavyotozwa kwa kiasi cha shilingi 100,000 na tozo za bidhaa zinazotengenezwa ndani ya nchi (*retention fees for domestic products*);

(b) Kufuta tozo za kudurufu cheti cha usajili wa vitendanishi inayotozwa kwa kiasi cha dola za Kimarekani 100;

(c) Kufuta tozo za ukaguzi wa maduka mapya ya kuuzia vyakula vinayotozwa kwa kiasi cha shilingi 50,000;

(d) Kufuta tozo za usajili wa maduka ya rejareja ya dawa za mifugo kati ya shilingi 50,000/= hadi shilingi 100,000;

(e) Kufuta tozo ya ukaguzi wa viwanda vya samaki nchini iliyokuwa inatozwa kwa kiwango cha kati ya shilingi 200,000 hadi shilingi 250,000;

(f) Kufuta tozo ya ukaguzi wa maduka mapya ya samaki ya shilingi 50,000; na

(g) Kufuta tozo ya leseni ya mwaka ya biashara ya samaki kati ya shilingi 50,000 hadi shilingi 300,000. (*Makofi*)

Lengo la hatua hizi ni kuweka mazingira rafiki ya kibiashara na uwekezaji ili kuchochaea uzingatiaji wa sheria kwa hiari na kuongeza wigo wa wadau wanautumia huduma za *TFDA*. Hatua hii inatarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 2,500.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Viwango Tanzania - *TBS*; napendekeza kufanya marekabisho ya Sheria ya Shirika la Viwango Tanzania kwa:-

(a) Kufuta tozo ya shilingi 50,000/= ya maombi ya alama ya ubora *transport cost and overhead fees*;

(b) Kufuta tozo ya nembo ya ubora (*TBS mark guarantee*) ya asilimia 15 ya tozo ya gharama za mwanzo za ukaguzi wa ubora (*transport costs and overhead fees*);

(c) Kufuta tozo ya dhamana ya cheti cha kutumia nembo ya ubora (*TBS mark licence*). Tozo hii hutozwa kwa kiwango cha asilimia 50 ya gharama za usafirishaji na upimaji wa Sampuli kutoka sokoni na viwandani;

(d) Kufuta tozo ya shilingi 50,000 ya ununuzi wa fomu ya maombi ya bidhaa zinazotoka nje kwa bidhaa zote;

(e) Kufuta tozo ya gharama za ugenzi (*calibration of equipment based on industrial metrology*). Tozo hii hutozwa kulingana na umbali wa sehemu, kwa mfano Dar es Salaam hadi chini ya umbali wa kilometra tano kutoka TBS ni shilling 10,000; umbali wa katni ya kilometra tano hadi saba kutoka TBS ni shilingi 50,000 na umbali wa zaidi ya kilometra saba kutoka TBS ni shilingi 100,000 kwa hizi zote zinafutwa; na

(f) Kufuta tozo ya asilimia 0.2 ya gharama ya mzigo na usafirishaji ya udhibiti wa vipodozi, vifaa tiba ikiwa ni pamoja na mipira ya kiume, mabomba ya sindano (*syringes*), *gloves*, pamba na bendeji, kwa hiyo tozo hii nayo inafutwa.

Lengo la hatua hii ni kupunguza mzigo kwa wafanyabiashara na wazalishaji, kupunguza gharama katika uendeshaji wa vifaa vyta viwandani na kupunguza tozo za kero. Hatua hii inatarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 2,687.4

Aidha, napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Chakula na Dawa (*TFDA*) kwenye eneo la usimamizi wa viwango ambao unajumuisha ubora na usalama wa chakula na vipodozi ili Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) liendelee kusimamia eneo la chakula na vipodozi kwa ujumla kama ilivyokuwa tangu mwaka 1975. Hivyo basi, Shirika la Viwango litachukua jukumu la kuunganisha utaratibu wa usajili wa majengo (*premises registration*), usajili wa bidhaa (*product registration*), udhibiti wa bidhaa (*certification*) na udhibiti wa bidhaa kutoka nje (*import inspection*) kwa ujumla. Mamlaka ya Chakula na Dawa (*TFDA*) itaendelea kusimamia madawa, vifaa tiba na vitendanishi ili kuongeza ufanisi katika eneo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali; napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Majumbani na Viwandani, Sura 182 kwa kufuta tozo zifuatazo:-

- (a) Kufuta tozo ya huduma ya kusitisha kibali cha awali na kutoa kibali kipya inayotozwa kwa kiwango cha dola za Kimarekani 50;
- (b) Kufuta tozo ya huduma ya kubadilisha taarifa za kibali inayotozwa kwa kiwango cha dola za Kimarekani 50;
- (c) Kufuta tozo ya usajili wa kampuni ya Wakala wa Forodha (*Clearing Agent*) inayotozwa kwa kiwango cha dola za Kimarekani 500 kwa kipindi cha usajili;
- (d) Kufuta tozo ya huduma ya kubadilisha taarifa za usajili inayotozwa kwa kiwango cha dola za Kimarekani 100 kila kipindi cha usajili;

(e) Kufuta tozo ya huduma ya ukaguzi wa dharura inayotozwa kwa kiwango cha dola za Kimarekani 300 kwa kila ukaguzi;

(f) Kufuta ada ya kulinda cheti cha usajili (*maintenance fee*) kwa viwanda vya magodoro inayotozwa kwa kiwango cha dola za Kimarekani 1,000 kwa kila mwaka;

(g) Kufuta ada ya kulinda cheti cha usajili kwa viwanda vya rangi inayotozwa kwa kiwango cha dola za Kimarekani 1,000 kwa mwaka;

(h) Kufuta ada ya kulinda cheti cha usajili kwa viwanda vya nguo inayotozwa kwa kiwango cha dola za Kimarekani 1,000 kwa mwaka;

(i) Kufuta ada ya kulinda cheti cha usajili kwa viwanda vya ngozi inayotozwa kwa kiwango cha dola za Kimarekani 1,000 kwa mwaka;

(j) Kufuta ada ya kulinda cheti cha usajili kwa viwanda vya plastiki inayotozwa kwa kiwango cha dola za Kimarekani 1,000 kwa mwaka;

(k) Kufuta ada ya kulinda cheti cha usajili kwa viwanda vinginevyo vikubwa inayotozwa kwa kiwango cha dola za Kimarekani 1,000 kwa mwaka;

(l) Kufuta ada ya kulinda cheti cha usajili kwa viwanda vidogo vidogo inayotozwa kwa kiwango cha dola za Kimarekani 250 kwa mwaka;

(m) Kufuta ada ya kulinda cheti cha usajili kwa wasambazaji wakubwa inayotozwa kwa kiwango cha dola za Kimarekani 1,000 kwa mwaka; na

(n) Kufuta ada ya kulinda cheti cha usajili kwa wasambazaji wa katika inayotozwa kwa kiwango cha dola za Kimarekani 500 kwa mwaka.

Aidha, napendekeza pia kufanya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi na udhibiti wa Kemikali za Majumbani na Viwandani Sura 182, ili kurekebisha viwango vya tozo kama ifuatavyo:-

- (a) Kutoza tozo ya shilingi 40,000 ya usajili wa kemikali kwa kila kemikali kwa kipindi cha usajili badala ya dola za Kimarekani 20;
- (b) Kutoza tozo ya shilingi 200,000 kwa wafanyabiashara wakubwa na shilingi 50,000 kwa wajasiriamali wadogo kwa kila cheti cha usajili (*certificate holder registration*);
- (c) Kutoza tozo ya shilingi 200,000 badala ya dola za Kimarekani 100 kwa wafanya biashara wakubwa na shilingi 50,000 kwa wafanyabiashara wadogo kwa usajili wa eneo la kuhifadhia kemikali (*Premises registration*);
- (d) Kutoza tozo ya shilingi 300,000 kwa siku kwa kila mtu ya kuchambua kemikali chakavu badala ya dola za Kimarekani 300;
- (e) Kutoza tozo ya shilingi 200,000 ya kuainisha au kuidhinisha njia ya kuteketeza kemikali badala ya dola za Kimarekani 500;
- (f) Kutoza tozo ya shilingi 300,000 kwa kila siku kwa kila mtu ya kusimamia kupakia, kusafirisha, kushusha na kuteketeza kemikali chakavu badala ya dola za Kimarekani 300;
- (g) Kutoza tozo ya shilingi 300,000 ya ukaguzi wa maghala na sehemu za kuhifadhia kemikali badala ya dola za Kimarekani 200;
- (h) Kutoza tozo ya shilingi 150,000 kwa kila siku kwa kila mtu kwa tathmini ya njia za Usafirishaji na Ukaguzi wa Dharura (*Transportation Routes Assessment and Emergency Inspection*) badala ya dola za Kimarekani 100;

(i) Kutoza tozo ya shilingi 150,000 kwa siku kwa kila mtu kwa kusindikiza kemikali hatarishi badala ya dola za Kimarekani 100; na

(j) Usafirishaji wa kemikali hatarishi na kemikali zingine ndani na nje ya nchi utatozwa tozo kama ambavyo tumeziainisha kwenye Jedwali Na. 3 kwenye kitabu cha hotuba.

Aidha, ili kutimiza matakwa ya sheria ya kutumia fedha za kitanzania, tozo zote zilizokuwa zinatozwa kwa dola za Kimarekani zitatozwa kwa fedha za Kitanzania isipokuwa kwa shehena za kemikali zinazoenda nje ya nchi (*on-transit*). Lengo la hatua hizi ni kupunguza wingi na ukubwa wa tozo ili kuweka mazingira bora ya biashara nchini. Aidha, mizigo ya kemikali inayopitishwa katika bandari ya Dar es Salaam itaongezeka na hivyo kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, sekta ya mifugo; napendekeza kufuta tozo mbalimbali kwenye sekta ya mifugo kama ifuatavyo:-

(a) Kufuta tozo ya shilingi 5,000 ya vibali vya vyombo vya kusafirisha maziwa chini ya lita 51;

(b) Kufuta tozo ya shilingi 50,000 ya usajili wa vituo vya kukusanya maziwa lita 201 kwa siku;

(c) Kufuta tozo ya shilingi 5,000 ya usajili wa wazalishaji wa maziwa chini ya lita 51 kwa siku;

(d) Kufuta tozo ya shilingi 500,000 ya usajili wa wasambazaji wa pembejeo za maziwa;

(e) Kufuta tozo ya shilingi 15,000 ya usajili wa wafugaji wadogo wa mifugo ya nyama;

(f) Kufuta tozo ya shilingi 50,000 ya usajili wa wafugaji wa kati wa mifugo ya nyama;

- (g) Kufuta tozo ya shilingi 75,000 ya usajili wa wafugaji wakubwa wa mifugo ya nyama;
- (h) Kufuta tozo ya shilingi 20,000 ya usajili wa wasimamizi wa minada ya awali;
- (i) Kufuta tozo ya shilingi 30,000 ya usajili wa wasimamizi wa minada ya upili na mipakani;
- (j) Kufuta tozo ya shilingi 50,000 ya usajili wa minada ya upili na mipakani;
- (k) Kufuta tozo ya shilingi 30,000 ya usajili wa wafanyabiashara wa minada ya awali;
- (l) Kufuta tozo ya shilingi 60,000 ya usajili wa wafanyabiashara wa minada ya upili na mipakani;
- (m) Kufuta tozo ya shilingi 100,000 ya usajili wa wafanyabiashara wa nyama na bidhaa zake nje ya nchi;
- (n) Kufuta tozo ya shilingi 1,000 ya kibali cha kusafirisha kuku nchini (vifaranga 100 kwa siku moja); na
- (o) Kufuta tozo ya shilingi 200 ya kibali cha kusafirisha kuku mkubwa nchini.

Hatua hii inatarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 16,689.8

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii; napendekeza kufuta ada ya leseni ya kufanya biashara ya utalii inayohusisha uwindaji wa kitaalamu (*professional hunting*) iliyokuwa inatozwa kwa dola za Kimarekani 200 (USD 200) kwa raia wa Tanzania na dola za Kimarekani 1000 (USD 1000) kwa raia wa kigeni. Lengo la hatua hii ni kupunguza tozo zinazotozwa katika sekta ya utalii, na kuvutia watalii. Hatua hii inatarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha takribani dola za Kimarekani 80,000.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji; napendekeza kufuta ada ya matumizi ya maji kwa watumiaji wenyе visima nyumbani ambayo... (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufuta ada ya matumizi ya maji kwa watumiaji wenyе visima nyumbani ambayo ilikuwa inatozwa kuanzia shilingi 100,000 na kuendelea kulingana na matumizi ya maji. Lengo la kufuta tozo hiyo ni kupunguza gharama kwa wananchi wanaochimba visima vya maji kwa matumizi binafsi nyumbani na kuwezesha upatikanaji wa maji hayo kwa gharama nafuu. Hata hivyo, ili kudhibiti uchimbaji holela wa visima, itabidi visima hivyo viendelee kusajiliwa na Bodi ya Maji za Mabonde. Hatua hii inatarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 1,961.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaendelea kufanya tathmini ya utekelezaji wa mpango kazi wa Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara (*blueprint*). Lengo ni kuendelea kuweka mazingira bora ya kuvutia uwekezaji, katika kipindi cha muda wa kati na muda mrefu. Hatua hii inatoa fursa kwa wajasiriamali kuanzisha biashara mpya zitakazo ongeza ajira na kukuza uchumi. Kwa kuzingatia kuwa Serikali imewekeza katika kuboresha mazingira ya udhibiti wa mazingira ya biashara kuititia mpango wa *blueprint*. Hivyo basi, ni matarajio na wito wa Serikali kwamba wawekezaji wa ndani na nje watachangamkia fursa hii kwa kuanzisha na kuendeleza uwekezaji mpya ili kukuza faida za biashara na kuweza kulipa kodi stahiki kwa hiari na kuongeza mapato ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatua za kisera na kiutawala katika kuboresha ukusanyaji wa mapato, napendekeza kuweka utaratibu mpya wa kuondoa mizigo bandarini ambapo wananchi wa kawaida wataruhusiwa kutoa mizigo yao bila ya kuwa na ulazima wa kutumia Wakala wa Forodha (*Clearing and Forwarding Agents*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, narudia tena, napendekeza kuweka utaratibu mpya wa kuondoa mizigo bandarini

ambapo wananchi wa kawaida wataruhusisha kutoa mizigo yao bila ya kuwa na ulazima wa kutumia Wakala wa Forodha (*Clearing and Forwarding Agents*). (*Makofi*)

Hata hivyo, utaratibu huu hautahusisha mizigo inayopitishwa hapa nchini kwenda nje ya nchi (*Transit Cargo*). Aidha, Mamlaka ya Mapato Tanzania itaandaa utaratibu wenyewe kueleweka kwa urahisi ili kuwawezesha wananchi kugomboa mizigo yao kwa gharama nafuu zaidi na bila kuchelewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inapendekeza kuchukua hatua mbalimbali za kisera na utawala kwa lengo la kuimarisha na kurahisisha ukusanyaji mapato. Hatua hizo ni pamoja na zifuatazo:-

Moja, ili kuondoa malalamiko ya wafanyabiashara dhidi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, imeamua kuanzisha kitengo huru cha kupokea malalamiko na taarifa za kodi (*Office of Tax Ombudsman*) ambacho kitaratibiwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Aidha, kitengo hiki kitahusisha kupokea na kupitia malalamiko ya taarifa za Kodi zitakazotolewa na walipakodi au watu wenyewe nia njema. Baadhi ya majukumu ya Kitengo hiki ni kama yafuatayo:-

(a) Kupokea malalamiko ya rushwa dhidi ya watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania; (*Makofi*)

(b) Kupokea malalamiko ya ukadiriaji wa kodi na uthamanishaji wa bidhaa usio wa haki wala uhalsia dhidi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania;

(c) Kupokea malalamiko ya matumizi ya nguvu katika ukusanyaji kodi dhidi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania;

(d) Kupokea malalamiko ya ufungaji wa biashara bila kufuata sheria na taratibu dhidi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania; na

(e) Kupokea malalamiko pamoja na kero nyingine zinazofanana na hayo niliyoyataja dhidi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mbili, ili kuongeza ukusanyaji wa mapato ya kodi za ndani, Serikali inakamilisha manunuzi ya mfumo unganishi wa kielektroniki (*Intergrated Domestic Revenue Administration System*) katika kukusanya kodi na mapato yasiyo ya kodi ili kuleta uwazi na ufanisi katika ukusanyaji wa mapato. Pia mfumo huu utarahisisha ulipaji wa kodi na kupunguza rushwa mionganoni mwa watumishi wasio waaminifu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatu kuendelea kusimamia matumizi ya mfumo wa kukusanya kodi wa kielektroniki (*Electronic Fiscal Device Management System*) ambao umefanyiwa maboresho makubwa na kuanza kazi tangu tarehe 1 Juni, 2019 ili kudhibiti na kubaini udanganyifu unaofanywa katika matumizi ya mfumo huo. Aidha, hatua hii itadhibiti uvujaji wa mapato katika urejeshaji wa kodi (*Tax refund*), utoaji wa risiti bandia na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nne, kutokana na wimbi la vijana wengi kujihusisha na michezo ya kubahatisha na kusahau majukumu ya ujenzi wa Taifa, Serikali ikishirikiana na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha imebuni na kutengeneza mfumo maalum ambao utatumika kudhibiti uchezaji wa michezo hii (*responsible gaming*). Pia mfumo huu utatumika kudhibiti udanganyifu ambao unafanywa na waendeshaji wa michezo ya kubahatisha ili Serikali ipate mapato yake halali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tano, kutokana na malalamiko ya walipa kodi kuhusu ukadiriaji wa kodi na uthaminishaji wa bidhaa usio na haki wala uhalisia, Serikali imeiagiza Mamlaka ya Mapato Tanzania kuanzisha dawati la kushughulikia mappingamizi ya makadirio ya kodi ambapo pingamizi za uthamanishaji na utambuzi litashughulikiwa ndani ya masaa 24. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sita, kutoa unafuu wa kutolipa kodi kwa kipindi cha miezi sita kuanzia wakati mfanyakishara au mwekezaji anapopewa Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (*TIN*). Hatua hii inatofautiana na hali ilivyo sasa ambapo mfanyakishara anapopewa *TIN* anaanza kufanyiwa tathmini (*tax assessment*) ya mapato yake ya biashara na kutakiwa kulipa kodi. Hatua hii itawezesha wafanyakishara na wawekezaji wapya kupata muda wa kujiardaa na mahitaji yanayotakiwa katika shughuli wanazofanya na kuondoa usumbufu au dhana ya woga wakati wa kuanzisha biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tarehe ya kuanza kutekeleza hatua mpya za kodi; hatua hizi za kodi zinazopendekezwa zitaanza kutekelezwa tarehe 1 Julai, 2019 isipokuwa pale ilipoelezwa vinginevyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sura ya bajeti kwa mwaka 2019/2020; kwa kuzingatia shabaha, malengo pamoja na sera za bajeti kwa mwaka 2019/2020, sura ya bajeti inaonesha kuwa jumla ya shilingi triliioni 33.11 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika kipindi hicho. Jumla ya mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa shilingi triliioni 23.05, sawa na asilimia 69.6 ya bajeti yote. Kati ya mapato hayo, Serikali inalenga kukusanya mapato ya kodi ya jumla ya shilingi triliioni 19.10 sawa na asilimia 12.9 ya Pato la Taifa. Mapato yasiyo ya kodi kwa mwaka 2019/2020 yanatarajiwa kuwa shilingi triliioni 3.18 na mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri ni shilingi bilioni 765.5.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatarajia kukopa shilingi triliioni 4.96 kutoka soko la ndani; kati ya kiasi hicho, shilingi triliioni 3.46 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva na kiasi cha shilingi bilioni 1.50 sawa na 1% ya Pato la Taifa ni mikopo mipyä kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Kwa lengo la kuongeza kasi katika utekelezaji wa miradi ya miundombinu, Serikali inatarajia kukopa shilingi triliioni 2.32 kutoka soko la nje kwa masharti ya kibashara.

Mheshimiwa Spika, washirika wa maendeleo wanatarajiwa kuchangia shilingi triliuni 2.78 ambayo ni asilimia nane ya bajeti. Misaada na mikopo hii inajumuisha miradi ya maendeleo shilingi triliuni 2.31; mifuko ya pamoja ya kisekta shilingi bilioni 199.5; na misaada na mikopo nafuu ya kibajeti (*General Budget Support-GBS*) shilingi bilioni 272.8.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha Serikali inapanga kutumia jumla ya shilingi triliuni 33.11 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi triliuni 20.86 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwa ni asilimia 63 ya bajeti ikijumuisha shilingi triliuni 9.72 kwa ajili ya ulipaji wa deni la Serikali na shilingi triliuni 7.56 kwa ajili ya mishahara. Aidha, shilingi triliuni 3.58 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ikijumuisha shilingi bilioni 460.5 kwa ajili ya matumizi yatokanayo na vyanzo vya ndani vya Halmashauri. Aidha, kwa mwaka 2019/2020, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2019 na maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya maendeleo yanatarajiwa kuwa shilingi triliuni 12.25, sawa na asilimia 37.0 ya bajeti yote, ambapo kiasi cha Shilingi triliuni 9.74 ni fedha za ndani na shilingi triliuni 2.51 ni fedha za nje. Kati ya fedha za maendeleo zilizotengwa, shilingi triliuni 2.48 ni kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa reli kwa kiwango cha *standard gauge*, shilingi triliuni 1.44 ni kwa ajili ya mradi wa kufua umeme Mto Rufiji, shilingi bilioni 788.8 ni kwa ajili ya mifuko ya reli, maji na REA, shilingi bilioni 450 ni kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, shilingi bilioni 288.5 kwa ajili ya elimu msingi bila ada. Aidha, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 600 kwa ajili ya kulipa madeni yaliyohakikiwa ya watumishi, watoa huduma na makandarasi wa barabara, maji na umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mfumo wa bajeti kama nilivyoeleza, tumeonesha sura ya bajeti kwa mwaka ujao wa fedha kwenye Jedwali A.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; bajeti hii ni nyenzo ya kufikia matarajio ya wananchi wetu. Hivyo, katika kuandaan

bajeti hii Serikali iliwashirikisha wadau mbalimbali wakiwemo, Kamati ya Bunge ya Bajeti, wafanyabiashara, taasisi za umma na binafsi, wananchi wa kawaida, na wataalam wa kodi hususan wale walioshiriki vikao vya kazi vya kikosi kazi cha maboresho ya kodi (*task force and think tank*).

Mheshimiwa Spika, kujadili na kushauri juu ya mapendeleko ya maboresho ya kodi na tozo mbalimbali; baadhi ya wadau walituletea maoni na ushauri kwa maandishi au barua pepe. Nakiri kuwa walitupatia mrejesho ambao umesaidia kuboresha sera na vipaumbele vya nchi yetu kwa mwaka ujao wa fedha na siku zizazo. Napenda kwa niaba ya Serikali kuwashukuru sana kwa michango hiyo mizuri ambayo tumejitahidi kuizingatia. Ni matarajio ya Serikali kwamba wadau hao wataendelea kufanya hivyo katika mchakato wa bajeti zitakazofuata.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka 2019/2020 inahusu kuendeleza juhudini za kujenga msingi wa uchumi wa viwanda ili kupanua fursa za ajira na kuchochlea ukuaji wa uchumi wa Taifa na ustawi endelevu wa jamii na hatimaye kuondokana na umaskini, ujingga na maradhi, hususan bajeti hii imelenga kwanza kuimarisha na kujenga miundombinu ya kisasa ili kuongeza uwezo wa Taifa katika uzalishaji viwandani hasa vile vinavyotumia malighafi zinazopatikana kwa wingi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, lakini pili kujenga mazingira mazuri ya kufanya biashara na uwekezaji kwa kushughulikia changamoto zilizobainishwa katika *blueprint*. Tatu, kuimarisha kilimo husasani uzalishaji wenyewe tija na masoko ya mazao. Kwa kuzingatia umuhimu mkubwa wa sekta hii katika uchumi wa Taifa na nne ni kudumisha amani na usalama katika Taifa na Kujenga misingi ya Taifa kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, safari ya kujenga Tanzania mpya imeiva, lakini haitakuwa rahisi hasa tukizingatia mabadiliko yanayoendelea katika uchumi wa dunia, ushindani mkali wa kibashara, mabadiliko ya haraka ya teknolojia na demografia na changamoto zinazotokana na mabadiliko ya

tabianchi. Hata hivyo, bahati nzuri ni kuwa katika historia ya nchi yetu, Watanzania ni watu jasiri katika mapambano dhidi ya changamoto zinazojitokeza na kila wakati zilipojitokeza tulizishinda kwa kutumia ubunifu na nguvu ya umoja wa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tuko imara zaidi chini ya uongozi shupavu wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Uchumi wetu unaendelea kukua kwa kasi kubwa, ambapo mwaka 2018 ulikua kwa asilimia 7.0 na kiwango cha umaskini wa mahitaji ya msingi kinazidi kupungua kutoka asilimia 28.2 mwaka 2011/2012 hadi asilimia 26.4 mwaka 2017/2018. Naamini pasipo shaka yoyote kwamba kwa umoja wetu, uongozi makini, kufanya kazi kwa bidii na kwa kutumia rasilimali za nchi yetu vizuri, tutaijenga Tanzania mpya, ambayo itakuwa kitovu kikuu cha uchumi yaani *economic hub* katika ukanda wa Afrika Mashariki katika muda usiozidi miongo miwili ijayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninapoelekea mwisho wa hotuba hii, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru washirika wetu wa maendeleo kwa misaada na mikopo nafuu wanayoendelea kutupatia katika kutekeleza miradi na programu mbalimbali za maendeleo nchini. Katika bajeti ya mwaka 2019/2020, washirika wa maendeleo kwa pamoja wanatarajia kuchangia jumla ya shilingi triliioni 2.78. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwatambue kwa kuwataja mmoja mmoja. Nikianza na nchi za Canada, China, Denmark, Finland, India, Ireland, Italia, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Norway, Poland, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Ujeruman, Uingereza na Uswisi. (*Makofi*)

Aidha, zipo taasisi za kimataifa ambazo ni Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*), Benki ya Dunia, *Arab Bank for Economic Development in Africa (BADEA)*, *Global Fund*, *Kuwait Fund*, *Abu Dhabi Fund*, Jumuiya ya Umoja wa Ulaya (*EU*), Benki ya Uwekezaji ya Ulaya, *OPEC Fund*, *Global Environmental Facility*, Shirika la Mapinduzi ya Kijani Afrika (*AGRA*), Mfuko wa kukinga Hatari ya Kimazingira, *Climate*

Development Special Fund, African Legal Support Facility, Dignity, Global Agriculture and Food Security Program na Mashirika ya Umoja wa Mataifa yakiwemo UNICEF, IFAD, UNDP, UNFPA, Shirika la Chakula na Kilimo (FAO) na United Nations Environment Programme (UNEP). (Makof)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutambua uhusiano mzuri tulionao na Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*), ni matarajio yetu kuwa misaada ya kiufundi na fedha zilizoahidiwa na marafiki zetu hawa zitatolewa kwa wakati na kwa kiasi kilichoahidiwa. Na sisi kwa upande wa Serikali tunaahidi kutumia misaada hiyo kama ilivyokusudiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kuwashimiza Waheshimiwa Mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao na taasisi za kimataifa hapa nchini Tanzania waongeze nguvu kukuza biashara kati ya nchi zao na nchi yetu na kuhamasisha wenye mitaji kutoka nchi zao kuja kuwekeza hapa Tanzania. Tanzania ni salama kwa uwekezaji wenye faida kwao na kwetu. Aidha, wafanye jitihada zaidi kuhamasisha watalii kuja kujionea vivutio vya utalii ambavyo ni fahari ya Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano inatambua na kuthamini michango yao katika maendeleo ya Taifa letu ili mradi isiambatane na masharti yanayohatarisha uhuru wa Tanzania (*national sovereignty*) au kwenda kinyume na mila na desturi zetu. Hata pale ambapo Serikali au mihimili mingine imefanya maamuzi ambayo hawakubaliani nayo, ni vema na haki washirika wetu wa maendeleo watupe muda wa kuyatafakari na kujadiliana nao tena kwa staha badala ya kuishinikiza Serikali ibadili uamuzi wake ndipo watoe fedha, jambo ambalo halikubaliki hata kidogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa Watanzania wenzangu, napenda kuwasilitiza tuendelee kushikamana katika kujengwa Tanzania mpya. Tuwe wazalendo na tena tukae macho daima kulinda na kutetea maslahi ya Taifa letu. Tuongeze

bidii kufanya kazi. Enzi za kutegemea wajomba hazipo tena na habari njema ni kuwa tukiamua tunaweza na Serikali ya CCM inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli imethibitisha ukweli huo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Serikali kupongeza mchango mkubwa wa wafanyabiashara na wananchi wote ambao wamelipa kodi kwa mujibu wa sheria. Aidha, napenda kutambua mchango adhimu wa mashirika na taasisi ambazo Serikali ina hisa yaliyotoa gawio au asilimia 15 ya mapato ghafi kuingia katika Mfuko Mkuu wa Hazina. Katika mwaka ujao wa fedha, Serikali inayataka mashirika yote ya umma na taasisi ambazo Serikali ina hisa kuhakikisha kuwa wanatoa gawio au mchango wa asilimia 15 ya mapato ghafi na Msajili wa Hazina asimamie kikamilifu utekelezaji wa maagizo haya ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama mnavyofahamu mwezi Oktoba, 2019 tutafanya uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Serikali kwa upande wake imejipanga kikamilifu katika maandalizi ikijumuisha mahitaji ya kibajeti kwa ajili ya kufanikisha uchaguzi huo. Ninawasihi wananchi wote wenye sifa wajitokeze kutumia haki yao ya msingi ya kupiga kura. Aidha, katika kuchagua viongozi wa ngazi hiyo, tafuteni Watanzania wenye sifa zifuatazo:-

- (i) Awe mchapakazi mwenye kujitoa sadaka kuwatumikia watu, hasa wananchi wa kawaida; (*Makofii*)
- (ii) Awe mwepesi kuona, kusikiliza na kuguswa na shida za wananchi wake. Tena awe jasiri katika kupigania haki za wanyonge na awe na uwezo na ubunifu katika kutatua kero za wananchi hao;
- (iii) Awe muadilifu anayechukia na kupiga vita rushwa na ufisadi kwa vitendo;
- (iv) Anayetambua fursa zilizopo katika eneo lake, kubuni mikakati ya kuwaendeleza wananchi anaowaongoza

na kuwatia watu wake hamasa ya kuthubutu kutumia fursa hizo; (*Makofi*)

(v) Awe mtetezi hodari wa kulinda mazingira na awe mpambanaji hodari dhidi ya athari za mabadiliko ya tabia ya nchi;

(vi) Awe mwenye kutoa abudu nyadhifa, anayetambua kuwa nafasi na vyeo tulivyopewa ni vya muda tu. Thamani halisi ya kiongozi ni kufanya kazi kwa bidii na kuacha kumbukumbu nzuri kwa ustawi wa eneo analoliongoza na Taifa kwa ujumla; (*Makofi*)

(vii) Awe kama mchezaji mzuri wa kiungo katika timu ya ushindi anayetambua kwamba mkono mmoja hauwezi kupiga makofi ya shangwe. (*Makofi*)

(viii) Awe mwenye kutambua kwamba kazi za kiongozi zina maana sana, kwa kuwa zinamuwezesha kubadilisha maisha ya maelfu ya Watanzania na hasa wanyonge kuwa bora zaidi. (*Makofi*)

(ix) Awe na uwezo wa kuwaeleza wananchi kinaganaga kuhusu Serikali yao inawapeleka wapi na wajibu wa kila mmoja ili waendelee kuiunga mkono; na (*Makofi*)

(x) Awe anatoka ndani ya chama cha siasa.... (*Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. MATTAR ALI SALUM: Rejea.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, awe...

MBUNGE FULANI: CCM! CCM! CCM! CCM! CCM!
CCM!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MBUNGE FULANI: CCM! CCM! CCM!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MBUNGE FULANI: Nyamazeni basi!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MBUNGE FULANI: CCM! CCM!

WABUNGE FULANI: *People's power.*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MBUNGE FULANI: CCM! CCM!

WABUNGE FULANI: *People's power.*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tusikilizane, naomba
mtulie. (*Kicheko/Makofi*)

WABUNGE FULANI: *People's power.*

MBUNGE FULANI: CCM! CCM! CCM!

WABUNGE FULANI: *People's power.*

SPIKA: Jamani naomba mtulie. (*Kicheko/Makofi*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MBUNGE FULANI: CCM! CCM!

SPIKA: Basi jamani.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

SPIKA: Basi, basi. (*Kicheko*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MBUNGE FULANI: Kaeni chini.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tusikilizane.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

SPIKA: Tusikilizane, tusikilizane!

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

SPIKA: Tusikilizane, Mheshimiwa hajamaliza hoja yake...

MBUNGE FULANI: *People's.*

WABUNGE FULANI: *Power.*

SPIKA: Najua...

MBUNGE FULANI: CCM Oyeee.

WABUNGE FULANI: CCM hoyeeee.

MBUNGE FULANI: CCM.

SPIKA: Kwa hiyo, inatosha.

MBUNGE FULANI: *Okay... (Kicheko)*

WABUNGE FULANI: CCM hoyeeee.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MBUNGE FULANI: CCM Oyeeee.

SPIKA: Inatosha, inatosha. *(Kicheko)*

MBUNGE FULANI: ...haki za wanyonge.

MBUNGE FULANI: Mbona haipo.

MBUNGE FULANI: CCM Oyeeeeee.

WABUNGE FULANI: Oyeeeeeee.

MBUNGE FULANI: CCM Oyeeee.

MBUNGE FULANI: CCM Oyeeee.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MBUNGE FULANI: CCM.

SPIKA: Inaonesha Oktoba...

MBUNGE FULANI: CCM.

SPIKA: Naomba tusikilizane Waheshimiwa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

SPIKA: Please, please, inatosha inatosha.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

SPIKA: Inatosha Waheshimiwa *please.* (*Makofi/Kicheko/Vigelegele*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Pokeeni basi.

Mheshimiwa Spika,...

SPIKA: Naomba... (*Kicheko*)

Naomba, naomba tuendelee. (*Kicheko*)

Waheshimiwa tulieni, tulieni kidogo.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, sifa ya ...

SPIKA: Hiyo ilikuwa *demo* ya Oktoba yaani kwa hiyo inatosha. (*Kicheko/Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MBUNGE FULANI: *People's*

MBUNGE FULANI: Acheni... (*Kicheko*)

SPIKA: Inatosha Waheshimiwa.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, naomba kurudia sifa ya kumi, awe, awe anatoka...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MBUNGE FULANI: Rudia.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, awe anatoka ndani ya chama cha siasa kinachotetea maslahi na haki za wanyonge na chama hicho ni CCM.

Mheshimiwa Spika, naomba nikiri kwamba sifa hizi nilizozitaja nimeazima kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila ridhaa yake. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, nimeziazima kutoka kwa Mheshimiwa... (*Makofi/Vigelegele*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, Nawaomba Viongozi wote tumuombee mpendwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ili Mwenyezi Mungu aendelee kumjalia afya njema, hekima, busara na kumuongoza kwa kila jambo analolifanya kuliletea Taifa letu maendeleo. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru viongozi wenzangu wa Wizara ya Fedha na Mipango ambao wamekuwa msaada mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika maandalizi na uratibu wa bajeti hii ya Watanzania. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, kipekee ninawashukuru Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji - Naibu Waziri wa Fedha na Mipango ambaye ni Mbunge mahiri wa Jimbo la Kondoa, Katibu Mkuu wa Hazina na Mpapaji Mkuu wa Serikali Bwana Dotto James pamoja na Naibu Makatibu Wakuu Bi. Amina Shabani, Dkt. Khatib Kazungu na Bwana Adolf Ndunguru

pamoja na watumishi wa ngazi zote wa Wizara ya Fedha na Mipango. (*Makofii/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile ninamshukuru Profesa Florence Luoga - Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania pamoja na Naibu Gavana Dkt. Yamungu Kayandabila, Dkt. Bernard Kibese na Bwana Julian Raphael Banzi kwa kusimamia vyema sekta nyeti ya fedha. (*Makofii/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi ya pekee napenda nimpongeze Dkt. Edwin Mhede kwa kuteuliwa na Rais kuwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania na ni matumaini yangu na ya Watanzania kuwa atakuwa chachu ya kujenga taswira mpya ya *TRA* inayoongeza mapato ya Serikali bila manyanyaso kwa wafanyabiashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru viongozi na watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Ofisi ya Msajili wa Hazina na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wakuu wote wa Idara na Vitengo, Taasisi na Wakala za Serikali zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na wafanyakazi wake wote kwa kazi nzuri wanazofanya kuendelea kunipa ushirikiano wa dhati katika kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi wa hali ya juu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru pia wananchi wenzangu wa Wilaya ya Buhigwe na Mkoa wetu wa Kigoma ambao walinilea na kunifundisha kufanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naishukuru familia yangu hususan mke wangu mpenzi na rafiki yangu Mbonimpaye, watoto na wajukuu wetu na leo bahati nzuri yuko mjukuu wetu Anna, Angela, Philipo, lakini pia ndugu jamaa na marafiki zetu wote tuliopewa na Mungu, ahsanteni sana kwa kuniombea msaada kwa Mungu kwa kazi hii, usiku na mchana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nami ninasema kwa kila mmoja wao, Bwana akubarikie na kukulinda, Bwana akuangazie nuru za uso wake na kukufadhili, Bwanaakuinulie nuru ya uso wako na kukupa amani. (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Amina.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, baraka hiyo inatoka kitabu cha Hesabu, Sura ya 6:24 – 26.

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa baraka zake na kuniwezesha kuwasilisha hotuba hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, apende kuendelea kunijalia uwezo na unyenyekevu wa kulitumikia Taifa letu na wananchi wake kwa uadilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa kunisikiliza, Mungu Ibariki Afrika, Mungu Ibariki Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi/Vigelegele*)

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO, MHESHIMIWA
DKT. PHILIP I. MPANGO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI
MAPENDEKEZO YA SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA
MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2019/20 - KAMA
ILIVYOWASILSIHWA MEZANI**

I. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kukubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2019/20. Hii ni bajeti ya nne ya Serikali ya awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bajeti hii inawasilishwa kwa kuzingatia matakwa ya Ibara ya 137 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka

1977, ikisomwa pamoja na kifungu cha 26 cha Sheria ya Bajeti namba 11 ya mwaka 2015.

2. Mheshimiwa Spika, hotuba hii inaambatana na vitabu vinne vya bajeti. Kitabu cha Kwanza ni Makadirio ya Mapato; Kitabu cha Pili ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala wa Serikali; Kitabu cha Tatu ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na Kitabu cha Nne ni Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, upo Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2019 pamoja na Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Serikali wa mwaka 2019 ambavyo ni sehemu ya bajeti hii.

3. Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumuinulia Mungu moyo wangu wote kwa shukrani, kwa kuwa amenijalia mema mengi katika maisha yangu na katika utumishi wangu kwa Taifa. Ninamshukuru kwa kuendelea kujalia nchi yetu amani na umoja na kutupatia safu ya juu ya uongozi wa Taifa hili unaomtanguliza Mungu katika kuwatumikia Watanzania wote na kujielekeza kutatua kero za wanyonge.

4. Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo kwa Mwenyezi Mungu, naomba nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye pia ni Amiri Jeshi Mkuu na Mwenyekiti wa CCM Taifa, kwa uongozi wake shupavu na wa mfano katika bara la Afrika hususan katika kufanya maamuzi magumu yenye maslahi mapana kwa Taifa. Katika kipindi cha uongozi wake: amesimamia kwa ujasiri uvunaji adili wa rasilimali za Taifa; ameongoza mapambano dhidi ya rushwa na ujisadi bila kigugumizi; amedhibiti biashara haramu ya madawa ya kulevyta; ameimarisha nidhamu na uwajibikaji katika utumishi wa umma; na ameendelea kusikiliza na kushughulikia malalamiko na kero za makundi mbalimbali katika jamii, wakiwemo wajasiriamali wadogo (wamachinga na mama/baba lishe), wafanyabiashara wadogo wa madini, wakulima na wafugaji,

na wafanyabiashara wa kati na wakubwa kutoka katika wilaya zote nchini. Vile vile, ameendelea kudumisha amani na usalama katika nchi. Aidha, amethubutu kutekeleza miradi mikubwa ya kielelezo ili kujenga Tanzania mpya. Nitaeleza hapo baadaye mafanikio makubwa ya Serikali ya Awamu ya Tano katika kuleta mabadiiliko chanya ya kiuchumi na kijamii nchini. Kwa sasa itoshe tu niseme kuwa yalihitajika maamuzi magumu kutoka kwa kiongozi jasiri kuelekeza utekelezaji wa mageuzi makubwa na miradi ya kielelezo ambayo yameleta maendeleo makubwa na ya kuvutia katika miaka hii mitatu na nusu tu! Watanzania tunayo kila sababu ya kujivunia kumpata kiongozi shupavu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli mwenye uthubutu na uzalendo wa hali ya juu.

5. Mheshimiwa Spika, pamoja na pongozi hizo, ninapenda kumshukuru kipekee Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini katika dhamana hii kubwa ya Waziri wa Fedha na Mipango na hivyo kuniwezesha kuandaa na kusoma hotuba ya bajeti kuu ya Serikali hivi sasa kwa mara ya nne mfululizo. Kwa unyenyekevu, ninasema asante sana Mheshimiwa Rais kwa heshima hii kubwa uliyonipatia mimi na wananchi wenzangu wa wilaya ya Buhigwe na mkoa wa Kigoma kwa ujumla. Ninayasema haya nikitambua kwamba wapo Watanzania wengi wenye sifa za kuwa Waziri wa Fedha na Mipango. Mimi ni nani basi hata nikateuliwa na kukabidhiwa majukumu haya makubwa? Kama alivyonijibu ye ye mwenyewe siku aliponiteua, kazi hii nimepewa kwa neema tu kutoka kwa Mungu. Hivyo, napenda niwaahidi tena Watanzania kuwa nitaendelea kuifanya kazi hii ya Mungu kwa uadilifu.

6. Mheshimiwa Spika, naamini Watanzania watakubaliana nami kuwa nguzo ya uongozi thabiti ni wasaidizi imara na wanaojituma. Hivyo, kwa namna ya pekee, napenda nimpongeze Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa busara na bidii katika kazi zake za kumsaidia Rais kuongoza Taifa letu. Nimpongeze pia Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Serikali ya

Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuiongoza Zanzibar kwa hekima, hali ambayo imewaletea wananchi wa Zanzibar maendeleo yanayoonekana katika kipindi cha uongozi wake. Kadhalika, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mbunge wa Jimbo la Ruangwa, kwa uongozi hodari ndani ya Serikali na hapa Bungeni pamoja na kumsaidia Rais kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa ahadi zilizomo katika llani ya CCM kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015. Vile vile kwa namna ya pekee sana nimpongeze Dkt. Bashiru Ally Kakurwa, Katibu Mkuu wa CCM kwa utendaji wake uliotukuka na kusimamia misingi ya Chama Cha Mapinduzi ya kupigania usawa wa binadamu na haki za wanyonge.

7. Mheshimiwa Spika, niwapongeze pia wakuu wa mihimili mingine ya dola kwa usimamizi na uongozi shupavu, hususan wewe Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Kongwa kwa kuongoza vema mhimili wa Bunge. Hakuna shaka hata kidogo na kila mtu sasa anajua kwamba Bunge hili ni chombo chenye nguvu sana chini ya Mheshimiwa Spika, Job Ndugai na Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb). Aidha, ninampongeza sana Mheshimiwa Profesa Ibrahim Hamisi Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania kwa uongozi makini wa mhimili wa Mahakama.

8. Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Balozi John Kijazi, Katibu Mkuu Kiongozi ambaye pia ni Katibu wa Baraza la Mawaziri na Mkuu wa Utumishi wa Umma, kwa kutekeleza kazi zake kwa weledi mkubwa.

9. Mheshimiwa Spika, napenda niwapongeze na kuwashukuru kwa dhati wakuu wote wa vyombo vyatofauti na usalama, makamanda na askari wote (wanaovaa na wasiovaa sare za majeshi) kwa utumishi wao makini na uzalendo wa hali ya juu. Kipekee naomba niwatambue Mkuu wa Majeshi, Jenerali Venance Salvatory Mabeyo; Inspekta Jenerali wa Polisi, Simon Nyakoro Sirro; Kamishna Jenerali wa Magereza, Dkt. Faustine Martin Kasike; Kamishna Jenerali wa

Uhamiaji, Dkt. Anna Peter Makakala; Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa, Dkt. Modestus Francis Kipilimba; Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Kamishna wa Polisi, Diwani Athuman Msuya; Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Madawa ya Kulevy, Rogers William Siang'a; na Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji, Thobias Andengenye. Hakika, Watanzania tunatembea kifua mbele na kutekeleza shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi bila wasiwasi kwa sababu vyombo vyetu nya ulinzi na usalama viko macho na imara kuliko chuma! Tunawaomba muendelee kutimiza wajibu wenu wa kulinda mipaka na amani ya nchi yetu kwa vivu na moyo wa kizalendo na hivyo kuzidi kuimarisha mazingira ya kuwasha moto wa maendeleo na ustawi wa Taifa letu na wananchi wake.

10. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee ninamshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Profesa Adelardus Lubango Kilangi kwa kutayarisha kwa wakati Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2019 na Muswada wa Sheria ya Matumizi wa mwaka 2019. Napenda pia nitumie fursa hii kumpongeza kwa dhati mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Jimbo la Kibakwe, na Makamu wake Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Jimbo la Maswa Magharibi, kwa umakini wao katika kuongoza shughuli za Kamati hii muhimu sana. Chini ya uongozi wao, Kamati ya Bajeti imetupatia maoni mengi na ushauri wa kujenga ambao umeisadnia sana Serikali katika kuboresha mapendekezo ya bajeti hii.

11. Mheshimiwa Spika, kwa kipindi chote ambacho nimekuwa kwenye nafasi hii, napenda nishuhudie kwa Bunge hili na Taifa kwa ujumla kwamba, Kamati hii ya Bajeti imetoa mchango mkubwa sana katika kuboresha sera za uchumi na bajeti kuliko Watanzania wengi wanavyofahamu. Kusema kweli wanastahili kutambulika kipekee. Kama kuna nishani au tuzo ya Spika kwa Kamati ya Bunge inayojitanabaisha kwa utumishi uliotukuka, basi kama itakupendeza Mheshimiwa Spika, napendekeza iwe Kamati ya kwanza kutunukiwa

heshma hiyo. Aidha, ninawapongeza Wenyeviti, Makamu wenyeviti na wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Bunge kwa michango yao wallyoitoa kupitia vikao vya kamati za kisekta katika kuboresha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara mbalimbali na Serikali kwa ujumla kwa mwaka 2019/20. Maboresho hayo yalilenga kuwapatia Watanzania maendeleo hususan uboreshaji wa huduma za kijamii na miundombinu.

12. Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka 2019/20 imeandaliwa kwa kuzingatia dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuainua wananchi wanyonge kiuchumi na kuboresha mazingira ya kufanya biashara na kuwekeza hapa nchini. Dhima kuu kama ilivyokubaliwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki bado itaendelea kuwa *"kujenga uchumi wa viwanda utakaочоchea ajira na ustawi endelevu wa jamii"*. Bajeti hili inaendelea kufungamanisha juhudzi za kuimarisha sekta ya viwanda na uendelezaji wa sekta ya kilimo inayoajiri wananchi wengi na hasa waishio vijiji huku msisitizo ukiwa katika kuhamasisha tija na uzalishaji, kujenga miundombinu ya kiuchumi, kutafuta masoko, kupunguza kero kwa wakulima, wafugaji, wavuvi, wafanyabiashara na wawekezaji na kuimarisha huduma za jamii.

13. Mheshimiwa Spika, leo asubuhi niliwasilisha Hotuba ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2019/20 ambapo nilieleza kwa kina mwenendo wa viashiria mbalimbali vya uchumi katika mwaka 2018. Aidha, katika hotuba hiyo, nilifafanua juu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2018/19 na kuainisha maeneo ya vipaumbele kwa mwaka 2019/20. Hivyo, katika hotuba hii, nitajielekeza kutoa tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2018/19 na ahadi zilizomo katika Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, kuwasilisha maboresho ya mfumo na viwango vya kodi na tozo mbalimbali, pamoja na mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2019/20, ambayo yanatoa picha ya namna gani Serikali inakusudia kuendelea kukuza uchumi, kuboresha kilimo, miundombinu, huduma na

kujenga uchumi wa viwanda ili kuongeza ajira na kuboresha ustawi wa Watanzania.

II. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2018/19

Mwenendo wa Mapato

14. Mheshimiwa Spika, Katika bajeti ya mwaka 2018/19, Serikali ilitarajia kupata jumla ya shilingi trillioni 32.48 kutoka katika vyanzo vyote vya ndani na nje. Mchanganuo wa mapato yaliyopatikana hadi Aprili 2019 ikilinganishwa na lengo la kipindi hicho ni kama ifuatavyo:

i. Mapato ya kodi yalifikia shilingi trillioni 12.9, sawa na asilimia 87.4 ya lengo;

ii. Mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi trillioni 2.04, sawa na asilimia 122 ya lengo. Mapato yasiyo ya kodi yalivuka lengo kutokana na kuimarika kwa matumizi ya teknolojia katika ukusanyaji wa maduhuli kwenye taasisi za Serikali kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Serikali wa Ukusanyaji wa Mapato (Government electronic Payment Gateway -GePG);

iii. Mapato ya Halmashauri yalifikia shilingi bilioni 529.25, sawa na asilimia 72 ya lengo;

iv. Misaada na Mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ilifikia shilingi trillioni 1.70 sawa na asilimia 86 ya lengo;

v. Mikopo ya ndani ikijumuisha mikopo ya kulipia dhamana za Serikali zilizoiva ilifikia shilingi trillioni 3.3, sawa na asilimia 57.4 ya lengo; na

vi. Mikopo ya masharti ya kibiashara ya nje ilifikia shilingi bilioni 692.3.

15. Mheshimiwa Spika, kutofikiwa kwa malengo ya mapato ya kodi kulitokana na sababu mbalimbali, zikiwemo;

ugumu wa kutoza kodi sekta isiyo rasmi; kuendelea kuwepo kwa upotevu wa mapato kunakosababishwa na tatizo la magendo hususan kupitia bandari bubu kwenye mwambao mrefu wa Bahari ya Hindi; na mwamko mdogo wa wananchi kudai risiti za kielektroniki wanapofanya manunuzi au baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu kutotoa risiti wanapofanya mauzo.

16. Mheshimiwa Spika, kutopatikana kwa mikopo ya ndani kama ilivyotarajiwa kumetokana na kupungua kwa washiriki katika soko la fedha la ndani hususan mifuko ya hifadhi ya jamii iliyokuwa kwenye zoezi la kuunganishwa. Kwa upande wa mikopo ya nje ya kibiashara, upungufu uliojiteze ilitokana na hali ya masoko ya fedha kimataifa kubana zaidi (tighter global financial conditions) hususan kuimarika kwa dola ya Marekani, na riba kubwa za mikopo. Hali hii pia ilipelekea majadiliano na taasisi za fedha za Kimataifa kuchukua muda mrefu ili kuhakikisha kuwa Serikali inapata mikopo hiyo kwa gharama zinazohimilika.

17. Mheshimiwa Spika, mwenendo wa upokeaji wa misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ulikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo baadhi ya Washirika wa Maendeleo kutotimiza ahadi zao kama walivyoahidi kwenye bajeti kinyume na misingi ya makubaliano kama ilivyoainishwa kwenye Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo Tanzania (Development Coperation Framework – DCF).

Mwenendo wa Matumizi

18. Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka 2018/19 iliyoidhinishwa na Bunge ilikuwa shilingi triliuni 32.48 ambapo shilingi triliuni 20.47 ni matumizi ya kawaida na shilingi triliuni 12.01 ni matumizi ya maendeleo. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Aprili 2019, Serikali imetoa jumla ya shilingi triliuni 22.19 zikijumuisha shilingi billioni 529.25 kutoka kwenye makusanyo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kati ya kiasi hicho, shilingi triliuni 16.75 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambazo zinajumuisha shilingi triliuni 6.28 kwa ajili ya mishahara ya

watumishi wa umma, shilingi triliioni 2.49 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi triliioni 7.98 kwa ajili ya kugharamia deni la Serikali na mahitaji mengine ya Mfuko Mkuu.

19. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili 2019 Serikali imetoa jumla ya shilingi triliioni 5.44 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo shilingi triliioni 4.89 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 547.38 ni fedha za nje. Hata hivyo, kiasi hiki hakijumuishi baadhi ya fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zilizopelekwa moja kwa moja kwenye utekelezaji wa miradi (D-Funds) ambazo hazikupita kwenye mfumo wa malipo wa Serikali. Fedha hizi zitajumuishwa pindi taratibu za kiuhasibu zitakapokamiliika mwishoni mwa mwaka wa fedha.

20. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mtaa hadi kufikia Aprili 2019 jumla ya shilingi bilioni 529.25 ambazo zinatokana na makusanyo yao ya ndani zimetumika. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 211.7 zimetumika kugharamia miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 317.55 zimetumika kugharamia matumizi ya kawaida.

21. Mheshimiwa Spika, mionganini mwa maeneo ya kimkakati ambayo yamepatiwa fedha katika kipindi cha Julai 2018 hadi Aprili 2019 ni pamoja na:

i. Kulipa mishahara ya watumishi kila mwezi kwa wakati ambapo hadi Aprili 2019 jumla ya shilingi triliioni 6.3 zimelipwa;

ii. Kuendelea kulipa madeni ya Serikali kwa mujibu wa mikataba ambapo jumla ya shilingi triliioni 5.7 zilitumika, ikijumuisha shilingi triliioni 2.8 kwa ajili ya kulipa mtaji wa deni la ndani kwa utaratibu wa "rollover".

iii. Kugharamia uendeshaji wa ofisi ambapo jumla ya shilingi triliioni 2.2 zimelipwa;

iv. Mradi wa kufua umeme utokanao na nguvu za maji katika Mto Rufiji ambapo kiasi cha shilingi bilioni 723.6 kimetolewa;

v. Kugharamia elimu msingi bila ada na mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, ambapo zimetolewa shilingi bilioni 616.9;

vi. Awamu ya Tatu ya Mradi wa Kupeleka Umeme Vijijini kuititia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) jumla ya shilingi bilioni 269.3 zimetolewa;

vii. Ununuzi na uendeshaji wa ndege mpya ambapo zimetolewa shilingi bilioni 238.8; na

viii. Kuendeleza ujenzi wa meli mpya katika maziwa makuu, zimetolewa shilingi bilioni 27.6.

Ulipaji wa Malimbikizo ya Madai

22. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhakiki na kulipa madeni ya wazabuni, makandarasi na watumishi ambapo hadi Mei 2019 kiasi cha shilingi bilioni 598.4 kimelipwa kati ya bajeti iliyotengwa ya shilingi bilioni 600.0 kwa mwaka 2018/19. Kati ya kiasi kilicholipwa shilingi bilioni 300.5 ni kwa ajili ya wakandarasi, shilingi bilioni 232.9 ni kwa ajili ya watoa huduma, na shilingi bilioni 65.0 ni kwa ajili ya watumishi. Aidha, Serikali imelipa malimbikizo ya kimshahara ya watumishi 790 waliostaafu kabla hawajalipwa, ambapo hadi Aprili, 2019 jumla shilingi bilioni 3.10 zililipwa.

23. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kulipa madai yaliyohakikiwa na kuchukua hatua mbalimbali kwa lengo la kupunguza ulimbikizaji wa madai ikiwa ni pamoja na kuhimiza uzingatiaji wa Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015; Sheria ya Ununuzi wa Umma SURA 410; Sheria ya Fedha za Umma SURA 348 na miongozo na maelekezo mbalimbali yanayotolewa na Serikali.

24. Mheshimiwa Spika, napenda nisitisize kuwa japokuwa rasilimali fedha zinazopatikana hazitoshi kugharamia mahitaji yote ya kawaida na miradi ya maendeleo, hakuna shaka kwamba kuititia jitihada tunazofanya hivi sasa, tunapanda

mbegu leo ambazo zimeanza na zitaendelea kuzaa matokeo mazuri ya Tanzania ya uchumi wa kati.

Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano katika Kutekeleza Ilani ya CCM 2015

25. Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano inatekeleza kwa dhati ahadi zake kama zilivyobainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17-2020/21 na vipaumbele vilivyobainishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa ufunguzi rasmi wa Bunge la 11 mnamo tarehe 20/11/2015.

26. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bajeti hii ni ya nne, niruhusu tujikumbushe kwa uchache maeneo ambayo Mheshimiwa Rais aliyawekea mkazo mkubwa mwanzoni mwa utawala wake. Maeneo hayo ni pamoja na: kuendeleza ukuaji wa uchumi na kujenga uchumi wa kipato cha kati; kuongeza mapato na kuimarisha usimamizi wa matumizi ya Serikali; kuendeleza na kuimarisha ujenzi wa miundombinu ya barabara na madaraja, viwanja vya ndege, reli mpya, bandari na umeme; ujenzi wa viwanda; kuongeza kasi ya kuzalisha ajira na kupunguza umaskini; kuhakikisha kwamba madini na maliasili zetu zinatumika kwa manufaa ya Taifa letu; kuboresha sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi; kuongeza ubora na upatikanaji wa huduma za maji, afya na elimu (ikiwa ni pamoja na kuweka mkazo katika viwango vya ubora wa elimu na stadi za kazi); mapambano dhidi ya rushwa na ujisadi; kuboresha mazingira ya uwekezaji; Kuendeleza utalii; kushughulikia migogoro ya ardhi; kurejesha nidhamu katika utumishi wa umma; na kuhakikisha kila mmoja wetu anafanya kazi.

27. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitatu na nusu ya uongozi wa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, mafanikio mengi yamepatikana katika maeneo niliyoyataja hapo juu, ikiashiria kwamba Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 inatekelezwa ipasavyo.

28. Mheshimiwa Spika, miongoni mwa mafanikio ya utekelezaji wa llani ya Uchaguzi ya CCM katika kipindi cha miaka mitatu na nusu ya Serikali ya Awamu ya Tano ni pamoja na:

- i. Ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*, ambapo hadi Aprili 2019 ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (km 300) umefikia asilimia 48.9 na kipande cha Morogoro – Makutupora (km 422), ujenzi umefikia asilimia 7.12. Mradi huu utakapokamilika utaboresha usafiri nchini na kuwezesha usafirishaji wa mizigo (mazao, mifugo, madini, mazao ya misitu) na abiria kwenda na kutoka nchi jirani zisizo na bahari (Uganda, Rwanda, Burundi, DRC) na kuiwezesha Tanzania kuwa kitovu cha biashara na huduma (trade and logistics hub) katika nchi za maziwa makuu. Aidha, mradi huu utapunguza uharibifu wa barabara unaotokana na usafirishaji wa mizigo mizito kwa malori, utapunguza msongamano wa shehena ya mizigo katika bandari ya Dar es Salaam na kutoa fursa za ajira;
- ii. Ufufuaji wa Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) ambapo hadi Aprili 2019 jumla ya ndege sita mpya zimenunuliwa na kuanza kutoa huduma za usafiri wa anga nchini (Dar es Salaam, Mwanza, Bukoba, Kigoma, Tabora, Dodoma, Iringa, Mbeya, Songea, Mtwara, Arusha, Mpanda) na Kimataifa (Hahaya – Comoro, Lusaka, Harare, Entebbe, Bujumbura). Aidha, ndege nyingine mpya aina ya Boeing 787-8 Dreamliner na Bombardier Q400 zinatarajiwa kuwasili nchini mwishoni mwa mwaka 2019. Hivi karibuni, ATCL inatarajiwa kuanza safari kwenda Mumbai (India), Johannesburg (Afrika Kusini) na Guangzhou (China). Kuimariswa kwa usafiri wa anga kutasaidia sana kukuza biashara na sekta ya utalii nchini;
- iii. Ujenzi wa jengo la tatu la abiria (Terminal III) na miundombinu yake katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere lenye uwezo wa kuhudumia abiria milioni sita kwa mwaka umekamilika;
- iv. Ujenzi wa barabara kuu na za mikoa kwa kiwango cha lami, ikiwemo daraja la juu la Mfugale katika makutano ya

TAZARA; ujenzi wa barabara ya juu yenye ngazi tatu (ubungo interchange) katika makutano ya Ubungo; barabara ya njia nane kutoka Kimara Dar es Salaam hadi Kibaha (km 19); daraja la Magufuli katika mto Kilombero; na kuanza ujenzi wa daraja jipya la Selander jjini Dar es Salaam ikijumuisha barabara unganishi zenyte urefu wa kilomita 5.2;

v. Ujenzi wa meli mpya za kubeba mizigo na abiria kwenye Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa;

vi. Kukamilika kwa upanuzi wa gati namba moja, kuanza ujenzi wa gati namba mbili, na kuendelea na ujenzi wa sakafu ngumu katika gati la kupakua na kupakia magari katika bandari ya Dar es Salaam. Upanuzi huu utawezesha meli kubwa kuingia na kutoka bandarini kwa ajili ya kushusha na kupakia mizigo;

vii. Ujenzi wa mradi wa kihistoria wa kufua umeme utokanao na nguvu ya maji katika Mto Rufiji wenye uwezo wa kuzalisha MW 2,115 ambapo ujenzi wa miundombinu wezeshi imekamilika na mkandarasi wa kutekeleza ujenzi huo ameshapatikana. Mradi huu utaiwezesha nchi yetu kuwa na umeme wa uhakika na wa gharama nafuu ambaao ni wa lazima katika jitihada na dhamira yetu kama Taifa ya kujenga uchumi wa viwanda. Mradi huu pia utafungua fursa za utalii, uvuvi na kilimo cha umwagiliaji; na

viii. Kuendelea na utekelezaji wa Mradi Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijiji (REA) ambapo hadi Mei 2019, jumla ya vijiji 7,127 vimeunganishiwa umeme.

29. Mheshimiwa Spika, yapo pia mafaniko makubwa yaliyopatikana katika kuongeza ubora na upatikanaji wa huduma za jamii kwa kipindi cha Awamu ya Tano ambayo ni pamoja na;

i. Kuendelea na utekelezaji wa ahadi ya kugharamia elimu msingi (kuanzia shule ya msingi hadi kidato cha nne) bila ada na kuongezeka kwa utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu;

- ii. Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya vuyo vikuu ikiwemo kukamilika na kuzinduliwa kwa maktaba ya kimataifa yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,100 kwa wakati mmoja katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;
- iii. Kuboreshwa kwa huduma za afya katika hospitali za rufaa, mikoa, wilaya, vituo vya afya na zahanati nchini. Aidha, upatikanaji wa dawa, vifaa tiba, vitendanishi na huduma za kibingwa umeimarika. Vile vile, idadi ya wagonjwa waliokuwa wanapelekwa kutibiwa nje imepungua na hivyo kuokoa fedha ambazo zingetumika kwa ajili ya matibabu nje ya nchi; na
- iv. Kuimarka kwa upatikanaji wa huduma za maji safi mijini na vijiji ambapo katika Jiji la Dar es Salaam umefikia asilimia 85, katika mikoa mingine asilimia 80, miji midogo asilimia 64 na vijiji asilimia 64.8.

30. Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine yaliyopatikana katika utawala wa Serikali ya Awamu ya Tano ni:

- i. Kutengamaa kwa viashiria vya uchumi jumla ikiwemo ukuaji wa Pato la Taifa kwa wastani wa asilimia 6.9 katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita (2016 – 2018), kukua kwa sekta ya kilimo kwa wastani wa asilimia 5.3, mfumuko wa bei wa tarakimu moja ya kiwango cha wastani wa asilimia 4.7 katika kipindi hicho, utulivu wa thamani ya shilingi, na kupungua kwa kiwango cha umaskini kutoka asilimia 28.2 hadi asilimia 26.4.
- ii. Serikali kuhamia makao makuu ya nchi, Dodoma na kuendeleza eneo la Mji wa Serikali kwa kujenga majengo 23 ya ofisi za wizara zote na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na miundombinu yake (umeme, maji, barabara).
- iii. Kudhibiti utoroshaji na uuzaaji wa madini nje ili kuwezesha Taifa kunufaika na rasilimali zake ikiwa ni pamoja na kufanya marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, kutunga Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusiana na Umiliki wa

Maliasili ya Mwaka 2017, ujenzi wa uzio kuzunguka eneo la migodi ya Tanzanite Mirerani na kuanzisha masoko ya madini;

iv. Kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Kuharakisha Maendeleo ya viwanda Nchini (Fast Tracking Industrialization Strategy). Aidha, sekta binafsi pamoja na mifuko ya hifadhi ya jamii zimewekeza kwenye miradi ya viwanda ambapo mifuko hiyo inaendeleza miradi 7 kat i ya miradi 25;

v. Mifumo ya kielektroniki ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato imeimarishwa;

vi. Usimamizi wa fedha za Serikali umeimarishwa, ikiwa ni pamoja na kuanzisha Akaunti Jumuifu ya Hazina;

vii. Kuimarishwa kwa taasisi za umma na zile ambazo Serikali ina hisa. Serikali imeendelea kufuatilia na kusimamia kwa karibu zaidi utendaji katika mashirika ya umma ili kuhakikisha kuwa michango na gawio stahiki inatolewa kwa Serikali. Katika kuimarisha mashirika ya umma na taasisi ambazo Serikali ina hisa, Serikali imepata mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na mashirika mengi ambayo yalikuwa hayatoi gawio na michango stahiki kwa Serikali kuanza kufanya hivyo. Mwaka 2015/16 kulikuwa na mashirika 13 tu yaliyotoa gawio kwa Serikali kiasi cha shilingi bilioni 119.2 na sasa yameongezeka kufikia mashirika 28 ambayo hadi Mei 2019 yalikuwa yametoa gawio la jumla ya shilingi bilioni 497.5.

viii. Serikali imefanya majadiliano yenyeye maslahi kwa Taifa na baadhi ya makampuni ikiwemo kampuni ya "Airtel Tanzania" ambayo yameleta mafanikio yafuatayo: Umiliki wa hisa za Serikali kuongezeka kutoka asilimia 40 hadi asilimia 49 bila kuzilipia, Mwenyekiti wa Bodi na Afisa Mkuu wa Ufundu (Chief Technical Officer) kuteuliwa na Serikali, Kampuni kuilipa Serikali shilingi bilioni moja kila mwezi kwa kipindi cha miaka mitano ambapo kiasi cha shilingi bilioni 3 kimeshalipwa kwa kipindi cha mwezi Aprili, Mei na Juni 2019, Kupatikana kwa kiasi cha dola za Marekani milioni moja kutoka kwa Mwenyekiti wa "Bharti Airtel" kama sehemu ya uwajibikaji kwa jamii (Corporate Social Responsibility) ambazo zimeelekezwa

kujenga hospitali mpya ya kisasa Dodoma, Kufutwa kwa madeni na madai ya "Bharti Airtel" kwa Airtel (T) kiasi cha shilingi bilioni 937 (Dola milioni 407.38), na Serikali kupata gawio maalum kutoka mapato ghafi ya Airtel Tanzania kwa mwaka 2019; na

ix. Mafanikio katika mapambano dhidi ya rushwa na ujisadi ambapo ripoti ya uwazi ya kimataifa (Transparency International) ya mwaka 2018 imeonesha Tanzania imeshika nafasi ya 16 kwa nchi za Afrika kusini mwa jangwa la Sahara ikilunganishwa na nafasi ya 27 mwaka 2015.

31. Mheshimiwa Spika, kwa matokeo haya niliyoeleza, ni wazi kabisa kuwa Taifa letu linakwenda mbele chini ya Serikali hii ya tano ya CCM na liko katika mwelekeo sahihi (moving forward in the right direction). Serikali ya CCM chini ya Jemadari Dkt. John Pombe Joseph Magufuli inawashukuru sana wananchi wote wa Tanzania waliotimiza wajibu wao wa msingi kwa kulipa kodi ipasavyo na hivyo kuwezesha Taifa kupata mafanikio hayo makubwa sana katika kipindi kifupi. Wananchi wamejitoa na kuonesha uzalendo wa hali ya juu kwa kushiriki kwenye ujenzi wa Tanzania mpya. Mafanikio haya pia ni matunda mazuri ya kutunza nidhamu katika usimamizi wa uchumi, udhibiti wa mianya ya upotevu wa mapato na matumizi yasiyo na tija ya fedha za umma. Bajeti hii ninayowasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu itaendelea kutekeleza malengo ya Serikali kama yalivyoanishwa katika llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/17-2020/21.

III. SERA ZA BAJETI KWA MWAKA 2019/20

Shabaha za Uchumi Jumla

32. Mheshimiwa Spika, Shabaha za uchumi jumla katika kipindi cha mwaka 2019/20 ni kama ifuatavyo:-

i. Pato la Taifa kukua kwa asilimia 7.1 mwaka 2019 kutoka ukuaji halisi wa asilimia 7.0 mwaka 2018;

- ii. Mfumuko wa bei kuendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja kati ya asilimia 3.0 hadi 4.5 katika kipindi cha muda wa kati;
- iii. Mapato ya ndani kufikia asilimia 15.8 ya Pato la Taifa mwaka 2019/20 kutoka matarajio ya asilimia 14.3 mwaka 2018/19;
- iv. Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.1 ya Pato la Taifa mwaka 2019/20 kutoka matarajio ya asilimia 12.1 mwaka 2018/19;
- v. Matumizi ya Serikali kufikia asilimia 22.7 ya Pato la Taifa mwaka 2019/20 kutoka matarajio ya asilimia 21.6 mwaka 2018/19; na
- vi. Nakisi ya bajeti inakadiriwa kufikia asilimia 2.3 ya Pato la Taifa mwaka 2019/20 kutoka matarajio ya asilimia 2.0 mwaka 2018/19.

Sera na Mikakati ya Kuongeza Mapato

33. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20, Serikali imekusudia kuongeza na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa lengo la kuiwezesha kugharamia shughuli za Serikali ikiwemo miradi mikubwa ya miundombinu na huduma za jamii. Katika kufanikisha azma hii, Serikali itatekeleza sera zifuatazo:

- i. Kuboresha mazingira ya kufanya biashara ili kuvutia uwekezaji, ukuaji wa biashara ndogo na za kati ili kupanua wigo wa kodi na mapato mengine ya Serikali;
- ii. Kurekebisha viwango vya kodi kwa lengo la kuhamasisha uzalishaji na kulinda viwanda vya ndani dhidi ya ushindani kutoka nje;
- iii. Kuboresha mazingira ya ulipaji kodi kwa hiari, upanuzi wa wigo wa kodi na matumizi ya TEHAMA katika usimamizi wa kodi;

- iv. Kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi ili kutatua changamoto za ukwepaji kodi na kupunguza upotevu wa mapato, pamoja na kuweka mkazo zaidi katika kutoa elimu kwa mlipakodi;
- v. Kuimarisha makusanyo yasiyo ya kodi kwa kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA;
- vi. Kuendelea kuwianisha na kupunguza tozo na ada mbalimbali zinazotozwa na wakala, taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na
- vii. Kuiongezea Mamlaka ya Mapato ya Tanzania uwezo hususan watumishi, vitendea kazi bora na mafunzo ili kutambua na kudhibiti mbinu za ukwepaji kodi.

34. Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo ya makadirio ya mapato ya ndani, Serikali imeandaa mikakati mahsus ya kiutawala itakayotekelawa katika kipindi cha muda wa kat. Mikakati hiyo inajumuisha:

- i. Kuongeza ufanisi katika usimamizi na ukusanyaji wa kodi za ndani kwa kutekeleza Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Mapato ya Ndani (Integrated Domestic Revenue Admistrative System-IDRAS);
- ii. Kupanua wigo wa kodi kuititia utambuzi na usajili wa walipakodi wapya pamoja na kuendelea na zoezi la urasimishaji wa sekta isiyo rasmi;
- iii. Kuwekeza kwenye maeneo ambayo Serikali inaweza kupata mapato zaidi hususan katika uvuvi wa bahari kuu kwa kujenga bandari ya uvuvi na ununuzi wa meli za uvuvi;
- iv. Kuimarisha uwezo wa ufuatiliaji na udhibiti wa uhamishaji wa faida unaofanywa na kampuni za kimataifa;
- v. Kuimarisha usimamizi wa misamaha ya kodi kwa kuhakikisha inaelekezwa kwenye miradi inayokusudiwa;

vi. Kuhakikisha kuwa maduhuli yote yanapitia katika Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (GePG) ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato; na

vii. Kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji katika taasisi za Serikali ili kuhakikisha kuwa michango stahiki ya taasisi za umma kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali inawasilishwa kwa wakati.

35. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa misaada na mikopo nafuu kutoka nje, Serikali itaendelea kuimarisha uhusiano na ushirikiano na Washirika wa Maendeleo. Aidha, Serikali itaendeleza mazungumzo na Washirika wa Maendeleo ili kila upande uzingatie misingi na kanuni za ushirikiano wa maendeleo pamoja na kuendeleza majadiliano ya kimkakati (Strategic Dialogue) na kumaliza tofauti za kisera au kimatazamo pindi inapojitekeza, pasipo kuathiri utoaji wa fedha za utekelezaji wa Bajeti ya Serikali.

36. Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo ya kibashara ya ndani na nje, Serikali itaimarisha uhamasishaji wa wadau katika soko la ndani kwa lengo la kuimarisha ushiriki wao katika minada ya dhamana za Serikali. Aidha, jitihada zinafanya ili kuvutia wawekezaji mbalimbali kutoka nje ya nchi wenye nia ya kuikopesha Serikali ili kuwezesha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo yenye tija kwa uchumi wa Taifa letu.

Sera za Matumizi

37. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20, Serikali itaendelea kusimamia nidhamu katika matumizi ya fedha za umma na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya matumizi hususan katika miradi ya maendeleo. Lengo kuu ni kuwa na matumizi bora ya fedha katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuhakikisha upatikanaji wa thamani ya fedha. Aidha, Serikali itaendelea kuhakiki, kulipa na kuzuia kuongezeka kwa malimbikizo ya madai kwa Serikali. Pia, Serikali itaendelea kuelekeza fedha kwenye maeneo ya kipaumbele yenye kuchochea ukuaji wa uchumi.

Maeneo ya vipaumbele kwa mwaka 2019/20

38. Mheshimiwa Spika, katika Hotuba niliyowasilisha asubuhi kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2019/20, niliainisha vipaumbele kwa mwaka 2019/20 ambavyo vitatekelezwa kwa kuzingatia umuhimu wa pekee wa kulinda mazingira nchini (environmental sustainability). Bajeti hii inalenga kutekeleza vipaumbele hivyo kama ifuatavyo:

i. **Viwanda na kilimo:** Katika kuendeleza azma ya kujenga uchumi wa viwanda, katika mwaka 2019/20 Serikali itajikita kuvutia uwekezaji zaidi kwenye viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana nchini kama vile mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, misitu na madini; kuzalisha bidhaa kwa ajili ya soko la ndani na ziada kwa ajili ya kuuza nje, pamoja na kuongeza fursa za ajira. Vile vile kama wote tunavyofahamu, sekta ya kilimo (mazao, uvuvi, mifugo na misitu) ni muhimu sana kwa uendelezaji wa viwanda Tanzania kwa kuwa sehemu kubwa ya malighafi za viwanda zinatokana na kilimo. Katika kuimarisha sekta hii, Serikali itaendelea kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo awamu ya pili (ASDP II) hususan kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora, pembejeo, huduma za ugani, masoko, miundombinu wezeshi na tafiti, ikiwa ni pamoja na kupeleka fedha zaidi kwenye maeneo wezeshi kwa kilimo na kutoa nafuu za kikodi. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha bodi za mazao, kuboresha na kuhamasisha uanzishwaji wa vyama vya ushirika vya mazao ili kuviwezesha kupata mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha kwa ajili ya kuwekeza kwenye shughuli mbalimbali za kilimo na uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo vya kuongeza thamani ya mazao.

ii. **Ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu:** Licha ya kutilia mkazo kuongeza ukuaji wa sekta kuu za uchumi zinazotegemewa na kuajiri Watanzania wengi, bajeti ya 2019/20 itaelekezwa kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya, elimu na ujuzi, chakula na lishe bora na huduma za maji safi na salama. Aidha, kuitia bajeti hii, msukumo

utawekwa katika kuongeza ubora wa nguvukazi ili iendane na mahitaji ya soko la ajira.

iii. Uboreshaji wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara naawekezaji: Bajeti hii imeweka msisitizo mkubwa katika kuendeleza ujenzi na ukarabati wa miundombinu hususan reli, bandari, nishati, barabara, madaraja, na viwanja vya ndege. Aidha, Serikali itaendelea kupitia na kuimarissha mifumo ya kisera, kisheria na kitaasisi, sambamba na kuimarissha ulinzi na usalama ili kushawishi na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje. Napenda niwahakikishie wafanyabiashara, wawekezaji na wananchi kwa ujumla kuwa kuanzia mwaka ujao wa fedha, Serikali itaanza kutekeleza kwa nguvu zaidi mpangokazi wa kuboresha mazingira ya biashara (*Blueprint for the Regulatory Reforms to improve the Business Environment*) ili mazingira ya biashara nchini yawe rafiki zaidi na yenye gharama nafuu.

iv. Ufuatiliaji na tathmini Bajeti hii pia inakusudia kuimarissha zaidi ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika ngazi zote. Aidha, Serikali itaimarissha usimamizi wa ukusanyaji mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa bajeti lakini wakati huo huo kuhakikisha kuwa ukusanyaji wa kodi unafanyika bila kuathiri biashara. Napenda kuwasitisiza tena watumishi wa TRA kwamba hairuhusiwi kufunga biashara ili kushinikiza mfanyabiashara alipe kodi au malimbikizo ya kodi lisipokuwa kwa kibali cha Kamishna Mkuu wa TRA.

IV. MABORESHO YA MFUMO WA KODI, ADA NA TOZO MBALIMBALI

39. Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho ya mfumo wa kodi ikiwemo baadhi ya viwango vya kodi, tozo na ada zinazotozwa chini ya Sheria mbalimbali na pia taratibu za ukusanyaji na usimamiaji wa mapato ya Serikali. Marekebisho haya yamezingatia dhamira ya Serikali ya kuendelea kuwa na mfumo wa kodi ambao ni tulivu na wa kutabirika (stable and predictable). Vilevile yanalenga pamoa na mambo mengine, kuchochea kasi ya ukuaji wa

uchumi hususan katika sekta ya kilimo, viwanda, kukuza ajira, na kuongeza mapato ya Serikali. Aidha, **Serikali imeanza kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara (BluePrint)** ulioidhinishwa mwaka 2017/18 kwa kuanza kupitia mfumo wa tozo na ada mbalimbali zinazotozwa na Mamlaka za Udhibiti kwa lengo la kupunguza au kuzifuta baadhi ya tozo na ada, kupunguza na kuondoa muingiliano katika kutoza tozo hizo. Marekebisho yanayopendekezwa yanahusu Sheria zifuatazo:-

- a. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148;
- b. Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332;
- c. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147;
- d. Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438;
- e. Sheria ya Usalama Barabarani, SURA 168;
- f. Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004;
- g. Sheria ya Bajeti, SURA 439;
- h. Marekebisho madogo madogo katika baadhi ya Sheria za Kodi na Sheria nyingine mbalimbali;
- i. Kuanza utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara (Blueprint) kwa kurekebisha Ada na Tozo mbalimbali;na
- j. Hatua za Kisera na Kiutawala katika Kuboresha ukusanyaji wa mapato.

a. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148

40. Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148 kama ifuatavyo:-

- i. Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye makasha yenye majokofu (HS Code 8418.69.90) yanayotumika kwenye Kilimo cha Kisasa cha mboga mboga (horticulture) kwa wakulima watakaoingiza makasha hayo kutoka nje ya nchi kwa matumizi ya kilimo. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama na kutoa unafuu katika uzalishaji na kuhamasisha kilimo cha kisasa cha mboga mboga nchini;

- ii. Kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 68(3)(d) ili kisihusise uuzaji wa mazao ghafi ya kilimo nje ya nchi. Lengo la hatua hii ni kuwawezesha wauzaji wa mazao ghafi ya kilimo nje ya nchi kuendelea kufanya biashara hiyo kwa kadri ya kibali kitakavyotolewa na Serikali;
- iii. Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vifaa vya kukaushia nafaka (Grain Drying Equipment HS Code 8419.31.00). Msamaha huu unatarajiwa kutoa unaafuu kwenye gharama za kukausha nafaka kwa ajili ya kuzihifadhi. Aidha hatua hii itachochea ukuaji wa kilimo cha mazao ya nafaka;
- iv. Kupunguza kiwango cha Kodi ya Ongezeko la Thamani kutoka asilimia kumi na nane (18) hadi asilimia sifuri (0) kwenye huduma ya umeme unaouzwa kutoka Tanzania Bara kwenda Tanzania Zanzibar ili kuwapunguzia gharama za maisha wananchi wa Tanzania Zanzibar. Serikali iliridhla na kuelekeza kuwa umeme unaouzwa kutoka Tanzania Bara kwenda Tanzania Visiwani utozwe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia sifuri;
- v. Kutoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa vilainishi vya ndege vinavyoingizwa nchini na waendeshaji wa ndani, Shirika la ndege la Taifa, au mashirika ya ndege yanayotambulika katika Mikataba ya Kimataifa ya Huduma za Anga (Bilateral Air Services Agreements) kwa Kufanya marekebisho ya Sehemu ya Pili ya Jedwali la Misamaha la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani katika kipengele cha 11. Hatua hii itawezesha nchi yetu kusaini Mikataba ya Kimataifa ya Huduma za Anga ambayo ilishindikana kusainiwa hapo awali kutokana na kutokuwepo kwa msamaha huo;
- vi. Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye tiketi za ndege, vipeperushi, kalenda, shajara, karatasi zenyenembo na sare za wafanyakazi zilizowekwa nembo ya Shirika husika la ndege, kwa kufanya marekebisho ya Sehemu ya Pili ya Jedwali la Misamaha la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kuongeza kipengele kipyaki kinachotoa msamaha pale vinapoingizwa nchini na mashirika ya ndege

yanayotambulika katika Mikataba ya Kimataifa ya Huduma za Anga. Hatua hii itawezesha nchi yetu kusaini Mikataba ya Kimataifa ya Huduma za Anga ambayo ilishindikana kusainiwa hapo awali kutokana na kutokuwepo kwa msamaha huo; na

vii. Kufuta msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani uliokuwa unatolewa kwenye tauzo za Kike (HS Code 9619.00.10) kwa kuwa haujawezesha kupatikana kwa bidhaa hiyo muhimu kwa bei nafuu kwa walengwa na badala yake unawanufaisha wafanyabiashara. Aidha, wakati Serikali ilipoweka msamaha huu ilitarajia kwamba wazalishaji wa tauzo za kike watazuza kwa bei nafuu baada ya kusamehewa kodi.

Hatua zote za Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa ujumla wake zinatarajiwa **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 1,646.7**

b. Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332

41. Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 kama ifuatavyo:-

i. Kupunguza kiwango cha Kodi ya Mapato ya Makampuni (Corporate Income Tax) kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato kutoka asilimia 30 hadi asilimia 25 kwa kipindi cha miaka miwili (2) kuanzia mwaka 2019/20 hadi mwaka 2020/21 kwa wawekezaji wapya wa viwanda vya kuzalisha tauzo za kike. Aidha, Serikali itaingia mkatuba wa makubaliano (Performance Agreement) na kila mwekezaji ambao utaainisha wajibu wa kila upande. Lengo la hatua hii ni kuvutia uwekezaji katika uzalishaji wa bidhaa hiyo muhimu, kuongeza ajira na mapato ya Serikali. Vile vile hatua hii itapunguza matumizi ya fedha za kigeni zinazotumika kuagiza bidhaa hiyo kutoka nje na kuhamasisha uzalishaji wake ndani ya nchi;

ii. Kusamehe Kodi ya Zui o inayotozwa kwenye gharama zinazoambatana na mikopo (mfano ada za bima, gharama

ya usimamizi, na uandaaji wa mkopo, na ada nyingine zinazoendana na gharama za mkopo) kwa mikopo inayotolewa na Benki, Taasisi za Fedha za nje na wahisani mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Serikali. Lengo la hatua hii ni kuiwezesha Serikali kupata mikopo kwa gharama nafuu na kwa muda mfupi. Aidha, msamaha huu utaiwezesha Serikali kutekeleza miradi yake kwa wakati;

iii. Kutoa msamaha wa kutengeneza hesabu ambazo zinatakiwa kuwasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa ajili ya ukokotoaji wa Kodi ya Mapato kutoka kiwango cha sasa cha shilingi milioni ishirini (20,000,000/=) hadi shilingi milioni mia moja (100,000,000/=). Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama kwa mlipa kodi ya kutafuta mtaalam (Certified Public Accountant) kwa ajili ya kutengeneza hesabu. Aidha, hatua hii inalenga pia kuchochaea ulipaji kodi wa hiari na kuongeza mapato ya Serikali; na

iv. Kusamehe kodi kwenye mauzo ghafi yasiyozidi shilingi milioni nne (4,000,000/=) kwa wenye vitambulisho vya wajasiriamali na kupunguza kiwango cha chini cha kodi kutoka shilingi laki moja na nusu (150,000/=) kwa mwaka hadi shilingi laki moja (100,000/=) kwa mwaka kama ilivyofafanuliwa kwenye Jedwali Na. 1 na Na. 2. Lengo la hatua hii ni kupunguza mzigo wa kodi kwa walipakodi wadogo pamoja na kuoanisha viwango vya kodi na kiwango cha chini kinachotakiwa kwa mfanyabiashara kutumia mashine ya kodi ya kielektroniki (EFD) ambacho kwa sasa ni shilingi milioni kumi na nne (14,000,000=). Aidha, hatua hii inalenga pia katika kusositiza matumizi ya mashine za kielektroniki (Electronic Fiscal Device- EFD) ili kuwezesha ukokotoaji wa kodi ulio sahihi na kuongeza ulipaji kodi wa hiari.

Jedwali Na.1: Viwango vya sasa vinavyotozwa kodi kwa Wafanyabiashara wasiotengeneza Vitabu nya Hesabu

Mauzo (Shilingi)	Kodi ya kulipa kwa Mfanyakibashara asiye na Kumbukumbu kamili kwa mujibu wa kifungu cha 35 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi	Kodi ya kulipa kwa Mfanyakibashara mwenye kumbukumbu kamili kwa mujibu wa kifungu cha 35 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi
Mauzo yasiyozidi Shilingi 4,000,000	Hamna	Hamna
Mauzo yanayozidi shilingi 4,000,000 lakini hayazidi shilingi 7,500,000	Shilingi 150,000	Asilimia 3 ya kiasi cha mauzo kinachozidi shilingi 4,000,000
Mauzo yanayozidi shilingi 7,500,000 lakini hayazidi shilingi 11,500,000	Shilingi 318,000	Shilingi 135,000 jumlisha asilimia 3.8 ya kiasi cha mauzo kinachozidi Shilingi 7,500,000
Mauzo yanayozidi shilingi 11,500,000 lakini hayazidi shilingi 16,000,000	Shilingi 546,000	Shilingi 285,000 jumlisha asilimia 4.5 ya kiasi cha mauzo kinachozidi Shilingi 11,500,000
Mauzo yanayozidi shilingi 16,000,000 lakini hayazidi shilingi 20,000,000	Shilingi 862,500	Shilingi 487,000 jumlisha asilimia 5.3 ya kiasi cha mauzo kinachozidi shilingi 16,000,000

Jedwali Na. 2: Viwango Vipya vinavyopendekezwa kutozwa kodi kwa Wafanyabiashara wasiotengeneza Vitabu nya Hesabu

Mauzo (Shilingi)	Kodi ya kulipa kwa Mfanyakibashara asiye na Kumbukumbu kamili kwa mujibu wa kifungu cha 35 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi	Kodi ya kulipa kwa Mfanyakibashara mwenye kumbukumbu kamili kwa mujibu wa kifungu cha 35 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi
Mauzo yasiyozidi Shilingi 14,000,000	Hamna	
Mauzo yanayozidi shilingi 4,000,000 lakini hayazidi shilingi 7,000,000	Shilingi 10,000,000	Asilimia 3 kiasi cha mauzo kinachozidi shilingi 4,000,000.
Mauzo yanayozidi shilingi 7,000,000 lakini hayazidi shilingi 11,000,000	Shilingi 250,000,000	Shilingi 90,000 jumlisha asilimia 3 kiasi cha mauzo kinachozidi Shilingi 7,000,000
Mauzo yanayozidi shilingi 11,000,000 lakini hayazidi shilingi 14,000,000	Shilingi 450,000,000	Shilingi 1230,000 jumlisha asilimia 3 ya kiasi cha mauzo kinachozidi Shilingi 11,000,000
Mauzo yanayozidi shilingi 14,000,000 lakini hayazidi shilingi 100,000,000	Shilingi 1450,000,000	Shilingi 1450,000 jumlisha asilimia 3.5 ya kiasi cha mauzo kinachozidi Shilingi 14,000,000

Hatua hizi za Kodi ya Mapato kwa ujumla wake zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 35,192.5**

c. **Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147**

42. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Kifungu cha 124(2), marekebisho ya viwango maalum vya Ushuru wa Bidhaa (specific duty rates) kwa bidhaa zote zisizo za petroli yanaweza kufanyika kila mwaka ili kuviwianisha na mfumuko wa bei na viashiria vingine vya uchumi jumla. Kwa msingi huo wa sheria, **napendekeza kutokufanya mabadiliko ya viwango maalum vya Ushuru wa Bidhaa kwa bidhaa zote zisizo za petroli**. Aidha, hatua hii inazingatia kiwango kidogo cha mfumuko wa bei nchini na azma ya Serikali ya kujenga Uchumi wa Viwanda, na hivyo kuhamasisha uwekezajii kwenye Sekta ya Viwanda, kuvillinda na hatimaye kukuza ajira na mchangano wa sekta hiyo kwenye Pato la Taifa. Hata hivyo, napendekeza kurekebisha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa kwa bidhaa chache tu kama ifuatavyo:-

i. **Kupunguza** Ushuru wa Bidhaa kwenye mvinyo uliotengenezwa kutokana na usindikaji wa matunda (kama ndizi, mabibo, rozela/choya, nyanya, nk) yanayozalishwa hapa nchini tofauti na zabibu kwa kiwango kinachozidi asilimia 75 kutoka shilingi **200** kwa lita hadi shilingi **61** kwa lita ikiwa ni punguzo la shilingi **139** kwa lita. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha ulipaji wa kodi wa hiari na pia kuvutia uwekezajii kwenye viwanda vidogo vidogo vya aina hii. Aidha, bei ya mvinyo huu kwa lita inafanana na bei ya vinywaji baridi;

ii. Kutoza Ushuru wa Bidhaa wa asilimia **10** kwenye nywele za bandia zinazotengenezwa ndani ya nchi na asilimia **25** kwenye nywele bandia zinazoagizwa kutoka nje ya nchi zinazotambuliwa kwa HS Code 67.03; 67.04 na 05.01. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali;

iii. Kusamehe Ushuru wa Bidhaa kwenye vilainishi vya ndege (lubricants) vinavyoingizwa nchini na Shirika la ndege la Taifa au mashirika ya ndege yanayotambulika katika

mikataba ya Kimataifa ya huduma za anga. Lengo la hatua hii ni kuiwezesha nchi yetu kusaini mikataba ya Kimataifa ya Huduma za Anga ambayo ilishindikana kusainiwa hapo awali kutokana na kutokuwepo kwa msamaha huo; na

iv. Kutoza Ushuru wa Bidhaa wa asilimia **10** kwenye bidhaa za mabomba na vifaa vya plastiki vinavyotumika kwenye ujenzi wa miradi ya ujenzi wa miundo mbinu ya maji kwa kuwa hivi sasa kuna viwanda vingi vyenye uwezo wa kuzalisha bidhaa hizo na kutosheleza mahitaji hapa nchini. Hatua hii inahusisha bidhaa za mabomba na plastiki zinazotambuliwa katika HS Code 39.17. Lengo la kuanzisha Ushuru wa Bidhaa kwenye bidhaa hizo ni kulinda viwanda na kuongeza fursa za kazi, ajira na mapato ya Serikali.

Hatua za Ushuru wa Bidhaa kwenye bidhaa zisizo za petroli kwa ujumla wake zinatarajiw **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 2,955.50**.

d. **Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438**

43. Mheshimiwa Spika; napendekeza kuongeza muda wa ziada wa miezi sita (6) hadi Disemba 2019 kwa walipa Kodi waliokubaliwa kulipa kodi wanazodaiwa kwa utaratibu maalum wa kusamehe malimbikizo ya nyuma ya riba na adhabu (Tax Amnesty on Interest and Penalties) kwa asilimia 100 kwa kufanya marekebisho ya Kifungu cha 70 (2) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015 . Hatua hii inapendekezwa kutokana na muitikio mzuri wa walipakodi wakati msamaha huo ulipotolewa mwezi Julai 2018 ambapo dhamira ya Serikali ilikuwa ni kutoa ahueni kwa walipakodi walikuwa na malimbikizo makubwa yanayoathiri biashara zao.

Hatua hiyo ya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi inatarajiw **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 367,000**.

e. **Sheria ya Usalama Barabarani, SURA 168**

44. Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usalama Barabarani, Sura 168 kama ifuatavyo:-

- i. Kuongeza muda wa Leseni za udereva kutoka miaka mitatu (3) ya sasa hadi miaka mitano (5);
- ii. Kuongeza tozo ya Leseni ya udereva kutoka shilingi elfu arobaini (40,000) kwenda shilingi elfu sabini (70,000); na
- iii. Kuongeza ada ya kadi ya usajili wa magari kutoka shilingi elfu kumi (10,000/=) hadi shilingi elfu hamsini (50,000/=); pikipiki za matairi matatu kutoka shilingi elfu kumi (10,000/=) hadi shilingi elfu thelathini (30,000/=) na pikipiki kutoka shilingi elfu kumi (10,000/=) hadi shilingi elfu ishirini (20,000/=).

Lengo la mapendekezo haya ni kupunguza gharama za kuchapisha leseni kwa kipindi cha miaka mitatu kwani leseni hizo zinaweza kudumu zaidi ya miaka mitano. Aidha, marekebisho haya pia yanalenga katika kuoanisha gharama za uchapishaji wa leseni na kipindi cha leseni husika.

Hatua hizi kwa pamoja zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 18,147.0**

f. **Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004**

45. Mheshimiwa Spika, kikao cha Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki cha Maandalizi ya Bajeti (Pre-Budget consultations of Ministers of Finance) kilichofanyika tarehe 3 Mei, 2019 mjini Arusha, kilipendekeza kufanya marekebisho ya Viwango vya Ushuru wa Pamoja wa Forodha (EAC – Common External Tariff “CET”) na Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC Customs Management Act, 2004) kwa Mwaka wa Fedha 2019/20. Mapendekezo hayo yanalenga katika kuendeleza viwanda, kukuza ajira na kuboresha maisha ya wananchi katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

46. Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Mawaziri wa Fedha ya kufanya marekebisho kwenye Viwango vya Pamoja vya Ushuru wa Forodha yanahusisha hatua mpya na zinazoendelea ambazo zimekuwa zikitekelezwa katika mwaka 2018/19.

i. Mapendekezo ya hatua mpya za viwango vya Ushuru wa Forodha ni kama ifuatavyo:-

a. Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia **10** hadi asilimia **0** kwenye malighafi ya kutengeneza taulo za watoto (Baby Diapers) zinazotengenezwa hapa nchini kwa mwaka mmoja. Aidha, Watakaonufaika na punguzo hili ni viwanda vinavyozalisha bidhaa hiyo hapa Tanzania na utaratibu utakaotumika katika kuagiza malighafi hizo ni ule wa kuwapa unafuu wa Ushuru wa Forodha *"Duty Remission"*. Aidha, Serikali itaendelea kutoza ushuru wa Forodha wa asilimia 25 kwa taulo za watoto (Baby Diapers) za kutoka nje ya nchi. Hatua hii inatarajiwa kutoa unafuu wa gharama za uzalishaji, ajira na mapato ya Serikali. Aidha ni matarajio ya Serikali kuwa viwanda vinavyonufaika na msamaha huu wa Ushuru wa Forodha vitazalisha bidhaa hizi muhimu kwa afya ya watoto na kuziwa kwa bei nafuu ili watanzania wengi waweze kuzinunua. Malighafi zitakazohusika katika msamaha huu ni zile zinazotumbulika katika HS Code 3506.91.00; PE Film HS Code 3926.90.90; Super Aborbent Polymer HS Code 3906.90.00; Wet Strength Paper HS Code 4803.00.00; Non Wovens HS Code 5603.11.00; Polyethylene Laminated Non Wovens HS Code 5903.90.00; Spandex HS Code 5402.44.00; na Dust Free Paper Hs Code 4803.00.00;

b. Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka kiwango cha asilimia **25** hadi asilimia **0** kwa mwaka mmoja kwenye vifaa vinavyotumika katika kukata, kung'arisha na kuongeza thamani ya madini ya vito. Hatua hii itawanufaisha wanaofanya shughuli hizo na utaratibu wa *"Duty Remission"* ndio utatumika katika kuagiza vifaa hivyo. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu wa gharama na kuhamasisha ukataji na usafishaji wa madini hayo hapa nchini na hivyo kuongeza thamani yake kabla ya kuuzwa. Aidha, hatua hii itaongeza mapato ya Serikali na ajira. Vifaa vitakavyohusika ni vile vinavyotambulika katika HS Codes 3606.90.00; 6804.10.00; 6813.20.00; 7018.90.00; 7020.00.99; 8202.20.00; 8202.99.00; 8203.20.00; 8205.10.00; 8423.89.90; 8513.10.90; na 9002.19.00;

- c. Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia **10** hadi asilimia **0** kwa mwaka mmoja kwenye makaratasi (HS Code 4805.11.00 na 4805.19.00) yanayotumika kama malighafi ya kutengeneza vifungashio vya mboga mboga kwa ajili ya kuuza nje ya nchi. Utaratibu wa "*Duty Remission*" utatumika ambapo viwanda vinavyotengeneza vifungashio hivyo tu ndivyo vitakavyonufaika. Lengo la kuondoaa Ushuru wa Forodha kwenye malighafi hizo ni kupunguza gharama ya utengenezaji wa vifungashio ili kulinda viwanda vya ndani dhidi ya ushindani wa nje, kuvutia uwekezaji katika uzalishaji wa vifungashio vya aina hii na hatimaye kuhamasisha uuzaaji nje wa mboga mboga kwa ajili ya kupata fedha za kigeni;
- d. Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia **25** hadi asilimia **0** kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya mbegu vinavyotumiwa na wazalishaji wa mbegu hapa nchini. vifungashio vitakavyohusika ni vile vinavyotambulika katika HS codes 3923.29.00; 6305.10.00; 4819.40.00; 7310.29.90; 6305.33.00; 6305.20.00; 6304.91.90; 7607.19.90. Lengo la hatua hii ni kuongeza ubora wa mbegu na pia kuzipa unafuu wa gharama Taasisi zinazozalisha mbegu hapa nchini. Aidha utaratibu wa "*Duty Remission*" utatumika katika kuagiza vifungashio hivyo;
- e. Kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia **25** hadi asilimia **0** kwa mwaka mmoja kwa utaratibu wa "*Duty Remission*" kwenye malighafi (Alluminium Alloys) zenye HS Code 7606.92.00 zinazotumika katika kutengeneza sufuria (Alluminium pots). Hatua hii inalenga katika kupunguza gharama za uzalishaji, kuhamasisha uzalishaji wa bidhaa hiyo muhimu hapa nchini, kulinda viwanda vya ndani ili viweze kuongeza uzalishaji wa kutosheleza mahitaji na kuongeza ajira;
- f. Ili kulinda na kuhamasisha uzalishaji wa kahawa hapa nchini pamoja na kuongeza mapato ya Serikali napendekeza kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia **25** hadi asilimia **35** kwa mwaka mmoja kwenye kahawa inayoagizwa nje ya nchi (HS Code 09.01);

- g. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia **10** au dola za kimarekani **125** kwa kila tani moja ya ujazo (Metric ton) kwenye bidhaa za chuma kwa mwaka mmoja kutegemea kiwango kipi ni kikubwa badala ya asilimia **10** pekee. Bidhaa hizo ni "*Flat -rolled products of iron or Non-alloy steel na Flat -rolled products of other alloy steel.*" Bidhaa hizi hutambulika katika HS Codes 7209.16.00; 7209.17.00; 7209.18.00; 7209.26.00; 7209.27.00; 7209.28.00; 7209.90.00; 7211.23.00; 7211.90.00; 7225.50.0 na 7226.92.00. Lengo la kuweka viwango hivyo vya Ushuru wa Forodha ni kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo na kulinda viwanda vya hapa nchini na ajira;
- h. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia **25** au dola za kimarekani **200** kwa kila tani moja ya ujazo (Metric ton) kwenye bidhaa za mabati kwa mwaka mmoja kutegemea kiwango kipi ni kikubwa badala ya asilimia **25** pekee. Ushuru huo unahusu bidhaa zinazotambulika katika HS Code 7212.30.00; 7212.40.00 na 7212.50.00. Hatua hii ina lengo la kulinda viwanda vya ndani kutohana na udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo zinapoingizwa kutoka nje (under-invoicing and under valuation), na kulinda ajira na mapato ya Serikali;
- i. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia **10** au dola za kimarekani **250** kwa kila tani moja ya ujazo (Metric ton) kwa mwaka mmoja kutegemea kiwango kipi ni kikubwa kwenye bidhaa za mabati zinazotambulika katika HS Code 7212.60.00 badala ya kutoza ushuru wa asilimia **10** pekee. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani kutohana na udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo zinapoingizwa kutoka nje (under-invoicing and under valuation), na kulinda ajira na mapato ya Serikali;
- j. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia **25** au dola za kimarekani **250** kwa kila tani moja ya ujazo (metric ton) kwenye bidhaa za mabati kwa mwaka mmoja kutegemea kiwango kipi ni kikubwa badala ya ushuru wa asilimia **25** pekee. Hatua hii inahusu bidhaa zinazotambulika katika HS codes 7210.41.00; 7210.49.00; 7210.61.00; 7210.69.00; 7210.70.00

na 7210.90.00. Lengo la hatua hiyo ni kuwalinda wazalishaji wa bidhaa hizo hapa nchini kutokana na ushindani wa nje;

k. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia **25** au dola za kimarekani **250** badala ya kiwango cha asilimia **25** au dola za kimarekani **200** kwa kila tani moja ya ujazo (metric ton) kwenye bidhaa za chuma kwa mwaka mmoja kutegemea kiwango kipi ni kikubwa kwenye nondo kwa mwaka mmoja. (Reinforcement bars and hallow profile). Hatua hii inahusu bidhaa zinazotambulika katika Hs codes 7213.10.00; 7213.20.00; 7213.99.00; 7214.10.00; 7214.20.00; 7214.30.00; 7214.90.00; 7214.99.00; 7215.10.00; 7215.50.00; 7215.90.00; 7225.90.00; 7225.92.00; 7225.99.00; 7306.30.00; 7306.50.00; 7306.61.00; 7306.69.00; na 7306.90.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha nondo hapa nchini na kuongeza ajira;

l. Kwa kuwa mbogamboga zinalimwa kwa wingi hapa nchini, napendekeza kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia **25** hadi asilimia **35** kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa za mboga mboga (horticultural products) zinazotambulika kwenye HS codes 0603.11.00; 0603.12.00; 0603.13.00; 0603.14.00; 0603.19.00; 0604.20.00; 0604.90.00; 0701.90.00; 0702.00.00; 0703.10.00; 0703.20.00; 0706.10.00; 0710.10.00; 0710.21.00; 0710.22.00; 0710.30.00; 0714.10.00; 0714.20.00; 0804.30.00; 0804.40.00; 0804.50.00; 0805.10.00; 0805.40.00; 0805.50.00; 0806.10.00; 0807.11.00; 0807.20.00; 0808.10.00; 0808.20.00. Aidha, hatua hii itaongeza mapato ya serikali; na

m. Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia **10** badala ya asilimia **0** kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa za fito za plastiki zijulikanazo kama *PVC Profiles* HS Code 3916.10.00; 3916.20.00; 3916.90.00 ambazo hutumika kwa ajili ya kutengenezea fremu za milango, madirisha n.k. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali.

ii. Mapendekezo ya kuendelea na utekelezaji wa viwango vya Ushuru wa Forodha vya mwaka 2018/19 ni kama ifuatavyo:-

- a. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia **25** badala ya asilimia **0** kwa mwaka mmoja kwenye karatasi zinazotambulika kwenye HS codes 4804.11.00; 4804.21.00; 4804.29.00; 4804.31.00 na 4804.41.00. Karatasi hizi ni zile zinazozalishwa na kiwanda cha Mufindi;
- b. Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia **35** hadi asilimia **10** kwa mwaka mmoja kwenye ngano inayotambulika kwa HS Code 1001.99.00 na HS Code 1001.99.90. Hatua hii imizingatia kwamba uzalishaji wa ngano katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki hautoshelezi mahitaji, na bidhaa hii ni muhimu katika kutengeneza vyakula mbalimbali. Lengo la Serikali ni kuwezesha Viwanda na walaji wa vyakula viliviyotengenezwa kwa ngano waweze kupata vyakula husika kwa bei nafuu na tulivu. Aidha utaratibu wa "*Duty Remission*" utaendelea kutumika katika kuagiza ngano hiyo ambapo Viwanda vinavyotumia ngano ya aina hii katika uzalishaji ndivyo vinavyohusika katika kutumia kiwango hicho nafuu cha Ushuru wa Forodha. Kutokana na mahitaji makubwa ya ngano katika Jumuia ya Afrika Mashariki na SADC, wakati umefika sasa kwa wananchi kuchangamkia fursa ya Kulima ngano katika maeneo mbalimbali nchini yanayofaa kwa kilimo cha ngano ikiwemo eneo la shamba la Basuto;
- c. Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia **0** kwa mwaka mmoja kwenye mashine za kielektroniki zinazotumika kukusanya mapato ya Serikali (Electronic Fiscal Device) zinazotambulika katika HS Code 8470.50.00;
- d. Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia **25** hadi asilimia **0** kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa ijulikanayo kama "*Printed Alluminium Barrier Laminates*" (ABL) HS Code 3920.10.90 ambayo hutumika kama malighafi ya kutengeneza dawa ya meno kwenye viwanda vya ndani;
- e. Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia **10** hadi asilimia **0** kwa mwaka mmoja kwa utaratibu wa "*Duty Remission*" kwenye bidhaa ya kutengeneza sabuni ijulikanayo kama RBD Palm Stearin (HS Code 1511.90.40);

- f. Kutoza kwa mwaka mmoja Ushuru wa Forodha wa asilimia **25** au dola za kimarekani **1.35** kwa kilo moja ya viberiti (safety matches) vnavyotambuliwa kwenye HS code 3605.00.00 kutegemea kiwango kipi ni kikubwa;
- g. Kutoza kwa mwaka mmoja Ushuru wa Forodha wa asilimia **25** au dola za kimarekani **350** kwa kila tani moja ya ujazo (Metric ton) kutegemea kiwango kipi ni kikubwa kwenye bidhaa za chuma za misumari zinazotambulika katika HS code 7317.00.00 (nails, tacks, drawing pins, corrugated nails, staples other than those of heading 83.05);
- h. Kutoza ushuru wa Forodha wa asilimia **35** badala ya asilimia **25** kwa mwaka mmoja kwenye soseji (sausages) na bidhaa za aina hiyo (HS code 1601.00.00);
- i. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia **35** badala ya asilimia **25** kwa mwaka mmoja kwenye chingamu (chewing gum) zinazotambulika katika HS code 1704.10.00;
- j. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia **35** badala ya asilimia **25** kwa mwaka mmoja kwenye peremende (HS code 1704.90.00);
- k. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia **35** badala ya asilimia **25** kwenye chokoleti (chocolates) HS code 18.06 kwa mwaka mmoja;
- l. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia **35** badala ya asilimia **25** kwenye biskuti (HS code 1905) kwa mwaka mmoja;
- m. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia **35** badala ya asilimia **25** kwa mwaka mmoja kwenye nyanya zilizosindikwa (tomato sauces) zinazotambulika katika HS code 2103.20.00;
- n. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia **60** badala ya asilimia **25** kwa mwaka mmoja kwenye maji (mineral water) yanayotambulika katika HS code 2201.10.00;

- o. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia **35** badala ya asilimia **25** kwenye nyama (meat and edible meat offal in chapter 2) kwa mwaka mmoja;
- p. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia **25** kwenye mafuta Ghafi ya kula (mfano alizeti, mawese, soya, mizeituni, nazi, karanga, mahindi n.k) kwa mwaka mmoja. Hatua hii inalenga katika kulinda na kuhamasisha uzalishaji wa mbegu za mafuta na mafuta ya kula hapa nchini. Nchi yetu ina fursa kubwa ya kukuza uzalishaji wa bidhaa hiyo. Hivyo, kuna umuhimu wa kuchochea na kuhamashisha uzalishaji wa mbegu za mafuta na uchakataji wa mafuta ghafi kwa kutumia mbegu zinazozalishwa hapa nchini. Lengo la hatua hii ni kuongeza ajira mashambani, viwandani na pia kulinda fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mafuta hayo nje ya nchi. Mafuta ghafi hayo yanatambulika kwenye HS code 1507.10.00; 1508.10.00; 1511.10.00; 1512.11.00; 1513.11.00; 1514.11.00; 1514.91.00; 1515.11.00; 1515.21.00; 1515.30.00;
- q. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia **35** badala ya asilimia **25** kwa mwaka mmoja kwenye mafuta ya kula yaliyochakatwa kwa kiwango cha mwisho (semi-refined, refined/double refined oil) mfano alizeti, mawese, soya, mizeituni, karanga, nazi, mahindi n.k. Ongezeko la Ushuru wa Forodha linatarajiwa kuhamasisha uchakataji wa mbegu za mafuta hapa nchini na kuongeza ajira viwandani na mashambani. Aidha ongezeko la Ushuru wa Forodha linahusu mafuta yote ya kula yaliyochakatwa yanayoingizwa nchini na yanayotambulika kwenye HS codes 1507.90.00; 1508.90.00; 1509.90.00; 1510.00.00; 1511.90.10; 1511.90.30; 1511.90.90; 1512.19.00; 1512.29.00; 1513.19.00; 1513.29.00; 1514.19.00; 1514.99.00; 1515.19.00; 1515.20.00; 1515.50.00; 1515.90.00;
- r. Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia **10** badala ya asilimia **0** kwenye "Gypsum Powder" HS code 2520.20.00 kwa mwaka mmoja;
- s. Kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia **100** hadi asilimia **35** kwa mwaka mmoja kwenye sukari ya matumizi ya kawaida (consumption sugar) inayoagizwa

kutoka nje ya nchi kwa vibali maalum kwa lengo la kuziba pengo (gap sugar) la uzalishaji hapa nchini. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani vinavyozalisha sukari, ajira na mapato ya Serikali;

t. Kutoza kwa mwaka mmoja Ushuru wa Forodha wa asilimia **35** kwenye mitumba inayoingia kutoka nje (badala ya asilimia **35** au dola za marekani **0.40** kwa kilo moja kutegemea kiwango kipi kikubwa);

u. Kusamehe Ushuru wa Forodha kwenye malighafi, vipuri na mashine vinavyotumika katika kutengeneza nguo na viatu vya ngozi. Aidha, Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wameridhia orodha iliyoanishwa (harmonized list) ya malighafi na vipuri ili kutoa msamaha wa Ushuru wa Forodha na kuziwezesha nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ziweze kufanya biashara kwa bidhaa za nguo na viatu vya ngozi vitakavyozalishwa ndani ya Jumuiya; na

v. Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kutoza Ushuru wa Mauzo nje (Export Levy) wa asilimia **10** kwenye ngozi iliyosindikwa kwa kiwango cha kati (wet blue). Lengo la hatua hii ni kuhamasisha usindikaji wa ngozi, kuongeza thamani, na kuongeza ajira katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

47. Mheshimiwa Spika, Mawaziri wa Fedha wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walifanya pia marekebisho kwenye Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC Customs Management Act, 2004*) kama ifuatavyo:-

i. Kufanya marekebisho katika kipengele cha 1 (a) Sehemu B ya Jedwali la Tano la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC-CMA, 2004) ili kuingiza vilainishi kwa ajili matengenezo ya ndege (Lubricants for Aircraft), sare (uniforms), kalenda, shajara na peni kwenye orodha inayopata msamaha wa Ushuru wa Forodha kwenye huduma za ndege. Lengo la kutoa msamaha huo ni kuiwezesha nchi

yetu kusaini mikataba ya Kimataifa ya Huduma za Anga ambayo haikuweza kusainiwa hapo awali kutokana na kutokuwepo kwa msamaha huo.

Hatua hizi za Ushuru wa Forodha kwa pamoja zinatarajiw **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 31,074.0**

g. Sheria ya Bajeti, SURA 339

48. Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha utekelezaji wa Miradi Mikubwa yenye manufaa kwa Taifa kama vile Ujenzi wa Miundombinu, Ununuzi wa Ndege, Mabehewa au Vichwa vya Treni, Miradi ya Umeme n.k, inapendekezwa kurekebisha Kanuni ya 23 ya Kanuni za Sheria ya Bajeti za mwaka 2015, ili kumpa Mamlaka Millipaji Mkuu wa Serikali kuongeza muda wa matumizi ya fedha za mwaka wa fedha uliomalizika hususan zinazohusu Miradi ya Maendeleo. Hivi sasa Kanuni hii imeweka ukomo wa miezi mitatu (3) wa kutumia fedha za mwaka wa fedha uliomalizika, ambapo baada ya muda huu wa miezi mitatu (3) kuisha, fedha hizo hupaswa kurejeshwa Mfuko Mkuu wa Serikali. Utaratibu huu wa sasa wa kurejesha fedha za miradi, Mfuko Mkuu wa Serikali baada ya kumalizika kwa muda wa miezi mitatu (3) unaathiri utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kutokana na kutokuwepo kwa fedha za kulipia Hati za Madai hadi hapo mgao mpya wa fedha utakapotolewa kwenye bajeti ya mwaka mpya wa fedha.

h. Marekebisho madogo madogo katika baadhi ya Sheria za Kodi na Sheria nyingine mbalimbali.

49. Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho mengine madogo madogo yasiyo ya kisera katika sheria mbalimbali za kodi pamoja na sheria nyingine ili ziwe sanjari na azma ya kurahisisha utekelezaji wake. Marekebisho hayo yataainishwa katika Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2019 na Matangazo ya Serikali (Government Notices).

i. Kuanza utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhiliti wa biashara (Blueprint) kwa kurekebisha Ada na Tozo mbalimbali.

50. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia matokeo ya mukutano wa Mh. Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na wafanyabiashara kutoka wilaya zote nchini uliofanyika ikulu, Dar es salaam, tarehe 7 Juni, 2019, Serikali inapendekeza kufuta au kupunguza ada na tozo **hamsini na nne (54)** zinazotozwa na Wizara, Idara na taasisi zinazojitegemea ili Kuondoa kero na urasimu kwa wafanyabiashara na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Hatua hizi ni sehemu ya kwanza ya utekelezaji wa **Mpango wa kuboresha Mfumo wa udhibiti wa Biashara (Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment)**. Aidha, hatua hii imelenga kuondoa muingiliano wa majukumu ya kiutendaji baina ya Wizara, Taasisi na Mamlaka za Udhiliti. Marekebisho hayo yataainishwa katika Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2019 na Matangazo ya Serikali (Government Notices). Marekebisho hayo yatajumuisha:-

II. Mamlaka ya Dawa (TFDA)

a. Kufuta tozo za Kushikilia usajili wa dawa za chanjo (Vaccines and Biologicals) inayotozwa kwa kiasi cha Dola za Kimarekani mia hamsini (150); dawa za mitishamba (Herbal medicines) inayotozwa kwa kiasi cha Dola za Kimarekani mia hamsini (150); vifaa tiba (medical devices) inayotozwa kwa kiasi cha Dola za Kimarekani mia moja (100); vitendanishi (diagnostics) inayotozwa kwa kiasi cha Dola za Kimarekani mia mbili hamsini (250); chakula kinachotozwa kwa kiasi cha Dola za Kimarekani mia moja (100); vipukusi (antiseptics and diagnostics) vinavyotozwa kwa kiasi cha shilingi laki moja (100,000/=); na tozo za bidhaa zinazotengenezwa ndani ya nchi (retention fees for domestic products);

b. Kufuta tozo za Kudurufu cheti cha usajili wa vitendanishi inayotozwa kwa kiasi cha Dola za Kimarekani mia moja (100);

- c. Kufuta tozo za ukaguzi wa maduka mapya ya kuuzia vyakula inayotozwa kwa kiasi cha shilingi elfu hamsini (50,000);
- d. Kufuta tozo za usajili wa maduka ya reja reja ya dawa za mifugo kati ya shilingi elfu hamsini (50,000/=) hadi shilingi laki moja (100,000/=);
- e. kufuta tozo ya ukaguzi wa viwanda vyta samaki nchini iliyokuwa inatozwa kwa kiwango cha kati ya shilingi laki mbili (200,000/=) hadi shilingi laki mbili na elfu hamsini (250,000/=);
- f. Kufuta tozo ya ukaguzi wa maduka mapya ya samaki ya shilingi elfu hamsini (50,000/=); na
- g. Kufuta tozo ya leseni ya mwaka ya biashara ya samaki kati ya shilingi elfu hamsini (50,000/=) hadi shilingi laki tatu (300,000/=).

Lengo la hatua hizi ni kuweka mazingira rafiki ya kibiashara na uwekezaji ili kuchochera uzingatiaji wa sheria kwa hiari na kuongeza wigo wa wadau wanautumia huduma za TFDA (customer base).

Hatua hii inatarajiwa **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 2,500.0**

II. Shirika la Viwango Tanzania

Napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Shirika la Viwango Tanzania kwa:-

- a. Kufuta tozo ya shilingi elfu hamsini (50,000/=) ya maombi ya alama ya ubora (TBS mark);
- b. Kufuta tozo ya nembo ya ubora (TBS mark guarantee) ya asilimia kumi na tano (15) ya tozo ya gharama za mwanzo za ukaguzi wa ubora (transport costs and overhead fees);
- c. Kufuta tozo ya dhamana ya cheti cha kutumia nembo ya ubora (TBS mark licence). Tozo hii hutozwa kwa kiwango cha

asilimia hamsini (50) ya gharama za usafirishaji na upimaji wa Sampuli kutoka sokoni na viwandani;

d. Kufuta tozo ya shilingi elfu hamsini (50,000/=) ya ununuzi wa fomu ya maombi ya bidhaa zinazotoka nje kwa bidhaa zote;

e. Kufuta tozo ya gharama za ugenzi (calibration of equipment based on industrial metrology). Tozo hii hutozwa kulingana na umbali wa sehemu (Kwa mfano Dar es salaam - chini ya umbali wa kilometra 5 kutoka TBS ni shillingi elfu kumi (10,000/=); umbali wa kati ya kilometra 5 hadi 7 kutoka TBS ni shilingi elfu hamsini (50,000/=); na umbali wa zaidi ya kilometra 7 kutoka TBS ni shilingi laki moja (100,000/=); na

f. Kufuta tozo ya asilimia 0.2 ya gharama ya mzigo na usafirishaji ya udhibiti wa vipodozi, vifaa tiba ikiwa ni pamoja na kondomu, mabomba ya sindano (syringes), glavu (gloves), pamba (cotton wool) na bendeji (bandage).

Lengo la hatua hii ni kupunguza mzigo kwa wafanyabiashara na wazalishaji, kupunguza gharama katika uendeshaji wa vifaa nya viwandani na kupunguza tozo za kero.

Hatua hii inatarajiwa **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 2,687.4**

Aidha, napendekeza kufanya marekebisho ya **Sheria ya Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA)** kwenye eneo la usimamizi wa viwango ambao unajumuisha ubora na usalama wa chakula na vipondozi ili Shirika la Viwango Tanzania (TBS) liendelee kusimamia eneo la chakula na vipodozi kwa ujumla kama ilivyo kuwa tangu mwaka 1975. Hivyo basi, Shirika la Viwango litachukua jukumu la kuunganisha utaratibu wa usajili wa majengo (premises registration), Usajili wa bidhaa (product registration), udhibiti wa bidhaa (certification) na udhibiti wa bidhaa kutoka nje (import inspection) kwa ujumla. Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) itaendelea kusimamia madawa, Vifaa Tiba na Vitendanishi ili kuongeza ufanisi katika eneo hili.

III. Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali

Napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Majumbani na Viwandani, Sura 182 kwa kufuta tozo zifuatazo:-

- a. Kufuta tozo ya huduma ya kusitisha kibali cha awali na kutoa kibali kipywa inayotozwa kwa kiwango cha Dola za Kimarekani hamsini (50);
- b. Kufuta tozo ya huduma ya kubadilisha taarifa za kibali inayotozwa kwa kiwango cha Dola za Kimarekani hamsini (50);
- c. Kufuta tozo ya usajili wa kampuni ya Wakala wa Forodha (Clearing Agent) inayotozwa kwa kiwango cha Dola za Kimarekani mia tano (500) kila kipindi cha usajili;
- d. Kufuta tozo ya huduma ya kubadilisha taarifa za usajili inayotozwa kwa kiwango cha Dola za Kimarekani mia moja (100) kila kipindi cha usajili;
- e. Kufuta tozo ya huduma ya ukaguzi wa dharura inayotozwa kwa kiwango cha Dola za Kimarekani mia tatu (300) kwa kila ukaguzi;
- f. Kufuta ada ya kulinda cheti cha usajili (maintenance fee) kwa viwanda vya magodoro inayotozwa kwa kiwango cha Dola za Kimarekani elfu moja (1,000) kila mwaka;
- g. Kufuta ada ya kulinda cheti cha usajili kwa viwanda vya rangi inayotozwa kwa kiwango cha Dola za Kimarekani elfu moja (1,000) kila mwaka;
- h. Kufuta ada ya kulinda cheti cha usajili kwa viwanda vya nguo inayotozwa kwa kiwango cha Dola za Kimarekani elfu moja (1,000) kila mwaka;
- i. Kufuta ada ya kulinda cheti cha usajili kwa viwanda vya ngozi inayotozwa kwa kiwango cha Dola za Kimarekani elfu moja (1,000) kila mwaka;

j. Kufuta ada ya kulinda cheti cha usajili kwa viwanda nya plastiki inayotozwa kwa kiwango cha Dola za Kimarekani elfu moja (1,000) kwa mwaka;

k. Kufuta ada ya kulinda cheti cha usajili kwa viwanda vinginevyo vikubwa inayotozwa kwa kiwango cha Dola za Kimarekani elfu moja (1,000) kwa mwaka;

l. Kufuta ada ya kulinda cheti cha usajili kwa viwanda vidogo vidogo inayotozwa kwa kiwango cha Dola za Kimarekani mia mbili hamsini (250) kwa mwaka;

m. Kufuta ada ya kulinda cheti cha usajili kwa wasambazaji wakubwa inayotozwa kwa kiwango cha Dola za Kimarekani elfu moja (1,000) kwa mwaka; na

n. Kufuta ada ya kulinda cheti cha usajili kwa wasambazaji wa kati inayotozwa kwa kiwango cha Dola za Kimarekani mia tano (500) kwa mwaka.

Aidha, napendekeza pia kufanya **marekebisho ya Sheria ya Usimamizi na udhibiti wa Kemikali za Majumbani na Viwandani Sura 182**, ili kurekebisha viwango nya tozo kama ifuatavyo:-

a. Kutoza tozo ya shilingi elfu arobaini (40,000/=) ya usajili wa kemikali kwa kila kemikali kwa kipindi cha usajili badala ya Dola za Kimarekani ishirini (20);

b. Kutoza tozo ya shilingi laki mbili (200,000/=) kwa wafanyabiashara wakubwa na shilingi elfu hamsini (50,000/=) kwa wajasiriamali wadogo kwa kila cheti cha usajili (Certificate holder registration);

c. Kutoza tozo ya shilingi laki mbili (200,000/=) badala ya Dola za Kimarekani mia moja (100) kwa wafanya biashara wakubwa na shilingi elfu hamsini (50,000/=) kwa wafanyabiashara wadogo kwa Usajili wa eneo la kuhifadhiya kemikali (Premises registration);

- d. Kutoza tozo ya shilingi laki tatu (300,000/=) kwa siku kwa kila mtu ya kuchambua kemikali chakavu badala ya Dola za Kimarekani mia tatu (300);
- e. Kutoza tozo ya shilingi laki mbili (200,000/=) ya kuainisha na kuidhinisha njia ya kuteketeza kemikali badala ya Dola za Kimarekani mia tano (500);
- f. Kutoza tozo ya shilingi laki tatu (300,000/=) kwa kila siku kwa kila mtu ya kusimamia kupakia, kusafirisha, kushusha na kuteketeza kemikali chakavu badala ya Dola za Kimarekani mia tatu (300);
- g. Kutoza tozo ya shilingi laki tatu (300,000/=) ya ukaguzi wa maghala na sehemu za kuhifadhiya kemikali badala ya Dola za Kimarekani mia mbili (200);
- h. Kutoza tozo ya shilingi laki moja na elfu hamsini (150,000/=) kwa kila siku kwa kila mtu kwa tathmini ya njia za Usafirishaji na ukaguzi wa dharura (Transportation Routes assessment and emergency inspection) badala ya Dola za Kimarekani mia moja (100);
- i. Kutoza tozo ya shilingi laki moja na elfu hamsini (150,000/=) kwa siku kwa kila mtu kwa kusindikiza kemikali hatarishi badala ya Dola za Kimarekani mia moja (100); na
- j. Usafirishaji wa kemikali hatarishi na kemikali zingine ndani na nje ya nchi utatozwa tozo kama zilivyoainishwa kwenye Jedwali Na. 3 hapa chini:-

Jedwali Na 3.

Kiasi cha kemikali kinachosafirishwa kwa MT	Ada ya sasa (USD)	Ada inayopendekezwa (USD)
Kati ya 0.1 - 10	1-2 kila MT	10
10.1 - 200		1 kila MT
201 - 1000		400
1001 - 5000		600
5001 - 10,000		800
10,001- 20,000		1,200
20,001- 40,000		1,500
40,001+		2,000

Aidha, ili kutimiza matakwa ya sheria ya kutumia fedha za kitanzania, tozo zote zilizokuwa zinatozwa kwa dola za kimarekani zitatozwa kwa fedha za Kitanzania isipokuwa kwa shehena za kemikali zinazoenda nje ya nchi (On-transit). Lengo la hatua hizi ni kupunguza wingi na ukubwa wa tozo ili kuweka mazingira bora ya biashara nchini. Aidha, mizigo ya kemikali inayopitishwa katika bandari ya Dar es salaam itaongezeka na hivyo kuongeza mapato ya Serikali.

Hatua hii inatarajiwa **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 450.0**

IV. Wizara ya Mifugo na Uvuvi- Sekta ya Mifugo

Napendekeza kufuta tozo mbalimbali kwenye Sekta ya mifugo kama ifuatavyo:-

- Kufuta tozo ya shilingi 5,000 ya vibali vya vyombo vya kusafirisha maziwa chini ya lita 51;
- Kufuta tozo ya shilingi 50,000 ya usajili wa vituo vya kukusanya maziwa lita 201 kwa siku;
- Kufuta tozo ya shilingi 5,000 ya usajili wa wazalishaji wa maziwa chini ya lita 51 kwa siku;

- d. Kufuta tozo ya shilingi 500,000 ya usajili wa wasambazaji wa pembejeo za maziwa;
- e. Kufuta tozo ya shilingi 15,000 ya usajili wa wafugaji wadogo wa mifugo ya nyama;
- f. Kufuta tozo ya shilingi 50,000 ya usajili wa wafugaji wa katiba mifugo ya nyama;
- g. Kufuta tozo ya shilingi 75,000 ya usajili wa wafugaji wakubwa wa mifugo ya nyama;
- h. Kufuta tozo ya shilingi 20,000 ya usajili wa wasimamizi wa minada ya awali;
- i. Kufuta tozo ya shilingi 30,000 ya usajili wa wasimamizi wa minada ya upili na mipakani;
- j. Kufuta tozo ya shilingi 50,000 ya usajili wa minada ya upili na mipakani;
- k. Kufuta tozo ya shilingi 30,000 ya usajili wa wafanyabiashara wa minada ya awali;

- l. Kufuta tozo ya shilingi 60,000 ya usajili wa wafanyabiashara wa minada ya upili na mipakani;
- m. Kufuta tozo ya shilingi 100,000 ya usajili wa wafanyabiashara wa nyama na bidhaa zake nje ya nchi;
- n. Kufuta tozo ya shilingi 1,000 ya kibali cha kusafirisha kuku nchini (vifaranga 100 kwa siku moja); na
- o. Kufuta tozo ya shilingi 200 ya kibali cha kusafirisha kuku mkubwa nchini.

Hatua hii inatarajiwa **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha takribani **shilingi milioni 16,689.8**

V. Wizara ya Maliasili na Utalii

Napendekeza kufuta ada ya Leseni ya kufanya biashara ya Utalii inayohusisha uwindaji wa kitaalamu (professional hunting) iliyoomba inatozwa kwa dola za kimarekani mia mbili (USD 200) kwa raia wa Tanzania na dola za kimarekani elfu moja (USD 1000) kwa raia wa kigeni. Lengo la hatua hii ni kupunguza tozo zinazotozwa katika sekta ya utalii, na kuvutia watalii. Hatua hii inatarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha takribani Dola za Kimarekani elfu themanini (USD 80,000).

VI. Wizara ya Maji

Napendekeza kufuta ada ya matumizi ya maji kwa watumiaji wenyewe visima nyumbani ambayo ilikuwa inatozwa kuanzia shilingi laki moja (100,000/=) na kuendelea kulingana na matumizi ya maji. Lengo la kufuta tozo hiyo ni kupunguza gharama kwa wananchi wanaochimba visima vya maji kwa matumizi binafsi nyumbani na kuwezesha upatikanaji wa maji hayo kwa gharama nafuu. Hata hivyo, ili kudhibiti uchimbaji holela wa visima, itabidi visima hivyo viendelee kusajiliwa na Bodi za Maji za Mabonde.

Hatua hii inatarajiwa **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha **shilingi milioni 1,961**

Aidha, Serikali itaendelea kufanya tathmini ya utekelezaji wa mpango kazi wa **Mpango wa kuboresha Mfumo wa udhibiti wa Biashara (BLUEPRINT)**. Lengo ni kuendelea kuweka mazingira bora ya kuvutia uwekezaji, katika kipindi cha muda wa kati na muda mrefu. Hatua hii inatoa fursa kwa wajasiriamali kuanzisha biashara mpya zitakazo ongeza ajira na kukuza uchumi. Kwa kuzingatia kuwa, Serikali imewekeza katika kuboresha mazingira ya udhibiti wa mazingira ya biashara, kupitia mpango wa BLUEPRINT, hivyo basi, ni matarajio na wito wa Serikali kwamba wawekezaji wa ndani na nje, watachangamkia fursa hii kwa kuanzisha na kuendeleza uwekezaji mpya ili kukuza faida za biashara na kuweza kulipa kodi stahiki kwa hiari na kuongeza mapato ya Serikali.

j. **Hatua za Kisera na Kiutawala katika Kuboresha ukusanyaji wa mapato**

51. **Mheshimiwa Spika**, napendekeza kuweka utaratibu mpya wa kuondoa mizigo bandarini ambapo wananchi wa kawaida wataruhusisha kutoa mizigo yao bila ya kuwa na ulazima wa kutumia Wakala wa Forodha (Clearing and Forwarding Agents). Hata hivyo, utaratibu huu hautahusisha mizigo inayopitishwa hapa nchini kwenda nje ya nchi (Transit Cargo). Aidha, Mamlaka ya Mapato Tanzania itaandaa utaratibu wenye kueleweka kwa urahisi ili kuwawezesha Wananchi kugomboa mizigo yao kwa gharama nafuu zaidi na bila kuchelewa.

52. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inapendekeza kuchukua hatua mbalimbali za Kisera na Utawala kwa lengo la kuimarisha na kurahisisha ukusanyaji mapato. Hatua hizo ni pamoja na:-

i. Ili kuondoa malalamiko ya wafanyakishara dhidi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, imeamua kuanzisha kitengo huru cha kupokea malalamiko na taarifa za kodi (Office of Tax Ombudsman) ambacho kitaratibiwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Aidha, kitengo hiki kitahusisha kupokea na kupitia malalamiko ya taarifa za Kodi zitakazotolewa na walipakodi au watu wenye nia njema. Baadhi ya majukumu ya Kitengo hiki ni kama yafuatayo:-

a. Kupokea malalamiko ya rushwa dhidi ya watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania;

b. Kupokea malalamiko ya ukadiriaji wa Kodi na uthamanishaji wa bidhaa usio wa haki wala uhalsia dhidi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania;

c. Kupokea malalamiko ya matumizi ya nguvu katika ukusanyaji kodi dhidi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania;

d. Kupokea malalamiko ya ufungaji wa biashara bila kufuata sheria na taratibu dhidi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania; na

e. Kupokea malalamiko pamoja na kero nyingine zinazofanana na hayo dhidi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania.

ii. Ili kuongeza ukusanyaji wa mapato ya kodi za ndani, serikali inakamilisha manunuvi ya mfumo unganishi wa kielektroniki (Intergrated Domestic Revenue Adminstration System- IDRAS) katika kukusanya kodi na mapato yasiyo ya kodi ili kuleta uwazi na ufanisi katika ukusanyaji wa mapato. Pia mfumo huu utarahisisha ulipaji wa kodi na kupunguza rushwa mionganoni mwa watumishi wasio waaminifu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania;

iii. Kuendelea kusimamia matumizi ya mfumo wa kukusanya kodi wa kielektroniki (Electronic Fiscal Device Management System) ambao umefanyiwa maboresho makubwa na kuanza kazi tangu tarehe 1 June, 2019, ili kudhibiti na kubaini udanganyifu unaofanywa katika matumizi ya mfumo huo. Aidha, hatua hii itadhibiti uvujaji wa mapato katika urejeshaji wa kodi (Tax refund), utoaji wa risiti bandia, n.k;

iv. Kutokana na wimbi la vijana wengi kujihusisha na michezo ya kubahatisha na kusahau majukumu ya ujenzi wa taifa, Serikali ikishirikiana na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha imebuni na kutengeneza mfumo maalum ambao utatumika kudhibiti uchezaji wa michezo hii (Responsible Gaming). Pia, Mfumo huu utatumika kudhibiti udanganyifu ambao unafanywa na waendeshaji wa michezo ya kubahatisha ili Serikali ipate mapato yake halali;

v. Kutokana na malalamiko ya walipa kodi kuhusu ukadiriaji wa kodi na uthamanishaji wa bidhaa usio na haki wala uhaliasia, Serikali imeiagiza Mamlaka ya Mapato Tanzania kuanzisha dawati la kushughulikia mappingamizi ya makadirio ya kodi ambapo pingamizi za uthamanishaji na

utambuzi litashughulikiwa ndani ya masaa ishirini na nne (24); na

vi. Kutoa unafuu wa kutolipa kodi kwa kipindi cha miezi sita (6) kuanzia wakati mfanyakia shara au mwekezaji anapopewa Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN). Hatua hii inatofautiana na hali ilivyo sasa ambapo mfanyakia shara anapopewa TIN anaanza kufanyiwa tathmini (tax assessment) ya mapato yake ya biashara na kutakiwa kulipa kodi. Hatua hii itawezesha wafanyakia shara na wawekezaji wapya kupata muda wa kujiandaa na mahitaji yanayotakiwa katika shughuli wanazofanya na kuondoa usumbufu au dhana ya woga wakati wa kuanzisha biashara. Mfano kuna mahitaji ya Leseni ya biashara na vibali vingine muhimu.

k. Tarehe ya Kuanza Kutekeleza Hatua Mpya za Kodi.

53. Mheshimiwa Spika, hatua hizi za kodi zinazopendekezwa zitaanza kutekelezwa tarehe 1 Julai, 2019, isipokuwa pale ilipoelezwa vinginevyo.

V. SURA YA BAJETI KWA MWAKA 2019/20

54. Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia shabaha, malengo pamoja na sera za bajeti kwa mwaka 2019/20, Sura ya Bajeti inaonesha kuwa jumla ya shilingi triliioni 33.11 zinatarajiwa kukusanya na kutumika katika kipindi hicho. Jumla ya mapato ya ndani (ikijumuisha mapato ya Halmashauri) yanatarajiwa kuwa shilingi triliioni 23.05, sawa na asilimia 69.6 ya bajeti yote. Kati ya mapato hayo, Serikali inalenga kukusanya mapato ya kodi ya jumla ya shilingi triliioni 19.10 sawa na asilimia 12.9 ya Pato la Taifa. Mapato yasiyo ya kodi kwa mwaka 2019/20 yanatarajiwa kuwa shilingi triliioni 3.18 na mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri ni Shilingi bilioni 765.5.

55. Mheshimiwa Spika, Serikali inatarajia kukopa shilingi triliioni 4.96 kutoka soko la ndani. Kati ya kiasi hicho, shilingi triliioni 3.46 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za

Serikali zinazoiva na kiasi cha Shilingi bilioni 1.50 sawa na asilimia 1.0 ya Pato la Taifa ni mikopo mipyä kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Kwa lengo la kuongeza kasi katika utekelezaji wa miradi ya miundombinu, Serikali inatarajia kukopa shilingi trillioni 2.32 kutoka soko la nje kwa masharti ya kibashara.

56. Mheshimiwa Spika, Washirika wa Maendeleo wanatarajiwu kuchangia shilingi trillioni 2.78 ambayo ni asilimia 8 ya bajeti. Misaada na mikopo hii inajumuisha miradi ya maendeleo shilingi trillioni 2.31; Mifuko ya Pamoja ya Kisekta shilingi bilioni 199.5; na Misaada na Mikopo nafuu ya Kibajeti (General Budget Support-GBS) shilingi bilioni 272.8.

57. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20, Serikali inapanga kutumia jumla ya shilingi trillioni 33.11 kwa matumizi ya kawalda na maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi trillioni 20.86 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwa ni asilimia 63.0 ya bajeti, ikijumuisha Shilingi trillioni 9.72 kwa ajili ya ulipaji wa deni la Serikali na shilingi trillioni 7.56 kwa ajili ya mishahara. Aidha, shilingi trillioni 3.58 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (Other Charges-OC) ikijumuisha shilingi bilioni 460.5 kwa ajili ya matumizi yatokanayo na vyanzo vya ndani vya Halmashauri. Aidha, kwa mwaka 2019/20, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2019 na maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

58. Mheshimiwa Spika, matumizi ya maendeleo yanatarajiwu kuwa shilingi trillioni 12.25, sawa na asilimia 37.0 ya bajeti yote, ambapo kiasi cha Shilingi trillioni 9.74 ni fedha za ndani na shilingi trillioni 2.51 ni fedha za nje. Kati ya fedha za maendeleo zilizotengwa, shilingi trillioni 2.48 ni kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa reli kwa kiwango cha *Standard Gauge*; shilingi trillioni 1.44 ni kwa ajili ya mradi wa kufua umeme Mto Rufiji; shilingi bilioni 788.8 ni kwa ajili ya mifuko ya Reli, Maji na REA; shilingi bilioni 450 ni kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu; na shilingi bilioni 288.5 kwa ajili ya elimu msingi bila ada. Aidha, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 600.0 kwa ajili ya kulipa madeni yaliyohakikiwa ya watumishi, watoa huduma na makandarasi wa barabara, maji na umeme.

59. *Mheshimiwa Spika*, kwa kuzingatia mfumo wa bajeti kama nilivyoeleza, sura ya bajeti kwa mwaka 2019/20 ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali A**.

Jedwali A: Mfumo wa Bajeti ya Mwaka 2019/20

		<i>Shilingi Milioni</i>
	Mapato	2019/20
A.	Mapato ya Ndani-Serikali Kuu	22,279,854.6
	(i) Mapato ya Kodi {TRA}	19,100,933.3
	(ii) Mapato yasiyo ya kodi	3,178,921.3
B.	Mapato ya Halmashauri	765,483.4
C.	Misada na Mikopo nafuu kutoka Washirika wa Maendeleo	2,783,676.1
	(i) Misada na Mikopo nafuu -GBS	272,812.6
	(ii) Misada na Mikopo nafuu ya Miradi	2,311,403.8
	(iii) Misada na Mikopo nafuu ya Kiseka	199,459.7
D.	Mikopo ya Ndani na Nje	7,276,395.7
	(i) Mikopo ya Nje	2,316,403.5
	(ii) Mikopo ya Ndani	1,499,774.2
	(iii) Mikopo ya Ndani- Rollover	3,460,218.0
	JUMLA YA MAPATO YOTE (A+B+C+D)	33,105,409.8
	Matumizi	
E.	Matumizi ya Kawaida	20,856,807.5
	o/w (i) Mfuko Mkuu wa Serikali	9,721,127.0
	-Malipo ya Riba Ndani	1,438,950.0
	-Malipo ya Mtaji Ndani (Rollover)	3,460,218.0
	-Malipo ya Mtaji Nje	1,976,098.0
	- Malipo ya Riba Nje	987,312.0
	- Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii	1,255,971.0
	- Matumizi Mengine ya Mfuko Mkuu	602,578.0
	(ii) Mishahara	7,558,974.4
	(iii) Matumizi Mengineyo (OC)	3,576,706.2
	- Malipo ya Madeni yaliyohakikiwa	160,000.0
	- Matumizi ya Halmashauri (own source)	460,539.5
	- Matumizi mengineyo	2,956,166.7
F.	Matumizi ya Maendeleo (Asilimia 37.0) ya BGT	12,248,602.3
	(i) Fedha za Ndani	9,737,738.8
	o/w Malipo ya Madeni yaliyohakikiwa	440,000.0
	o/w Matumizi ya Halmashauri	304,943.9
	o/w Miradi mingine	8,992,794.9
	(ii) Fedha za Nje	2,510,863.5
	JUMLA YA MATUMIZI YOTE (E+F)	33,105,409.8
	NAKISI YA BAJETI (ASILIMIA YA PATO LA TAIFA)	2.3%

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

VI. HITIMISHO

60. Mheshimiwa Spika, bajeti ni nyenzo ya kufikia matarajio ya wananchi wetu. Hivyo, katika kuandaa bajeti hii, Serikali iliwashirikisha wadau mbalimbali wakiwemo, Kamati ya Bunge ya Bajeti, wafanyabiashara, taasisi za umma na binafsi, wananchi wa kawaida, na wataalam wa kodi hususan wale walioshiriki vikao vya kazi vya kikosi kazi cha maboresho ya kodi (*Task Force and Think Tank*) kujadili na kushauri juu ya mapendekezo ya maboresho ya kodi na tozo mbalimbali. Baadhi ya wadau walituletea maoni na ushauri kwa maandishi au barua pepe. Nakiri kuwa walitupatia mrejesho ambaa umesaidia kuboresha será na vipaumbele vya nchi yetu kwa mwaka 2019/20 na siku zijazo. Napenda kwa niaba ya Serikali kuwashukuru sana kwa michango hiyo mizuri ambayo tumejitahidi kuizingatia. Ni matarajio ya Serikali kwamba wadau hao wataendelea kufanya hivyo katika mchakato wa bajeti zitakazofuata.

61. Mheshimiwa Spika, bajeti ya 2019/20 inahusu kuendeleza juhudini za kujenga msingi wa uchumi wa viwanda ili kupanua fursa za ajira na kuchochaea ukuaji wa uchumi wa Taifa na ustawi endelevu wa jamii na hatimaye kuondokana na umaskini, ujinga na maradhi. Hususan, bajeti hii imelenga:

i. Kuimarisha na kujenga miundombinu ya kisasa ili kuongeza uwezo wa Taifa katika uzalishaji viwandani hasa vile vinavyotumia malighafi zinazopatikana kwa wingi hapa nchini na kutoa huduma bora (afya, elimu na maji) kwa wananchi. Aidha, miundombinu hiyo itasaidia kuongeza biashara nchini, kikanda na kimataifa;

ii. Kujenga mazingira mazuri ya kufanya biashara na uwekezaji kwa kushughulikia changamoto zilizobainishwa katika mpango wa kuboresha mazingira ya biashara (Blueprint);

iii. Kuimarisha kilimo (uzalishaji wenye tija na masoko ya mazao, ufugaji, uvuvi, na misitu) kwa kuzingatia umuhimu mkubwa wa sekta hii katika uchumi wa Taifa (chakula, ajira,

kipato cha mwananchi, mchango katika fedha za kigeni na muunganiko wa sekta hii na maendeleo ya viwanda);

iv. Kudumisha amani na usalama katika Taifa; na Kujenga misingi ya Taifa kujitegemea kiuchumi

62. **Mheshimiwa Spika**, safari ya kujenga Tanzania mpya imeiva lakini haitakuwa rahisi hasa tukizingatia mabadiliko yanayoendelea katika uchumi wa dunia, ushindani mkali wa kibiasara, mabadiliko ya haraka ya teknolojia na demografía na changamoto zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi. Hata hivyo, bahati nzuri ni kuwa, katika historia ya nchi yetu, Watanzania ni watu jasiri katika mapambano dhidi ya changamoto zinazojitokeza na kila wakati zilipojitokeza tulizishinda kwa kutumia ubunifu na nguvu ya umoja wa Watanzania.

63. **Mheshimiwa Spika**, hivi sasa tuko imara zaidi chini ya uongozi shupavu wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Uchumi wetu unaendelea kukua kwa kasi kubwa, ambapo mwaka 2018 ulikua kwa asilimia 7.0 na kiwango cha umaskini wa mahitaji ya msingi kinazidi kupungua kutoka asilimia 28.2 mwaka 2011/12 hadi asilimia 26.4 mwaka 2017/18. Naamini pasipo shaka yoyote kwamba kwa umoja wetu, uongozi makini, kufanya kazi kwa bidii na kwa kutumia rasilimali za nchi yetu vizuri, tutaijenga Tanzania mpya, ambayo itakuwa kitovu kikuu cha uchumi (Economic hub) katika ukanda wa Afrika Mashariki katika muda usiozidi miongo miwili ijayo.

64. **Mheshimiwa Spika**, ninapoelekea mwisho wa hotuba hii, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Washirika wetu wa Maendeleo kwa misaada na mikopo nafuu wanayoendelea kutupatia katika kutekeleza miradi na programu mbalimbali za maendeleo nchini. Katika bajeti ya mwaka 2019/20, Washirika wa Maendeleo kwa pamoja wanatarajia kuchangia jumla ya shilingi triliioni 2.78. Naomba niwatambue kwa kuwataja mmoja mmoja: Nikianza na nchi za Canada, China, Denmark, Finland, India, Ireland, Italia, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Norway, Poland, Sweden,

Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Ujerumani, Uingereza, na Uswisi. Aidha, zipo taasisi za kimataifa ambazo ni: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia, Arab Bank for Economic Development in Afrika (BADEA), Global Fund, Kuwait Fund, Abu Dhabi Fund, Jumuiya ya Umoja wa Ulaya (EU), Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), OPEC Fund, Global Environmental Facility (GEF), Shirika la Mapinduzi ya Kijani Afrika (AGRA), Mfuko wa kukingga Hatari ya Kimazingira (GRMF), Climate Development Special Fund, African Legal Support Facility (ALSF), Dignity, Global Agriculture and Food Security Program (GAFSP), na Mashirika ya Umoja wa Mataifa yakiwemo UNICEF, IFAD, UNDP, UNFPA, Shirika la Chakula na Kilimo (FAO), na United Nations Environment Programme (UNEP). Napenda pia kutambua uhusiano mzuri tulionao na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF). Ni matarajio yetu kuwa misaada ya kiufundi na fedha zilizoahidiwa na marafiki zetu hawa zitatolewa kwa wakati na kwa kiasi kilichoahidiwa. Nasi kwa upande wa Serikali tunaahidi kutumia misaada hiyo kama ilivyokusudiwa.

65. Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kuwashimiza Waheshimiwa Mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao na taasisi za kimataifa hapa nchini Tanzania waongeze nguvu kukuza biashara kati ya nchi zao na nchi yetu na kuhamasisha wenye mitaji toka nchi zao kuja kuwekeza hapa Tanzania. Tanzania ni salama kwa uwekezaji wenye faida kwao na kwetu. Aidha, wafanye jitihada zaidi kuhamasisha watalii kuja kujiona vivutio vya utalii, ambavyo ni fahari ya Tanzania.

66. Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano inatambua na kuthamini michango yao katika maendeleo ya Taifa letu ili mradi islambatane na masharti yanayohatarisha uhuru wa Tanzania (national sovereignty), au kwenda kinyume na mila na desturi zetu. Hata pale ambapo Serikali au mihimili mingine imefanya maamuzi ambayo hawakubaliani nayo, ni vema na haki washirika wetu wa maendeleo watupe muda wa kuyatafakari na kujadiliana nao kwa staha badala ya kuishinikiza Serikali ibadili uamuzi

wake ndipo watoe fedha, jambo ambalo halikubaliki hata kidogo.

67. Mheshimiwa Spika, kwa Watanzania wenzangu, napenda kuwasilitiza tuendelee kushikamana katika kujenga Tanzania mpya. Tuwe wazalendo na tena tukae macho daima kulinda na kutetea maslahi ya Taifa letu. Tuongeze bidii kufanya kazi. Enzi za kutegemea wajomba hazipo tena na habari njema ni kuwa: "Tukiamua Tunaweza" na Serikali ya CCM inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli imethibitisha ukweli huo.

68. Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Serikali kupongeza mchango mkubwa wa wafanyabiashara na wananchi wote ambao wamelipa kodi kwa mujibu wa sheria. Aidha, napenda kutambua mchango adhimu wa mashirika na taasisi ambazo Serikali ina hisa yaliyotoa gawio au asilimia 15 ya mapato ghafi kuingia katika Mfuko Mkuu wa Hazina. Katika mwaka ujao wa fedha, Serikali inayataka mashirika yote ya umma na taasisi ambazo Serikali ina hisa kuhakikisha kuwa wanatoa gawio au mchango wa asilimia 15 ya mapato ghafi na Msajili wa Hazina asimamie kikamilifu utekelezaji wa maagizo haya ya Serikali.

69. Mheshimiwa Spika, kama mnavyofahamu, mwezi Oktoba mwaka huu wa 2019 tutafanya uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Serikali kwa upande wake imejipanga kikamilifu katika maandalizi ikijumuisha mahitaji ya kibajeti kwa ajili ya kufanikisha uchaguzi huo. Ninawasihi wananchi wote wenye sifa wajitokeze kutumia haki yao ya msingi ya kupiga kura. Aidha, katika kuchagua viongozi wa ngazi hiyo, tafuteni Watanzania wenye sifa zifuatazo:

- i. Awe mchapakazi mwenye kujitoa sadaka kuwatumikia watu, hasa wananchi wa kawaida;
- ii. Awe mwelesi kuona, kusikiliza na kuguswa na shida za wananchi wake. Tena awe jasiri katika kupigania haki za wanyonge na awe na uwezo na ubunifu katika kutatua kero za wananchi hao;

- iii. Awe mwadilifu, anayechukia na kupiga vita rushwa na ufisadi kwa matendo;
- iv. Anayetambua fursa zilizopo katika eneo lake, kubuni mikakati ya kuwaendeleza wananchi anaowaongoza na kuwatia watu wake hamasa ya kuthubutu kutumia fursa hizo;
- v. Awe mtetezi hodari wa kulinda mazingira na mpambanaji dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi;
- vi. Mwenye kutoabudu nyadhifa; anayetambua kuwa nafasi na vyeo tulivyopewa ni vya muda tu. Ni vya kupita! Thamani halisi ya kiongozi ni kufanya kazi kwa bidii na kuacha kumbukumbu nzuri kwa ustawi wa eneo analoliongoza na Taifa kwa ujumla;
- vii. Awe kama mchezaji mzuri wa kiungo katika timu ya ushindi, anayetambua kwamba mkono mmoja hauwezi kupiga makofii ya shangwe;
- viii. Awe mwenye kutambua kwamba kazi za kiongozi zina maana sana kwa kuwa zinamwezesha kubadilisha maisha ya maelfu ya Watanzania, hasa wanyonge, kuwa bora zaidi;
- ix. Awe na uwezo wa kuwaeleza wananchi kinaganaga kuhusu Serikali yao inawapeleka wapi na wajibu wa kila mmoja ili waendelee kuiunga mkono; na
- x. Awe anatoka ndani ya chama cha siasa kinachotetea maslahi na haki za wanyonge na chama hicho ni CCM!

Naomba nikiri kuwa, sifa hizi nilizozitaja nimeziazima kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila ridhaa yake!

70. Mheshimiwa Spika, nawaomba viongozi wote wa dini pamoja na waumini wote kila mmoja kwa imani yake, tuendelee kumwombea Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ili Mwenyezi Mungu aendelee kumjalia afya njema, hekima, busara na

kumwongoza kwa kila jambo alifanyalo kuliletea Taifa letu maendeleo.

71. Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru viongozi wenzangu wa Wizara ya Fedha na Mipango, ambao wamekuwa msaada mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara na maandalizi na uratibu wa bajeti hii ya Watanzania. Kipekee ninawashukuru Mheshimiwa Dkt. Ashatu K. Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango ambaye ni Mbunge mahiri wa Jimbo la Kondoa; Katibu Mkuu HAZINA na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Bwana Doto M. James, pamoja na Naibu Makatibu Wakuu, Bi. Amina Kh. Shaaban, Dkt. Khatibu M. Kazungu na Bwana Adolf H. Ndunguru pamoja na watumishi wa ngazi zote wa Wizara ya Fedha na Mipango. Vile vile, ninamshukuru Profesa Florens D. Luoga, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania pamoja na Naibu Gavana Dkt. Yamungu Kayandabila, Dkt. Bernard Kibesse na Bwana Julian Raphael Banzi kwa kusimamia vema sekta nyeti ya fedha. Kwa nafasi ya kipekee, napenda nimpongeze Dkt. Edwin Mhede kwa kuteuliwa na Rais kuwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Ni matumaini yangu na ya Watanzania kuwa atakuwa chachu ya kujenga taswira mpya ya TRA itakayoongeza mapato ya Serikali bila manyanyaso kwa wafanya biashara.

72. Mheshimiwa Spika, ninawashukuru viongozi na watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Taktamu, Ofisi ya Msajili wa Hazina na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao. Nawashukuru Wakuu wote wa Idara na Vitengo, Taasisi na Wakala za Serikali zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na wafanyakazi wake wote kwa kazi nzuri wanazofanya na kuendelea kunipa ushirikiano wa dhati katika kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi wa hali ya juu.

73. Mheshimiwa Spika, niwashukuru pia wananchi wenzangu wa Wilaya ya Buhigwe na mkoa wetu wa Kigoma ambao walinilea na kunifundisha kufanya kazi. Mwisho kabisa naishukuru familia yangu, hususan mke wangu mpenzi na rafiki yangu Mbonimpaye, watoto, wajukuu, ndugu, jamaa na

marafiki zetu wote tuliopewa na Mungu. Asanteni kwa kuniombea msaada wa Mungu katika kazi hii, usiku na mchana. Nami ninasema kwa kila mmoja wao:

*"Bwana akubarikie na kukulinda,
Bwana akuangazie nuru za uso wake, na kukufadhili,
Bwana akuinulie uso wake, na kukupa amani"*

Hesabu 6: 24-26.

Nimalizie kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa baraka zake na kuniwezesha kuwasilisha hotuba hii. Aidha, apende kuendelea kunijalia uwezo na unyenyekevu wa kulitumikia Taifa letu na wananchi wake kwa uadilifu. Asanteni sana Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa kunisikiliza.

MUNGU IBARIKI AFRIKA, MUNGU IBARIKI TANZANIA

74. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:
Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono kwa kiasi kikubwa sana, ahsante sana Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango tunakushukuru sana kwa kutupatia hotuba yako ambayo imechukua takribani masaa mawili kuiwasilisha, tunakushukuru tena. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge mkiangalia *title* ya kitabu hiki mtaona hiki alichowasilisha Mheshimiwa Waziri imeandikwa pale Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2019/2020. Kwa hiyo, alichokisoma hapa bado ni mapendekezo ya Serikali kwenu ninyi Waheshimiwa Wabunge. (*Makofii*)

Kwa hiyo, mnayo wiki nzima kuanzia Jumatatu inayofuata ya kujadiliana humu ndani na kutoa maoni kuhusiana na mapendekezo haya, halafu iko siku tutapiga kura kila Mbunge kwa jina lake kuhusiana na hoja hii ya

Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango ili kuihitimisha hoja hiyo.

Kwa hiyo, nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na timu nzima ya Wizara ya Fedha na Mipango na Serikali kwa ujumla. Chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa jinsi ambavyo imeweza kuandaliwa hotuba hii au hoja hii ambayo imependekezwa Bungeni iliyosheheni mambo mengi muhimu mazuri kwa nchi yetu, mambo mengi sana yameguswa maeneo mengi yameguswa kwenye kilimo, viwanda, uwekezaji, miundombinu, elimu, afya, maji na kadhalika, kila sekta. (*Makofi*)

Tumeona jinsi ambavyo utitiri wa Kodi umerekebishwa na kuwekwa sawa, vitengo vili vyokuwa vinalalamikiwa sana, *TFDA, TBS, Mkemia Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi*, kodi nyingi sana zimerekebishwa, kufutwa na kadhalika.

Mpaka hata mawigi yamekumbukwa safari hii.
(*Kicheko/Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

SPIKA: Na bado wiki ijayo kuna mapendelekezo yanakuja naamini wengine watapendekeza kucha, kope nazo ziingie, wanja. (*Kicheko/Makofi*)

MBUNGE FULANI: Na kope.

SPIKA: Na kadhalika, na kadhalika, tunaipongeza sana Serikali kwa kweli msingi tulioanza nao ni msingi imara sana, hii kweli ni bajeti ya nne, ni bajeti ambayo inazidi kuimarisha ile misingi ambayo Awamu ya Tano ilianza nayo, tunapongeza sana Serikali. (*Makofi*)

Sasa Waheshimiwa Wabunge tunao wageni wengi ambaao ningependa kuwatambulisha na ni wageni muhimu

naomba tuwe na utulivu ili tuweze kuwafahamu wote walio tupu heshima ya kufika kama mnavyoona *gallery* zetu zimejaa sitawenza kumtambulisha kila mmoja wao lakini nitajitahidi.

Lakini kabla ya wote naomba nimlete mgeni wangu maalum hapa ili nipate nafasi ya kuendelea na utambulisho nianzie hapa mezani.

(Hapa Ndugu Theresia Jacob Kavishe Aliingia Ukumbini)

SPIKA: Ehehe, naomba usimame hapa. Ehehe, hapo hapo. *(Makofi)*

Huyu anaitwa Theresia Jacob Kavishe ni mtumishi wa Ofisi ya Spika, ni mtumishi ambaye aliajiriwa akiwa bado binti mdogo na bado anatumikia Ofisi ya Spika, mkiona mambo yanafanikiwa hapa ni kutokana na *support* kubwa tunaipata kutoka kwa watu ambao wako nyuma yetu wasioonekana. *(Makofi)*

Nimemsimamisha hapa Theresia, hata Katibu wa Bunge anashangaa kuna nini hapa? Kwa sababu mtumishi huyu ametumikia maspika kadhaa katika Ofisi ya Spika, kwa mara ya kwanza kabisa alipoajiriwa alimtumikia Spika, Mzee Adam Sapi Mkwawa. *(Makofi/Vigelegele)*

Baada ya hapo akamtumikia Mzee Msekwa/Spika Msekwa, baada ya hapo akamtumikia Spika Samuel Sitta, baada ya hapo amemtumikia Spika Anne Semamba Makinda na mpaka leo hii, bado yuko kwenye ofisi yangu anaendelea na mimi kunitumikia na kunipa ushirikiano. Ni nadra sana kuwa na mtumishi, katika Ofisi nyeti kama hiyo kwa miaka yote hiyo. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Kweli.

SPIKA: Ni uaminifu wa hali ya juu sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Kwa hiyo kwa kweli nimemuita kumpongeza na kumpa mkono mbele yenu, tunakushukuru sana. Yeye ni wa ngazi ile tu ya uhudumu lakini kwa kweli amefanya kazi yake kwa miaka yote naomba tumpigie makofi ya pongezi Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi/Vigelegele*)

MBUNGE FULANI: Tumpe na hela, apewe hela.

SPIKA: Ahsante sana Theresia siku zote yuko ofisini hakuna cha Jumamosi yuko ofisini, Jumapili inafunguliwa ofisi anakuwepo, sikuu zote yuko ofisini kwa miaka yote hiyo. (*Makofi/Vigelegele*)

Kwa hiyo, Katibu wa Bunge huyu mtumishi bwana ehehe na bahati nzuri Mkuu wa Utumishi wa Umma yupo nitamtambulisha hapo juu baadae kidogo apate zawadi ya shillingi millioni kumi. (*Makofi/Vigelegele/Kicheko*)

Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge na makofi haya pande zote yanaonesha jinsi ambavyo anatumika kwa uaminifu kabisa wala hana tatizo. (*Makofi/Vigelegele*)

Sasa kuhusu wageni Waheshimiwa Wabunge naomba nianze na mgeni wetu wa kwanza, Katibu Mkuu Kiongozi - Balozi John Kijazi, ahsante sana. Mheshimiwa Balozi karibu sana, tunafurahi kuwa pamoja naye. (*Makofi*)

Wanaofuata ni viongozi waandamizi wa Chama cha Mapinduzi, wanaongozwa na Katibu Mkuu wa CCM - Dkt. Bashiru Ally Kakurwa, ahsante sana na karibu sana. (*Makofi*)

Katibu Mkuu wa Chama, amefuatana na Naibu Katibu Mkuu Bara - Ndugu Rodrick Lazaro Mpogole, ahsante sana. (*Makofi*)

Pia yupo Naibu Katibu Mkuu Zanzibar - Ndugu Abdallah Juma Saadala, karibu sana. (*Makofi*)

Lakini pia yuko Katibu Mkuu UWT Taifa - Ndugu Queen Mlozi, karibu sana. (*Makofi/Vigelegele*)

Lakini pia yupo M-NEC na mmiliki wa Kampuni ya ASAS Ndugu Salim Abri kutoka Iringa, ahsante sana Salim Abri tunakushukuru sana kwa ushirikiano ambao huwa unatupatia na leo umewakilisha Watanzania wafugaji na umeona mambo ya wafugaji yalivyoenda hapa. (*Makofi*)

Pia ninao wageni maalum ambao ni Waheshimiwa Mawaziri Wakuu Wastaifu, tunaye Waziri Mkuu Mstaifu Mheshimiwa Kayanza Peter Pinda. (*Makofi/Vigelegele*)

Waheshimiwa Wabunge nafikiri toka alivyostaifu hapa hajaja kututembelea, kumbukumbu zangu ni sahihi! Haya basi leo amekuja Mzee Pinda hebu mpeni makofi ambayo yanamstahili. Ahsante sana. (*Makofi/Vigelegele*)

Lakini pia yupo Waziri Mkuu Mstaifu, Mheshimiwa John Samwel Malecela, ahsante sana Mzee Malecela kwa kututembelea, jina lake la wenyeji linaitwa Chiguyemisi. (*Makofi/Vigelegele*)

Pia tunao Wakuu wa Vyombo vyta Ulinzi na Usalama, tuna Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa - Ndugu Edward Nyamanga, tuna mwakilishi wa Inspeksi Jenerali wa Jeshi la Polisi - Kamishna Benedict Wakulyamba, tuna Mwakilishi wa Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa - Kanali David Msakulo, ahsante; tuna Mwakilishi wa Kamishna Jenerali wa Magereza CP. Tusekile Sandambila. (*Makofi/Vigelegele*)

Tuna Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Ndugu Thobias Andengenye, ahsante sana; tuna Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar akimwakilisha Kamishna Jenerali wa Uhamiaji Ndugu Johari Masoud Sururu. (*Makofi/Vigelegele*)

Tunaye Kaimu Kamishna wa Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevy, Ndugu Valite Mwashusa; tuna Naibu Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Brigedia Jenerali John Mbung'o, ahsante; tuna Mratibu Msaidizi Mkuu wa Baraza la

Usalama wa Taifa, Brigendia Jenerali Masele Machanga.
(Makofi)

Pia tunao watendaji wakuu wa Serikali akiwemo Katibu Mkuu Wizara ya Fedha - Ndugu Doto James, yupo Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha - Ndugu Adolf Ndunguru, yupo Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha - Dkt. Khatibu Kazungu, yupo Naibu Katibu Mkuu Maboresho - Ndugu Amina Shaban, yupo Msajili wa Hazina - Ndugu Athumani Mbutuka, yupo Gavana wa Benki Kuu - Profesa Florens Luoga, Kamishna Mkuu wa *TRA* - Dkt. Edwin Mhede, Naibu Kamishna Mkuu wa *TRA* - Ndugu Msafiri Mdibo, yupo Naibu Msajili wa Vyama vyaa Siasa - Ndugu Mohamed Ahmed, Iakini pia yupo Mtendaji Mkuu wa Mahakama - Ndugu Hussein Katanga. *(Makofi)*

Pia tuna viongozi waandamizi kutoka Mkoa wa Dodoma, wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dkt. Binilith Mahenge, karibu sana Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa na mwenyeji wetu, karibu sana. Mstahiki Meya wa Dodoma, Profesa Davis Mwamfupe, Profesa Mwamfupe mwalimu wangu karibu sana. Pia yupo Katibu wa Kikosi Kazi cha Taifa cha kuratibu mpango wa Serikali kuhamia Dodoma - Ndugu Meshack Bandawe. Ahsante karibu sana Bandawe kutoka NSSF. *(Makofi)*

Pia familia ya Waziri wa Fedha na Mipango wapo; yupo Mama Waziri Mpango Ndugu Mbonimpaye Mpango, hyo ndiyo shemeji yetu jamani Mama Waziri wa Fedha, ahsante sana. Safari hii hata Katibu Mkuu Dotto naye ameleta mke wake, kumbe ana mke Katibu Mkuu. *(Makofi/Kicheko)*

Jamani mtani wangu huyu nimefuta kauli, Ndugu Irene Doto James, ahsante sana, karibu sana Irene, karibu sana shemeji yangu. Pia yupo mkwe wa Mheshimiwa Waziri Mpango anaitwa Ndugu Emmanuel Kuwese, karibu sana Emmanuel. Wako wageni maalum kabisa wa Mheshimiwa Waziri ambao ni wajukuu zake, Angela. Angela yuko wapi! Ahsante sana Angela, karibu sana karibu sana. *(Makofi)*

Pia tuna Mabalozi kadhaa, tunaanza na Balozi wa Denmark - Mheshimiwa Eina Jensen, ahsante Mheshimiwa Balozi karibu sana; Balozi wa Rwanda - Mheshimiwa Eugene Kayihura, ahsante sana; Balozi wa Angola - Mheshimiwa Joel Cuvuna, karibu sana Balozi; Balozi wa Malawi - Mheshimiwa Glad Munthali; Balozi wa Ubelgiji - Mheshimiwa Peter Van Acket; Kaimu Balozi wa Zimbabwe - Mheshimiwa Martin Tavenyika, ahsante; Kaimu Balozi wa Finland - Mheshimiwa Heine Pauli, ahsante; Mkuu wa Ofisi Ndogo ya *World Food Program* Dodoma - Ndugu Nima Sitta, karibu sana; Mwakilishi wa Balozi wa Switzerland - Ndugu Luca Etter; Mkuu wa Kitengo cha Sera kutoka *UNICEF* - Ndugu Paul Ufford, ahsante; Mwakilishi Mkazi wa *UN Women* - Hodan Addou; Mwakilishi wa Balozi wa Kenya - Ndugu Habiba Feby; Mwakalishi wa *DFID* Tanzania - Ndugu Francis Sampa; Mwakilishi wa *IMF* Tanzania - Ndugu Rutachurururwa; Mwakilishi wa Balozi wa Msumbiji - Madam Sulumide, karibu sana jirani. (*Makofi/Vigelegele*)

Kama kuna wengine nitakuwa labda sijapata majina yao lakini hayo ndiyo niliyonayo kwa sasa.

Watumishi wastaa fu wa Ofisi ya Bunge, Ofisi ya Bunge immealika baadhi ya watumishi wake wastaa fu safari hii, akiwemo Ndugu John Joel Nchwali. Yuko wapi John Joel, ooh! Eeh yule pale, karibuni sana JJ. Karibu sana. (*Makofi*)

Pia yupo Ndugu Japhet Sagasii, karibu sana Sagasii. Wabunge wapya mtawashangaa kidogo, lakini hawa ndiyo magwijji wenye we waliofanya kazi hapa kwa miaka mingi sana. (*Makofi*)

Pia yupo Ndugu Eliachim Mrema, Eliachim Mrema, ahsante sana nashukuru sana kukuona, karibu sana. (*Makofi*)

Yupo Ndugu Goodchance Kombe, karibu sana Kombe, huyu alikuwa ndiyo Mweka Hazina wetu wa miaka mingi sana, kabisa. (*Makofi/Kicheko/Vigelegele*)

Yupo Ndugu Abdallah Selemani, Abdallah huyo! Abdallah hebu simama tena bwana, huyu alikuwa mhudumu wetu humu ndani kwa miaka mingi sana sana, sana na alifanya kazi kwa uaminifu mkubwa. Tunashukuru kukuona una afya nje kabisa. (*Makofi/Kicheko/Vigelegele*)

Pia yupo Ndugu Abdallah Gora, ahsante sana na karibuni sana. Tunapowaona tunafurahi sana. (*Makofi*)

Pia tunao Makatibu Wakuu wa Wizara, naomba Makatibu Wakuu wa Wizara wote pale mlipo Wizara mbalimbali naomba msimame wote, Makatibu Wakuu. Ahsateni sana Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu, ahsanteni sana kwa kufika kwenu. (*Makofi*)

Tuna viongozi wa CCM wa Mkoa wa Dodoma, pale mlipo naomba msimame. Viongozi wa CCM Mkoa wa Dodoma, wale pale wengine. (*Makofi*)

Viongozi wa dini kutoka Mkoa wa Dodoma pale mlipo naomba msimame ahsante sana, karibuni sana. (*Makofi*)

Wawakilishi wa Vyama vyा Siasa vyenye uwakilishi Bungeni, naomba msimame, wengine wako kule. /see, wale wa kwenu mbona hawajaja jamani? Wako wapi! (*Kicheko*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

SPIKA: Viongozi wa Taasisi za Elimu ya Juu, karibuni na Wakuu wa Mashirika na Taasisi mbalimbali za Wizara ya Fedha toka Wizarani na hapa katika Mkoa Dodoma pia karibuni sana. (*Makofi*)

Pia nilikuwa nimemruka Mwakilishi wa Mkuu wa Majeshi ambaye ni Kanali Ramson Mwaisaka ambaye ni *Base Commander* wa Dodoma, karibu sana samahani kukuruka, ahsante sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

Basi Waheshimiwa Wabunge kwa hatua hii tuliyofikia naomba niwashukuruni sana kwa usikivu mliokuwa nao mkubwa wakati wa kusikiliza hotuba ya bajeti na uchangamfu pia mliounesha pale mlipoguswa pale kwa maandalizi ya kwamba Oktoba/Novemba iko kazi ya kufanya, kwa hiyo ni changamoto za kawaida.

Waheshimiwa Wabunge, samahani kuna ukurasa ambaao vijana wangu hawakuwa wameniletea; ninaye Mwenyekiti wa Benki ya *CRDB* - Ndugu Ally Husseini Laay, tafadhalii Mwenyekiti wa Benki ya *CRDB* ahsante sana na karibu sana, nasikia Jumapili tunalo Bonanza pamoja na *CRDB*. (*Makofi*)

Tunaye pia Mtendaji Mkuu wa *CRDB* - Ndugu Abdulmajid Mussa Nsekela, ahsante sana Abdulmajid. Eeh, inaonekana timu ya *CRDB* imeshawasili tayari kwa ajili ya mechi hiyo, mechi mbalimbali za Jumapili, lakini pia Mjumbe wa Bodi - Ndugu Martin Warioba kutoka Benki ya *CRDB*, karibu sana Martin, karibu sana. (*Makofi/Vigelegele*)

Lakini pia kuna Waheshimiwa Mabalozi ambaao sasa nimepata majina yao, naomba nimtambulisse Balozi wa Norway - Mheshimiwa Elisabeth Jacobsen, Balozi wa Norway ahsante sana na karibu sana Balozi Elisabeth; Balozi wa Ufaransa - Mheshimiwa Fredric Clavier, ahsante sana; Balozi wa Sweden - Mheshimiwa Anders Sjoberg, karibu sana; Balozi wa Ireland - Mheshimiwa Paul Sherlock, ahsante sana karibuni sana; Naibu Balozi wa Burundi - Mheshimiwa Ndayishimiye na Balozi wa Brazil - Mheshimiwa Antonios A. M. Cesar. Karibuni sana na samahani sana Waheshimiwa Mabalozi mezani kwangu hapa mambo yalijichanganya kidogo, mtwie radhi sana. (*Makofi*)

Pia naomba nimtambulisse kipekee kabisa Katibu Mkuu wa Chama cha *CUF* - Ndugu Khalifa Suleman Khalifa, ahsante sana. Huyu ni Mbunge wa miaka mingi, sasa ndiyo Katibu Mkuu wa Chama cha *CUF*, hongera sana. (*Makofi/Vigelegele*)

Pia nilimruka Katibu wa *Organization* wa Chama cha Mapinduzi - Ndugu Pereira Silima, ahsante sana. Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. (*Makofii/Vigelegele*)

Basi nawashukuru sana kwa ushirikiano ambao tumekuwa nao kwa siku ya leo; kama nilivyosema kwa hiyo siku ya kesho Ijumaa hatukutani ili kutoa nafasi ya Waheshimiwa Wabunge kuweza kupitia vitabu vile ambavyo tumepewaa/ambavyo tumegaiwa, ni vingi na vina majedwali mengi, kwa hiyio Ijumaa, Jumamosi, Jumapili; tutakutana Jumatatu saa tatu kamili asubuhi ndiyo tunaanza kwa ajili ya mjada. Mjadala ambao utaendelea hadi tarehe ambayo tutaambiya, nadhani tarehe 25 Juni kama sikosei, lakini tutapewaa tarehe maalum ambayo sasa tutakutana kwa ajili ya kupiga kura.

Naomba kila mmoja wetu asome vizuri vitabu hivi illi uchangiaji wetu uje uwe na maana zaidi katika kuishauri Serikali ni maeneo gani ya kuboresha zaidi, maeneo gani ya kurekebisha, maeneo gani ya kuweka sawa katika hoja hii nzuri sana ambayo Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango ameileta mbele yetu sisi Wabunge, tunatakiwa tufanye hivyo kwa niaba ya wananchi wa Tanzania.

Kwa hatua hiyo basi, naomba nahirishe shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 12.35 Bunge Lilahirishwa hadi Siku ya Jumatatu,
Tarehe 17 Juni, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*